**9 MEI, 2024**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Ishirini na Mbili– Tarehe 9 Mei, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* - KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MHE. REGINA N. QWARAY K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI, NA MAZINGIRA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge, Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* - KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**SPIKA:** Maswali kwa Waziri Mkuu, nimuite Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Waziri Mkuu anayo taarifa ambayo anataka kuwajulisha ninyi pamoja na watanzania ataanza na hiyo kama muda utaruhusu basi mtamuuliza maswali. Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ametuwezesha kuwa na mwendelezo mzuri wa Kikao hiki cha Ishirini na Mbili cha Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge lako Tukufu tukiwa na afya njema na huku tukiendelea kutekeleza majukumu yetu kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, kama inavyofahamika Kanuni zetu za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 limetoa fursa ya uwepo wa maswali ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu kwa siku ya Alhamisi. Vilevile Kanuni ya 44(4) kimeruhusu Waziri Mkuu kutumia kipindi cha maswali ya papo kwa papo kutoa taarifa au ufafanuzi kuhusu suala lolote linalohusiana na shughuli za Serikali na lenye maslahi kwa umma.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kanuni hiyo naomba Bunge lako Tukufu sasa liridhie niwasilishe taarifa kuhusu Kimbunga Hidaya kilichotokea tarahe 03 Mei, 2024 katika Pwani ya Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Spika, kama mtakumbuka siku ya tarehe 03 Mei, 2024 Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu Mheshimiwa Jenista Mhagama Mbunge, alitoa taarifa ya tahadhari ya kuwepo kwa Kimbunga Hidaya mbele ya Bunge lako Tukufu kutokana na taarifa iliyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania *(TMA)* siku ya tarehe 01 Mei, 2024.

Mheshimiwa Spika, tangu mwanzoni mwa mwezi Aprili, 2024 eneo la Pwani ya Afrika Mashariki lilitawaliwa na mgandamizo mdogo wa hewa ambao ulisababisha mvua nyingi katika eneo kubwa la Pwani hiyo. Mnamo tarahe 30 Aprili, 2024 mifumo ya hali ya hewa iliendelea kuimarika zaidi na kutengeneza mgandamizo mdogo wa hewa uliokuwa na mzunguko wa upepo katika eneo la Latitudo 7.62 Kusini na Longitudo 45.06 Mashariki ikiwa na kiasi cha mgandamizo wa hewa wa *hectopascal* 1003 na upepo mkali wenye kasi ya kilomita 50 kwa saa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa mifumo ya hali ya hewa ulionesha kuwa mgandamizo huo mdogo wa hewa ulikuwa ukielekea Magharibi kuja Pwani ya nchi yetu. Hivyo ilipofikia asubuhi ya Jumatano tarehe 01 Mei, 2024 mgandamizo huo mdogo wa hewa ulifikia kiwango cha *hectopascal* 1001 na kasi ya upepo wa kilomita 60 kwa saa katika eneo la Latitudo 8.4 kusini na longitudo 45.58 mashariki ikiwa ni takribani kilomita 630 Mashariki mwa Pwani ya Mtwara.

Mheshimiwa Spika, ilipofika usiku wa tarehe 01 Mei, 2024 mgandamizo huo mdogo wa hewa ulikuwa takribani kilomita 550 Mashariki mwa Mtwara pia mgandamizo huo ulioimarika zaidi na kufika hadhi ya kimbunga cha kiwango cha kati chenye kasi ya upepo wa kilomita 70 kwa saa.

Mheshimiwa Spika, inapofikia hatua hii vimbunga hupewa majina ambapo mgandamizo huo mdogo wa hewa ulipewa jina la Hidaya, *moderate trans tropical storm*. Uchambuzi wa mifumo ya hali ya hewa ulionesha Kimbunga Hidaya kilikuwa kikiendelea kuelekea Pwani ya Tanzania kwa siku ya alhamisi tarehe 02 Mei, 2024 kimbunga hicho kiliendelea kuimarika na kufika hadhi ya *severe tropical storm* yenye kiwango cha mgandamizo wa hewa wa *hectopascal* 985 na kasi ya upepo wa kilomita 110 kwa saa.

Mheshimiwa Spika, ilipofika ijumaa asubuhi tarehe 03 Mei, 2024 kimbunga hicho kiliimarika zaidi na kufikia hadhi ya kimbunga kamili *(tropical cyclone)* kikiwa na kiwango cha mgandamizo wa hewa ya *hectopascal* 976 na kasi ya upepo wa kilomita 140 kwa saa. Wakati huo Kimbunga Hidaya kilikuwa takribani kilomita 342 Mashariki ya Pwani ya Mtwara.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umbali huo vipindi vya mvua na upepo mkali unaozidi kilomita 40 kwa saa vilianza kujitokeza katika maeneo ya Mikoa ya Lindi na Mtwara kuanzia mchana wa siku hiyo ambapo hali hiyo ilijitokeza kama ilivyotabiriwa na wataalam wetu na ilipofika usiku wa ijumaa tarehe 03 Mei, 2024 athari zilianza kujitokeza katika maeneo ya Pwani mwa nchi yetu ikiwemo katika vituo vya hali ya hewa ya Mtwara, Kilwa, Zanzibar na Dar es Salaam ambapo upepo mkali uliozidi kilomita 40 kwa saa uliweza kupimwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika kipindi hicho vipindi vya mvua kubwa viliweza kushuhudiwa katika maeneo ya Mtwara na Lindi wakati huo kimbunga kilikuwa kinasogea karibu kabisa na Pwani ya nchi yetu katika eneo la bahari kwa takribani kilomita 170 Mashariki mwa Pwani ya Mafia na kilomita 230 kutoka Pwani ya Kilwa kikiwa na mgandamizo wa hewa wa kiasi cha *hectopascal* 985 na kasi ya upepo wa kilomita 120 kwa saa.

Mheshimiwa Spika, hadi ilipofika asubuhi ya jumamosi tarehe 04 Mei, 2024 kimbunga kilikuwa kimeshafika katika Kisiwa cha Mafia ambapo athari zake zilisambaa umbali wa takribani kilomita 200. Hata hivyo wakati Kimbunga Hidaya kilipokaribia Pwani ya nchi yetu kilianza kupoteza nguvu yake kwa kiasi kikubwa ambapo ni hali ya kawaida kwa kimbunga kinapofika eneo la nchi kavu kimbunga hicho kilipoingia Mafia kilikuwa na hadhi ya *severe tropical storm* kikiwa na kiwango cha mgandamizo wa hewa wa *hectopascal* 993 na kasi ya upepo wa kilomita 100 kwa saa.

Mheshimiwa Spika, kwa siku nzima ya Jumamosi tarehe 04 Mei, 2024 kitovu cha kimbunga hiki kiliendelea kuwemo ndani ya Kisiwa cha Mafia. Aidha, mawingu ya mvua yalikuwa yakiambatana na kimbunga hicho yalisambaa katika maeneo ya kusini mwa nchi hususan katika Mikoa ya Lindi, Mtwara, Morogoro, Pwani na maeneo jirani na kuweza kusababisha vipindi vya mvua kubwa kwa baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Spika, hadi ilipofika saa sita usiku wa tarehe 04 Mei, 2024 mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa ulionesha kuwa kimbunga hicho kimepoteza nguvu yake na kuanza kurejesha hali

ya utulivu, hivyo kuruhusu shughuli mbalimbali kuendelea ambazo zilisimama kutokana na hali iliyojitokeza.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uwepo wa Kimbunga Hidaya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania *(TMA)* ilitoa tahadhari ya maeneo yatakayofikiwa ikihusisha maeneo mbalimbali ya mikoa iliyo katika ukanda wa Pwani, Bahari ya Hindi na maeneo ya jirani. Mikoa hiyo ni Mtwara, Lindi, Pwani ikijumuisha visiwa vya Mafia, Dar es Salaam, Tanga, Morogoro na Visiwa vya Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa katika vipindi kadhaa vya hivi karibuni nchi yetu imepitiwa katika majanga mbalimbali yaliyosababishwa na mabadiliko ya tabia nchi. Hivyo, sambamba na juhudi za kibinadamu katika kukabiliana na majanga hayo, majanga haya ni ya asili na hakuna namna tunaweza kuzuia mvua kubwa kunyesha pamoja na vimbunga kutokea katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uwepo wa tishio la kimbunga hiki Serikali kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania *(TMA)* iliendelea kufatilia kwa karibu mifumo ya hali ya hewa kwa kutumia mbinu mbalimbali za utabiri wa hali ya hewa kama vile kutumia picha za *satellite* na mifumo ya kimahesabu ya *computer* ya hali ya hewa.

Mheshimiwa Spika, vilevile kulikuwa na vikao vya kitaalam vilivyokuwa vikifanyika mara kwa mara kwa njia ya mtandao. Vikao hivyo vilihusisha Idara ya Uratibu wa Maafa iliyopo Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi Kuu ya Utabiri wa Hali ya Hewa Dar es Salaam na Dodoma, Ofisi ya Hali ya Hewa Zanzibar, Ofisi ya Hewa Kanda ya Kusini iliyopo Mtwara na Ofisi ya Hali ya Hewa iliyopo Kilwa Masoko Mkoani Lindi.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa uwezo wa utabiri wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania umeendelea kuimarika kwa kiasi kikubwa kama ilivyoelezwa katika taarifa yangu ya tarehe 25 Aprili, 2024 kwa Bunge lako Tukufu kwamba kuimarika kwa mamlaka hiyo kunatokana na uwekezaji mkubwa ambao Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uwekezaji mkubwa aliofanya katika sekta ya Hali ya Hewa na kuiwezesha nchi yetu kutabiri masuala ya hali ya hewa kwa ufasaha mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na tishio la Kimbunga Hidaya jopo la wataalam bingwa wa Mamlaka ya Hali ya Hewa lilifanya kazi kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya kufanya mikutano kwa njia ya mitandao na kufanya ufatiliaji wa kina. Jopo hilo lilikutana na kufanya tathmini ya mwenendo wa kimbunga na kutoa taarifa kwa umma, wadau na mamlaka husika kila baada ya siku tatu kuanzia tarehe 01 Mei, 2024 hadi tarehe 05 Mei, 2024.

Mheshimiwa Spika, hatua hii ilienda sambamba na kutoa taarifa rasmi kwa kutumia vyombo mbalimbali vya mawasiliano ikiwemo redio, televisheni, magazeti, simu za mikononi na mitandao mbalimbali ya kijamii kama vile *YouTube*, *Facebook* na *Instagram*.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliendelea kuwajulisha wananchi juu ya uwepo wa kimbunga hiki na kuwataka kuchukua tahadhari. Aidha, Serikali ilitoa maelekezo mahususi ya hatua zinazopaswa kuchukuliwa kwa kamati za maafa, ngazi za mikoa hadi vijiji na taasisi zote zinazohusika na masuala ya dharura ikiwemo taasisi za ufatiliaji na uokoaji wa huduma za afya za dharura.

Mheshimiwa Spika, uwepo wa kimbunga hiki hapa nchini umesababisha mvua kubwa na upepo mkali katika Mikoa ya Pwani hasa Wilaya za Rufiji, Mafia, Kibiti, Mkoa wa Lindi Wilayani Kilwa, Mkoa wa Mtwara, Halmashauri ya Mtwara Vijijini, Manispaa ya Mtwara Mikindani, Mkoa wa Morogoro, Halmashauri ya Ifakara na maeneo mengine jirani na Ifakara.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Mafia kimbunga kimeleta athari mbalimbali katika Kata saba ambazo ni; Kilindoni, Miburani, Kiegayani, Kibondo, Ndagoni, Balemi na Kirogwe. Madhara yaliyotokea ni uharibifu wa mali, miundombinu mbalimbali ikiwemo makazi ya watu, shule, miundombinu ya afya,

ikiwemo hospitali ya wilaya imezingirwa na maji, masoko na taasisi nyingine za umma na binafsi. Vilevile barabara zimechimbika na kuangukiwa na miti mikubwa, nguzo za umeme zimekatika na kuanguka na kukosekana kwa huduma ya maji kutokana na kukosekana kwa umeme. Aidha, mmomonyoko wa udongo umetokea katika bandari yetu iliyoko Wilayani Mafia.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Rufiji Vijiji 6 vya Ngarambe Mashariki, Ngarambe Magharibi, chumbi A na B Nyamwage na Mbwara vimeathirika kutokana na mvua kubwa na upepo mkali. Katika Kijiji cha Chumbi A nyumba moja imeanguka, katika Kijiji cha Chumbi B ambapo kipo jirani na kambi ya waathirika wa mafuriko nyumba 10 zimejaa maji. Katika Kata ya Mbarwa miundombinu ya barabara kutoka Nyamagwe kwenda Tawi na Nyamagwe kwenda Mbwara imeharibika. Aidha, katika Kijiji cha Mbwara nyumba 37 zimepata athari za kuta kuanguka na kuezuliwa mapaa yake.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Kibiti vijiji 10 katika kata sita vimepata athari kiasi kutokana na mvua kubwa na upepo ambapo vijiji vilivyoathrika ni Kijiji cha Mchinga, Twasalie, Kiasi, Ruma, Hombwe na Jaja, Kiechuru, Maparoni, Hanga na Mbwera Magharibi. Madhara yaliyotokea katika vijiji hivyo ni pamoja na kuathirika kwa miundombinu ya makazi, soko na kuanguka kwa minazi.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Kilwa vijiji 13 katika kata 11 vimeathirika na mvua na upepo mkali ambapo madhara mbalimbali yametokea yakijumuisha vifo vya watu watatu kaya 178 zenye watu 941 zimezingirwa na maji, shule moja imezingirwa na maji, barabara kuu ya Lindi kuelekea Dar es Salaam imekatika katika kipande cha Somanga chenye urefu wa mita 200 kukwama kwa takribani magari 126 ikiwemo mabasi ya abiria, malori na magari binafsi.

Mheshimiwa Spika, inakadiriwa takribani watu 2,534 walikwama kwa sasa baadhi ya abiria na magari wamerudia njiani, njia ya Lindi Mjini wengine wamesafiri kupitia njia ya Songea kuelekea Dar es Salaam, wengine kurudi Dar es Salaam kutokea Somanga. Aidha, taasisi za umma, binafsi, makazi na wananchi

yalizingirwa na maji ikiwemo kituo cha Songasi ambapo watu 31 walizingirwa na maji katika mtambo wa kuchakata gesi.

Mheshimiwa Spika, katika Manispaa ya Mtwara vijiji sita, kata sita vimeathiriwa na mvua na upepo kutokana na athari za kimbunga hicho. Madhara mbalimbali yaliyotokea yanajumuisha nyumba 18 kubomoka na kusababisha watu kukosa makazi. Aidha, katika Wilaya ya Mtwara Kijiji cha Msimbati katika Kata ya Msimbati kimeathiriwa na mvua na upepo mkali uliosababishwa na kimbunga hicho. Madhara mbalimbali yaliyotokea yanajumuisha nyumba 21 kubomoka na nyingine 38 zimezingirwa na maji na kusababisha watu 42 kukosa makazi.

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri ya Mji wa Ifakara kata nne za Viwanja Sitini Basa, Kibaoni, Nakatindiuka vimeathirika kwa kiasi kikubwa kutokana na athari ya mvua ambazo zimesababisha mafuriko baada ya mto Lumeho kujaa na kumwaga maji kwenye makazi ya watu katikati ya Mji wa Ifakara. Athari zilizotokea ni pamoja na vifo vya watu saba nyumba zilizoboka ni 43 nyumba zilizozingirwa na maji ni 512, kuharibiwa kwa miundombinu na barabara zinazounganisha wilaya na wilaya barabara za vijiji na mitaa pamoja na miundombinu ya Reli ya *TAZARA*.

Mheshimiwa Spika, aidha, miundombinu ya barabara na makalvati hususan katika Tarafa ya Ifakara kutopitika kabisa kutokana na kujaa maji. Aidha, mazao mbalimbali yenye jumla ya hekari 23,501 vimeathirika ikiwemo mahindi, mpunga na mazao mengine mchanganyiko na mifugo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwezi Mei maeneo ya Kilwa na Mtwara yamerekodi kiwango kikubwa cha mvua kilichotokana na kimbunga hicho. Kwa kawaida wastani wa mvua kwa kituo cha Kilwa ni milimita 96.6 na kwa kituo cha Mtwara ni milimita 54. Hata hivyo, kuanzia tarehe 3 hadi 4 Mei, 2024 jumla ya milimita 316 za mvua zilipimwa katika Kituo cha Kilwa sawa na asilimia 327 ya kiwango cha mwezi. Kwa upande wa Mtwara jumla ya milimita 99 zilipimwa katika muda huu ambazo ni sawa na asilimia 183 za kiwango cha mwezi Mei.

Mheshimiwa Spika, kwa hali ya kawaida mvua ya milimita 316 iliyonyesha Kilwa kwa saa 36 ni sawa na mvua ya miaka mitatu kwa Mwezi Mei, yaani Mwezi Mei, 2024, Mei, 2025 na Mei, 2026. Hiki ni kiwango kikubwa sana na ndiyo maana kumekuwa na madhara ya uharibifu wa miundombinu mbalimbali kule Wilayani Kilwa.

Mheshimiwa Spika, nguvu ya upepo ulioambatana na kimbunga hiki katika nyakati tofauti ilifikia kilometa 140 kwa saa kasi ambayo ni kubwa sana. Wakati kinafika Mafia taarifa za Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania zilionesha kuwa upepo ulikuwa na kasi ya kilometa 110 kwa saa na mvua kubwa ambayo imeleta athari zilizoripotiwa.

Mheshimiwa Spika, kiujumla hadi sasa, mvua inayonyesha ikiambatana na upepo mkali katika maeneo yote imesababisha vifo vya watu watano, majeruhi saba ambapo kaya 7,023 zenye watu 18,862 zimeathirika. Umetokea uharibifu wa makazi ya watu ambapo jumla ya nyumba 2,098 zimeathirika, kati ya hizo nyumba 678 zimebomoka kabisa, nyumba 877 zimeharibika kiasi na nyumba 543 zimezingirwa na maji.

Mheshimiwa Spika, vilevile tumeona miundombinu ya barabara na madaraja ikisombwa na maji, nguzo za umeme zinadondoka na kwa upande mwingine kimbunga hicho kimeathiri maeneo ya kutolea huduma yakiwemo majengo ya taasisi mbalimbali za umma kama vile shule na vituo vya kutolea huduma za afya. Athari nyingine zinazotokana na kimbunga hicho ni pamoja na kusimama kwa shughuli za kiuchumi kama vile uvuvi, kilimo na biashara. Vilevile, kimbunga hicho kimesababisha uharibifu wa chakula na madhara ya kisaikolojia.

Mheshimiwa Spika, Hatua Zilizochukuliwa na Serikali. Kutokana na athari ya kimbunga hiki katika maeneo mbalimbali hapa nchini Serikali imechukua hatua za haraka, ili kukabiliana na athari zilizojitokeza. Hatua hizo zimezishirikisha Wizara za Kisekta, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya pamoja na wadau wote muhimu. Aidha, kamati za usimamizi wa maafa kwa ngazi mbalimbali zimeshirikishwa kukabiliana na maafa yaliyojitokeza.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Pwani hatua zilizochukuliwa katika Wilaya ya Rufiji na Kibiti ni pamoja na kutoa huduma za afya ya akili, msaada wa kisaikolojia na kijamii kwa waathirika 1,941 (1,501 Kibiti na 440 Rufiji). Kuwaunganisha waathirika 24 (12 wanatoka Rufiji na 12 Kibiti) waliokambini na huduma za matibabu na hivyo, kufanya idadi ya waathirika waliofikiwa na huduma hiyo hadi sasa kufikia 912. Kutoa elimu ya usafi, ulinzi na usalama wa mtoto kwa waathirika 1023.

Mheshimiwa Spika, misaada kwa ajili ya waathirika imeendelea kupokelewa na kutolewa kwa waathirika, ambapo hadi sasa misaada ya chakula na malazi iliyotolewa ni pamoja na unga wa mahindi, unga wa ngano, mchele, mahindi, maharage, mafuta ya kula, sukari, magodoro 2,126, mablanketi, chandarua, shuka, mahema, ndoo na matenki ya maji.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Mafia hatua zilizochukuliwa ni pamoja na wananchi waliokosa makazi baada ya nyumba zao kubomoka na kuzingirwa na maji kuunganishwa na ndugu na majirani, ili kupata hifadhi ya muda. Shirika la Umeme *TANESCO* wamefanya marekebisho ya nguzo zilizoanguka na huduma ya umeme imerejea kwa baadhi ya sehemu. Kukata na kuondoa miti iliyozuia mawasiliano ya barabara na kuendelea kutoa misaada ya kibinadamu kwa waathirika ikiwa ni pamoja na kurejesha hali ya miundombinu.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Lindi hatua zilizochukuliwa Wilayani Kilwa ni pamoja na kuendesha zoezi la utafutaji na uokoaji ambapo jumla ya watu 4,080 wameokolewa katika maeneo mbalimbali, kurejesha hali ya miundombinu ya barabara kuu ya Lindi – Dar es salaam ambapo *TANROADS* wapo eneo la tukio. Mheshimiwa Waziri, Innocent Bashungwa yuko eneo la tukio na kazi inaendelea. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, juhudi za urejeshaji wa Daraja la Somanga – Mtama zinafanyika, ili magari yaliyokwama yaendelee na safari. Kuanzisha makazi ya muda kwenye shule za msingi, ambapo kwa sasa wananchi wapo kwenye vituo vitatu vya makazi ya muda ambavyo ni Shule ya Msingi Mchakama, Shule ya Msingi Mhatwe na Shule ya Msingi Ndende. Mahitaji ya

chakula ikiwemo unga, maharage na mafuta ya kula vimepelekwa kwa waathirika na Kamati ya Usimamizi wa Maafa ya Mkoa na Wilaya ya Kilwa imeendelea kuimarishwa na kuunda kamati ndogo-ndogo kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika uratibu na usimamizi, ili kukabiliana na madhara yaliyojitokeza.

Mheshimiwa Spika, aidha juhudi za kuokoa watu zimefanyika kwa kupeleka *fiber boat* kupitia kikosi cha Jeshi la Zimamomto na Uokoaji, ambapo watu wanaendelea kupokelewa Somanga Mjini, afya zao ni nzuri na wanaendelea kuhudumiwa. Vilevile, kwa upande wa shule zilizozingirwa na maji wanafunzi 92 wa kidato cha sita wamehamishiwa katika kituo cha mitihani kwenye Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, Kilwa.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mtwara. Wananchi waliokosa makazi baada ya nyumba zao kubomoka na kuzingiriwa na maji katika Manispaa ya Mtwara na Wilaya ya Mtwara Vijijini wameendelea kuunganishwa kwa ndugu na jamaa kwa ajili ya hifadhi ya muda.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Morogoro. Hatua zilizochukuliwa katika Halmashauri ya Mji wa Ifakara, Mkoani Morogoro, ili kupunguza athari kwa wananchi ni pamoja na waathirika ambao nyumba zao zimebomoka na kuzingirwa na maji kuhamishiwa katika maeneo ambayo ni salama, hususani majengo ya shule. Vilevile waathirika hawa wameendelea kupatiwa misaada ya kibinadamu kama chakula, vifaa vya malazi pamoja na dawa za kibinadamu. Kufanya tathimini ya uharibifu wa miundombinu ya barabara, madaraja na makaravati kupitia *TANROAD* na *TARURA*. Pia, kutoa elimu ya kukabiliana na magonjwa yanayoambukiza kama vile kipindupindu na kufanya tathimini ya mbegu kwa ajili ya uzalishaji wa mazao ya chakula.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kufanya tathmini sambamba na kurejesha miundombinu muhimu ikiwemo kufanya ukarabati wa miundombinu ya umeme iliyoharibika, ukarabati wa barabara na ujenzi wa madaraja ya muda, kazi ambayo inasimamiwa kikamilifu na sote tunamshuhudia Mheshimiwa Innocent Bashungwa ambaye ni Waziri wa Ujenzi akiendelea

kusimamia matengenezo ya barabara iliyo katika. Kwa kweli, natumia nafasi hii kumpongeza sana yeye pamoja na timu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Hali Halisi ya Sasa. Kwa mujibu wa tathmini iliyofanyika sasa hakuna tishio la Kimbunga Hidaya hapa nchini ambacho athari zake zimetokea sana katika Wilaya za Mafia na Kilwa. Hata hivyo, kama ilivyoripotiwa hapo awali mvua za masika zitaendelea kunyesha katika maeneo ya Kanda ya Ziwa, Nyanda za Juu Kaskazini Mashariki mwa Pwani na Pwani ya Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, Maeneo ya Msisitizo. Kama tulivyosikia na kushuhudia kupitia vyombo vya habari, athari za Kimbunga Hidaya zinahitaji hatua za haraka na ushiriki wa wadau wote katika mfumo wa usimamizi wa maafa. Hivyo basi, ninapoelekea kuhitimisha taarifa yangu, naomba sasa niweke msisitizo kuhusu masuala yafuatayo:-

(i) Katika maelezo niliyoyatoa siku ya Alhamisi, tarehe 25 Aprili, 2024 wakati wa Kipindi cha Maswali ya Papo kwa Papo hapa Bungeni, nilisisitiza kuwa Kamati za Maafa za Wilaya na Mikoa ziendelee kuchukua hatua stahiki ikiwemo kutoa tahadhali kwa wananchi na kuwasaidia kwa wakati pindi maafa yanapojitokeza. Leo nasisitiza tena kuwa, sambamba na kamati hizo Wizara zote za Kisekta zinazohusika na usimamizi wa maafa ziendelee kushirikiana na Kamati hizo za Mikoa na Wilaya, ili kuharakisha suala la kurejesha hali kuwa ya kawaida.

(ii) Wananchi wachukue tahadhari pindi wanapopata taarifa za uwepo wa mabadiliko makubwa ya hali ya hewa. Tuendelee kuisikiliza Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, ni muhimu wananchi wakasikiliza taarifa za hali ya hewa ikiwemo kimbunga na dhoruba za aina yoyote, kufuata na kuchukua tahadhari baada ya taarifa hizo. Aidha, watoe ushirikiano kwa waokoaji pamoja na kuzingatia maelekezo yote kuhusu tahadhari zinazotolewa.

(iii) Narudia kusisitiza kuwa, kila mamlaka iweke kipaumbele cha kutenga fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli za usimamizi wa maafa. Suala la kutenga fedha ni muhimu kwani linaongeza uwezo wa kitaasisi wa kukabiliana na maafa. Waheshimiwa Mawaziri na Wakuu wa Mikoa, simamieni eneo hili la bajeti ya maafa.

(iv) Taasisi zote zinazohusika na masuala ya kuratibu shughuli za uokoaji ziandae utaratibu wa kutoa elimu kwa wananchi pamoja na kuwajengea utayari wa kukabiliana na majanga. Endeleeni na utaratibu wa kutoa mafunzo kwa vijana waliopo katika maeneo husika, ili waweze kushiriki kikamilifu katika kushughulikia dharura mbalimbali zinazojitokeza kwenye maeneo yao.

(v) Wakala wa Barabara *(TANROADS)*, Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini *(TARURA)* na Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* waelekeze nguvu ya matengenezo kwenye maeneo ambayo miundombinu imeharibika, ili kurejesha huduma mapema.

(vi) Nawasihi wananchi wote kuendelea kushirikiana na Serikali kuwasaidia kwa hali na mali wenzetu wanaokumbwa na athari mbalimbali ikiwemo mafuriko na hasa tuendelee kushirikiana na wenzetu waliokumbwa na athari ya kimbunga kwa kuwa, mafanikio katika kurejesha hali yanahitaji mchango wa kila mmoja wetu.

(vii) Kamati za Maafa katika ngazi zote ziendelee kuhakikisha kuwa misaada inayotolewa inawafikia waathirika wa maafa. Simamieni utaratibu uliowekwa, ili kuwawezesha waathirika wote kupata misaada ya kibinadamu pamoja na huduma zote muhimu zilizoletwa kwa ajili yao.

(viii) Timu za uokoaji zihakikishe wananchi waliokwama kutokana na maafa ikiwemo kukatika kwa barabara

wanapata msaada wa haraka kuwawezesha kufika maeneo yaliyo salama.

Mheshimiwa Spika, narudia tena kutoa pole kwa waathirika wote wa Kimbunga Hidaya. Nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge wenzangu na wananchi wote kuwa, Serikali inaendelea kuchukua hatua zote muhimu za kuhakikisha kwamba, inarejesha hali katika kipindi kifupi.

Mheshimiwa Spika, kipekee namshukuru sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa miongozo na maelekezo yake wakati wote na kushughulikia maafa yaliyojitokeza. Hakika Mheshimiwa Rais amekuwa mstari wa mbele katika kuchukua hatua madhubuti za uokoaji, urejeshaji wa miundombinu na kupeleka mahitaji muhimu ya kijamii kwa waathirika wetu.

Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii kutambua na kuwapongeza watendaji wa Serikali, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa na Waheshimiwa Mawaziri kwa jitihada kubwa walizozifanya za kushiriki kikamilifu usiku na mchana katika kusimamia zoezi la uokoaji, kuwahudumia waathirika na kuhakikisha kwamba, miundombinu iliyoharibika inatengemaa. Aidha, narudia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa michango yenu kwa waathirika wetu, viongozi mbalimbali, taasisi za dini na wadau wote ambao wamekuwa wakifanya kazi bega kwa bega na Serikali kwa kutoa misaada kwa waathirika ikiwa ni pamoja na kuwatia moyo. Pia, naipongeza Serikali kwa ujumla wake katika kutoa huduma mbalimbali kwa waathirika.

Mheshimiwa Spika, naendelea kusisitiza kuwa masuala ya maafa ni mtambuka na yanahitaji ushiriki wa kila mmoja wetu. Kwa pamoja yote yanawezekana na siku zote umoja ni nguvu. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu ahsante sana kwa taarifa hiyo uliyoitoa na Waheshimiwa Wabunge muda umekwisha. *(Makofi)*

Tunaendelea, Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI *ndc* – KATIBU WA BUNGE**:

**MASWALI YA KAWAIDA**

**SPIKA:** Maswali ya kawaida Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Norah Waziri Mzeru, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 287

**Serikali Kuajiri Walimu wa Kutosha**

**MHE. NORAH W. MZERU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaajiri Walimu wa kutosha kutokana na ongezeko kubwa la Wanafunzi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Zainab Katimba, majibu.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikifanya jitihada kila mwaka kuajiri Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari. Katika kipindi cha Mwaka 2020/2021 hadi 2022/2023, Serikali iliajiri walimu 29,879 wakiwemo walimu 16,598 wa shule za msingi na walimu 13,281 wa shule za sekondari.

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2023/2024 Serikali inatarajia kuajiri walimu 12,000 ambao watapangiwa vituo vya kazi katika maeneo yenye upungufu, ili kupunguza upungufu uliopo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nora Waziri Mzeru, swali la nyongeza.

**MHE. NORAH W. MZERU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina swali moja la nyongeza. Pamoja na kazi nzuri ya Serikali katika kuendelea kuajiri walimu. Je, Serikali ina

mkakati gani wa kuboresha mazingira ya kazi na motisha kwa walimu, hususan wale wanaoishi na kufanya kazi vijijini? Hili ni muhimu, ili kuzuia walimu wengi wanaokimbilia mijini na kusababisha upungufu wa walimu vijijini. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, hoja ya Mheshimiwa Mbunge ni hoja ya msingi na Serikali inatambua umuhimu wa motisha kwa walimu, hasa wale wanaofanya kazi vijijini, ili waweze kufanya kazi kwa hamasa. Kwa hiyo, mkakati wa Serikali katika eneo hili kwanza ni kujenga nyumba za kuishi kwa walimu, ili kuboresha mazingira yao ya kazi wanapokuwa wanafanya kazi katika maeneo yao ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Serikali imekwishajenga nyumba 253 ambazo zinabeba familia mbili. Kwa hiyo, hii ni sehemu ya mkakati wa kuboresha mazingira ya walimu wanaofanya kazi vijijini.

Mheshimiwa Spika, pili, Serikali inaendelea kuhakikisha kwamba, walimu wanalipwa malimbikizo yao na stahiki zao kwa wakati. Katika Mwaka 2022/2023 Serikali imelipa jumla ya shilingi bilioni 22.73 za madeni ya walimu yasiyokuwa ya mishahara. Kwa hiyo, hii ndiyo mikakati ambayo Serikali inaendelea kufanya, ili kuhakikisha walimu wanaofanya kazi vijijini wanafanya kazi kwa hamasa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, Mbunge wa wa Muhambwe, sasa aulize swali lake.

Na. 288

**Ujenzi wa Miundombinu Shule ya Sekondari Mkugwa, Muhambwe**

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga miundombinu ya Shule ya Sekondari Mkugwa ikiwemo Mabweni, Bwalo na Madarasa, Muhambwe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Shule ya Sekondari Mkugwa ina jumla ya wanafunzi 546, kidato cha tano wapo 377 na kidato cha sita 169. Vyumba vya madarasa vinavyohitajika ni 14 na vyumba vilivyopo ni 14 hivyo, hakuna upungufu. Mabweni yanayohitajika ni nane, yaliyopo ni saba na upungufu ni bweni moja. Juhudi zinafanywa na Halmashauri ya Kibondo kutafuta fedha za kuongeza bweni moja, ili kuondokana na upungufu uliopo.

Mheshimiwa Spika, shule haina bwalo wanafunzi wanatumia jengo lililokuwa la sanaa na maonyesho katika eneo ilipokuwa kambi ya wakimbizi. Jengo hili ni dogo likilinganishwa na wanafunzi 546 waliopo shuleni kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, kuanzia Mwaka 2025/2026 Serikali itaendelea kutenga fedha za kujenga bwalo na miundombinu mingine kila mwaka wa fedha katika shule zisizokuwa na bwalo kwa kuanzia na Shule ya Sekondari ya Mkugwa.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali kwa majibu yake mazuri. Pomoja na majibu hayo, je, Serikali haioni ipo sababu ya kuleta pesa kwa haraka, kwa ajili ya mabinti hawa 500 ambao wanakula hovyo-hovyo bila kuwa na bwalo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Shida iliyopo Mkugwa Sekondari, ipo pia Usagara na Kumgogo. Je, Serikali haioni ipo sababu ya kutenga pesa kwa haraka kwa hizi shule za kidato cha tano na sita, ili kunusuru maisha ya Watoto hawa mashuleni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Majibu.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Tayari nimekwishakutana na Mheshimiwa Mbunge na tumezungumza kwa kina kuhusiana na changamoto hizi za miundombinu katika shule zake alizozitaja. Kwa hiyo, naendelea kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kama tulivyoongea, suala hili linafanyiwa kazi na kupitia mapato ya Halmashauri, Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kujenga bwalo katika Shule hiyo ya Mkugwa Sekondari.

Mheshimiwa Spika, pia, kuhusu swali lake la pili la kujenga miundombinu katika Shule ya Kidato cha tano na sita pia nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutaliwekea kipaumbele suala hili, ili fedha ziweze kutengwa na kujenga miundombinu hii muhimu kwa ajili ya wanafunzi katika shule hizi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Janejelly James Ntate, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Rita Kabati.

Na. 289

**Ajira za Wataalam wa Maabara Katika Shule za Sekondari Nchini**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI K.n.y. MHE. JANEJELLY J. NTATE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaajiri wataalamu wa maabara shule za sekondari, ili kupunguza mzigo kwa walimu wa sayansi kufanya kazi kama wataalamu wa maabara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwepo kwa wataalamu wa maabara shuleni. Wataalamu wa maabara ni wasaidizi muhimu wa walimu wa masomo ya sayansi hasa katika kufundisha kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, kati ya Mwaka 2020/2021 hadi 2022/2023 Serikali iliajiri wataalamu wa maabara 165 ambao walisambazwa katika shule mbalimbali za Serikali kadiri ya mahitaji. Serikali itaendelea kuajiri wataalamu wa maabara kila mara nafasi za kuajiri zinapotolewa kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, kwa sasa walimu wa masomo ya sayansi wamekuwa wakitumika kuandaa vifaa na kemikali kwa ajili ya mazoezi kwa vitendo na mitihani.

Mheshimiwa Spika, natumie fursa hii kuwapongeza walimu wetu wa masomo ya sayansi nchini kwa kazi nzuri wanayoifanya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba niulize maswali madogo mawili. Kwanza, napongeza majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Je, walimu kuandaa vifaa vya maabara hamuoni kama mnapunguza muda wa mwalimu kuandaa masomo yake?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa kuwa Kutunza Maabara ni fani inayotambulika; je, kwa kufanywa na mtu ambaye hana utaalamu hamuwezi kusababisha madhara ya kiutendaji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba nijibu maswali yake yote mawili kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuhusu upungufu wa wataalamu wa maabara lakini Serikali inaendelea na jitihada ya kuhakikisha kwamba inaajiri wataalamu hao wa maabara. Kwa wakati huu Serikali inatumia walimu hawa wa sayansi ili

kuhakikisha kwamba wanafunzi wanaendelea na masomo yao. Sasa sababu ya msingi pia ya kuwatumia walimu wa sayansi ni kwamba walimu wa sayansi na wataalamu wa maabara fani zao zinaingiliana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo katika mafunzo mwalimu wa sayansi anaweza kufanya kazi ile ambayo mtaalamu wa maabara anaifanya. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jitihada hizi ni za makusudi kabisa ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wanaendelea kupata elimu na hasa katika masomo ya sayansi. Serikali inaendelea na utaratibu wa kuajiri hawa wataalamu wa maabara na wakishaajiriwa wale walimu wa sayansi wataendelea na kazi zao nao wataalamu wa maabara wataendelea na kazi zao za kitaalamu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Makamu wa Rais, Muugano na Mazingira Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Lubala Mabula, Mbunge wa Ilemela, sasa aulize swali lake.

Na. 290

**Kukamilisha Ujenzi wa Kingo za Mto Msuka – Ilemela**

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Kingo za Mto Msuka Ilemela utakamilika ili kuepusha vifo vya mara kwa mara pindi mvua zinaponyesha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Kingo za Mto Msuka unaendelea ambapo hadi sasa ujenzi wa daraja na kingo zake

zenye urefu wa takribani meta 500 umekamilika. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Manispaa ya Ilemela kupitia Mradi wa *Tanzania Cities Transforming Infrastructure and Competitiveness* ambao unafadhiliwa na Benki ya Dunia imeomba kiasi cha shilingi bilioni 6.7 kwa ajili ya ujenzi wa barabara na kukamilisha ujenzi wa Kingo za Mto Msuka ambapo ujenzi wake utaendelea baada ya fedha hizo zilizoombwa kupatikana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, swali la nyongeza.

**DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uwezo wa Manispaa ya Ilemela ni mdogo kukabiliana na athari za mafuriko. Je, Serikali haioni sasa ni muda mwafaka wa kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha mto huu ambao ni kilometa 4.9 badala ya kutegemea pesa za wafadhili ambazo hazina uhakika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwenye jibu lake la msingi ameongea kwamba ujenzi unaendelea; je, Mheshimiwa Waziri anatambua kwamba wataalamu wamemdanganya kwa kuwa ujenzi ule umesimama toka 2018, yuko tayari kuambatana na mimi ili akajionee mwenyewe? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA**: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mabula.

Mheshimiwa Spika, kutokana na athari kubwa iliyojitokeza ya maji, maji ambayo yameenda kuharibu miundombinu ya *school,* maji ambayo yameenda kuharibu makazi ya wananchi lakini baadhi ya shughuli nyingine pia zimeathirika. Nimwahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika bajeti ya fedha ijayo tutahakikisha ujenzi wa Kingo za Mto Msuka tunahakikisha tunatenga fedha kwa ajili ya kuupa kipaumbele. Hilo asiwe na wasiwasi nalo na tutahakikisha kwamba tunaenda kuondoa changamoto hiyo.

Mheshimiwa Spika, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba nipo tayari kuambatana na yeye kwenda kuona athari ambayo imejitokeza na kuona namna ambavyo tunaweza tukawasaidia wananchi. Baada ya Bunge hili nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakwenda pamoja kwenda kuona ahari iliyojitokeza, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 291

**Upatikanaji wa Vitabu Shule za Msingi**

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA** aliuliza:-

Je, nini mpango wa Serikali kuwezesha upatikanaji wa vitabu Shule za Msingi ambazo zimeanza mtaala mpya wa Kingereza kuanzia darasa la kwanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Juma Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, katika kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi kwa madarasa yaliyoanza kutumia mtaala ulioboreshwa yaani darasa la awali, darasa la kwanza na darasa la tatu. Serikali imechapa na kusambaza nakala 9,818,251 za mihtasari, vitabu vya kiada na kiongozi cha mwalimu kwa mchanganuo ufuatao:-

(i) Nakala 509,582 za mihtasari na mtaala ulioboreshwa wa elimu ya awali, msingi na sekondari;

(ii) Nakala 8,000,000 za vitabu vya kiada vya kimacho (maandishi ya kawaida) kwa darasa la awali, darasa la kwanza na darasa la tatu kwa shule zinazotumia Kiswahili na Kiingereza kama lugha za kufundishia;

(iii) Nakala 43,785 za vitabu vya maandishi yaliyokuzwa;

(iv) Nakala 6,990 za vitabu vya Breli; na

(v) Nakala 1,183,568 za viongozi vya mwalimu.

Mheshimiwa Spika, vitabu hivi vimesambazwa kwa uwiano kati ya 1:2 - 1:4 (kitabu kimoja kwa wanafunzi wawili mpaka kitabu kimoja kwa wanafunzi wanne), nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea, swali la nyongeza.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali vitabu ambavyo vimesambazwa na ambavyo havijasambazwa ni sawa sawa na asilimia tisa; je, Serikali imejipanga vipi kukamilisha asilimia tisa zilizobaki?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kutokana na Jiografia ya Mkoa wetu wa Tabora na ukubwa na ni ya kwanza kwa ukubwa kwa nchi nzima. Je, Serikali ina mpango mkakati gani wa kuhakikisha mkoa huu unapata kipaumbele katika usambazaji wa vitabu? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jacqueline, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna baadhi ya mikoa ambayo vitabu hivi havijafika kwa 100% na naomba niitaje mikoa hiyo kama ifuatavyo: ni Mkoa wa Iringa, Katavi, Mara, Mbeya, Mtwara, Mwanza, Rukwa, Shinyanga, Simiyu, Songwe pamoja na Tabora aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge. Nimwondoe hofu Mheshimiwa

Mbunge kazi ya upelekaji wa vitabu hivi vilivyosalia asilimia tisa inaendelea na tunakadiria mpaka kufika mwisho wa mwezi huu tutakuwa tumekamilisha usambazaji wa vitabu hivi kwa 100%.

Mheshimiwa Spika, katika eneo lake la pili kuhusiana na suala la Tabora kuipa kipaumbele, nimwondoe wasiwasi kwa vile tunatarajia ndani ya mwezi huu vitabu hivi viwe vimefika katika mikoa yote ukiwemo na Mkoa wa Tabora basi na Mkoa wa Tabora nao tutaupa kipaumbele kuhakikisha kwamba ndani ya Mwezi huu wa Tano vitabu hivi vyote vinafika kwa 100%, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kweli mjitahidi kwa sababu mitihani watoto watafanya inayolingana, wale waliopata kwa muda na wale waliochelewa kupata. Kwa hiyo ni muhimu mlipe kipaumbele hili jambo, kama ulivyosema mwezi huu maana yake mwanzoni mwa Juni tayari watoto wote wawe wamepata vitabu. Ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Madini, Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 292

**Kusaidia Wachimbaji Wadogo wa Madini Ulanga**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia Wachimbaji Wadogo wa Madini Wilaya ya Ulanga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Madini, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, majibu.

**WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuwasaidia wachimbaji wadogo nchini wakiwemo wachimbaji wa madini wa Wilaya ya Ulanga unahusisha mambo yafuatayo:-

(i) Kuwekeza zaidi katika utafiti wa kina kugundua uwepo wa madini katika maeneo mbalimbali ili kuwaongoza vizuri wachimbaji wadogo;

(ii) Utoaji wa Leseni za uchimbaji kwa wachimbaji wadogo;

(iii) Kutoa elimu ya matumzi ya teknolojia sahihi ya uchimbaji ili kuongeza tija;

(iv) Huduma ya uchorongaji kwa gharama nafuu kupitia Shirika la Madini Tanzania *(STAMICO);*

(v) Upatikanaji wa mikopo nafuu kwa wachimbaji; na

(vi) Fursa ya ukodishaji wa mitambo na vifaa chini ya usimamizi wa *STAMICO.*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri. Licha ya majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili madogo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wachimbaji hawa wamefanya kazi hii ya uchimbaji kwa muda mrefu (kwa miaka mingi) kwa shida. Je, haya majibu mazuri uliyoyatoa mpango huu utatekeleza lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; kwa kuwa hawa wachimbaji wadogo wengine tayari wana leseni kwenye vitalu hivyo wanavyochimba kwa shida. Je, kuna mpango gani wa Serikali wa kuwaunganisha na wawekezaji ili waweze kufanya uchimbaji wa ubia? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji tumekwisha kuanza utekelezaji wa mpango huu ambao

nimeuainisha tayari mwaka 2022 timu ya *GST* ilitumwa kwa ajili ya kufanya utafiti. Utafiti ule ulikamilika na ukawasilishwa katika ofisi za wilaya ambayo pia imeainisha maeneo ambayo yana sehemu rafiki ya uchimbaji kwa wachimbaji wadogo. Pia zoezi la utoaji wa leseni linaendelea na kuwaunganisha pia na Benki na Taasisi za fedha kazi hii inaendelea. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge ya kwamba siyo kwamba tunategemea kuanza inaendelea hivi sasa na wachimbaji wa Wilaya ya Ulanga pia watanufaika katika hili.

Mheshimiwa Spika, la pili la kuhusu kuwatafutia wachimbaji hawa wawekezaji; kwa mujibu wa Sheria ya Madini Kifungu cha 8(3) kimeeleza wazi na kimetoa nafasi ya wachimbaji wadogo kupata msaada wa kiufundi pale ambapo wanaweza kuwapata wawekezaji wa kuingia nao makubaliano. Sisi kama Wizara tutaendelea kuwasimamia wachimbaji wadogo ili waweze kupata msaada huu wa kiufundi na waongeze tija katika uzalishaji wao sambamba na hilo pia tumekuwa tukifanya mikutano mbalimbali na safari mbalimbali za nje ya nchi kuwakutanisha na wawekezaji wakubwa ambao wanaweza kuingia nao ubia kwa ajili ya kuongeza tija kwenye uzalishaji wao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sebastian Kapufi, swali la nyongeza.

**MHE. SABASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Spika, nini kauli ya Serikali katika kutatua mgogoro wa muda mrefu wa Kikundi cha Kagera dhidi ya Serikali ya Kijiji cha Dirifu katika Manispaa ya Mpanda?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kama unayo majibu umjibu Mheshimiwa Mbunge, kama unaujua huo mgogoro lakini kama huufahamu Mbunge anaruhusiwa kuleta kama swali la msingi kwa sababu ni mgogoro mahususi.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, mgogoro huo naufahamu na nataka nimwahidi Mheshimiwa Mbunge nitakwenda mwenyewe kwa ajili ya utatuzi wa mgogoro huo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Vedastus Manyinyi swali la nyongeza.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Shirika la *STAMICO* ndio walezi wa wachimbaji wadogo huku, nafikiri shirika lina jukumu kubwa la kufanya biashara. Ni lini sasa hawa wachimbaji wadogo watakuwa na kurugenzi yao inayowasimamia kuhakikisha kwamba wanaweza kufanya shughuli zao vizuri? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge chini ya Ofisi ya Kamishna kipo kitengo maalum kwa ajili ya wachimbaji wadogo ambao wanasimamia na kuwashughulikia wachimbaji wadogo. Kazi ambayo wanaifanya *STAMICO* ni kazi ya ulezi ambayo pia imesaidia sana hasa kuboresha uchimbaji mdogo hapa nchini Tanzania. Kwa hiyo vyote viwili hivi vinafanya kazi kwa pamoja na ndiyo maana tunaona wachimbaji wadogo wameendelea kuwa na mchango mkubwa katika uchumi wa Taifa letu la Tanzania kupitia sekta ya madini kwa sababu ya ushirikiano wa maeneo haya mawili ya Ofisi ya Kamishna pamoja na *STAMICO* kama mlezi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Salim Alaudin Hasham, Mbunge wa Ulanga, sasa aulize swali lake.

Na. 293

**Ujenzi wa Barabara ya Ifakara – Malinyi - Mahenge Hadi Lupiro**

**MHE. SALIM A. HASHAM** aliuliza:-

Je, lini Serikai itajenga Barabara ya Ifakara – Malinyi – Namatumbo – Mahenge Mjini hadi Lupiro kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshasaini mkataba wa ujenzi wa Barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupiro – Malinyi – Londo – Lumecha kwa utaratibu wa *EPC + F*. Kwa kawaida, ujenzi wa barabara kwa utaratibu wa *EPC + F* unahusisha kufanya usanifu wa barabara kabla ya kuanza ujenzi. Kwa sasa mkandarasi ameanza na anaendelea na usanifu wa kina. Aidha, Serikali na wakandarasi wanaendelea na taratibu za kupata fedha kwa ajili ya malipo ya awali kwa miradi yote ya *EPC + F* ikiwemo barabara hii, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salim Alaudin Hasham, swali la nyongeza.

**MHE. SALIM A. HASHAM:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza waswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa sababu Mkoa wa Morogoro ni Mkoa wa Kimkakati, je, Serikali haioniumuhimu wa kuharakisha ujenzi wa Barabara hizo ili kuondoa adha inayowakumba wananchi wa Jimbo la Ulanga, Mlimba, Kilombero pamoja na Malinyi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kutokana na adha kubwa wanayoipata Wana-Ulanga na ni kilio cha miaka mingi sana cha Wana-Ulanga kama Serikali inaendelea kutafuta bajeti kubwa ya kutatua kero ya kuunganisha mikoa. Je, Serikali haioni umuhimu hata wa kuunganisha hizi wilaya mbili za Malinyi na Ulanga kwa sababu adha yake imekuwa ni kilio cha miaka mingi sana? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunajua Mkoa wa Morogoro ni kati ya mikoa yenye uzalishaji mkubwa sana wa chakula lakini pia na shughuli mbalimbali ikiwemo madini katika wilaya yake. Ndiyo maana Serikali imekuja na utaratibu wa kutaka kuijenga hii

Barabara yote kuanzia Ifakara - Malinyi lakini pia Lupiro kwenda Mahenge Mjini na ndiyo maana katika kuiunganisha hii Wilaya ya Ulanga na Mahenge tunaunganisha pale Lupiro kwenda Mahenge na kuiunganisha kutoka Lupiro kwenda Malinyi. Dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba hii barabara inajengwa kwa kiwango cha lami.

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mbunge wa Msalala, sasa aulize swali lake.

Na. 294

**Ujenzi wa Barabara ya Solwa – Kahama**

**MHE. IDDI K. IDDI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Solwa hadi Kahama kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami kwa Barabara ya Kahama – Solwa yenye urefu wa kilometa 79.96 unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Hadi sasa jumla ya kilometa 6.1 zimekamilika kujengwa. Aidha, kazi za ujenzi wa jumla ya kilometa 1.2 zinaendelea katika Miji ya Ngaya (meta 400), Bulige (meta 400) na Solwa (meta 400) na umefikia 68%. Kwa sehemu iliyobaki, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuendelea na kazi ya ujenzi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, swali la nyongeza.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza la nyongeza ni lini sasa Serikali itaanza rasmi ukarabati wa Barabara inayotoka Ntobo – Busangi - Ngaya mpaka Didiya kwa kuwa tayari barabara hii imeshapandishwa hadhi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili nilitaka kufahamu ni lini sasa Serikali itamaliza mapema mchakato wa upembuzi yakinifu Barabara inayotoka Busisi - Nyang'hwale - Chela mpaka Busangi mpaka Kahama? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya kwanza aliyoitaja tayari tumeshasaini na sasa hivi tunachosubiri tu ni kumkabidhi mkandarasi (*site possession)* ili aweze kuanza ujenzi wa hiyo Barabara. Kuhusu baarabara hizo alizozisema ya kutoka Busisi - Ngoma hadi Kharumwa na Kharumwa hadi Nyankumbu na Kharumwa - Nyangoko hadi Kahama tuko tunaendelea na usanifu. Pia, Barabara ya Kharumwa - Nyankumbu na Kharumwa – Nyangoko hadi Kahama tuko kwenye hatua za mwisho za kukamilisha manunuzi ya mhandisi mshauri, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Kilimo Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa.

Na. 295

**Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji Tarafa ya Igominyi**

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA K.n.y. MHE. DEODATUS P. MWANYIKA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga miundombinu ya umwagiliaji kwenye maeneo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tarafa ya Igominyi – Njombe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeanzisha mkakati wa muda mrefu wa kuwawezesha wakulima wadogo wa chai katika Mkoa wa Njombe kwa kuwawekea miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba yao. Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji ndani ya Tarafa ya Igominyi yenye hekta 1,021.52 itanufaisha zaidi ya wakulima 934 kutoka katika Vijiji vya Iboya, Ihanga, Itipula, Mgala, Igoma, Iwungilo, Ngalanga, Uliwa, Kifanya, Lilombwi, Lwangu, Luponde na Utengule.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeanza utekelezaji kwa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika Mashamba ya Igoma, Lwangu, Iwungilo, Kifanya na *IRECO* ambapo ujenzi wa miundombinu yake utaanza katika mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zitaendelea katika mashamba yaliyobaki kwa ajili ya kupata makadirio ya gharama za uwekaji wa miundombinu ya umwagiliaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, swali la nyongeza.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, ni lini Serikali itaboresha skimu ya umwagiliaji Nyamalulu Jimboni Busanda?

Swali la pili, ni upi mkakati wa Serikali kutumia Ziwa Victoria kuhakikisha kwamba skimu za umwagiliaji zinajengwa na tunaweza kuboresha uzalishaji wa mazao ya chakula?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kuhusu maboresho katika skimu ya Nyamalulu katika Jimbo la Busanda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hili

lipo katika mpango na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, mkakati kuhusu Ziwa Victoria tunaendelea nao kwa sababu tuna mkakati wa pamoja kati ya Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maji pamoja na Mifugo na Uvuvi ili kuhakikisha maji yale tutakayoyatumia yaweze kuwanufaisha wananchi katika maeneo hayo yote matatu ambayo nimeyataja. Kwa hiyo, lipo katika mipango ya Serikali na litatekelezeka, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Maji Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 296

**Kusambaza Maji ya Ziwa Tanganyika Mkoa wa Rukwa**

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kukamilisha mradi wa maji kutoka Ziwa Tanganyika na kusambaza katika Mkoa wa Rukwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum Rukwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha huduma ya maji safi na usafi wa mazingira inaimarika katika Mkoa wa Rukwa, Serikali imekamilisha upembuzi yakinifu wa awali wa kutumia chanzo cha Ziwa Tanganyika ambacho ni cha uhakika. Hadi sasa, taratibu za manunuzi za kumpata mtaalam mshauri wa usanifu wa kina wa kutoa maji Ziwa Tanganyika na kuyapeleka katika Mikoa ya

Rukwa, Katavi mpaka Kigoma zimeanza na zitakamilika katika mwaka 2024/2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa Wilaya ya Nkasi ina changamoto kubwa ya maji. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kupeleka mpango wa dharura ikiwemo kuchimba visima na mabwawa?

Swali la pili, ni lini mradi wa Isale utakamilika? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bupe nelson Mwakang'ata, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuwapigania wananchi wa Mkoa wa Rukwa katika miradi yetu ya maji na hakika kweli tunaendelea kushirikiana nae kuhakikisha kwamba tunatatua changamoto za maji.

Mheshimiwa Spika, Serikali tunao mpango wa muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu lakini mradi unaoendelea ni mpango wa muda mrefu. Ni kweli bado kuna changamoto ambapo Serikali tumeamua kuchimba visima vitatu ambavyo vinaenda kutatua changamoto ya maji na kuna visima vingine vitatu tunaenda kuvichimba katika mwaka huu wa fedha lakini visima hivyo vitakamilika katika mwaka wa fedha ujao. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali kuhakikisha kwamba wananchi wake wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, vilevile swali la pili, mradi wa Isale mpaka sasa umefikia asilimia 75 ya utekelezaji wake, mradi huo

unagharimu takribani shilingi milioni 643, mpaka sasa Serikali imeshamlipa mkandarasi takribani shilingi milioni 262. Kwa hiyo, tunaamini kabisa kwamba mkandarasi ataendelea kwa kasi ile ile ili akamilishe mradi huu na tunaamini kwamba kwa sababu mkandarasi mwenyewe anaitwa *Vibe International* tunaamini kwamba atakuwa *site* ili akamilishe miradi hii kwa wakati na wananchi wapate maji safi na salama, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Minza Mjika, swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona.

Je, ni lini Serikali itamaliza kero ya maji katika Kata ya Malili, Ngasamo na Shigala Wilayani Busega? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunao mradi mkubwa wa Ziwa Victoria ambapo Serikali tayari imeshaingia mkataba na mkandarasi, tayari yuko *site*. Mradi huo utapita katika Wilaya ya Busega, Bariadi mpaka Itilima na kwa awamu ya pili utapita Maswa na Meatu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo tunaendelea na miradi midogo midogo, tunavyo visima ambavyo vinaendelea kuchimbwa katika Wilaya ya Busega na Wilaya nyingine lakini nimuombe Mheshimiwa Mbunge tuendelee kushirikiana kwani miradi hiyo itakapokamilika basi tukaendelee kuisemea Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwani utekelezaji wake ni kwa mujibu wa Ilani ya uchaguzi, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Amandus Chinguile, swali la nyongeza.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia Mto

Ruvuma kumaliza kabisa tatizo la maji katika Mikoa ya Ruvuma, Mtwara na Lindi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Nachingwea kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa mradi huu ni mradi wa kimkakati kwa Mikoa ya Ruvuma, Mtwara na Lindi, kwa kutambua umuhimu huo na Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakifuatilia sana akiwemo Mheshimiwa Mbunge wa Nachingwea, Serikali inaendelea na mapitio ya usanifu wa mradi huu wa kutoa maji kutoka Mto Ruvuma ili yafike mpaka Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa Serikali imeshafikia katika hatua nzuri na tuombe tu kwamba pindi tutakapoenda katika hatua ya utekelezaji Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kushirikiana kuhakikisha kwamba waweze kutoa ushauri, michango na maoni yao tutayapokea na kuyaingiza katika utekelezaji halisi, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Serikali inaweza kuharakisha kutoa kibali cha ujenzi wa uboreshaji wa maji Mjini Namtumbo, kwani ipo katika Bajeti hii ya 2023/2024?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimwa Vita Kawawa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jana nimekutana na Mheshimiwa Vita Kawawa na akawasilisha changamoto hii. Nimhakikishie kwamba suala hili nililifikisha kwenye mamlaka husika na tayari kibali kama ambavyo Mheshimiwa Waziri wetu anasema, Wizara ya Maji lengo letu ni kufikisha huduma ya maji safi na salama, hatutakuwa kikwazo. Kwa hiyo, kibali hicho kitatoka mara moja na mradi huo

utaanza mara moja bila kuwa na kikwazo chochote, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Naleta tangzo nililonalo hapa mbele ambalo ni tangazo la wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Tutaanza na wageni waliopo jukwaa la Spika. Kwanza, tutaanza na wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Maji Mheshimniwa Jumaa Aweso. Yupo Mhandisi Mwajuma Waziri ambaye ni Katibu Mkuu, ahsante sana. *(Makofi)*

Tunae Ndugu Agnes Kisaka Meena - Naibu Katibu Mkuu, ahsante sana. *(Makofi)*

Tunae Mheshimiwa Halima Omary Dendegu - Mkuu wa Mkoa wa Singida, karibu sana. *(Makofi)*

Tunae Ndugu Fadhili Maganya - Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi CCM – Taifa, ahsante sana. *(Makofi)*

Tunae Ndugu Joshua Mirumbe - Naibu Katibu Mkuu Jumuiya ya Wazazi Taifa. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Riziki Kingwande - Naibu Katibu Mkuu Umoja wa Wanawake Tanzania wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Tunae Ndugu ustadhi Rajabu Abdallah - Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Tanga, karibu sana. *(Makofi)*

Tunae Dkt. James Andilile Mkurugenzi Mkuu – *EWURA*, karibu sana. Haya ahsanteni sana. *(Makofi)*

Tunae Mhandisi Mbogo Futakamba Mwenyekiti wa Bodi ya Maji ya Kitaifa, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Mhandisi Abdallah Mkufunzi - Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Taifa wa Maji. *(Makofi)*

Yupo Mhandisi Ngwisa Mpembe - Mwenyekiti Bodi ya Bonde la Ziwa Nyasa. *(Makofi)*

Yupo Mhandisi Herbert Kashilila - Mwenyekiti wa Bodi ya Bonde la Ziwa Rukwa. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Ruth Koya - Mwenyekiti wa Bodi ya *RUWASA*. *(Makofi)*

Yupo *SSP* Issakwisa Mwasajobe - Mwenyekiti Bodi ya Maji *DUWASA*. *(Makofi)*

Yupo ndugu Laston Msongole - Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Maji *DAWASA*. *(Makofi)*

Tunae Ndugu Victoria Elangwa - Mwenyekiti wa Bodi ya *EWURA*. *(Makofi)*

Ndugu Abdallah Mahmoud Abdallah - Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Pangani. *(Makofi)*

Mhandisi Ngosi Mwihava - Mwenyekiti wa Kamati ya Maji ya Bodi ya *EWURA*. *(Makofi)*

Ndugu Clement Kizegalo - Mkurugenzi Mkuu *RUWASA*. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Rajab Aweso, Ndugu Omary Aweso na Ndugu Hussein Aweso hawa ni Baba Mdogo na Baba Mkubwa wa Mheshimiwa Aweso. Sasa hapa nimeshindwa kujua yupi ndiyo mdogo na yupi ndiyo mkubwa lakini tunawakaribisha sana Bungeni. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Fatuma Omary Masanga -Mama Mzazi wa Mheshimiwa Aweso, karibu sana, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Kauthar Tarimo Mke wa Mheshimiwa Waziri Aweso, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Mheshimiwa Zainab Abdallah Mke wa Mheshimiwa Aweso, haya ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Ndugu Mtanga Aweso ambaye ni shangazi yake. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Khadija Aweso Dada yake. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Mariam Jumaa Aweso mtoto wake. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Aweso Jumaa Aweso mtoto wake, haya ahsante sana. *(Makofi*

Yupo Ndugu Salim Aweso mtoto wake, haya ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wenu, yupo mgeni wa Mheshimiwa Abubakari Asenga ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Ifakara Jimbo la Kilombero, Mkoa wa Morogoro, karibu sana. *(Makofi)*

Tunae mgeni wa Mheshimiwa Stanslaus Mabula ambaye ni rafiki yake kutoka Musoma. *(Makofi)*

Tunae mgeni wa Mheshimiwa Michael Mwakamo ambae ni rafiki yake kutoka Kibaha. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa kepteni Abbas Ali Mwinyi ambao ni Wanachama wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Mjini Magharibi, Zanzibar.

Wapo wageni saba wa Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally Wajumbe wa Kamati Tendaji ya Mkoa wa Tabora, wakiongozwa na Katibu wa Umoja wa Wanawake Tanzania wa Chama cha Mapinduzi, Mkoa wa Tabora, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 37 wa Mheshimiwa Noah Saputu ambao ni wanafunzi 34 na wakufunzi watatu kutoka Chuo cha Uandishi wa Habari na Mahusiano ya Kimataifa *(The Arusha East Training Institute)* kutoka Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wapo wanafunzi 92 na walimu 8 wa Shule ya Awali na Msingi ya Peter Vigne kutoka Mkoa wa Morogoro, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi wanne kutoka Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hao ndiyo wageni tulionao Bungeni asubuhi hii. *(Makofi)*

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, Hoja ya Dharura.

**SPIKA:** Mheshimiwa Timotheo Mnzava hoja ya dharura.

**JAMBO LA DHARURA**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, ninasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 54 kwa sababu ya kuzingatia muda naomba nisiisome. Nasimama kuomba ridhaa na nafasi yako ili niweze kutoa hoja ya dharura kwamba Bunge lako Tukufu liahirishe kwa muda shughuli zake kama zilivyoorodheshwa kwenye Shughuli za Bunge leo ili kujadili jambo mahsusi.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa kata zaidi ya tisa za Tarafa ya Bungu Wilaya ya Korogwe ni wananchi wanaoishi kwa kutegemea shughuli za kilimo na zao lao kubwa la kilimo ni zao la chai. Wananchi hawa wanachukua chai yao mashambani wanauza kwenye viwanda viwili vya *Ambangulu Estate* na *Dindira Tea Estate* vilivyopo kule Korogwe. Kwa zaidi ya miezi miwili sasa viwanda vile vimefungwa na mwekezaji huyu amesimamisha

kupokea chai inayotoka kwa wananchi, kwa sababu hiyo wananchi hawana sehemu ya kuuza chai yao.

Mheshimiwa Spika, maisha ya wananchi wetu ni magumu sana kwa sababu zao hili ndiyo kitu pekee wanachokitegemea kwa ajili ya maisha yao ya kila siku. Natambua Wizara ya Kilimo ilishaunda timu ikaituma kule, wakakuta hali ya mashamba ya mwekezaji ni mbaya na hali ya viwanda ni mbaya. Mashamba ya mwekezaji kwa zaidi ya miaka 15 hayajapata mbolea hata kilo moja na mwekezaji huyu amefunga viwanda kuanzia Mbeya mpaka Mkoa wa Tanga, hivi tunavyozungumza hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Wizara kuunda timu hakuna hatua yoyote ya haraka na ya dharura iliyochukuliwa mpaka sasa. Wananchi wanateseka, hawana maeneo ya kupeleka chai yao, hawapati fedha na maisha yamekuwa ni magumu sana.

Mheshimiwa Spika, naomba ridhaa yako ili uniruhusu niweze kutoa hoja, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, huyu ndiye mwekezaji wa viwanda vya Lupembe pia au siyo huyu?

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, hapana ila ana mashamba mengine kule Rungwe. *(Makofi)*

**SPIKA:** Huyo ni mwekezaji aliyeko Rungwe?

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, mwekezaji huyu ana mashamba na viwanda kwenye maeneo mbalimbali ya nchi yetu ikiwemo Korogwe lakini pia na maeneo ya kule Rungwe Mkoa wa Mbeya. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ili niweze kujua hoja hii kama ni dharura au siyo, Waziri wa Kilimo yuko hapa, hali iko namna gani, kama kuna jambo ambalo mnalifanya kama Serikali ama imeshindikana Serikalini ili tujadili hapa ndani ili tuwashauri nini cha kufanya, Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa alichokisema Mheshimiwa Mnzava. Hoja ya Mheshimiwa Mnzava ni sahihi. Kampuni mbili ambazo zilibinafsishiwa mashamba, Kampuni ya *Mohammed Enterprises* na Kampuni ya *DL Group*. *DL Group* ndiye huyu uliyemtaja wa maeneo ya Lupembe na *Mohammed Enterprises* ni maeneo ya Rungwe na Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka tu kumuomba Mheshimiwa Mnzava na Waheshimiwa Wabunge wote, najua kazi wanayoifanya kufuatilia jambo hili. Kama Wizara tumemuandikia barua baada ya kupeleka *technical team* kufanya *assessment* juu ya *whether* alipobinafsishiwa alifanya *investment* yoyote mpaka sasa na anaendelea kuwa na *commitment* ya kufanya kazi ile? Tulimuandikia barua ya kutokufunga viwanda kwa sababu kuna mashamba yake na mashamba ya wakulima wadogo lakini amefunga vile viwanda. Ile ni mali yake lakini ilikuwa ni mali ya umma aliyouziwa kwa makubaliano maalum na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama Wizara naomba mtupe nafasi kama Serikali. Sasa hivi timu yetu ya Wizara itamuita, kama hana nia ya kuyaendeleza mashamba haya, tutayachukua kama Serikali na tutayafanyia *valuation* kutokana na *status* iliyoko sasa kwa sababu hayajafanyiwa *development for a very long time*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeshakutana na *DL Group* wiki iliyopita, yeye ameshakubali, tumeanza maongezi kwa ajili ya viwanda viwili vilivyoko Lupembe na Mohammed tutamuita tuweze kuchukua hatua. Niwahakikishie tu wakulima wa Tanga na Rungwe kwamba Serikali inaendelea kulifanyia kazi jambo hili na tutalichukulia hatua. Tutarudisha Sekta ya Chai kwenye uzalishaji kama ilivyokuwa inatarajiwa huko mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, changamoto moja tu ya zao la chai ni kwamba inapotakiwa kuvunwa inabidi ivunwe, la sivyo inakomaa kule kwenye mashamba. Sasa kama imechukua miezi miwili mnatarajia kuchukua muda gani mpaka mfike hayo

maamuzi ili wale wakulima wasije wakaanza kukata ile michai? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, siwezi kusema *exactly* ndani ya muda gani lakini ninaamini kwamba, kwa kuwa tayari tumeshapata idhini kutoka kwa Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kuya-*offtake* haya mashamba; kama yeye hataweza kuendeleza kama inavyotakiwa na kuheshimu makubaliano yaliyokuwepo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba mtupe muda angalau *before* Bunge hili halijaisha, tutaleta taarifa ndani ya Bunge lako juu ya *status* tuliyofikia na *Mohammed Enterprises* na wenzie. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Timotheo Mnzava, akileta hoja ambayo inawahusu wananchi wa jimbo lake lakini ameeleza kwamba changamoto hiyo wanayoipitia, wanaipitia na wakulima wa sehemu nyingine. Hapa mmenisikia nikitaja Lupembe kwa sababu nimeshamsikia Mheshimiwa Mbunge wa Lupembe akizungumzia jambo hili mara kadhaa na kwa sababu ya changamoto ambayo ipo kwenye zao la chai. Kwa sababu siyo zao ambalo linaweza kusubiri kwamba yale mazao yake yaendelee kuwepo shambani wakati tukiendelea kusubiri. Wale wananchi lazima waendelee kuvuna. Ili chai iendelee kuota, lazima uvune na usipovuna inakomaa na ikikomaa hauwezi tena kuja kuifanyia kazi yoyote.

Mheshimiwa Waziri, kwa mazingira hayo kwa sababu si viwanda vyote vya chai nchini ambavyo vimefungwa, au vimefungwa vyote? Si vipo ambavyo vinafanya kazi? Mheshimiwa Waziri simama tu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba viwanda vinavyofanya kazi ni vile ambavyo viko kwenye *catchment area* ambayo chai ikivunwa ndani ya ule muda wa kusafirisha inaweza kuendelea kuwa na ubora. Ukiangalia Tanga, ukiacha kiwanda kilichoko Lushoto ambacho kinahudumia wakulima wa *catchment* ya Lushoto, hawa walioko Korogwe ni lazima wahudumiwe na hivyo viwanda viwili vilivyoko katika hilo eneo.

**SPIKA:** Sawa, sasa Mheshimiwa Waziri kwa hali hii ambayo hatuna hakika na muda, yaani kwamba itachukua muda gani ili wakulima waendelee kuvuna chai yao ili zao la chai liendelee kuwa zao. Wote tunafahamu kama nilivyosema, changamoto ya chai huwa ina kipindi cha kuvunwa. Serikali kwa sasa itazame namna kwa sababu wao wamefunga kiwanda lakini kiko pale labda kama mashine zimeharibika. Kama mashine hazijaharibika wasindike kwa ile ngazi ya mwanzo wakati mnaendelea na haya mazungumzo. Kwa sababu mtu kama ameweka kufuli maana yake wakulima wanaendelea, chai iko shambani na hawana cha kufanya na wanapata hasara. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mtazame namna hawa wamiliki wa viwanda wafungue ili isindikwe wakati mnaendelea na haya mengine kwa ngazi ile ya mwanzo kabisa. Mkisema mtaiacha tu itaenda miezi tutarudi kule nyuma kuna maeneo ambayo miti ya chai ilikatwa wakapanda mazao mengine, wakarejea huku baada ya kuona uwekezaji uliofanywa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri kwa kweli jitahidini katika kipindi hiki, hizo kampuni kwa sababu mnasema mna mazungumzo nao; ya kwanza kabisa pa kuanzia wafungue ili wananchi wapate pa kupeleka chai yao ili isiharibikie shamabani kwa sababu itakuwa ni hasara kubwa sana kwao. Maana hiyo ardhi huwezi kupanda kitu kingine ukishapanda chai. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nashindwa kuitoa hoja hii kwamba ni ya dharura kwa sababu tayari Serikali inaendelea kulifanyia kazi jambo hili. Ni dhahiri…; majibu ni yale yale, sasa ungekuwa umeniambia mwanzo maana hapa nimeshasema, nashindwa kuitoa hoja kwa hiyo siwezi kumeza maneno yangu mimi mwenyewe nimeshayasema. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa kuwa Serikali inalifanyia kazi jambo hili, tuipe muda kama Mheshimiwa Waziri alivyoomba ila tunachoiambia sasa Serikali ni kwamba; hawa watu waruhusu viwanda vyao visindike ile chai ya wakulima ili wasipate hasara, wakati nyinyi sasa mnaendelea kuzungumza kama Serikali ivichukue ama hapana. *(Makofi)*

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, hoja ya dharura.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo majina ni mengi sana ya Wabunge ambao mnataka kuchangia hoja ya maji. Waheshimiwa Wabunge, huyu atakuwa Mbunge wa mwisho kusimama. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi.

**JAMBO LA DHARURA**

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nimesimama kwa Kanuni ya 54 kujadili jambo la dharura lenye maslahi ya umma. Kama unavyofahamu wakati huu sasa ni wakati wa mavuno kwenye maeneo yetu. Kwenye Jimbo la Msalala kuna tabia ambayo imezuka ya maafisa mapato kuwafuata wakulima kwenye maeneo yao ambayo wanavuna mpunga, kwenye mashamba yao na kuwalazimisha kulipa ushuru wa mazao wakiwa wanavuna mazao kutoa shambani kwenda nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo wale ambao wanawakuta barabarani, wanawakamata na wanawapeleka kwenye halmashauri. Jambo la kusikitisha zaidi, ni kwamba wanaanza kuwafanyia matendo ya unyanyasaji, kuwazungusha, kuwaviringisha kwenye *blocks* na kuwanyanyasa pamoja na kuwapa mateso makali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hoja hii, naomba nitoe hoja ya dharura Bunge lako liweze kujadili jambo ambalo linaendelea kwa maslahi ya umma ambayo mpaka sasa wananchi wa Jimbo la Msalala wanahofia kutoa mazao yao shambani kwa sababu ya unyanyasaji na kukamatwa kwao kwenye maeneo hayo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hao ni watu wa halmashauri au ni watu wa Mamlaka ya Mapato?

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ni watu wa halmashauri.

**SPIKA:** Sasa halmashauri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, suala la Mheshimiwa Mbunge, kama alivyolileta hapa, tuseme sisi Ofisi ya Rais TAMISEMI tumelichukua, tutalifanyia kazi na tutawasiliana naye ili tuone kama hali hiyo kweli inatokea tutajua nini cha kufanya lakini kama alivyosema, sisi Ofisi ya Rais, tumelipokea. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jana Mheshimiwa Tabasam aliniandikia hapa hoja kama hiyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri huenda lipo kweli kwa sababu yule ni Mbunge wa Sengerema na huyu ni Mbunge wa Msalala.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika na Mbarali.

**SPIKA:** Mbarali pia? Haya, Waheshimiwa Wabunge kwa sababu bado tupo hapa Bungeni na hizi changamoto zimeelezwa na Wabunge na wengine mnaeleza bila kuwasha visemeo kwa sababu sijawapa nafasi lakini nimewasikia; kwamba ni changamoto ambayo imetokea maeneo mengi. Watu wanaenda kudai ushuru wakati mkulima anatoa shambani na kupeleka nyumbani. Katika mazingira hayo kwa kweli hayuko kwenye biashara, sasa hiyo pesa ya kulipa ushuru atakuwa ameitoa wapi au siku hizi unachukuliwa ushuru wa mazao? *(Makofi/Kicheko)*

Kwa sababu kama ametoka kuvuna anapeleka nyumbani au anapeleka kwenye ghala sasa ameuza saa ngapi ili alipe huo ushuru? Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, amesema hapa Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba wamelichukua kwa hivyo sisi tutasikia baada ya kulichukua mnawaelekeza nini hao watu wa halmashauri. Mnawaelekeza nini Wakurugenzi kuhusu hoja hii?

Kwa sababu msipotoa hayo maelekezo hao wananchi wataendelea kupata hiyo changamoto na kwa kweli labda kama siku hizi ushuru umekuwa ni wa gunia moja, magunia mawili kwa hiyo wanabeba kwenye malori. Pungufu ya hapo, kutoa

shambani kupeleka nyumbani siyo biashara pale. Kwa hiyo, anasubiriwa afanye biashara ili ndiyo alipe ushuru. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tusubiri Serikali itasema nini katika siku hizi chache baada ya kulifuatilia jambo hili. Ikiwa litaendelea baada pengine ya wiki ijayo tutatazama nini cha kufanya. Ahsante sana. *(Makofi)*

Nilikuwa nimesema huyo atakuwa ni Mheshimiwa Mbunge wa mwisho kusimama kwa leo kwa sababu hoja ya maji ninayo majina ya Wabunge wengi sana hapa. Kwa hiyo, inabidi tuokoe muda au tuukomboe wakati.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso aje awasilishe Hoja ya Wizara yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, asiyeshukuru watu hata Mungu hawezi kumshukuru. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Baada ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, Mbunge, kuwasilisha taarifa ya Kamati iliyochambua utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Maji ya mwaka 2023/2024 na kupokelewa na Bunge lako Tukufu, ninaomba sasa kutoa hoja kwamba, Bunge lako likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2024/2025. Naomba hotuba yangu yote iingie kwenye Kumbukumbu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia uhai, afya njema na kutuwezesha kukutana siku ya leo. Aidha, kwa namna ya kipekee nitumie fursa hii kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi imara na wa vitendo aliouonyesha katika kipindi cha miaka mitatu ya Serikali yake ya Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ametuonyesha kwa vitendo sisi wasaidizi wake maana halisi ya uongozi unaojali mahitaji ya wananchi na maslahi mapana ya nchi kupitia falsafa aliyoiasisi ya *4R* inayomaanisha; Maridhiano, Ustahimilivu, Mageuzi na Ujenzi wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi watu wa Sekta ya Maji ni mashahidi na wanufaika wakubwa wa uongozi wake mahiri na namna pekee ya kumshukuru Mheshimiwa Rais ni kuendelea kumuombea kwa Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema na maisha marefu na kufanya kazi kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuendelea kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini…

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Wabunge punguzeni sauti kidogo. Mnazungumza mambo ya msingi sana lakini mko hapa ndani. Kama ni lazima kuzungumza kwa sauti sana unatoka nje halafu unarejea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuendelea kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini katika nafasi hii ya Waziri wa Maji. Heshima na imani aliyonipa ni kubwa sana na kupitia Bunge lako Tukufu niendelee kumuahidi kwamba nitaendelea kuitumikia nafasi hii kwa uadilifu, uaminifu na uwezo alionijalia Mwenyezi Mungu katika kuhakikisha Serikali inatimiza malengo ya kuwapatia wananchi vijijini na mijini huduma ya uhakika na toshelevu ya maji safi na salama. Pia, kuhakikisha maji

ya kutosha yanapatikana kwa ajili ya shughuli nyingine za kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, kwa kazi kubwa anayoifanya katika kutimiza azma ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuijenga Tanzania kuwa nchi yenye maendeleo na uchumi shindani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, napenda kumshukuru Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge, kwa uongozi wake mahiri, na kwa namna anavyosimamia kikamilifu uwajibikaji wa viongozi na watumishi Serikalini kwa lengo la kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, naomba kumshukuru Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuwatumikia wananchi katika nafasi hizo zote mbili muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wenu mahiri, kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu. Aidha, natoa pongezi nyingi kwako wewe Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Rais wa Muungano wa Mabunge Duniani *(IPU)* na kuweka historia ya kuwa mwanamke wa kwanza kutoka Afrika kuchaguliwa kutumikia nafasi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuchaguliwa kwako kwenye nafasi hiyo ya juu, yenye hadhi na ushawishi mkubwa duniani ni uthibitisho wa umahiri na weledi wako katika kutekeleza majukumu yako na kwa hakika umeijengea heshima kubwa nchi yetu. Mimi nikutakie kila la heri na Mwenyezi Mungu akufanyie wepesi katika majukumu yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza na kumshukuru Naibu Spika, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya. Pia, nitumie nafasi hii kuwashukuru Wenyeviti wote akiwemo, Mheshimiwa Najma

Murtaza Giga, Mbunge, Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge na Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge, kwa kazi nzuri wanazofanya kwenye Bunge letu Tukufu. Pia, tunatoa pongezi kubwa kwa Wabunge wote kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuwatumikia wananchi na kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu kwenye majimbo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kwa ushirikiano wao wa karibu wanaonipa katika utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Maji. Kamati imefanya kazi kubwa ya kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri uliotolewa na Kamati umekuwa msaada mkubwa wakati wa maandalizi ya bajeti ya Wizara yangu. Napenda kuiahidi Kamati kuwa tutaendelea kutoa ushirikiano, kupokea maoni na ushauri na kuufanyia kazi kwa ajili ya maendeleo ya Sekta ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa pole kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Waheshimiwa Wabunge, familia za marehemu pamoja na Watanzania wote kwa vifo vya wapendwa wetu Hayati Alhaji Ali Hassan Mwinyi, Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili na Hayati Edward Ngoyai Lowassa, Waziri Mkuu Mstaafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, naomba kutoa pole kwako wewe Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu, familia za marehemu, ndugu na wananchi wa majimbo ya Mbarali na Kwahani kwa vifo vya Mheshimiwa Francis Leonard Mtega aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali na Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa pole kwa wananchi wa Wilaya za Hanang', Rufiji, Liwale, Kilombero, Arusha, Malinyi pamoja na maeneo mbalimbali nchini waliokuwa na mafuriko yaliyotokana na mvua za *El Nino* na masika. Mafuriko hayo yamesababisha madhara makubwa kwa Taifa ikiwemo, watu kupoteza maisha, majeruhi, uharibifu wa mali na miundombinu ya barabara, umeme, maji pamoja na kadhia nyingine mbalimbali. Aidha, niwashukuru wadau wote walioshirikiana na Wizara yangu na Serikali kwa ujumla katika kuhakikisha waathirika wa maafa hayo wanapata huduma muhimu ya maji safi na salama na huduma nyingine za kibinadamu ikiwemo chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue fursa hii, kumshukuru kwa mara nyingine, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge, kwa hotuba yake aliyoiwasilisha hapa Bungeni kwa umahiri mkubwa. Hotuba hiyo, imetoa dira na mwelekeo wa utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Awamu ya Sita kwa kipindi cha mwaka 2024/2025 pamoja na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, 2020-2025. Aidha, nawapongeza Mawaziri wenzangu walionitangulia kuwasilisha hoja zao na Wabunge waliochangia hoja hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa pongezi za dhati kwa kuwa tupo katika dunia shindani. Mtu anapofanya jambo vizuri ni vyema ukampongeza. natumia nafasi hii kwa dhati ya moyo wangu, kuipongeza *Dar Young Africans* kwa kuendelea kusambaza maji nchi nzima. Mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni, kwa kweli Yanga hii haikamatiki wala haishikiki. Niseme wazi kabisa kwamba kwa upande wetu wa Msimbazi tuendelee kujipanga; na kwa kuwa sisi ni chama kubwa tutajipanga vizuri. Ukubwa ni kuvumilia, tuendelee kuvumilia nina imani haya ni mapito, tutaendelea kufanya vivuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya ya utangulizi naomba sasa kuchukua fursa hii sasa kuwasilisha hotuba ya bajeti ya wizara yangu yenye sehemu kuu tano ambazo ni; hali ya sekta ya maji nchini, mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2023/2024, mafanikio yaliyopatikana, changamoto na hatua

zilizochukuliwa na mpango na bajeti ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya sekta ya maji nchini. Naomba sasa kuelezea hali ya sekta ya maji nchini inayojumuisha rasilimali za maji, huduma za ubora wa maji na huduma ya maji na usafi wa mazingira ya vijijini na mijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya rasilimali za maji na ubora wa maji. Nchi yetu inakadiriwa kuwa na rasilimali za maji zinazofaa kwa matumizi mbalimbali za wastani wa mita za ujazo bilioni 126 kwa mwaka. Kiasi hicho kinahusisha maji juu ya ardhi mita za ujazo bilioni 105 na maji chini ya ardhi mita za ujazo bilioni 21. Kwa idadi ya watu milioni 59.8 kwa Tanzania Bara kwa mujibu wa Sensa ya Mwaka 2022, inaonyesha kuwa kiasi cha maji kilichopo kwa mtu ni mita za ujazo 2,105. Kiasi hicho kipo juu ya kiwango cha chini cha mita za ujazo 1,700 cha mahitaji ya maji kwa mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa. Hali hiyo inaonyesha kuwa, nchi yetu ipo juu ya kiwango cha uhaba wa maji *(water stress)*. Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi na uharibifu wa vyanzo vya maji kiwango hicho kinaweza kupungua zaidi endapo hatua stahiki hazitachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, Taifa letu lina usalama wa maji, lina maji mengi kwenye maziwa, mito, mabwawa na chini ya ardhi. Kazi yetu kama Wizara ya Maji ni kuyafikisha maji hayo kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya ubora wa maji. Ubora wa maji katika vyanzo vya maji hutofautiana kulingana na jiografia na mabadiliko ya tabia nchi, shughuli za kibinadamu na hali ya miamba. Takwimu zinaonyesha hali ya ubora wa maji kwenye vyanzo vya maji juu na chini ya ardhi, inawezesha ustawi wa ikolojia na hivyo vinaweza kuendelezwa kwa matumizi ya sekta mbalimbali. Pamoja na hali hiyo ya ubora wa maji, bado kunahitajika jitihada za pamoja za kuzuia uchafuzi na pia kurejesha na kuimarisha ubora wa maji katika vyanzo.

Mheshimiwa Spika, vilevile maji yanayosambazwa vijijini na mijini yameendelea kukidhi viwango vya kitaifa vya ubora wa maji

kwa matumizi ya kunywa na kupikia pamoja na shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa hali ya upatikanaji wa maji vijijini; upatikanaji wa huduma ya maji vijijini umefikia wastani wa asilimia 79.6 mwezi Disemba, 2023 kutoka wastani wa asilimia 77 mwezi Disemba, 2022. Ongezeko hilo limetokana na kutekelezwa kwa miradi ya maji 632 yenye vituo 7,956 vya kuchotea maji vyenye uwezo wa kuhudumia wananchi 4,740,959. Hali hiyo inafanya jumla ya wananchi wanaopata huduma ya maji kufikia 34,950,368 kati ya wananchi 39,232,999 wanaoishi maeneo ya vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali ni kuona zaidi ya asilimia 85 ya wananchi wa vijijini wanapata huduma ya maji safi na salama ifikapo mwaka 2025. Nataka kuwahakikishia ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge wa majimbo ya vijijini kama Pangani; tunakoelekea tunahama kutoka kwenye vituo vya kuchotea maji na kuelekea kwenye kuunganisha maji katika kaya na nyumbani. Kwa kuwa vijijini kuna nyumba nzuri zinazohitaji huduma hiyo, wananchi wa vijijini nisikieni, endeleeni kujenga nyumba nzuri, maji ya kuweka ndani yanakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na usafi wa mazingira mijini. Upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo ya mijini, umefikia wastani wa asilimia 90 mwezi Disemba, 2023 kutoka wastani wa asilimia 88 mwezi Disemba, 2022. Ongezeko hilo limetokana na kukamilika kwa miradi ya maji 85 inayohudumia wakazi 4,641,505 wa maeneo ya mijini. Dhamira ya Serikali kuona zaidi ya asilimia 95 ya wakazi wa mijini, wanapata huduma ya maji safi na salama ifikapo mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma ya uondoshaji maji taka, mtandao unaotoa huduma hiyo nchini, umefikia kilometa 1,455.93 mwezi Aprili, 2024. Idadi ya wateja waliounganishwa katika mtandao imefikia 58,650. Kwa maeneo yasiyofikiwa na mtandao huduma ya majitaka hutolewa na magari maalum ambayo hukusanywa na kutibiwa kwenye mabwawa ya kutibu maji taka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Katika mwaka 2023/2024, Fungu namba 49 Wizara ya Maji liliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 756.2, ambapo kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 60.3 ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 695.8 ni fedha za maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo shilingi bilioni 407.1 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 288.7 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida shilingi bilioni 42.3 ni kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi wa wizara, *RUWASA* na Chuo cha Maji na shilingi bilioni 18 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi mwezi Aprili, 2024, wizara imepokea jumla ya shilingi bilioni 638.7 sawa na asilimia 84.5 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 593.4 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo shilingi bilioni 356.9 sawa na asilimia 87 ni fedha za ndani, na shilingi bilioni 236.5 sawa na asilimia 81.9 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida jumla ya shilingi bilioni 45.3 zimetolewa, ambapo shilingi bilioni 36.5 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 8.8 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo. Utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo kwa mwaka 2023/2024, umeainishwa katika maeneo ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji, huduma za ubora wa maji, huduma za usambazaji maji safi na usafi wa mazingira vijijini na mijini na kazi mbalimbali zitakazotekelezwa katika taasisi chini ya wizara pamoja na masuala mtambuka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji. Usimamizi wa rasilimali za maji unahusisha ujenzi na ukarabati wa vituo vya kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji, udhibiti wa matumizi ya maji na migogoro, ujenzi na usajili wa mabwawa, udhibiti wa uchimbaji wa visima, ulinzi na uhifadhi wa vyanzo vya maji na kuzuia uchafuzi wa vyanzo. Hapa naomba kusema, usimamizi wa rasilimali za maji ni sayansi na vilevile ni suala la kijamii. Sisi Wizara ya Maji, tumejifunza kuwa jamii siku zote

ipo na iko tayari, na inaposhirikishwa kuna mafanikio makubwa. Waheshimiwa Wabunge ndio wawakilishi wa jamii na hivyo wizara itaendelea kuwashirikisha katika usimamizi wa rasilimali za maji. Tunaomba hii iwe moja ya ajenda yenu kuu majimboni. Sauti ya Mheshimiwa Mbunge ni kubwa, tufikishieni shukrani zetu kwa wananchi wenu. Maelezo ya kina kuhusu usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji, yanapatikana kwenye ukurasa wa 14 – 28 wa kitabu cha hotuba yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na ubora wa maji wizara imeendelea kuhakikisha maji yanayosambazwa vijijini na mijini yanakidhi viwango vya kitaifa vya ubora wa maji kwa matumizi ya kunywa na kupikia pamoja na shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, falsafa yetu ni falsafa ya afya, kwamba unanawa kabla ya kula. Hivyo, wizara yetu inahakikisha wanachi wanakunywa maji yenye ubora unaokubalika kitaifa na kimataifa na wananawiri. Afya ndio mtaji wa kila kitu. Maelezo ya kina kuhusu masuala ya ubora wa maji yanapatikana kwenye ukurasa wa 28 – 33 wa kitabu cha hotuba yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na huduma ya maji safi na usafi wa mazingira vijijini, Serikali imeendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji vijijini kwa kujenga, kukarabati, kupanua mitandao ya kusambaza maji na kuimarisha usimamizi wa huduma ya maji. Katika mwaka 2023/2024 Serikali ilipanga kutekeleza jumla ya miradi 1,546 katika maeneo mbalimbali ya vijijini. hadi mwezi Aprili, 2024 jumla ya miradi 632 yenye vituo 7,956 imetekelezwa na kutoa huduma kwa wanachi wapatao 4,740,959.

Mheshimiwa Spika, aidha, utekelezaji wa miradi ya maji 872 vijijini upo katika hatua mbalimbali. Baadhi ya miradi mikubwa ya maji vijijini inayoendelea na utekelezaji ni pamoja na Miradi ya maji Ruangwa, Lindi, Nachingwea, Mkinga, Horohoro, Diburuma, Songe, Morong'anya – Morogoro Vijijini, Monduli, Ukiluguru, Sumve hadi Koromije na Ilujamate huko Buhingo. Katika kuongeza kasi ya utekelezaji wa rasilimali za maji na utekelezaji wa miradi ya maji Serikali ilinunua mitambo 25 ya uchimbaji visima na seti tano za mitambo ya ujenzi wa mabwawa. Mwongozo wa matumizi ya

mitambo hiyo umetolewa ili itumike kwa ufanisi na kuleta tija iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/24 Serikali kupitia mitambo hiyo, imekwishachimba visima zaidi ya 266 kwenye maeneo mbalimbali vijijini. Hapa nina salamu za Waheshimiwa Wabunge kutoka kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Pamoja na Wizara ya Maji kufikia asimilia 79.6 vijijini, pamoja na kufikia asilimia 90 ya upatikanaji wa maji mijini, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameielekeza Wizara ya Maji kufanya tathmini hali ya upatikanaji wa maji vijijini pamoja na mijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya tathmini ya upatikanaji wa maji vijijini tumejiuliza maswali yafuatayo. Nchi yetu ina vijiji vingapi? Nchi yetu ina vijiji takribani 12,318. Tumeshafika vijiji vingapi? Tumeshafika vijiji 9,737. Tumebakisha vijiji vingapi? Tumebakisha vijiji 2,581. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameielekeza Wizara ya Maji kupitia mitambo ya uchimbaji visima ambayo ameipa katika kila mkoa mtambo wake, ametuelekeza katika bajeti hii, ukiachana na miradi ambayo tutakwenda kuipitisha katika bajeti hii, Mheshimiwa Dtk. Samia Suluhu Hassan ametoa zawadi maalum kwa kila Mheshimiwa Mbunge wa jimbo, kwamba anakwenda kuchimba visima vitano vitano katika kila jimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kurudia, katika mitambo ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameitoa katika kila mkoa, amekwishatupatia shilingi bilioni zaidi ya 50, ameelekeza, kila Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu Mbunge ndiye anayeishi na wanachi, anayelala na mgonjwa, ndiye anayejua mihemo ya mgonjwa; kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge mtatupa Wizara ya Maji maeneo matano ya vijijini na mjini ambako unaona kwamba kuna changamoto ya maji. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa zawadi maalum katika kila Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo, tunakwenda kuchimba visima vitano katika kila jimbo. Hivi ni nani kama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu, kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni Rais ambaye hapatikani kila mahali. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan hapatikani kila wakati. Waheshimiwa Wabunge tumempata, lazima tumtumie kwa maslahi ya Watanzania. Itoshe kusema, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni suluhu ya matatizo kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali inaendelea na ujenzi wa mabwawa ya ukubwa wa kati na madogo katika maeneo mbalimbali hususan maeneo kame. Hadi mwezi Aprili, 2024, wizara imekamilisha ujenzi na ukarabati wa mabwawa 14 na inaendelea na ujenzi wa mabwawa 25. Mabwawa yaliyokamilika ni Uhelera na Bahimakuru katika Wilaya ya Bahi, Igumangobo na Ilambambasa (Maswa), Ng'walukwa (Shinyanga), Ngofila (Kishapu), Qang'dend (Karatu), na Horohoro na Mbuta (Mkinga), Chole (Kisarawe), Kwamaizi (Handeni), Makame (Kiteto), Enguikumet (Monduli) na Bwawa la Mwadila Wilayani Maswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imeendelea kuzihamasisha taasisi za kijamii, asasi na watu binafsi ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa uvunaji wa maji ya mvua kupitia mapaa ya majengo. Pia Serikali imejenga matenki ya mfano kwenye maeneo ya shule, zahanati na masoko katika halmashauri mbalimbali nchini. Kazi ya mitambo ya kujenga mabwawa ya Mheshimiwa Mama Samia imejidhihirisha katika Majimbo ya Bahi, Maswa, Kishapu, Karatu, Mkinga, Kisarawe, Handeni, Kiteto na Monduli na kwingineko kwa kuchimba mabwawa kwa kutumia wataalamu wa wizara. Kazi hii inaendelea na ndiyo kwanza kunakucha, kama ni mkongo, ndiyo kwanza unaanika maua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile katika kuhakikisha kwamba kunakuwa na uendelevu wa huduma ya maji vijijini, wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inatekeleza programu na miradi ifuatayo: -

Mheshimiwa Spika, Programu ya Uendelevu wa Huduma ya Maji Vijijini. Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Dunia inatekeleza programu ya Malipo kwa Matokeo *(P4R)* kwa gharama za Dola za

Marekani 350,000,000. Awali, utekelezaji wa programu hiyo umefanyika katika halmashauri za wilaya 86, kwenye mikoa 17. Kupitia programu hiyo, jumla ya miradi 540 katika vijiji 1,118 imetekelezwa inayonufaisha wananchi wapatao milioni 4.1. Matokeo hayo yamevuka lengo la awali na kunufaisha wanachi 3,000,000.

Mheshimiwa Spika, hivyo, katika Mkutano wa Mawaziri wa Maji na Fedha wa Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika uliofanyika Adis Ababa nchini Ethiopia mwezi Novemba, 2023, Benki ya Dunia iliitambua Tanzania kuwa kinara katika utekelezaji wa programu hiyo. Kutokana na mafanikio hayo, Tanzania imeongezewa fedha za programu kutoka Dola za Marekani 350,000,000 hadi 654,000,000 na kuongeza mikoa inayonufaika kutoka 17 hadi 25, na halmashauri kutoka 86 hadi 137. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa naomba kusema, kwamba kwa mara mbili mfululizo, Tanzania imealikwa na Benki ya Dunia kutoa ushuhuda na uzoefu wa kuwa kinara wa *P4R* duniani. Hii imefanyika mwezi Machi, 2023 Jijijini New York, Marekani wakati wa Mkutano wa Umoja wa Mataifa kuhusu Maji. Vilevile imefanyika Novemba, 2023 Adis Ababa, Ethiopia wakati wa mkutano wa mawaziri wa maji na fedha wa Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika, hata kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu analijua hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika, Dkt. Victoria Kwakwa, ameipongeza Tanzania kwa kuwa kinara wa kutekeleza *PforR* duniani. Narudia; katika nchi zaidi ya 40, katika mabara matatu, Tanzania ndiyo kinara wa *P4R* duniani, narudia tena, Tanzania ndiyo *number one* katika kutekeleza *P4R* duniani. Mama Samia anaupiga mwingi sana hadi unamwagika. Sasa *P4R* ipo mikoa 25 na halmashauri za wilaya 137. *P4R* inang'arisha vijiji vya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa naomba kutoa maua kwa Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge, Wizara ya Maji ilikuwa wizara ya kero na lawama, hasa maeneo ya vijijini. leo, tulikuwa tukijenga mradi, Mheshimiwa Waziri mradi unatoa maji

ukiondoka unaondoka na maji yako. Mlifanya mageuzi hasa katika maeneo ya vijijini mkasema kuna haja ya uanzishwaji wa Taasisi *RUWASA* mwaka 2019. Haya ndiyo mafanikio na maamuzi ya Bunge lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kukukabidhi rasmi barua ya Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia ambayo ametoa pongezi na kuthibitisha Tanzania kuwa kinara juu ya *P4R*. Haya ni maamuzi ambayo umefanya pamoja na Waheshimiwa wa Bunge Tukufu, kwa ruhusa yako. *(Makofi)*

*(Hapa Waziri wa Maji alikwenda kumkabidhi Spika barua ya pongezi na kuthibitisha Tanzania kuwa kinara juu ya P4R iliyotolewa na Rais wa Benki ya Dunia)*

**WAZIRI IWA MAJI:** Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu huduma za maji na usafi wa mazingira vijijini, yanapatikana kwenye ukurasa wa 33 – 42 wa kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na huduma ya maji safi na usafi wa mazingira mijini, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imeendelea kujenga, kukarabati na kupanua miundombinu ya maji safi na usafi wa mazingira katika maeneo ya mijini. Katika mwaka 2023/2024, jumla ya miradi 244 ilipangwa kutekelezwa ambapo hadi mwezi Aprili, 2024 miradi 85 imekamilika na miradi 159 ipo kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji. utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maji safi na usafi wa mazingira katika miji mikuu ya mikoa, miji mikuu ya wilaya, miji midogo na miradi ya kitaifa ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maji na usafi wa mazingira mijini ni kama ifuatavyo. Mradi wa maji na usafi wa mazingira katika Jiji la Arusha.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji na Usafir wa Mazingira katika Jijii Arusha, Wizara imekamilisha utekelezaji wa mradi wa safi na usafi wa Mazingira katika Jiji la Arusha kwa gharama za Dola za Marekani milioni 233.9. Kukamilika kwa mradi huo kumeongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 40 hadi lita

milioni 200 kwa siku, hivyo kukidhi mahitaji ya maji kwa Jiji la Arusha, kuongezeka kwa huduma ya uondoaji wa majitaka kutoka kwa asilimia 7.6 hadi 30 na kupunguza upotevu wa maji kutoka asilimia 48 hadi 39. Kazi iliyobaki ni kundelea na usambazi wa maji katika maeneo ya Kiseriani, Sekeleni, Muyavalo, Shangarai, Maweni, Karangai, Msitu wa Mbogo, Shambarai, Bulukamatiba, Valeska, Patanumbe, Kinyaki, Siwandeti, Tarakwa na Kata ya Kiutu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huduma ya maji katika Jiji la Arusha ni ya uhakika na hivyo inalinda na kulipa hadhi Jiji la Arusha ambalo ni kitovu cha utalii nchini. Huduma ya Maji Arusha inapeperusha ajenda ya *Royal Tour,* ajenda ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suhuluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuboresha huduma ya maji safi katika Mkoa wa Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Pwani. Wizara inatekeleza miradi mbalimbali ya kutolesha huduma ya maji safi na usafi wa mazingira katika Mkoa wa Dar es salaam pamoja na Miji ya Kibaha, Kisarawe, Mkuranga, Chalinze na Bagamoyo Mkoa wa Pwani. Hadi mwezi Aprili, 2024 utekelezaji wa kipande cha kwanza na cha pili cha Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Usambazaji Maji kutoka Visima Virefu vya Kimbiji kwa gharama ya shilingi bilioni 21.28 umekamilika na kunufaisha wakazi 250,000 wa Chanika, Luzando, Mpela Chamazi, Kitunda, Kinyerezi, Temeke, Kisarawe, Kibaha, Dar – Kimbiji, Kigamboni, Tuangoma, Mkuranga, Kongowe, Mbagala, Kurasini, Mtoni, Keko na Chang'ombe.

Mheshimiwa Spika, vilevile kipande cha tatu Mradi wa Ujenzi wa Mtandao wa Mabomba ya Maji wa Kimbiji, Kigamboni utekelezaji umefikia asilimia 75 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024. Kwa upande wa Kibamba maeneo yatakayonufaika ni pamoja na Msakuzi, Makabe, Msumi A, Msumi B, Msumi C, Mpiji Magohe na Tegeta A. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara imeanza kujenga mtandao wa usambazaji maji na matenki ya kuhifadhi maji Kusini mwa Dar es saalam kwa gharama ya shilingi bilioni 35.15. Hadi mwezi Aprili, 2024 utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 19 na unatarajiwa

kukamilika mwezi Desemba, 2024 na kunufaisha wakazi 450,000 wa maeneo ya Bangulo, Mwanagati, Kitunda, Kipunguni, Majohe, Kivule, Magole, Msongola, Chanika na Charambe.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara inatekeleza mradi wa usambazi maji safi maeneo yaliyo nje ya mtandao kwa gharama ya shilingi bilioni 22. Hadi mwezi Aprili, 2024 utekelezaji umefikia asilimia 96 na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Mei, 2024 na kunufaisha wakazi 215,380 wa maeneo ya Kisewe, Magengeni, Dovya, Mwembe Bamia, Mianzini, Mwanamtoti, Butiama, Mjeule, Upendo, Tungi Magogoni, Feri, Nzasa A, Somelo, Kifurukwe, Kichangani, Yangeyange, Vumba na yaliopo Kigamboni, Temeke na Ilala.

Mheshimiwa Spika, Jiji la Dar es Salaam ni Jiji kubwa ni Jiji la kibiashara na mboni ya Taifa, heka heka zake ni kama Sherehe za Christmas au Eid. Hivyo Wizara iko macho na huduma za maji katika Jiji la Dar es salaam, Waheshimiwa Majimbo yanahudumiwa na *DAWASA*, ahsanteni sana kwa ushirikiano wenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali inaendelea kujenga Bwawa la Kimkakati la Kidunda litakalo hudumia Jiji la Dar es Salaam na maeneo ya Mkoa wa Pwani na Morogoro Vijijini ambapo ujenzi umefikia asilimia 18. Wazo la ujenzi wa Bwawa la Kidunda ni la miaka na miaka, tangu miaka ya 1950 Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere amelikuta na ameliendeleza. Baada ya miaka zaidi ya 60 Mama Dkt. Samia anajenga Bwawa la Kidunda tena kwa fedha za ndani, hakika hii inadhihirisha umuhimu wa kazi kubwa na nzuri ameifanya Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bwawa hili ni mwarubaini wa shida ya maji katika Majimbo ya Chalinze, Bagamoyo, Kibamba, Ubungo, Kawe, Kinondoni, Ilala, Kigamboni, Segerea, Ukonga, Kisarawe, Mkuranga, Mbagala, Kibaha Mjini, Kibaha Vijijini na sehemu mbalimbali za Morogoro Vijijini. Waheshimiwa Wabunge mambo yako bam bam, tena bam bam sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuboresha huduma ya maji safi katika Jiji la Dodoma, Wizara imeendelea kutekeleza mipango ya muda

mfupi inayolenga kukabiliana na adha ya upatikanaji wa maji katika Jiji la Dodoma, ambapo hadi mwezi Aprili, 2024 Wizara imekamilisha utekelezaji wa awamu ya kwanza wa Mradi wa ujenzi na Uboreshaji wa Mtandao wa Maji Safi Nzuguni unahudumia wakazi 75,968 wa maeneo ya Nzuguni, Ilazo, Swaswa na Kisasa.

Mheshimiwa Spika, aidha. Awamu ya pili ya mradi wa pili imeanza kwa gharama ya shilingi bilioni 5.51 na utanufaisha wakazi wapatao 80,000. Vilevile utekelezaji wa mradi wa kupanua na kuboresha huduma ya maji safi Dodoma na Chamwino unaogharimu shilingi bilioni 4.18 unaendelea na umefikia asilimia 40 na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2024 na kunufaisha wakazi 150,000 wa Dodoma na Chamwino.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na taratibu za maandalizi za Ujenzi wa Bwawa la Mkakati la Falukwa litakalohudumia Jiji la Dodoma na Wilaya za Chemba, Chamwino na Bahi. Kazi inayoendelea ni mapitio ya usanifu wa Bwawa pamoja na uandaaji wa mpango wa kulinda na kutunza mazingira katika vyanzo vya maji, vitakavyopeleka maji kwenye bwawa, ujenzi unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, kuboresha huduma ya maji safi katika Jiji la Mwanza na maeneo ya pembezoni, Wizara ya Maji kwa kushirikiana na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya pamoja na Shirika la Maendeleo la Ufaransa imekamilisha utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Ujenzi wa Chujio la Butimba kwa gharama ya takribani shilingi bilioni 80. Mradi huo ulihusisha kukamilisha kwa mradi huo kumeboresha huduma ya maji kwa wakazi wapato 450,000 katika Jiji la Mwanza kwa maana ya Nyamagana na Ilemela. Maeneo yanayonufaika na mradi huo ni pamoja na Nyegezi, Luchelele, Kishiri, Igoma, Nyamuhongolo katika Jimbo la Nyamagana na hadi katika Jimbo la Mama yangu Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula pale Ilemela. Aidha, kazi iliyobaki ni Ujenzi wa matenki matano yatakayo sambaza maji katika maeneo ya Fumagira, Nyamazobe, Usagara, Kisesa na Buhongwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile utekelezaji wa mradi wa kupanua mtandao wa usambaji maji katika Miji ya Magu na Misungwi unagharimu shilingi bilioni 1.94 unaendelea hadi mwezi Aprili, 2024. Utekeleza umefikia asilimia 70 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024. Pia utekelezaji wa kuboresha mfumo wa usambazaji maji katika Jiji la Mwanza unao gharimu shilingi bilioni 4.62 umefikia asilimia 70 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024 na kunufaisha wakazi wapatao 33,000.

Mheshimiwa Spika, Kanda ya Ziwa yote Mungu amewapendelea kwa kuwapa Ziwa Victoria. Wizara inahakikisha mnapata maji safi, salama na yenye kutosheleza kutoka kwenye Ziwa Victoria, Wahenga walisema kula uhondo kwa taka matendo pasi matendo utakula uvundo. Mradi wa Butimba, umedhihirisha kuwa kwa nia njema na juhudi za Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassana Mwanza sasa mnaendelea kula uhondo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuboresha huduma ya maji safi katika Jiji la Mbeya, ukipigana vita ya ugenini, nyumbani lazima kuwe na amani. Wizara inaendelea kutekeleza Mradi wa Kuboresha Huduma ya Maji Safi katika Jiji la Mbeya kwa kutumia chanzo cha Mto Kiwira, unaogharimu jumla ya zaidi ya bilioni 99.66. Mradi huo utaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 66.5 hadi lita 184 kwa siku, hadi mwezi Aprili, 2024 ujenzi wa banio na tenki la maji lenye ujazo wa lita milioni tano ulikuwa umefikia asilimia 11. Mradi unatarajiwa kukamilika 2025 na kunufaisha wakazi zaidi milioni 1.45 kwa Jiji la Mbeya. Mji wa Mbalizi na Vijiji vya Mbulu, Mbeya *One*, Swaya Juu na Malangali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Wizara inatekeleza kipande cha kwanza cha pili cha mradi cha kuboresha huduma ya maji katika Kata za Mwansekwa na Iganzo kwa gharama ya shilingi bilioni 5.2. Utekelezaji katika kipande cha kwanza umefikia asilimia 90 na kipande cha pili asilimia 76. Mradi umeanza kuzalisha maji lita milioni mbili kwa siku na umeanza kutoa huduma kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa majukumu makubwa uliyonayo ya kuongoza Mhimili wa Bunge na kuwa Rais wa *(IPU)* Duniani

unahitaji utulivu mkubwa. Ili kuteleza majukumu hayo ya kitaifa na kimataifa mradi wa Kiwira na shughuli nyingine za maji Mkoani Mbeya zinalenga kukupa wewe na Wabunge wote wana maji ya kutosha na yenye kutosheleza. Hapa nikuhakikishie suala la maji Jijini Mbeya niache mimi hatutokuwa kikwazo kama Wizara kuhakikisha wana-Mbeya wanapata maji safi, salama na yenye kutosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji Mugango – Kiabakari, Mradi wa Maji wa Mugango – Kiabakari tumekweisha ukamilisha na mradi huu ni fahari kubwa ya kuendelea kumuenzi Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kupitia upatikanaji wa maji katika Vijiji vya Butiama na Wilaya za Butiama kwa ujumla pamoja na Mheshimiwa Profesa Mashuhuri Sospeter Muhongo katika kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Same – Mwanga – Korogwe, Wizara kwa kushirikiana na *BADEA, OPEC Fund* na Kuwait *Fund* inatekeleza Mradi wa Maji wa Same – Mwanga – Korogwe. Utakao hudumia Miji ya Same na Mwanga pamoja na Vijiji 38 vya Wilaya za Same na Mwanga na Vijiji vitano vya Wilaya vya Korogwe. Hadi mwezi Aprili, 2024 utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 86.7 na kwa sasa upo kwenye majaribio ya kutoa maji kutoka chanzo na kuyapeleka kwenye chujuo, mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Juni na utakuwa na uwezo wa kuhudumia wananchi 456,931 wa Wilaya za Same, Mwanga pamoja na Korogwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi huu wa Same – Mwanga – Korogwe ni Mradi ambao ungetutitia doa sana Wizara yetu ya Maji. Mradi ambao ungeifedhehesha, sana Wizara ya Maji, ni mradi ambao ulionekana kama mradi ambao umeshindikana. Nitumie nafasi hii kumshukuru Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan alivyoingia alisema kipaumbele chake cha kwanza ni Mradi wa Same – Mwanga kipaumbele chake cha pili ni Mradi wa Same – Mwanga kipaumbele chake cha tatu ni Mradi wa Same – Mwanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe taarifa kwa Waheshimiwa Wabunge mradi huu ambao ulikuwa mgumu leo hii Dkt. Samia Suluhu Hassan ameugeuza biskuti, leo tunaenda kuhakikisha wananchi wanaenda kupata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa naomba Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo ya Mwanga, Same Magharibi, Same Mashariki na Korogwe Vijijini muendelee kuungana na Wizara ya Maji katika kusoma Wakorintho 6:2. Inayosema wakati uliokubalika na kulisikia siku ya wokovu nakulisaidia tazama wakati uliokubalika ndiyo sasa, tazama siku ya wokovu ndiyo sasa, wakati wa maji ya Same – Mwanga ndiyo huu. Mama Dkt. Samia anaweka historia Same – Mwanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Miji 28. Wizara inaendelea kutekeleza mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Miji 28, ambapo Miji 24 inatekelezwa kwa fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya India kupitia *Exim Bank* ya India. Miji 4 inatekelezwa kwa fedha za ndani kwa mujibu wa Mkataba, mradi huo Miji 28 inatarajiwa kukamilika mwaka 2025/2026 na utanufaisha wananchi katika Miji ya Handeni, Muheza, Pangani, Korogwe, Kilwa, Mosoko, Nanyumbu, Ifakara, Rujewa, Makambako, Wanging'ombe, Njombe, Chunya, Chamwino, Chemba, Manyoni, Singida, Kihomboi, Mugumu, Kaliua, Urambo, Sikonge, Kasulu, Mpanda, Geita, Chato, Kayanga, Mafinga, Makonde, Songea na Rorya – Tarime. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wa Miradi ya Miji 28 ni wenu, tunaomba muendelee kuusimamia na Wizara itaendelea kuwashirikisha katika kila hatua zote za utekelezaji wa mradi huu, anaelala na mgonjwa ndiye anayejua mihemo yake. Nyinyi Waheshimiwa Wabunge ndiyo mko na mgonjwa mnajua Mradi wa Miji 28 tushirikiane, lazima katika kila mji na mradi wote tupate pointi tatu na magoli kibao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi katika Mkoa wa Simiyu, mradi huo unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani *(KfW)* na mfuko wa mabadiliko ya tabianchi *(green*

*climate fund-GCF)* kwa gharama ya shilingi bilioni 444.6. Mradi huo unatekelezwa kwenye Wilaya tano za Busega, Bariadi, Itilima, Maswa na Meatu katika Mkoa wa Simiyu na unahusisha usanifu na ujenzi wa miundombinu ya uzalishaji, uhifadhi na usambazaji maji katika wilaya hizo.

Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Aprili, 2024 kazi zinazoendelea ni ujenzi wa matenki ya maji sita yenye jumla ya ujazo wa lita milioni 39.5, upimaji na uhakiki wa njia kuu ya kulaza mabomba. Kwa wastani utekelezaji umefikia asilimia 4 na unatarajiwa kukamilika mwezi Februari, 2026 na kunufaisha wananchi wapatao 662,000 kwenye wilaya hizo. Maelezo ya kina kuhusu huduma ya maji na usafi wa mazingira Mijini kwenye ukarasa wa 43 hadi 82 ya kitabu cha Hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, Mpango kabambe wa Taifa wa Maji *(National Water Master Plan),* Wizara kwa kushirikiana na wadau imeanza kuandaa mpango kabambe wa Taifa wa maji katika Mikoa ya Rukwa, Dodoma na Njombe na zoezi hilo litaendelea katika mikoa mingine iliyobakia katika mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, gridi ya Taifa ya maji. Wizara inaendelea na maandalizi ya gridi ya Taifa ya maji na kwa sasa hatua iliyofikiwa ni kuajiri mtalamu mshauri anayetarajiwa kufanya upembuzi yakinifu kwa mpango huo. Aidha, Wizara imeanza kutumia vyanzo vikubwa vya maji vya uhakika ikiwemo Maziwa, Mito mikubwa na Mabwawa kwa ajili ya kusambaza huduma ya maji kwenye maeneo ambayo hayana vyanzo vya uhakika wa maji. Kwa mfano Mradi wa Kutoa Maji wa Ziwa Victoria ambao umenufaisha Miji ya Kahama, Shinyanga, Tinde, Nzega, Tabora, Igunga na Sheluhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile taratibu za manunuzi ya kumpata mtalamu mshauri kutoa maji ya Ziwa Victoria, Tanganyika na kuyapeleka katika Mikoa ya Katavi, Rukwa, mpaka Kigoma zimeanza. Pia Wizara imesaini Mkataba na mtalamu mshauri atakayefanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mradi wa kuyatoa maji ya Ziwa Victoria na kuyapeleka Jiji la Dodoma. Waheshimiwa Wabunge, Majimbo yaliyokuwa katika mwambao

wa Maziwa ya Tanganyika, Nyasa na Victoria pamoja na maeneo kame mtoto wenu *National Water Grid* karibu anazaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Maziwa ya Tanganyika, Nyasa na Victoria pamoja na Mto Ruvuma yana asilimia 25 ya maji yote matamu duniani. Hivyo maono hayo makubwa ya Mama Dkt. Samia lazima yatekelezwe na sisi Wizara ya Maji hatutokuwa kikwazo. Narudia Mradi wa *National Water Grid* ni maono makubwa ya Taifa linalojiamini na kuthubutu taifa hilo ni Tanzania chini ya Mama Dkt. Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matumizi ya dira za maji za malipo kabla. Wizara imeanza kutumia teknolojia ya matumizi ya dira za maji za malipo kabla *(pre-paid water meter)* kwa lengo la kupunguza maji yanayopotea na malalamiko yanayohusiana na ankara za maji. Hadi mwezi Aprili, 2024 jumla ya wateja 13,526 katika maeneo ya vijijini na mijini wamefungiwa dira hizo zikiwemo za Mamlaka za Maji za Iringa ambayo imefungiwa dira 6,544, Dodoma 1085 na Mamlaka ya Maji Tanga dira 627, kwa upande wa vijijini *RUWASA* imewafungia dira wateja 1,846 kwenye mikoa mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 4 Machi, 2024. Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan alielekeza Wizara ya Maji kuongeza kasi ya ufungaji wa dira za maji za malipo kabla ili kuwafikia wananchi wote nchini. Katika kutekeleza agizo hilo Wizara, imeandaa mkakati wa kuongeza kasi ya ufungaji wa dira za maji za malipo kabla, ambapo kupita mkakati huo asilimia 50 ya wateja wa maji vijijini na maji mijini watafungiwa dira hizo ifikapo Desemba, 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili ni agizo la Mama Dkt. Samia kwa Wizara ya Maji nasi tunamuhakikishia Mama kupitia Ezra 10 mstari wa 4 kuwa kazi tunaiweza na timu ya Wizara iko imara kuitenda kwa ukamilifu. Naomba Waheshimiwa Wabunge tuhamasishe wananchi kufunga dira za malipo kabla ya matumizi, hizi ni *LUKU* za maji, hii ndiyo dunia ya kisasa na huu ndiyo muelekeo. Napenda kumuhaidi Mheshimiwa Rais, kuwa lugha yetu ni *pre-paid meter* na maono yetu ni kuwa na viwanda vya *pre-paid meter. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya Sekta ya Maji katika Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024, katika kipindi cha Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2023/2024 chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Sekta ya Maji imepata mafanikio makubwa yafuatayo:-

(i) Kuongezeka kwa hali ya upatikanaji wa huduma ya maji vijijini kutoka wastani wa asilimia 77 mwezi Desemba, 2022 hadi asilimia 79.6 mwezi Desemba, 2023 na mijini kutoka wastani wa asilimia 88 mwezi Desemba, 2022 hadi asilimia 90 mwezi Desemba, 2023;

(ii) Kupatikana kwa chanzo kipya cha fedha za utekelezaji wa miradi ya maji kupitia hati fungani. Ambapo Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Tanga, imekuwa ya kwanza kuzindua uuzaji wa hati fungani ya kijani yenye thamani ya bilioni 53.12. Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tanga imekuwa Taasisi ya kwanza Tanzania na Afrika Mashariki kuingia katika soko la hisa na imepata fedha shilingi bilioni 54.72, sawa na 103%.

Mheshimiwa Spika, narudia imevunja rekodi ya kuwa taasisi ya kwanza Tanzania na Afrika Mashariki huu ni ubunifu na uthubu mkubwa na tunawashukuru sana Watanzania na Waheshimiwa Wabunge kwa kununua hisa hizi za Mamlaka ya Maji Tanga hili ni funzo kuwa *it can be done play your part. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuishukuru sana Wizara ya Fedha, kwa ushirikiano wao mkubwa mpaka kuweza kutufikisha katika suala hili la hati fungani, lakini pia kuishukuru Benki ya *NBC,* kwa kuratibu vizuri na kuweza kulifanikisha jambo hili. Lakini kwa namna ya kipekee niipongeze Bodi ya Tanga *UWASA* lakini pia kumpongeza Mkurugenzi makini kabisa *Engineer* Hilly kwa uthubutu wake mkubwa na kuweza kulifanikisha jambo.

Mheshimiwa Spika, tatu kufikiwa malengo ya Programu ya *P4R* kwa muda uliopangwa, hivyo Benki ya Dunia kuitambua Tanzania kuwa nchi ya kwanza kufanya vizuri katika nchi zaidi ya

40 duniani zinazotekeleza programu hiyo kwa kipindi miaka miwili. Hii *standard* umeiweka wewe, wewe ni Mbunge wa madunia na sisi hata utekelezaji wetu wa miradi ya maji tunakwenda kidunia dunia Mungu akubariki sana Mheshimiwa Spika, *(Makofi)*.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa miradi mikubwa na ya kimkakati ukiwepo Mradi wa Maji wa Jiji la Arusha, Buting'wa, Mugango, Kyabakari, Butiama na Bunda. Kuanza kwa utekelezaji wa mpango na Gridi ya Taifa ya Maji kwa kutumia vyanzo vikubwa vya maji, ikiwemo maziwa, mito na mabwawa kupeleka maji katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kuimarika kwa mazingira ya kazi kutokana na kuimarika na kuanza kutumika kwa jengo jipya la Ofisi la Wizara ya Maji lililopo Mtumba, pamoja na ununuzi wa vitendea kazi ikiwemo magari 124, pikipiki 191 na kompyuta 95. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa ujenzi na ukarabati wa mabwawa 14 ya ukubwa wa kati na madogo ya kuvuna maji ya mvua kwenye maeneo mbalimbali nchini yenye uwezo wa kuhifadhi maji lita bilioni 1.86. Kuongezeka kwa ufanisi katika uchimbaji wa visima na ujenzi wa mabwawa kwa kutumia mitambo iliyonunuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio haya, ukimuona kobe juu ya mti ujue amepandishwa. Huu ni usimamizi na ufuatiliaji wa Waheshimiwa Wabunge, Mwenyezi Mungu awabariki sana. Huu ni usimamizi mzuri wa Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya wote nchini kwa kazi kubwa na nzuri kwa miradi ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa sababu ya usimamizi mzuri wa uhakiki wa Chama Cha Mapinduzi kupitia Viongozi wa Chama, tumewaona katika miradi mbalimbali mijini na vijijini. Leo tumemuona Mwenyekiti wa Wazazi yupo hapa, kaka yangu Fadhili, pia tumemuona *Engineer* wa Maji ambaye ni Mwenyekiti wa Mkoa wa Tanga, kaka yangu Ustadh Rajab pamoja na Mwenyekiti wa Wilaya ya Pangani, Dulla Bonge na kaka yangu

Abdallah Mahmud. Wameweza kusimamia na kufuatilia kuhakikisha Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inatekelezeka katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, natambua pia, mchango wa Wakuu wa Wilaya wote nchini. Namuona Mkuu wetu wa Wilaya ya Pangani, Lushoto, Korogwe, Tanga Mjini pamoja na Handeni wameweza kujumuika na sisi katika kuhakikisha tunaweza kufanikisha bajeti hii katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Changamoto Zilizojitokeza na Hatua Zilizochukuliwa. Maelezo ya kina kuhusu changamoto na hatua za kukabiliana nazo, yanapatikana katika ukurasa wa 105 na 108 wa Kitabu cha Hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Vipaumbele na Mpango wa Bajeti wa Mwaka 2024/2025. Wizara imeweka vipaumbele ambavyo vitazingatiwa katika Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2024/2025. Vipaumbele hivyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuendelea na usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji. *(Makofi)*

(ii) Kukamilisha utekelezaji wa miradi inayoendelea na ujenzi wa miradi mikubwa.

(iii) Kuendelea kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuongeza kasi ya uvunaji wa maji ya mvua, kupitia ujenzi wa mabwawa makubwa na ya kimkakati kwa kushirikiana na sekta za mifugo, kilimo, utalii na mazingira. *(Makofi)*

(iv) Kuimarisha matumizi ya mitambo ya uchimbaji visima na mabwawa iliyonunuliwa, ili kufikisha huduma ya maji kwenye vijiji ambavyo havina huduma.

(v) Kukamilisha uundaji wa Mpango kabambe wa Taifa wa Maji *(Water Master Plan)* pamoja na *National Water Grid*.

(vi) Kupunguza upotevu wa maji na kuendelea kukarabati miundombinu chakavu. Kufunga mifumo ya kuweza kutambua maeneo yenye mivujo *(IALMS)*. Kushirikisha Viongozi wa Serikali za Mitaa kwa ajili ya kutoa taarifa za upotevu wa maji kwa wakati.

(vii) Kuongeza kasi za ufungaji wa dira za malipo kabla ya matumizi *(pre-paid meter),* ili kuongeza makusanyo na kupunguza malalamiko ya wateja.

(viii) Kuongeza kasi ya uwekezaji wa miundombinu ya uendeshaji majitaka kwenye miji mikuu ya mikoa na wilaya.

(ix) Kuimarisha utoaji wa huduma ya maji safi kupitia mamlaka za maji safi na mazingira na *CBWSOs,* kwenye eneo la maunganisho ya wateja wapya na kuhakikisha saa za upatikanaji wa huduma ya maji zinaongezeka.

(x) Kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika uwekezaji na uendeshaji wa miradi na *scheme* za maji.

Mheshimiwa Spika, Mpango na Bajeti kwa mwaka 2025 umezingatia vipaumbele vinavyotajwa hapo juu pamoja na masuala ya uendelezaji wa rasilimali za maji, usimamizi wa huduma za ubora wa maji, huduma ya maji safi, usimamizi wa mazingira vijijini na mijini na kujenga uwezo wa Wizara na taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Huduma ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini. Katika Mwaka 2024 Wizara imepanga kuendelea kutekeleza jumla ya miradi 1,054 ya usambazaji maji vijijini katika maeneo mbalimbali ikiwemo maeneo yanayozunguka vyanzo vya Bwawa la Kidunda na vijiji vilivyopitiwa na Mradi wa Same, Mwanga. Aidha, kuendelea kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika utoaji wa huduma za maji kuzijengea uwezo *CBWSOs,* ili kuimarisha uwezo wa kujiendesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Huduma ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mijini. Katika Mwaka 2024/2025 Wizara kwa kushirikiana

na wadau wa maendeleo pamoja na sekta binafsi imepanga kutekeleza jumla ya miradi 245 ya maji kwenye maeneo ya maji mijini, ukiwemo Mradi wa Kutoa Maji Mto Ruvuma kwenda Mtwara, Mradi wa Kutoa Maji Mto Momba kwenda Momba na Tunduma, kutoa maji kutoka *Tank* la Busenye kwenda Nyamuswa na kuanza usanifu wa Mradi wa Kutoa Maji Mto Rufiji Kwenda Lindi na Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara imepanga kutekeleza ujenzi wa Mradi wa Maji Kutoka Mto Ruvuma mpaka Mtwara. Pia uondoshaji wa majitaka katika miji mikuu ya mikoa, miji mikuu ya wilaya na miji midogo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Jiji la Dodoma. Wizara itaanza ujenzi wa Mradi wa Bwawa la Farkwa na mpango wa muda mrefu ni kutekeleza mradi wa kutoa maji ya Ziwa Victoria kwenda Jiji la Dodoma kupitia Singida.

Mheshimiwa Spika, Huduma ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini. Katika Mwaka 2024 naomba maelezo ya kina yapatikane katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Jiji la Dodoma kama nilivyoeleza, tunatekeleza mradi wa kuyatoa maji ya Ziwa Victoria kwenda jiji la Dodoma, kupitia Singida.

Mheshimiwa Spika, pia, Wizara imepanga kuboresha huduma ya maji katika maeneo ya vijijini kwa kuhakikisha maunganisho kwa wateja yanafanyika ndani ya siku saba.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Wizara ya Maji ni kuboresha huduma kwa wateja. Tumeona katika baadhi ya mamlaka, mwananchi anataka kuunganishiwa maji, inatumika wakati mwingine zaidi ya miezi miwili hadi mitatu. Nataka niwaambie Wakurugenzi wa Mamlaka za Maji, kipimo cha maunganisho ya maji kwa wateja ni ndani ya siku saba.

Mheshimiwa Spika, pia kipimo cha watendaji wa Wizara ya maji, naomba mnisikie, ni upotevu wa maji. Haiwezekani leo Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu

unakwenda kuitembelea Mamlaka ya Maji anakwambia upotevu wa maji ni asilimia 45, hatuwezi kuwa na Mkurugenzi wa aina hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haiwezekani Serikali i-*invest* pesa kwa ajili ya kutoa maji kwa wananchi halafu leo maji yapotee, wananchi hawana maji. Mkurugenzi wa namna hiyo tutakuweka pembeni na wala hatutakuwa na mswalie Mtume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nawapongeza Wakurugenzi kwa kazi kubwa na tunathamini kazi nzuri ambazo mnazifanya. Hiki sasa ndicho kitakachokuwa kipimo cha Wizara yetu ya Maji.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni la uboreshaji wa maji. Wakati mwingine tunashangazwa kuona Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji anakwenda kumkatia mwananchi siku ya sikukuu, unakwenda kumkatia mwananchi maji wakati mwingine *weekend,* haiwezekani. Niwaombe Wakurugenzi wa Mamlaka zote za Maji ni marufuku kumkatia mwananchi maji siku ya sikukuu ama siku za *weekend.* Tufuate taratibu na Sheria waheshimiwa Wakurugenzi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo hatutasamehe ni, yapo mambo tutasamehe lakini, kuna baadhi ya mambo hatutasamehe kama Mkurugenzi ambaye atabambikizia mwananchi bili ya maji hatutakusamehe. Tutakuchukulia hatua, ili kuongeza ufanisi katika Mamlaka zetu za Maji.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nitoe shukrani zangu za dhati. Kipekee napenda kutumia fursa hii kuwashukuru wananchi pamoja na wadau mbalimbali kwa ushirikiano wao katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu. Kwa mwaka 2023/2024 maandalizi ya bajeti hii yamezingatia mchango, maoni na mapendekezo ya wadau katika kuweka vipaumbele vya sekta.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa nchi rafiki, washirika wa maendeleo, sekta binafsi na taasisi zisizo za kiserikali, mashirika ya dini, wadau wengine wakiwemo wakandarasi, wazabuni na wataalamu washauri kwa

ushirikiano wanaoutoa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu. Aidha Serikali inawaahidi kuendelea kulinda viwanda vya ndani katika kutekeleza miradi ya maji.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee naomba nimpongeze Naibu Waziri wangu wa Maji, Mheshimiwa Mhandisi Andrea Mathew Kundo, amenipa ushirikiano mkubwa na ninataka niseme kwa muda mfupi ambao ameingia amekwishaanza kutema cheche. Mungu akubariki na akufanyie wepesi Mheshimiwa Kundo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee namshukuru aliyekuwa Naibu Waziri wangu *Eng.* Maryprisca Mahundi. Mafanikio haya tuliyoyapata nilifanya kazi kwa ukaribu na dada yangu *Eng.* Maryprisca Mahundi. Mungu akubariki na akufanyie wepesi. Pia, Katibu wetu Jamal Katundu ambaye ameleta mchango mkubwa katika Wizara yetu ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia natumia nafasi hii kumpongeza na kumshukuru Katibu Mkuu wetu wa Wizara ya Maji, *Eng.* Mwajuma Waziri. Haya yote tunayozungumza, miradi hii mikubwa ya kimkakati, yote ame-*design Engineer* Mwajuma Waziri. Mradi huu wa Same, Mwanga, ambao ulikuwa mgumu kukamilika kwake, ameingia kwa muda mfupi na kazi ameikamilisha, *Engineer* Mwajuma Waziri. Kwa mwili unaweza kumuona mdogo-dogo, nataka nikuhakikishie sindano ndogo ndiyo inayoshona madera na makoti. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Naibu Katibu Mkuu wa Wizara yetu ya Maji, Mama yangu Meena. Sisi katika Wizara yetu ya maji tunamuita *Aunt* wa Wizara pia, ni Mama Mchungaji. Ukiangalia safu ya Wizara yetu, sisi wote watatu, Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wote ni vijana; ametuletea Shangazi wa Wizara, anatulea vizuri na tumejipanga vizuri kuhakikisha kwamba, tunakwenda kumtua mwanamama ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee pia, naomba nieleze furaha kubwa niliyonayo. Naendelea kuishukuru familia yangu na Wananchi wa Jimbo la Pangani kwa ushirikiano wao

mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Pia, kwa namna ya kipekee nawapongeza sana Wakurugenzi wote, Wakuu wa Vitengo na Menejimenti ya Wizara ya Maji, watumishi wote wa Wizara ya Maji bila kuwasahau Wenyeviti wa Bodi na Taasisi zake, Madereva, Wahudumu na Waendesha Ofisi kwa ushirikiano wanaonipatia pamoja na kujituma katika utekelezaji wa Majukumu ya Sekta ya Maji.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha kwa mwaka 2024/2025; baada ya maelezo hayo ninaomba sasa kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 627,778,338,000 kwa ajili ya Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2024/2025 ambapo, shilingi 69,662,959,000 ni fedha za Matumizi ya Kawaida na shilingi 558,115,379,000 ni fedha za Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kati ya Fedha za Matumizi ya Kawaida fhilingi 17,542,812,000 ni kwa ajili ya kugharamia matumizi mengineyo *(OC)*. Shilingi 52,120,147,000 ni kwa ajili ya kulipa mishahara ya Watumishi wa Wizara, *RUWASA*, Mfuko wa Taifa wa Maji na Chuo cha Maji. Kwa upande wa fedha za maendeleo, ni shilingi 340,463,656,000 sawa na 61% ni fedha za ndani na shilingi 217,651,723,000 sawa na 39% ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine ninaomba kutoa shukrani zangu za dhati kwako na kwa Mheshimiwa Rais, pamoja na Waheshimiwa Wabunge, bila kuisahau Wizara ya Fedha kwa ushirikiano Mkubwa ambao mmetupatia chini ya Mheshimiwa Mwigulu pamoja na Naibu Waziri wake.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Waheshimiwa Wabunge Jeshi la Wizara ya Maji lipo tayari kuendelea na kazi ya kumtua mama ndoo kichwani katika mwaka 2024/2025. Jeshi hili ni kubwa na lina weledi wa kutosha. Tupo tayari kuendelea kuuza Duka la Chama cha Mapinduzi, kama mlivyotutuma. Ninaomba sasa muungane na Wizara ya maji katika kuimba wimbo wa Tenzi za Rohoni unaosema, usinipite mwokozi unapozuru wengine. Waheshimiwa Wabunge msitupite Wizara yetu ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**9 MEI, 2024**

## HOTUBA YA WAZIRI WA MAJI MHE. JUMAA HAMIDU AWESO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA MAJI KWA MWAKA 2024/2025 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### 1. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, baada ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, **Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga (Mb)** kuwasilisha taarifa ya Kamati iliyochambua utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Maji ya mwaka 2023/24 na kupokelewa na Bunge lako Tukufu, ninaomba sasa kutoa hoja kwamba, Bunge lako likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2024/25.

2. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutupatia afya njema na kutuwezesha kukutana kwa siku ya leo. Aidha, kwa moyo wa unyenyekevu mkubwa ninamuomba Mwenyezi Mungu atujalie busara, hekima na kutuongoza vema wakati wa kujadili wasilisho la hotuba yangu pamoja na bajeti kuu ya Serikali kwa nia thabiti ya kujenga taifa letu na kuendeleza ustawi wa wananchi wetu.

3. **Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee na dhamira ya dhati ya moyo wangu napenda kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa uongozi imara, madhubuti na wa vitendo aliotuonesha katika kipindi cha miaka mitatu chini ya Serikali yake ya Awamu ya Sita. Mheshimiwa Rais ameonesha uongozi mahiri unaojali shida za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi ili kuhakikisha nchi yetu inasonga mbele katika nyanja mbalimbali za maendeleo.

4. **Mheshimiwa Spika**, katika uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, sote tumeendelea kushuhudia utumishi wenye kujali utu wa watu na kujenga nchi yetu kwa pamoja kupitia falsafa ya *4R* (Maridhiano, Ustahilimivu, Mageuzi na Kujenga upya

Taifa letu) iliyoasisiwa na Mheshimiwa Rais. Aidha, Mheshimiwa Rais ameendelea kuimarisha mahusiano na mashirikiano kati ya nchi yetu na nchi nyingine pamoja na taasisi na jumuiya za kimataifa na hivyo, kung'arisha taswira ya nchi yetu kwenye anga za kimataifa na kufungua fursa mbalimbali za maendeleo. Hakika sote tunapaswa kumshukuru Mheshimiwa Rais na kumuombea kwa Mwenyezi Mungu amjalie afya njema, amzidishie busara na hekima ili aweze kuendelea kutekeleza majukumu yake.

5. **Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine tena naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa kuendelea kuniamini katika nafasi hii ya Waziri wa Maji. Heshima na imani niliyopewa na Mheshimiwa Rais ni kubwa sana, ninaahidi kupitia Bunge lako Tukufu kuwa nitaitumikia nafasi hii kwa uadilifu na uaminifu mkubwa, na kwa uwezo wangu wote ili kuhakikisha matarajio na imani yake kwangu yanafikiwa; na muhimu zaidi ni kuhakikisha huduma ya maji safi, salama na ya kutosheleza inawafikia wananchi wote wa vijijini na mijini.

6. **Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango** kwa kazi kubwa anayoifanya katika kutimiza azma ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuijenga Tanzania kuwa nchi yenye uchumi shindani.

7. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)**, kwa uongozi wake mahiri, ufuatiliaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo na kusimamia kikamilifu uwajibikaji wa viongozi na watumishi mbalimbali serikalini kwa lengo la kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora na wanayostahili. Sote tumekuwa tukishuhudia na kuona namna anavyotekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu akiwa ndani na nje ya Bunge.

8. **Mheshimiwa Spika**, naomba pia kumshukuru Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, **Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb)** kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuwatumikia wananchi. Usimamizi na maelekezo yake yamekuwa ni chachu katika utendaji wa Serikali na maendeleo ya taifa kwa ujumla.

9. **Mheshimiwa Spika**, naomba niwashukuru Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb)** na Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mheshimiwa Mussa Azan Zungu (Mb),** kwa uongozi mahiri wa kuliongoza Bunge letu Tukufu. Aidha, naomba kutoa pongezi kubwa kwa Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Rais wa Muungano wa Mabunge Duniani (IPU) na kutengeneza historia ya kuwa mwanamke wa kwanza kutoka Afrika kuchaguliwa kutumikia nafasi hiyo. Kuchaguliwa kwako kwa nafasi hiyo ya juu na yenye ushawishi mkubwa duniani ni uthibitisho wa kutosha kuhusu umahiri na weledi wako katika kutekeleza majukumu yako na kwa hakika umeijengea heshima kubwa nchi yetu. Vilevile, naomba niwapongeze Wenyeviti wa Bunge, **Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb), Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika (Mb) na Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mb)** kwa kazi nzuri wanazozifanya kwenye Bunge letu Tukufu. Pia, natoa pongezi kubwa kwa wabunge wote kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuwatumikia wananchi na ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu kwenye maeneo yao.

10. **Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa **Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira** kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya sekta ya maji. Kamati imefanya kazi kubwa ya kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2023/24 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2024/25. Maoni na ushauri uliotolewa na Kamati umetusaidia wakati

wa maandalizi ya bajeti ya Wizara yangu. Napenda kuiahidi Kamati kuwa tutaendelea kutoa ushirikiano, kupokea maoni na ushauri wao na kuufanyia kazi kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya maji.

11. **Mheshimiwa Spika**, natoa pole kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi**, Waheshimiwa Wabunge, familia za marehemu pamoja na Watanzania wote kwa vifo vya wapendwa wetu **Hayati Alhaji Ali Hassan Mwinyi**, Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili na **Hayati Edward Ngoyai Lowasa**, Waziri Mkuu Mstaafu. Vilevile, naomba kutoa pole kwako wewe Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu, familia za marehemu, ndugu na wananchi wa majimbo ya Mbarali na Kwahani kwa vifo vya **Mheshimiwa Francis Leonard Mtega** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali na **Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

12. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa pole kwa wananchi wa Wilaya za Hanang', Rufiji, Arusha pamoja na maeneo mbalimbali nchini walioathirika na mafuriko yaliyotokana na mvua za Elinino. Mafuriko hayo yamesababisha madhara makubwa kwa taifa ikiwemo watu kupoteza maisha, majeruhi, uharibifu wa mali na miundombinu ya barabara, umeme, maji na kadhia nyingine mbalimbali. Aidha, niwashukuru wadau wote walioshiriki na wanaoendelea kushirikiana na Serikali katika kutoa misaada mbalimbali ya kusaidia wananchi walioathirika na maafa ya mafuriko hayo.

13. **Mheshimiwa Spika**, naomba pia nichukue fursa hii, kumshukuru Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)** kwa hotuba yake aliyoiwasilisha hapa Bungeni kwa umahiri wa hali ya juu. Hotuba hiyo, imetoa dira na mwelekeo wa utekelezaji wa kazi za Serikali. Vilevile, hotuba hiyo imeelezea mapitio ya uendeshaji wa shughuli za Serikali ya Awamu ya Sita kwa kipindi cha mwaka 2023/24 pamoja na utekelezaji

wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2020 – 2025). Aidha, nawapongeza Mawaziri wenzangu wote walionitangulia kuwasilisha hoja zao na Wabunge waliochangia hoja hizo.

14. **Mheshimiwa Spika**, Mpango na Bajeti ya Wizara yangu umezingatia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26); Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2020 – 2025); Sera na Mikakati ya Maendeleo ya Kitaifa na Kimataifa; Sheria, Kanuni na Miongozo pamoja na maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge na wadau mbalimbali.

15. **Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, napenda sasa kuchukua fursa hii kuwasilisha hotuba ya bajeti ya Wizara yangu yenye sehemu kuu tano (5) kama ifuatavyo:- Hali ya Sekta ya Maji nchini; Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2023/24; Mafanikio yaliyopatikana; Changamoto na Hatua zilizochukuliwa; na Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2024/25.

## 2. HALI YA SEKTA YA MAJI NCHINI

16. **Mheshimiwa Spika**, naomba nichukue fursa hii kuelezea hali ya Sekta ya Maji nchini inayojumuisha hali ya rasilimali za maji, ubora wa maji na upatikanaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira vijijini na mijini kama ifuatavyo:-

### 2.1. Hali ya Rasilimali za Maji

17. **Mheshimiwa Spika**, nchi yetu inakadiriwa kuwa na rasilimali za maji zinazofaa kwa matumizi mbalimbali za wastani wa **mita za ujazo bilioni 126** kwa mwaka. Kiasi hicho kinahusisha maji juu ya ardhi **mita za ujazo bilioni 105** na maji chini ya ardhi **mita za ujazo bilioni 21** kwa mwaka. Kwa idadi ya watu milioni 59.8 wa Tanzania Bara kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, inaonesha kuwa kiasi cha maji kilichopo kwa kila mtu kwa mwaka ni takribani wastani wa **mita za ujazo 2,105**. Kiasi hicho kipo juu ya kiwango cha chini cha mita za ujazo 1,700 cha mahitaji ya maji kwa mtu kwa

mwaka kinachokubalika kimataifa. Hali hiyo, inaonesha kuwa nchi yetu ipo juu ya kiwango cha uhaba wa maji (*water stress*). Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa vyanzo vya maji unaosababishwa na shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii zisizokuwa endelevu, kiwango hicho kinaweza kupungua hadi kufikia mita za ujazo 883 kwa mtu ifikapo mwaka 2035 endapo hatua stahiki hazitachukuliwa. Hivyo, kuna umuhimu wa kuchukua hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kulinda rasilimali za maji.

18. **Mheshimiwa Spika**, takwimu zilizopo zinaonesha kuwa katika mwaka 2023, mahitaji ya maji kwa sekta mbalimbali nchini yalikuwa wastani wa **mita za ujazo bilioni 64**. Inakadiriwa mahitaji hayo yataongezeka hadi kufikia wastani wa **mita za ujazo bilioni 80.2** kwa mwaka ifikapo mwaka 2035. Kwa kuzingatia kiasi cha rasilimali za maji zilizopo, nchi yetu ina kiasi cha kutosha cha rasilimali za maji zinazoweza kukidhi mahitaji ya maji kwa sekta mbalimbali. Hata hivyo, kutokana na mwenendo wa kuongezeka kwa mahitaji ya maji kunakosababishwa na ongezeko la watu pamoja na ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii, Serikali itaendelea kuwekeza katika utunzaji wa vyanzo vya maji, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuboresha ufanisi katika matumizi ya maji kwa lengo la kuepusha nchi yetu kuwa na uhaba wa maji.

19. **Mheshimiwa Spika**, wastani wa kiwango cha mvua nchini katika mwaka wa kihaidrolojia wa Novemba 2022 – Oktoba 2023 ulikuwa **milimita 1200**. Kiwango hicho hutofautiana katika maeneo mbalimbali kutokana na tabia tofauti za hali ya hewa. Maeneo ya nyanda za juu kusini yalipata mvua za wastani wa **milimita 800** hadi **1700**, ukanda wa kaskazini **milimita 600** hadi **1600**, ukanda wa pwani **milimita 650** hadi **1200** na ukanda wa magharibi **milimita 500** hadi **1300**. Vilevile, katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2023 hadi Aprili, 2024 kumekuwa na mvua za El-nino na mvua za masika ambazo zimekuwa juu ya wastani ikilinganishwa na miaka mingine iliyopita. Kutokana na mvua hizo, kwa ujumla hali ya maji katika vyanzo vya maji imekuwa juu ya wastani na

kusababisha mito, mabwawa na maziwa kujaa maji na maeneo mengine kupata mafuriko.

### 2.2. Hali ya Ubora wa Maji

20. **Mheshimiwa Spika**, ubora wa maji katika vyanzo vya maji hutofautiana kulingana na jiografia, tabianchi na mabadiliko ya tabianchi, shughuli za kibinadam na hali ya miamba. Takwimu zinaonesha hali ya ubora wa maji kwenye vyanzo vya maji juu na chini ya ardhi inawezesha ustawi wa ikolojia na hivyo vinaweza kuendelezwa kwa matumizi ya sekta mbalimbali. Pamoja na hali hiyo ya ubora wa maji, bado kunahitajika jitihada za pamoja za kuzuia uchafuzi na pia, kurejesha na kuimarisha ubora wa maji wa asili katika vyanzo vya maji.

21. **Mheshimiwa Spika**, maji yanayosambazwa vijijini na mijini yameendelea kukidhi viwango vya kitaifa vya ubora wa maji ya kunywa hivyo, kulinda afya ya jamii kwa ujumla. Hali hii inatokana na uwekezaji uliofanywa na Serikali kwa kushirikina na wadau mbalimbali katika ujenzi wa miundombinu ya kusafisha na kutibu maji pamoja na usimamizi na udhibiti wa ubora wa maji katika mifumo ya usambazaji maji kuanzia kwenye vyanzo hadi kwa watumiaji.

### 2.3. Hali ya Upatikanaji wa Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini

22. **Mheshimiwa Spika**, Serikali ina azma ya kuhakikisha wananchi wanaoishi maeneo ya vijijini wanapata huduma bora na endelevu ya maji safi na salama kwa zaidi ya **asilimia 85** ifikapo mwaka 2025. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali imeendelea na jitihada za kujenga na kukarabati miradi ya maji pamoja na kupanua mitandao ya kusambaza maji na kuimarisha usimamizi wa huduma ya maji vijijini. Jitihada hizo zimewezesha kuongezeka kwa hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kutoka wastani wa **asilimia 77** mwezi Desemba, 2022 hadi kufikia wastani wa **asilimia 79.6** mwezi Desemba, 2023. Kiwango kilichoongezeka kimetokana na kutekelezwa kwa miradi **632** yenye vituo vya

kuchotea **7,956** vyenye uwezo wa kuhudumia wananchi **4,740,959**. Hali hiyo, inafanya jumla ya wananchi wa vijijini wanaopata huduma ya maji kufikia **34,950,368** kati ya wananchi **39,232,999** waishio vijijini kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022.

23. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa usafi wa mazingira, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Afya imeendelea kutekeleza Kampeni ya Taifa ya Usafi wa Mazingira kwenye maeneo ya vijijini. Kupitia Kampeni hiyo, elimu kuhusu umuhimu wa usafi wa mtu binafsi imeendelea kutolewa na vyoo vya mfano na miundombinu ya kunawia mikono imejengwa kwenye shule na zahanati. Kampeni hiyo imekuwa na matokeo chanya ambapo kwa sasa zaidi ya **asilimia 97** ya wananchi vijijini wanatumia vyoo vya msingi.

### 2.4. Hali ya Upatikanaji wa Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini

24. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imeendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo ya mijini kwa kujenga, kukarabati na kupanua miradi ya maji. Lengo ni kuhakikisha zaidi ya **asilimia 95** ya wakazi wa mijini wanapata huduma ya maji safi na salama ifikapo mwaka 2025. Hadi mwezi Desemba 2023, upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo ya mijini umefikia wastani wa **asilimia 90** ikilinganishwa na wastani wa **asilimia 88** katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Ongezeko hilo limetokana na kukamilika kwa miradi **85** ya maji inayohudumia wakazi **4,641,505** wa maeneo ya mijini.

25. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa huduma ya uondoshaji majitaka, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa miundombinu ya majitaka kwenye maeneo mbalimbali nchini. Hadi mwezi Aprili 2024, mtandao wa majitaka umefikia **kilomita 1,455.93** ikilinganishwa na **kilomita 1,416.9** za mwezi Aprili 2023. Vilevile, idadi ya wateja waliounganishwa katika mtandao imefikia **58,650** kutoka

wateja **56,923** katika kipindi hicho. Kwa maeneo ambayo hayajafikiwa na mtandao wa majitaka, huduma ya uondoshaji majitaka hutolewa na magari maalum ya majitaka ambayo huyapeleka kwenye mabwawa ya majitaka kwa ajili ya kusafishwa na kutibiwa.

## 3. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24

### 3.1. Upatikanaji wa Fedha

26. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2023/24, Fungu 49 – Wizara ya Maji liliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 756,205,106,000.00**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 60,375,474,000.00** zilikuwa ni fedha za matumizi ya kawaida na **Shilingi 695,829,632,000.00** zilikuwa ni fedha za maendeleo. Hadi mwezi Aprili 2024, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 639,485,602,279.06** sawa na **asilimia 84.6** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, **Shilingi 593,398,121,378.53** ni za kutekeleza miradi ya maendeleo na **Shilingi 46,087,480,900.53** ni za matumizi ya kawaida.

#### 3.1.1. Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

27. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2023/24, Wizara ya Maji - Fungu 49 ilitengewa jumla ya Shilingi **60,375,474,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 42,339,913,000.00** ni kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi wa Wizara, RUWASA na Chuo cha Maji na **Shilingi 18,035,561,000.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi mwezi Aprili, 2024 jumla ya **Shilingi 46,087,480,900.53** sawa na **asilimia 76.3 ya** fedha zilizoidhinishwa zimetolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 36,527,791,160.00** ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na **Shilingi 9,559,689,740.53** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

#### 3.1.2. Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

28. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa miradi ya maendeleo, katika mwaka 2023/24, Wizara ya Maji - Fungu 49 ilitengewa

**Shilingi 695,829,632,000.00**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 407,064,860,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 288,764,772,000.00** ni fedha za nje. Hadi mwezi Aprili 2024, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 593,398,121,378.53** sawa na **asilimia 85.3** ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha zilizopokelewa, **Shilingi 356,910,567,637.62** ni fedha za ndani zilizoidhinishwa na **Shilingi 236,487,553,740.91** ni fedha za nje zilizoidhinishwa.

### 3.2. Utekelezaji wa Programu na Miradi Mbalimbali ya Maji

29. **Mheshimiwa Spika**, miradi ya maji inatekelezwa kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ambayo ipo katika Awamu ya Tatu inayotekelezwa kuanzia mwaka 2022/23 hadi 2025/26. Utekelezaji katika mwaka 2023/24 umeainishwa katika maeneo ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji, huduma za ubora wa maji, huduma za usambazaji maji na usafi wa mazingira vijijini na mijini; na kazi mbalimbali zinazotekelezwa katika Taasisi chini ya Wizara pamoja na masuala mtambuka.

#### 3.2.1. Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

30. **Mheshimiwa Spika**, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini unatekelezwa kupitia Bodi za Maji za Mabonde tisa (9) ambazo zimepewa majukumu yakufanya tathmini na ufuatiliaji wa rasilimali hizo; kuhifadhi na kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji; kugawa maji kwa sekta mbalimbali kwa kuzingatia mahitaji na kiasi cha maji kilichopo; na kuendeleza rasilimali za maji.

##### 3.2.1.1. Usimamizi wa Rasilimali za Maji

31. **Mheshimiwa Spika**, usimamizi wa rasilimali za maji unahusisha ujenzi na ukarabati wa vituo vya kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji, udhibiti wa matumizi ya maji na migogoro, udhibiti wa ujenzi na usajili wa mabwawa, udhibiti wa uchimbaji wa visima, ulinzi na uhifadhi wa vyanzo vya maji na kuzuia uchafuzi wa vyanzo. Hadi mwezi Aprili 2024, kazi

zilizotekelezwa katika eneo la usimamizi wa rasilimali za maji ni kama ifuatavyo:-

### (a) Tathmini na Ufuatiliaji wa Rasilimali za Maji

#### *(i) Ujenzi na Ukarabati wa Vituo vya Kufuatilia Mwenendo wa Rasilimali za Maji*

32. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Bodi za Maji za Mabonde imeendelea kufanya ukarabati na kujenga vituo vipya vya kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji ili kuhakikisha takwimu sahihi na za uhakika za rasilimali za maji zinapatikana. Takwimu hizo hutumika katika kufanya maamuzi ya uwekezaji kwenye miradi ya maendeleo inayohusiana na maji ikiwemo miradi ya usambazaji maji, ujenzi wa mabwawa ya kufua umeme na miradi ya umwagiliaji. Hadi mwezi Aprili 2024, vituo **51** vimekarabatiwa na vituo **11** vimejengwa hivyo, kuwa na jumla ya vituo **1,276**. Kati ya vituo hivyo, vituo **187** ni vya kufuatilia mwenendo wa mvua, vituo **129** vya kufuatilia hali ya hewa, vituo **318** vya kufuatilia mtiririko wa maji kwenye mito, vituo **18** vya kufuatilia kina cha maji ya maziwa, vituo **15** vya kufuatilia kina cha maji katika mabwawa, vituo **60** vya kufuatilia kiasi cha mashapo (*sediments*) katika mito, vituo **112** vya kufuatilia mwenendo wa maji chini ya ardhi na vituo **437** vya kufuatilia ubora wa maji. ***Kiambatisho Na. 1*** kinaonesha utekelezaji wa usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji hadi mwezi Aprili, 2024.

#### *(ii) Udhibiti wa Matumizi ya Maji na Migogoro*

33. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kusimamia matumizi bora ya rasilimali za maji na kudhibiti migogoro inayojitokeza kwa kutoa elimu kuhusu sheria na kanuni za usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji pamoja na kuchukua hatua mbalimbali kunapotokea ukiukwaji wa sheria. Aidha, udhibiti huo unalenga kuhakikisha uwepo wa matumizi sawia ya maji kulingana na mahitaji na upatikanaji wa rasilimali hiyo. Hadi mwezi Aprili 2024, Wizara kupitia Bodi za Maji za Mabonde

imetoa vibali vipya **948** kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya maji hivyo, kuwa na jumla ya vibali **13,260** vya matumizi ya maji vilivyotolewa. Takwimu hizo za vibali zinasaidia kujua kiasi cha maji kwa matumizi ya sekta mbalimbali za kiuchumi. Aidha, hadi mwezi Aprili 2024, migogoro **23** kati ya **28** ya matumizi ya maji ilitatuliwa. Migogoro iliyobaki ipo katika hatua mbalimbali za utatuzi.

***(iii) Udhibiti wa Ujenzi na Usajili wa Mabwawa***

34. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kusajili, kudhibiti ujenzi na usalama wa miundombinu ya mabwawa ya maji na mabwawa ya topesumu kwa kutoa vibali vya ujenzi na miongozo ya matumizi na usalama wa mabwawa. Hadi mwezi Aprili 2024, vibali **vinne (4)** vya ujenzi wa mabwawa ya maji vimetolewa na mabwawa **mawili** (**2)** yaliyokidhi vigezo vya usalama wa mabwawa yamesajiliwa. Vilevile, **vibali 9** vya ujenzi wa mabwawa ya topesumu vimetolewa ambapo bwawa **moja (1)** la topesumu limesajiliwa.

***(iv) Udhibiti wa Uchimbaji wa Visima***

35. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kudhibiti uchimbaji na uendelezaji wa visima vya maji kwa kuratibu usajili wa kampuni za utafiti na uchimbaji wa visima pamoja na kutoa leseni na vibali vya uchimbaji ili kuhakikisha rasilimali ya maji chini ya ardhi inatumika kwa usahihi na sawia kulingana na uwepo wake na mahitaji. Hadi mwezi Aprili 2024, jumla ya **leseni 51** za makampuni ya uchimbaji visima, **leseni 78** za wachimbaji na **leseni 7** za utafiti wa maji chini ya ardhi zimetolewa na hivyo, kuwa na jumla ya **leseni 100** za kampuni za uchimbaji **leseni 117** za wachimbaji na leseni **22** za taasisi na makampuni ya utafiti wa maji chini ya ardhi. Aidha, jumla ya vibali **764** vya kuchimba visima vya maji katika maeneo mbalimbali vimetolewa na hivyo, kuwa na jumla ya **vibali 6,836** vya kuchimba visima vilivyotolewa.

36. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Sekta zote zinazohusiana na maji inatekeleza Mpango wa Uhifadhi na Utunzaji wa Vidakio nchini wa mwaka 2021-2035. Kazi

zinazotekelezwa zinahusisha kutambua, kuhifadhi na kulinda vyanzo vya maji ili kuhakikisha vinakuwa endelevu. Hadi mwezi Aprili 2024, jumla ya vyanzo vipya **314** vya maji juu ya ardhi vimetambuliwa na kati ya hivyo, vyanzo **37** vimewekewa mipaka. Kwa ujumla vyanzo vilivyotambuliwa vimefikia **3,296** na kati ya hivyo, vyanzo **327** vimewekewa mipaka na vyanzo **59** vimetangazwa kwenye Gazeti la Serikali kuwa maeneo tengefu.

37. **Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Aprili 2024, kupitia kampeni ya upandaji wa miti rafiki wa maji katika vyanzo vya maji, miti **1,078,197** imepandwa kwenye maeneo mbalimbali nchini na hivyo, jumla ya miti yote iliyopandwa kufikia **3,620,000**. Kampeni hiyo inatekelezwa kwa kuzingatia Azimio la pamoja kuhusu ushirikiano katika utunzaji wa rasilimali za maji unaohusisha Wizara zenye dhamana ya Maji, Mazingira, Kilimo, Nishati, Madini, Ardhi, TAMISEMI, Maliasili na Mifugo.

38. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, katika kuhakikisha jamii inashirikishwa kwenye usimamizi wa rasilimali za maji na kuongeza ufanisi wa usimamizi katika ngazi ya jamii, Wizara imeendelea kuunda na kuzijengea uwezo Jumuiya za Watumia Maji ambapo hadi mwezi Aprili 2024, Jumuiya **saba (7)** zimeundwa na hivyo kuwa na jumla ya Jumuiya za Watumia Maji **199**. Pia, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa utunzaji na uhifadhi wa vyanzo vya maji, madhara ya uharibifu wa vyanzo vya maji, na elimu ya Sheria na Kanuni mbalimbali za usimamizi wa rasilimali za maji.

***(v) Udhibiti wa Uchafuzi wa Vyanzo vya Maji***

39. **Mheshimiwa Spika**, katika kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji, Wizara imeendelea kusimamia shughuli za utiririshaji wa majitaka kwenye mazingira. Hadi mwezi Aprili 2024, **vibali 24** vya kutiririsha majitaka vimetolewa kwa kampuni na taasisi mbalimbali na hivyo, kuwa na jumla ya vibali vya kutiririsha majitaka vilivyotolewa kwenye mabonde yote kufikia **231**.

### *(b) Majukwaa ya Wadau wa Maji*

40. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika usimamizi wa rasilimali za maji kupitia Mipango Shirikishi ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji (*Integrated Water Resources Management and Development Plan - IWRMDP*). Lengo ni kuhakikisha uwepo wa matumizi bora na endelevu ya rasilimali za maji. Hadi mwezi Aprili 2024, jumla ya majukwaa **saba (7)** ya wadau yamefanyika ambapo katika ngazi ya mabonde majukwaa **sita (6)** na ngazi ya Taifa jukwaa **moja (1)**. Vilevile, vikao **viwili (2)** vya vikundi kazi vya Jukwaa la Taifa vimefanyika. Kufanyika kwa majukwaa hayo kumesaidia kuhamasisha wadau kuendelea kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji.

### *(c) Mfumo wa Kielekroniki wa Kusaidia Ufanyaji wa Maamuzi katika Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji*

41. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea na maandalizi ya mfumo wa kielektroniki wa Kusaidia Ufanyaji wa Maamuzi katika Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji (*Operational Decision Support System - ODSS)*. Mfumo huo unahusisha mifumo midogo ya utoaji taarifa za rasilimali za maji *(Water Resources Management Information System)*, vibali vya matumizi ya maji *(Water Use Permit Analysis Tool)*, utabiri wa mafuriko na tahadhari *(Flood Forecasting and Early Warning System),* utabiri wa misimu ya maji katika vyanzo vya maji *(Seasonal and Flow Prediction Tools)* na uendeshaji wa mabwawa ya maji *(Dam Operational Support Tool)*. Hadi mwezi Aprili 2024, Wizara imekamilisha maandalizi ya mifumo midogo ya utabiri wa mafuriko na tahadhari, utabiri wa misimu ya maji katika vyanzo vya maji, uendeshaji wa mabwawa ya maji na mfumo wa utoaji taarifa kwa wadau. Aidha, mtaalam mshauri anaendelea na maandalizi ya mfumo wa vibali vya matumizi ya maji na uhakiki wa mfumo wa utabiri wa mafuriko.

### *(d) Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Majishirikishi*

42. **Mheshimiwa Spika**, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji katika vyanzo vya majishirikishi unalenga kulinda maslahi na kutumia fursa zilizopo kwa manufaa ya nchi wanachama. Tanzania ina vyanzo vya majishirikishi 14 ambavyo ni maziwa ya Victoria, Tanganyika, Nyasa, Natron, Chala na Jipe pamoja na Mito ya Kagera, Mara, Malagarasi, Momba, Mwiruzi, Umba, Ruvuma na Songwe. Ushirikiano na nchi wanachama unahusisha nchi za Burundi, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Uganda, Malawi, Msumbiji na Zambia. Nchi nyingine tunazoshirikiana nazo ni Angola, Botswana, Eritrea, Ethiopia, Misri, Namibia, Sudan, Sudan Kusini na Zimbabwe. Ushirikiano huo hufanyika kupitia Mikataba na Hati za Makubaliano iliyoanzisha taasisi za kikanda na kimataifa ikiwemo Taasisi ya Mpito ya Bonde la Mto Nile, Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria, Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi na Kamisheni ya Bonde la Mto Ruvuma. Katika mwaka 2023/24, utekelezaji wa shughuli za usimamizi na ushirikiano wa rasilimali za majishirikishi ulifanyika kama ifuatavyo:-

#### *(i) Taasisi ya Mpito ya Bonde la Mto Nile*

43. **Mheshimiwa Spika**, katika Bonde la Mto Nile utekelezaji wa mradi wa usimamizi wa maji chini ya ardhi katika mwambamaji *(aquifer)* wa Kagera kati ya Tanzania, Burundi, Rwanda na Uganda unaogharimu **Dola za Marekani 5,329,452** kupitia ufadhili wa Mfuko wa Mazingira *(Global Environmental Facility-GEF)* unaendelea. Hadi mwezi Aprili 2024, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na maandalizi ya mtandao wa kufuatilia mwenendo wa maji chini ya ardhi kupitia mfumo wa *Managed Aquifer Recharge;* kujenga uwezo wa nchi wanachama katika usimamizi wa maji chini ya ardhi; na kuandaliwa kwa mpango kazi wa kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji chini ya ardhi kitaifa na kikanda.

***(ii) Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe***

44. **Mheshimiwa Spika**, kupitia Kamisheni ya Bonde la Mto Songwe, Tanzania na Malawi zinatekeleza Programu ya Maendeleo ya Bonde la Mto Songwe (*Songwe River Basin Development Programme*) inayolenga kutatua changamoto za mafuriko kwa kujenga mabwawa kwenye mto huo. Aidha, mabwawa hayo yatatumika kuzalisha umeme, kilimo cha umwagiliaji pamoja na matumizi mengine. Kwa sasa, hatua inayoendelea ni kutafuta fedha ambapo majadiliano na Benki ya Maendeleo ya Afrika na makampuni ya wawekezaji yanaendelea ikiwa ni pamoja na kuandaa mkataba wa kuuziana umeme *(Power Purchase Agreement)* kati ya Tanzania na Malawi. Vilevile, mradi wa hifadhi ya mazingira katika maeneo ya Ileje (Tanzania) na Chitipa (Malawi), na mradi wa kuimarisha ushirikiano wa pamoja katika usimamizi wa maliasili *(strenghthen transboundary corporation and integrated natural resources management)* unaohusisha kutabiri mafuriko na kutoa taarifa za tahadhari unaendelea ambapo mtandao wa kufuatilia mwenendo wa maji na kufanya utabiri umejengwa.

***(iii) Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria***

45. **Mheshimiwa Spika**, kupitia Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria, Serikali inatekeleza mradi wa ujenzi wa miundombinu ya majitaka katika Jiji la Mwanza chini ya Programu ya Pamoja ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji ya Bonde la Ziwa Victoria. Hadi mwezi Aprili 2024, Serikali imekamilisha usanifu na kuanza taratibu za kumpata mkandarasi wa ujenzi na upanuzi wa mtandao wa majitaka kwa awamu ya kwanza itakayogharimu **Euro 5,300,000**. Vilevile, jumla ya **Euro 45,000,000** zimepatikana kutoka Serikali ya Ujerumani na Umoja wa Ulaya kwa ajili ya kupanua mtandao wa majitaka pamoja na kujenga uwezo wa taasisi. Aidha, maadhimisho ya 12 ya Siku ya Bonde la Mto Mara yaliyofanyika tarehe 12-15 Septemba, 2023 Serengeti, Mkoani Mara yalihusisha Kongamano la Kisayansi kuhusu uhifadhi wa mazingira ya Bonde la Mto huo na

upandaji wa miti rafiki wa maji **10,000** katika Bonde na Bwawa la Manchira.

***(iv) Maandalizi ya Miradi ya Majishirikishi***

46. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha usimamizi wa rasilimali za majishirikishi na ushirikiano, Serikali inashirikiana na nchi wanachama kuandaa miradi mbalimbali ya usimamizi na ushirikiano wa majishirikishi. Hadi mwezi Aprili 2024, kupitia Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Africa *(SADC)*, Tanzania itanufaika na mradi wa uchimbaji visima **vitatu (3)** katika eneo la Nzuguni, Jijini Dodoma utakaogharimu **Dola za Marekani 125,000**.

47. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara imeandaa maandiko ya miradi ifuatayo: mradi wa kusimamia Bonde la Mto Ruvuma *(Strengthening integrated transboundary source-to-sea management of the Ruvuma River Basin and its coastal zones to ensure ecosystem health and livelihood security)* utakaogharimu **Dola za Marekani 7,763,000** kwa ufadhili wa Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi *(Global Environmental Facility - GEF)* utakaotekelezwa kwa kushirikiana na nchi za Msumbiji na Malawi pamoja na mashirika ya *the International Union for Conservation of Nature (IUCN)* na *Global Water Partnership Southern Africa (GWPSA)*; mradi wa kusimamia maji chini ya ardhi katika mwambamaji wa Kilimanjaro *(Unlocking the groundwater potential of the Kilimanjaro Water Tower)* utakaogharimu **Dola za Marekani 8,000,000.00** kwa ufadhili wa *GEF* utakaotekelezwa kwa kushirikiana na nchi ya Kenya pamoja na mashirika ya Food and Agricultural Organization *(FAO)* na *UNESCO*; na mradi wa usimamizi wa Bonde la Mto Zambezi (*Strengthening Zambezi River Basin Management towards Climate Resilience and Ecosystem Health*) utakaogharimu **Dola za Marekani 10,566,750.00** kwa ufadhili wa *GEF* utakaotekelezwa kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika.

*(e) Kituo Mahiri cha Rasilimali za Maji*

48. **Mheshimiwa Spika**, Kituo Mahiri cha Rasilimali za Maji kimeanzishwa kupitia Awamu ya Pili ya Mradi wa Kusaidia Sekta ya Maji unaotekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia. Lengo la kituo hicho ni kuzijengea uwezo Taasisi zinazosimamia rasilimali za maji katika maeneo ya tafiti za kina na ugezi (*callibration*) wa vifaa vya kukusanyia takwimu za rasilimali za maji. Hadi mwezi Aprili 2024, Kituo kimewajengea uwezo Wataalam **102** wa Bodi za Maji za Mabonde na Wizara katika matumizi ya *model* mbalimbali za kubaini na kutambua kiasi cha maji kilichopo katika maeneo yasiyo na mtandao wa kufuatilia mwenendo wa maji mitoni pamoja na kutumia *Remote Sensing* na *GIS* kutambua maeneo ambayo yanapatikana maji chini ya ardhi.

49. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Kituo Mahiri kimeendelea kushirikiana na Chuo kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), *University College of London (UCL), Institute of Development Studies (IDS), University of Sussex (UOS),* na *Cardiff University* kufanya utafiti wa kutambua njia mbadala za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ili kuhakikisha upatikanaji endelevu wa huduma za maji katika maeneo kame ya Mkoa wa Dodoma ikihusisha Wilaya za Chemba, Chamwino, Bahi na Kongwa. Mradi huo unafadhiliwa na *Climate Adaptation and Resilience in Tropical Drylands (CLARITY)* kwa gharama ya **Shilingi 2,464,800,000**.

### 3.2.1.2. Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

*(a) Utafutaji wa Vyanzo vya Maji*

50. **Mheshimiwa Spika**, uendelezaji wa rasilimali za maji unahusisha utafutaji na uendelezaji wa vyanzo vya maji chini na juu ya ardhi ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya kuvuna maji ya mvua kama vile mabwawa; na kufanya utafiti na uchimbaji wa visima virefu nchini. Kwa upande wa maji chini ya ardhi, Serikali imeendelea kufanya utafiti kwa lengo la kutatua changamoto ya maji kwenye maeneo yasiyo na

vyanzo vya uhakika wa maji juu ya ardhi. Utafiti huo husaidia kubainisha maeneo na miamba yenye hifadhi ya maji chini ya ardhi kwa ajili ya kuyaendeleza ambapo hadi sasa jumla ya maeneo 172 yanayodhaniwa kuwa na maji mengi chini ya ardhi yametambuliwa nchini kote. Kwa sasa kazi inayoendelea ni uchimbaji visima 112 vya uchunguzi kwenye mabonde ya Pangani, Wami Ruvu, Rufiji na Bonde la Kati. Hadi mwezi Aprili 2024, uchimbaji wa visima 17 umekamilika na utafiti unaendelea kwenye maeneo yaliyobaki.

**(b) Ujenzi na Ukarabati wa Mabwawa**

***(i) Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Farkwa***

51. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea na utekelezaji wa mradi wa bwawa la Farkwa kwa lengo la kukabiliana na upungufu wa maji katika Jiji la Dodoma pamoja na Wilaya za Chemba, Chamwino na Bahi; kuzuia mafuriko; na shughuli nyingine za kijamii na kiuchumi. Hadi mwezi Aprili 2024, Wataalamu Washauri wamepatikana na wanaendelea na kazi ya mapitio ya usanifu wa bwawa. Aidha, Wizara imeunda timu ya wataalam wa usalama wa mabwawa watakaohakikisha masuala ya usalama wa bwawa katika ngazi zote za utekelezaji wa mradi. Vilevile, kazi ya uandaaji wa mpango wa kulinda na kutunza mazingira katika vyanzo vya maji vitakavyopeleka maji kwenye bwawa inaendelea. Ujenzi wa bwawa unatarajiwa kuanza mwezi Septemba, 2024 baada ya kupatikana kwa mkandarasi.

***(ii) Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Kidunda***

52. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea na ujenzi wa bwawa la Kidunda unaogharimu **Shilingi 329,466,814,886.00**. Ujenzi wa bwawa hilo unalenga kuimarisha utiririshaji wa maji wa Mto Ruvu ili uwe na maji katika kipindi chote cha mwaka kwa ajili ya kulisha mitambo ya kuzalisha maji ya Ruvu Juu na Ruvu Chini; kuzuia mafuriko; kuzalisha umeme Megawati 20; kilimo cha umwagiliaji; na shughuli nyingine za kijamii na kiuchumi zinazotumia maji. Hadi mwezi Aprili 2024, kazi zinazoendelea kutekelezwa ni pamoja na ukarabati wa

barabara yenye urefu wa kilomita 75 kutoka Ngerengere hadi eneo la mradi; ujenzi wa makazi ya wafanyakazi; kuimarisha kingo na tuta la muda la kukinga ujenzi wa *power house* na *spill way*; ujenzi wa barabara za ndani; na usanifu wa mkondo wa umeme kutoka Kidunda kwenda *Chalinze Substation*. Kazi zilizokamilika ni ujenzi wa makazi ya muda ya mkandarasi na ofisi; uchunguzi wa miamba na mtiririko wa maji eneo la ujenzi; ujenzi wa tuta la kukinga eneo la ujenzi wa mchepusho; na ujenzi wa nyumba ya kuzalisha umeme. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 17.9**.

***(c) Ujenzi na Ukarabati wa Mabwawa ya Ukubwa wa Kati na Madogo***

53. **Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na adha ya uhaba wa maji hususan kwenye maeneo kame, Wizara imeendelea na ujenzi wa mabwawa ya ukubwa wa kati na madogo katika maeneo mbalimbali nchini. Hadi mwezi Aprili 2024, Wizara imekamilisha ujenzi na ukarabati wa mabwawa **14**. Mabwawa yaliyokamilika ni Uhelera na Bahimakuru katika Wilaya ya Bahi; Igumangobo na Ilambambasa (Maswa); Ng'walukwa (Shinyanga); Ngofila (Kishapu); Qang'dend (Karatu); na Horohoro na Mbuta (Mkinga); Chole (Kisarawe); Kwamaizi (Handeni); Makame (Kiteto), Enguikumet II (Monduli) na bwawa la Mwadila Wilayani Maswa. Kati ya hayo, mabwawa **mawili (2)** ya Kwamaizi na Makame yamejengwa kwa kutumia seti mpya za ujenzi wa mabwawa zilizonunuliwa na Serikali.

54. **Mheshimiwa Spika**, aidha, ujenzi na ukarabati wa mabwawa **26** unaendelea kwenye maeneo mbalimbali nchini ambapo kati ya hayo, mabwawa **manne (4)** yanajengwa kwa kutumia seti mpya za mitambo ya ujenzi wa mabwawa. Mabwawa hayo ni Kwenkambala katika Wilaya ya Handeni, Kizengi (Kaliua), Lepruko (Monduli) na Kwamjembe (Bagamoyo). Vilevile, seti za mitambo hiyo mipya zinatumika katika ujenzi wa mabwawa madogo **nane (8)** kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kupitia Programu ya *Build Better Tommorow* inayosimamiwa na Wizara ya Kilimo katika Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma.

(d) Uvunaji wa Maji ya Mvua

55. **Mheshimiwa Spika**, uvunaji wa maji ya mvua kupitia mapaa ya majengo ni muhimu, hususan katika kukabiliana na uhaba wa upatikanaji wa maji kwenye maeneo kame. Kutokana na umuhimu huo, Wizara imeandaa Mwongozo wa Uvunaji wa Maji ya Mvua wa Mwaka 2020 mahususi kwa ajili ya kusaidia jamii na taasisi mbalimbali katika kujenga miundombinu bora ya kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua kupitia mapaa ya nyumba. Hadi mwezi Aprili 2024, miundombinu ya kuvuna maji ya mvua imejengwa kwenye shule **760**; hospitali, zahanati na vituo vya afya **(701)**, ofisi za Serikali za vijiji, Halmashauri, masoko, mahakama na ofisi za CBWSOs **(697)** na Taasisi za dini **(255)**. Aidha, Serikali imeendelea kuzihamasisha Taasisi za Kijamii, Asasi na Watu Binafsi kujenga miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua kwenye majengo yao.

### 3.2.2. Huduma za Ubora wa Maji

56. **Mheshimiwa Spika**, ubora wa maji ni kigezo muhimu katika kutoa maamuzi ya matumizi ya maji kwa shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchimi kwa lengo la kulinda afya ya jamii na mifumo ya ikolojia. Huduma za ubora wa maji hutolewa kupitia Maabara 17 za Ubora wa Maji zilizopo katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Tanga, Mtwara, Ruvuma, Iringa, Mbeya, Rukwa, Kigoma, Singida, Dodoma, Manyara, Arusha, Kagera, Mara, Shinyanga na Mwanza. Katika mwaka 2023/24, Wizara ilipanga kuendelea kutekeleza shughuli za usimamizi wa ubora wa maji kwa kuhakiki na kufuatilia ubora wa maji kwenye vyanzo 2,091, skimu 4,600 za usambazaji maji vijijini na mijini na mifumo 150 ya uchakataji majitaka; kuhakiki ubora wa madawa ya kusafisha na kutibu maji kabla ya ununuzi na wakati wa matumizi; na kutoa elimu kuhusu viwango vya ubora wa maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

57. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara ilipanga kuwezesha uandaaji na utekelezaji wa mipango ya usalama wa maji inayohimili mabadiliko ya tabianchi kwa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira **34** na Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamiii **100**; na kuendelea kuboresha utendaji

kazi wa Maabara za Ubora wa Maji kwa kuzipatia vitendea kazi, pamoja na kuwezesha maabara **saba (7)** za ubora wa maji kudumisha hadhi ya ithibati.

***(a) Ubora wa Maji katika Vyanzo***

58. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha vyanzo vya maji vinatumika pasipo kuathiri ikolojia, Wizara imeendelea kuhakiki na kufuatilia ubora wa maji katika vyanzo vya maji juu na chini ya ardhi. Hadi mwezi Aprili 2024, jumla ya vyanzo vya maji **1,625** vilihakikiwa ubora wake ikiwemo visima **(1,501)**, maziwa **manne (4)**, mito (**86**), mabwawa **manne (4**) na chemchemi **(30)**. Matokeo ya uhakiki na ufuatiliaji yanaonesha hali ya ubora wa maji katika vyanzo hivyo inaridhisha na inaendelea kulinda afya ya ikolojia licha ya kuwepo kwa changamoto za uchafuzi katika baadhi ya vyanzo vya maji juu ya ardhi na uwepo wa kiwango kikubwa cha madini ya chumvichumvi kwa vyanzo vya maji chini ya ardhi.

***(b) Ubora wa Maji kwa Matumizi ya Majumbani***

59. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuhakikisha jamii inapata maji safi na salama kwa kuhakiki na kufuatilia ubora wa maji yanayosambazwa na Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs), Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira, Taasisi Binafsi pamoja na vyanzo vya maji vinavyomilikiwa na watu binafsi. Hadi mwezi Aprili 2024, jumla ya **skimu 763** za maji vijijini na **skimu 185** za maji mijini zilifanyiwa uhakiki na ufuatiliaji ambapo jumla ya sampuli za maji **4,461** zilikusanywa na kuhakikiwa ubora wake. Matokeo ya uhakiki yameonesha kuwa sampuli **3,190** sawa na **asilimia 71.5** zilikidhi viwango na sampuli **1,271** sawa na asilimia **28.5** hazikukidhi viwango vya kitaifa vya ubora wa maji ya kunywa. Changamoto kubwa katika skimu za usambazaji maji ni uwepo wa kiasi kikubwa cha madini ya *Fluoride*, Chumvi, Chuma na Manganese pamoja na Tope *(turbidity)* kwa baadhi ya skimu. Katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuchukua hatua za kupunguza madini hayo

kwenye maji. Vilevile, Wizara imeendelea kuzijengea uwezo CBWSOs; Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira pamoja na taasisi na watu binafsi kuhusu namna bora ya kudhibiti na kuboresha ubora na usalama wa maji ili kulinda afya ya jamii ikiwa ni pamoja udhibiti wa magonjwa ya milipuko ikiwemo kipindupindu.

60. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuratibu uwezeshaji wa uandaaji na utekelezaji wa Mipango ya Usalama wa Maji (*Water Safety Plans*) kwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira na Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii ili kuhakikisha ubora wa maji unadhibitiwa kuanzia kwenye vyanzo hadi kwa watumiaji. Hadi mwezi Aprili 2024, Wizara imewezesha kuandaliwa kwa mipango ya usalama wa maji kwa Mamlaka za maji na usafi wa mazingira za Dar es Salaam, Tabora, Dodoma, Musoma, Njombe, Mwanza na Bukoba. Aidha, Wizara imeendelea kusisitiza uzingatiaji wa miongozo na viwango mbalimbali vya usimamizi wa ubora wa maji ya kunywa ikiwa ni pamoja na Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji wa Maji ya Kunywa na Uandaaji wa Taarifa wa Mwaka 2018; Mwongozo wa Kitaifa wa Kusafisha na Kutibu Maji wa Mwaka 2020; na Viwango vya Ubora wa Maji ya Kunywa vya Kitaifa (TZS 789:2018).

***(c) Ubora wa Maji kwa Matumizi Mengineyo***

61. **Mheshimiwa Spika**, ubora wa maji ni kigezo muhimu katika matumizi ya maji kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi. Uhakiki na ufuatiliaji wa ubora wa maji kwa matumizi ya kiuchumi husaidia kutumika kwa maji yenye ubora stahiki na kuwezesha kupatikana kwa matokeo bora kwa kazi iliyotarajiwa hali inayochochea ukuaji wa biashara na uchumi wa nchi kwa ujumla. Hadi mwezi Aprili 2024, Wizara imehakiki na kufuatilia ubora wa maji kwa kukusanya jumla ya sampuli **288** za maji ambapo sampuli **62** ni kwa ajili ya matumizi ya viwandani, ujenzi **(100)**, umwagiliaji **(59)** na sampuli **58** kwa ajili ya shughuli za utafiti. Matokeo yalionesha **asilimia 99** ya sampuli zilikidhi viwango kwa matumizi yaliyokusudiwa na **asilimia 1** ya sampuli hazikukidhi viwango kutokana na uwepo wa kiwango kikubwa cha chumvi katika maji.

***(d) Uhakiki wa Madawa ya Kusafisha na Kutibu Maji***

62. **Mheshimiwa Spika**, katika kuongeza ufanisi wa madawa ya kutibu na kusafisha maji, Serikali imeendelea kuhakiki ubora wa madawa yanayotumika kutibu na kusafisha maji wakati wa ununuzi na kipindi cha matumizi. Hadi mwezi Aprili 2024, jumla ya sampuli **19** za madawa ya kusafisha na kutibu maji yanayotumika kwenye Taasisi mbalimbali yalichunguzwa ubora wake ambapo sampuli **saba (7)** zilikuwa za madawa ya kusafisha maji aina ya *Aluminium Sulphate* (Shabu) na sampuli **12** za madawa ya kutibu maji aina ya *Calcium Hypochlorite*. Matokeo yamebaini kuwa sampuli zote za madawa hayo zilikidhi viwango vinavyokubalika.

***(e) Ubora wa Majitaka Yanayorudishwa Kwenye Mazingira***

63. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuhakiki na kufuatilia ubora wa majitaka katika mifumo ya majitaka ili kuhakikisha majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira yanakidhi viwango vya ubora unaokubalika. Hadi mwezi Aprili 2024, majitaka kutoka mifumo **10** ya kusafisha majitaka ya mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira na mifumo **54** ya kusafisha majitaka ya viwanda na taasisi nyingine yalihakikiwa ubora wake. Matokeo yalionesha majitaka kukidhi viwango vya ubora wa kurudishwa kwenye mazingira kwa **asilimia 42**. Majitaka ambayo hayakukidhi viwango yalitokana na kutokuwepo kwa kiasi cha kutosha cha hewa ya *oxygen*. Mamlaka za maji na viwanda ambavyo majitaka hayakukidhi viwango vya ubora, ushauri wa kitaalam ulitolewa ili kuongeza ufanisi wa mifumo ya kusafisha na kutibu majitaka.

***(f) Uimarishaji wa Maabara za Maji***

64. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuziimarisha maabara za ubora wa maji ili ziweze kutoa huduma bora za ubora wa maji nchini. Hadi mwezi Aprili 2024, Wizara imeziwezesha maabara za ubora wa maji za Dar es Salaam na Mwanza kununua vifaa vya upimaji wa madini tembo pamoja na kufanya matengenezo ya mashine za *Inductive Couple*

*Plasma (ICP) na Atomic Absorption Spectroscopy (AAS)* ambazo zina uwezo wa kupima kwa pamoja na kwa ufanisi viashiria vingi zaidi vya ubora wa maji.

65. **Mheshimiwa Spika**, aidha, ili kuongeza ufanisi katika uchunguzi, Wizara imeziwezesha maabara za ubora wa maji kushiriki mazoezi ya kujipima uwezo yanayoratibiwa na mashirika mbalimbali ya kimataifa yakiwemo SADCMET na BIPEA. Matokeo yameonesha maabara za ubora wa maji kuwa na uwezo wa kupima viashiria mbalimbali vya ubora wa maji kwa usahihi hivyo, majibu kutoka katika maabara hizo kukubalika Kimataifa. Vilevile, Wizara imeziwezesha maabara **saba (7)** za ubora wa maji zenye hadhi ya ithibati ambazo ni Dar es Salaam, Singida, Shinyanga, Mwanza, Musoma, Kigoma na Bukoba kuendelea kudumisha hadhi hiyo.

### 3.2.3. Huduma za Usambazaji Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini

66. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kujenga, kukarabati, kupanua mitandao ya kusambaza maji pamoja na kuimarisha usimamizi wa huduma ya maji katika maeneo ya vijijini. Lengo ni kuhakikisha wananchi waishio vijijini wanapata huduma ya majisafi na salama kwa zaidi ya **asilimia 85** ifikapo mwaka 2025. Kutokana na kukamilika kwa utekelezaji wa miradi mbalimbali, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji vijijini imeongezeka kutoka wastani wa **asilimia 77** mwezi Desemba, 2022 hadi kufikia wastani wa **asilimia 79.6** mwezi Desemba, 2023. Aidha, kwa upande wa usafi wa mazingira, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, imeendelea kubainisha maeneo ya kujenga miundombinu ya kutibu na kusafisha majitaka ambapo hadi sasa Halmashauri za Wilaya za Ludewa, Njombe na Nkasi zimekamilisha Mpango Kabambe wa Maji na Usafi wa Mazingira. Ukamilishaji wa Mpango huo unaendelea katika Wilaya zilizobaki za Mikoa ya Rukwa na Njombe. Maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa shughuli zinahusu huduma ya majisafi na usafi wa mazingira vijijini ni kama ifuatavyo:-

### 3.2.3.1. Utekelezaji wa Baadhi ya Miradi ya maji Vijijini

67. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2023/24, Wizara ilipanga kutekeleza jumla ya miradi **1,546** katika maeneo ya vijijini. Hadi mwezi Aprili, 2024, miradi **632** yenye jumla ya vituo **7,956** imetekelezwa na inatoa huduma kwa wananchi **4,740,959** ***(Kiambatisho Na. 2)***. Aidha, utekelezaji wa miradi **872** unaendelea na ipo kwenye hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mabwawa **18** ya kuvuna maji ya mvua. Maelezo kuhusu utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maji vijijini ni kama ifuatavyo:-

***(a) Mradi wa Maji Ruangwa, Lindi na Nachingwea***

68. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeanza utekelezaji wa mradi wa kutoa maji Mto Nyangao uliopo Wilaya ya Lindi kwenda Wilaya tatu (3) za Lindi, Ruangwa na Nachingwea kwa gharama ya **Shilingi 119,555,923,438.00**. Mradi huo unatekelezwa kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza inahusisha kupeleka maji kwenye vijiji 29 ambapo katika Wilaya ya Ruangwa, vijiji 25; Nachingwea vijiji vitatu (3); na Lindi kijiji kimoja (1).

69. **Mheshimiwa Spika**, kazi zinazotekelezwa katika awamu ya kwanza ya mradi ni ujenzi wa chanzo cha maji, ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji ya umbali wa kilomita 211, ujenzi wa mfumo wa kutibu maji, ujenzi wa vituo viwili vya kusukuma maji, ujenzi wa matanki sita (6) ya kuhifadhi maji yenye jumla ya lita 4,750,000, ujenzi wa nyumba tatu (3) za watumishi na Ofisi ya CBWSO. Hadi mwezi Aprili, 2024 utekelezaji umefikia **asilimia 18** na unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2024. Awamu ya pili ya mradi inahusisha ujenzi wa tanki la kukusanyia maji lenye ujazo wa lita 50,000, ujenzi wa tanki la kuhifadhi maji lenye ujazo wa lita 100,000, ujenzi wa vituo 30 vya kuchotea maji na ulazaji wa mabomba yenye urefu wa kilomita 105. Utekelezaji wa awamu hiyo utaanza baada ya kukamilika kwa awamu ya kwanza. Mradi utakapokamilika utawanufaisha wananchi wapatao 130,000 wa vijiji 56 ambapo katika Wilaya ya Ruangwa vijiji 34; Wilaya ya Nachingwea vijiji 21 na Wilaya ya Lindi kijiji kimoja (1).

***(b) Mradi wa Maji Mkinga – Horohoro***

70. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutekeleza mradi wa maji Mkinga – Horohoro kwa gharama ya **Shilingi 35,899,392,562.00**. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na ujenzi wa matanki nane (8) yenye ujazo wa lita milioni 1.29; ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa kilomita 196; ujenzi wa vituo 60 vya kuchotea maji na ofisi ya CBWSO. Hadi mwezi Aprili, 2024, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 36** na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2024. Kukamilika kwa mradi huo kutawanufaisha wananchi 74,795 wa Mji wa Horohoro na vijiji 37 vya Wilaya ya Mkinga.

***(c) Mradi wa Maji Diburuma - Songe***

71. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeanza utekelezaji wa mradi wa maji Diburuma - Songe uliopo Wilaya ya Kilindi Mkoa wa Tanga kwa kutumia chanzo cha maji cha Mto Diburuma kwa gharama ya **Shilingi 22,956,445,680.00**. Mradi huo unahusisha ujenzi wa matanki 11 yenye jumla ya ujazo wa lita milioni 2.2; ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa kilomita 155.7; ujenzi wa mtambo wa kutibu maji; ununuzi na ufungaji wa pampu mbili zenye uwezo wa kuzalisha maji lita 48,000 kwa saa; ujenzi wa vituo 60 vya kuchotea maji na ofisi ya CBWSO. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2025 na kuwanufaisha wananchi 75,224 waishio kwenye Vijiji 24 vya Kikunde, Mafulila, Tunguli, Msamvu, Mtoro, Lusane, Kitingi, Mapanga, Ngeze, Kwekivu, Lusimbi, Mheza, Misheni, Sambu, Kigunga, Kwamba, Mvungwe, Vilindwa, Songe, Bokwa, Nkama, Kwastemba, Kwamwande na Masigalu katika Wilaya ya Kilindi.

**(d) Mradi wa Maji Morong'anya - Morogoro Vijijini**

72. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea kutekeleza mradi wa maji Morong'anya wilayani Morogoro kwa gharama ya **Shilingi 23,186,021,991.00**. Mradi utahudumia vijiji 19 vya Kalundwa, Kibwaya, Tandai, Mkuyuni, Madamu, Luholela, Mwarazi, Kivuma, Kungwe, Kikundi, Lukonde, Vuleni, Lubungo, Muhunga - Mkola, Newland, Kibuko, Maseyu, Kinonko na

Gwata. Kazi zinazotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa banio la maji, mtambo wa kusafisha na kutibu maji, matanki 12 yenye jumla ya ujazo wa lita milioni 1.84, vituo 100 vya kuchotea maji na Ofisi ya CBWSO; na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa kilomita 117. Hadi mwezi Aprili 2024, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 80** na umeanza kutoa huduma kwenye vijiji 10. Mradi unatarajiwa kukamilika Mwezi Juni, 2024 na kunufaisha wananchi wapatao 52,000.

***(e) Mradi wa Maji Ukiliguru, Sumve hadi Koromije***

73. **Mheshimiwa spika**, Wizara inaendelea kutekeleza mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda Miji ya Usagara, Ukiliguru, Sumve hadi Koromije na vijiji 24 vya Wilaya za Misungwi na Kwimba kwa gharama ya **Shilingi 32,756,175,561.00**. Mradi huo unahusisha ujenzi wa chanzo cha maji, matanki sita (6) yenye jumla ya ujazo wa lita milioni 5.63, mtambo wa kusafisha na kutibu maji, vituo 80 vya kuchotea maji, jengo la pampu, nyumba moja (1) ya watumishi na ofisi mbili (2) za CBWSO; ununuzi na ufungaji wa pampu; na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa kilomita 261.1. Hadi mwezi Aprili, 2024 utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 30** na unatarajiwa kukamilika mwezi machi, 2025 na kuwanufaisha wananchi 162,377.

***(f) Mradi wa Maji Ilujamate - Buhingo***

74. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeanza kutekeleza mradi wa maji Ilujamate - Buhingo unaotoa maji Ziwa Victoria kwenda vijiji 16 vya Gukwa, Mbalama, Buhunda, Mwagimagi, Kifune, Gulumungu, Lukanga, Nyambiti, Busongo, Ng'hamve, Nyamayinza, Songiwe, Seeke, Buhingo, Kabale na Mwasagela kwa gharama ya **Shilingi 2,469,397,202.00**. Mradi huo unahusisha ujenzi wa matanki **matatu** (3) yenye jumla ya ujazo wa lita 800,000, vituo 50 vya kuchotea maji na ofisi moja (1) ya CBWSO; ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa kilomita 97.43. Hadi mwezi Aprili 2024, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 20** na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2024 na kuwanufaisha wananchi wapatao 61,088.

***(g) Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria kutoka Kahama kwenda Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu***

75. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imekamilisha maandalizi kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maji Ushetu kwa gharama ya **Shilingi 44,271,886,678.17**. Mradi huo utachukua maji kutoka bomba kuu la Kahama - Shinyanga na kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa kilomita 164.6; ujenzi wa matanki matatu (3) yenye jumla ya ujazo wa lita 900,000, vituo 35 vya kuchotea maji na ofisi ya CWBSO; na kuunganisha wateja wa majumbani wapatao 1,000. Kwa sasa mradi upo kwenye hatua za kumuajiri mkandarasi na utekelezaji unatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi Mei, 2024 na kukamilika ndani ya Miezi 24. Kukamilika kwa mradi huo kutanufaisha wananchi 234,455 waishio kwenye Vijiji 54 vya Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu.

***(h) Mradi wa Matumizi ya Dira za Maji za Malipo ya Kabla***

76. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia RUWASA kwa kushirikiana na Chuo cha Ufundi Arusha (ATC), Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), na Dar Teknohama Business Incubator - (DTBi) chini ya Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH) inatekeleza mradi wa kubuni, kuunda na kufunga dira za maji za malipo kabla ya matumizi katika skimu za maji vijijini ili kudhibiti upotevu wa maji pamoja na mapato ya mauzo ya maji. Kupitia mradi huo, jumla ya dira 300 zinazoendana na mazingira ya vijijini zitabuniwa na kuundwa. Hadi mwezi Aprili 2024, jumla ya dira 150 zimeundwa na kufungwa kwa majaribio kwenye skimu mbalimbali za maji na kuonesha ufanisi katika ufanyaji kazi.

**3.2.3.2. Programu ya Uendelevu wa Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini**

77. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Dunia inatekeleza Programu ya Uendelevu wa Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Awali, Programu hiyo ililenga kuongeza na kuboresha upatikanaji wa huduma ya

maji na usafi wa mazingira kwenye Halmashauri za Wilaya **86** katika mikoa **17** na kujenga uwezo kwa taasisi zinazosimamia huduma ya maji vijijini. Programu ilipangwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia 2019/20 - 2024/25 na ilipangwa kunufaisha wananchi **milioni 3**. Gharama za utekelezaji wa programu hiyo zilikuwa ni **Dola za Marekani milioni 350** na utekelezaji unafanyika kwa utaratibu wa Malipo kwa Matokeo, yaani *Program for Results* almaarufu *PforR*.

78. **Mheshimiwa Spika**, kupitia programu hiyo, jumla ya miradi **540** imetekelezwa hadi sasa yenye vituo vya kuchotea maji **4,569** na kunufaisha wananchi wapatao **milioni 4.1** katika vijiji **1,118**. Matokeo hayo, yamevuka lengo la awali la kuhudumia wananchi **milioni 3** na hivyo, katika Mkutano wa Mawaziri wa Maji na Fedha wa Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika uliofanyika Addis Ababa nchini Ethiopia mwezi Novemba 2023, Benki ya Dunia iliitambua Tanzania kuwa kinara katika utekelezaji wa Programu hiyo. Kutokana na mafanikio hayo, Tanzania imeongezewa fedha za Programu kutoka **Dola za Marekani milioni 350** hadi **Dola za Marekani milioni 654** na kuongeza mikoa inayonufaika kutoka **17** hadi **25** na kutoka Halmashauri **86** hadi **137**.

### 3.2.3.3. Matumizi ya Teknolojia ya Nishati Jadidifu *(Renewable Energy)*

79. **Mheshimiwa Spika**, katika kupunguza gharama za uendeshaji ili kufikia lengo la kuwa na huduma endelevu ya maji vijijini, Wizara kupitia RUWASA kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, REA pamoja Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB) inatekeleza mradi wa kupunguza au kuondoa matumizi ya nishati ya dizeli ("*Accellerating Solar Water Pumping Via Innovative Financing - ASWPIF*). Mradi huo utatekelezwa kwenye skimu 332 za maji vijijini. Jumla ya skimu 100 zimepangwa kubadilishwa kutoka kutumia nishati ya dizeli na kufungiwa mifumo ya umeme jua katika Mikoa ya Dodoma (47), Singida (25), Shinyanga (12) na Mtwara (16). Hadi mwezi Aprili 2024, jumla ya skimu **65** zimebadilishiwa mifumo ya dizeli na kuwekewa mifumo inayowezesha matumizi ya umeme wa gridi pamoja na

umeme jua katika mikoa ya Dodoma **(25)**, Singida **(17)**, Shinyanga **(11)** na Mtwara **(12)**.

**3.2.3.4. Uimarishaji wa Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii**

80. **Mheshimiwa Spika**, Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (*Community Based Water Supply Organizations - CBWSOs*) vina jukumu la kuhakikisha uendelevu wa miradi ya maji vijijini kwa kuendesha na kufanya matengenezo madogo ya skimu za maji. Kwa kutambua umuhimu wa vyombo hivyo, pamoja na kupunguza gharama za uendeshaji wa skimu, Serikali imeendelea kuunda, kusajili, kuunganisha na kuzijengea uwezo CBWSOs zilizopo. Hadi mwezi Aprili, 2024, Wizara kupitia RUWASA imeunda na kusajili CBWSOs **100** na kuunganisha CBWSOs **517** hivyo, kufanya jumla ya idadi ya CBWSO zilizosajiliwa kuwa **1,382**. Katika kuimarisha utendaji kwenye vyombo hivyo, CBWSOs zimeajiri wataalam **5,342** katika kada za ufundi, uhasibu pamoja na kada saidizi. Uwepo wa wataalam hao umeboresha hali ya uendeshaji na utoaji wa huduma ya maji vijijini.

81. **Mheshimiwa Spika**, RUWASA iliwezesha CBWSOs **136** kuandaa Vitabu vya Hesabu (*Financial Statements*) za mwaka 2022/2023 na kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*). Ripoti ya *CAG* imeonesha kati ya CBWSOs zilizokaguliwa, **133** sawa na **asilimia 98** zimepata hati safi. Vilevile, katika kuimarisha udhibiti wa mapato ya fedha za umma, RUWASA imeziwezesha CBWSOs **661** katika mikoa **16** kujiunga katika Mfumo wa *GePG* na kuanza kukusanya mapato ya mauzo ya maji kupitia mfumo huo.

**3.2.3.5. Mitambo ya Uchimbaji wa Visima na Mabwawa**

82. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeandaa Mwongozo wa Matumizi ya Mitambo 25 ya Uchimbaji Visima na Seti 5 za Mitambo ya Ujenzi wa Mbawawa ili mitambo hiyo itumike ipasavyo na kuleta tija iliyokusudiwa. Mwongozo huo unaainisha namna bora ya matumizi ya mitambo ikiwemo

utaratibu wa muda wa ufanyaji kazi, muda wa matengenezo kinga na matengenezo makubwa ya mitambo.

83. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2023/24, Wizara imekamilisha uchimbaji wa visima **289** kwenye maeneo mbalimbali ya vijijini. Kati ya hivyo, visima **283** vimechimbwa kwa kutumia seti za mitambo mipya na visima **sita (6**) vimechimbwa na mitambo mingine ikiwemo kampuni binafsi.

84. **Mheshimiwa Spika**, aidha, Wizara imefanya tathimini na kuandaa mpango wa kufikisha huduma ya maji kwenye maeneo ambayo hayana huduma hiyo. Kupitia mpango huo, Serikali imepanga kuchimba visima vitano (5) katika kila jimbo la uchaguzi kwenye maeneo ya vijijini katika mikoa yote 25 ya Tanzania Bara ambapo jumla ya visima **900** vyenye gharama ya **Shilingi 58,800,000,000** vinatarajiwa kuchimbwa. Hadi sasa kazi ya uchimbaji visima imeanza katika mikoa ya Kigoma na Songwe na utafiti unaendelea kwenye mikoa mingine. Aidha, kipaumbele cha mpango huo kitatolewa kwenye maeneo ambayo hayajafikiwa na huduma na hakuna mradi wowote unaondelea.

### 3.2.4. Huduma za Usambazaji wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini

85. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo imeendelea kujenga, kukarabati na kupanua miundombinu ya majisafi na majitaka katika maeneo ya mijini kwa lengo la kuimarisha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji na usafi wa mazingira kwa wakazi wote waishio mijini. Katika mwaka 2023/24, jumla ya miradi 244 ilipangwa kutekelezwa ambapo hadi mwezi Aprili 2024, miradi **85** imekamilika ***(Kiambatisho Na. 3)*** na miradi **159** inaendelea na ipo kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji. Utekelezaji wa baadhi ya miradi ya usambazaji maji na usafi wa mazingira katika Miji Mikuu ya Mikoa, Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo, na Miradi ya Kitaifa ni kama ifuatavyo:-

### 3.2.4.1. Miradi ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Miji Mikuu ya Mikoa

#### *(a) Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Jiji la Mbeya*

86. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea na utekelezaji wa mradi wa majisafi katika Jiji la Mbeya kwa kutumia chanzo cha Mto Kiwira kwa gharama ya **Shilingi 99,659,532,284.92**. Mradi huo unalenga kuongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 66.5 kwa siku hadi lita milioni 184 kwa siku pamoja na kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Jiji la Mbeya. Hadi mwezi Aprili 2024, ujenzi wa banio na tanki la kuhifadhi maji lenye ujazo wa lita milioni 5 unaendelea na utekelezaji umefikia **asilimia 11**. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Machi, 2025 na kuwanufanisha wakazi wapatao 1,452,751.

87. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara inatekeleza kipande cha kwanza na cha pili cha mradi wa kuboresha huduma ya majisafi katika Kata za Mwansekwa na Iganzo kwa gharama ya **Shilingi 5,200,000,000**. Utekelezaji wa kipande cha kwanza umefikia **asilimia 90** na kazi zinazotekelezwa zinahusisha ujenzi wa chujio la maji na ujenzi wa tanki la lita milioni 2. Utekelezaji wa kipande cha pili umefikia **asilimia 76** na kazi zinazotekelezwa ni ujenzi wa banio katika vyanzo vya Hanzya na Hasara pamoja na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa kilomita 15.8 ambapo kilomita 7.8 zimelazwa. Mradi umeanza kuzalisha maji **lita milioni 2** kwa siku na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024 na utawanufaisha wakazi wapatao 42,000 wa kata za Mwansekwa na Iganzo.

#### *(b) Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Mji wa Geita na Maeneo ya Pembezoni*

88. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imekamilisha utekelezaji wa mradi wa maji Katoro - Buseresere uliogharimu **Shilingi 1,300,315,203**. Kazi zilizotekelezwa ni ununuzi na ulazaji wa mabomba katika njia kuu ya kusafirisha maji umbali wa kilomita 5, ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa kilomita 35 na uunganishaji wa wateja wapya **850**. Mradi

huo unahudumia wakazi wapatao **1,200** wa maeneo ya Katoro na Buseresere.

89. **Mheshimiwa Spika**, aidha, Wizara inaendelea na utekelezaji wa mradi wa upanuzi wa mtambo wa kusafisha na kutibu maji Nyankanga kwa gharama ya **Shilingi 1,100,000,000**. Hadi mwezi Aprili 2024, kazi zilizotekelezwa ni ujenzi wa tanki la maji la lita 100,000; ujenzi wa nyumba ya pampu; ujenzi wa miundombinu ya kutibu maji; na ununuzi na ufungaji wa pampu mbili (2) zenye uwezo wa kuzalisha maji lita 150,000 kwa saa. Kazi iliyobaki ni ununuzi na ufungaji wa pampu yenye uwezo wa kuzalisha maji lita 300,000 kwa saa. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 95** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024. Mradi utakapokamilika utawanufaisha wakazi wapatao 3,000 wa Nyankanga.

90. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara imekamilisha mradi wa upanuzi wa mtandao wa maji katika Mji wa Geita kwa gharama ya **Shilingi 613,822,621.50**. Mradi unatoa huduma ya maji kwa wakazi wapato **3,000** wa Mji wa Geita. Kazi zilizotekelezwa ni ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji yenye umbali wa kilomita 45; ununuzi wa pikipiki 15; ununuzi wa mabomba yenye jumla ya urefu wa kilomita 10 kwa ajili ya maunganisho ya wateja; na ufungaji wa jenereta la ofisi.

***(c) Mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Jiji la Arusha***

91. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imekamilisha utekelezaji wa mradi wa majisafi na usafi wa Mazingira katika Jiji la Arusha kwa gharama ya **Dola za Marekani 233,915,581**. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na uchimbaji wa visima **56**; ujenzi wa mabwawa mapya **18** ya kutibu majitaka; upanuzi na ukarabati wa miundombinu na mifumo ya majisafi na majitaka maeneo ya katikati ya Jiji; ujenzi wa vyoo **42** vya mfano vyenye jumla ya matundu **184**; ujenzi wa mtandao mpya wa majitaka umbali wa kilomita **180.503**; ujenzi wa mitambo ya kusafisha maji; ujenzi wa ofisi **tatu (3)** za kanda, Karakana na Bohari katika eneo la Safari *City*; ujenzi wa mtambo wa kusafisha na kutibu maji; ujenzi wa ofisi kuu; na

upanuzi wa mtandao wa majitaka nje ya maeneo ya katikati ya Jiji; ufungaji wa mfumo wa mawasiliano; ujenzi wa matanki; na ujenzi wa mfumo wa kuchanganya maji (*blending*). Kwa sasa mradi upo katika muda wa matazamio. Kukamilika kwa mradi kumeongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 40** kwa siku hadi **lita milioni 200** kwa siku; muda wa upatikanaji wa huduma ya majisafi kutoka **saa 12** za sasa hadi **saa 24** kwa siku; huduma ya uondoaji wa majitaka kutoka **asilimia 7.6** za sasa hadi **asilimia 30**; kupunguza upotevu wa maji kutoka **asilimia 48** hadi **asilimia 39**; na kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama.

92. **Mheshimiwa Spika**, aidha, Wizara inaendelea na ujenzi wa mradi wa majisafi Oldonyosambu kwa gharama ya **Shilingi 6,382,532,295.20**. Hadi mwezi Aprili 2024, kazi zilizotekelezwa ni ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa kilomita 21.6 kati ya kilomita 37.34 zilizopangwa; ujenzi wa vituo viwili (2) vya kusukuma maji; ujenzi wa tanki la lita 350,000 kati ya matanki matatu (3) yenye lita 575,000; na ujenzi wa vituo 15 vya kuchotea maji. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 47** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2025. Mradi utakapokamilika utawanufaisha wakazi wapato 29,449 wa Oldonyosambu.

93. **Mheshimiwa Spika**, pia, Wizara inatekeleza ujenzi wa mradi wa majisafi Mageri - Ngorongoro kwa gharama ya **Shilingi 6,105,995,066.21**. Hadi mwezi Aprili 2024, kazi zilizotekelezwa ni ujenzi wa chanzo, ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa kilomita 6 kati ya kilomita **28** zilizopangwa, ujenzi wa matanki 17 ya kupunguza msukumo wa maji, ujenzi wa matanki sita (6) yenye jumla ya lita 975,000 na ujenzi wa vituo 64 vya kuchotea maji. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 52** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2025. Mradi utakapokamilika utawanufaisha wakazi wapatao 33,969 wa Mageri - Ngorongoro.

***(d) Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Jiji la Tanga na Maeneo ya Pembezoni***

94. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea na awamu ya pili ya ujenzi pamoja na uboreshaji wa mradi wa maji katika maeneo ya Mabokweni - Kibafuta, Chongoleani na Mleni unaogharimu **Shilingi 516,551,200**. Mradi huo unahusisha ununuzi na ulazaji wa mabomba umbali wa kilomita 11.7, ununuzi na ufungaji wa pampu, ujenzi wa chemba 33, ujenzi wa nguzo za alama 147 na ujenzi wa vituo 10 vya kuchotea maji. Hadi mwezi Aprili 2024, kazi zilizotekelezwa ni ununuzi na ulazaji wa mabomba umbali wa kilomita 9.2; ununuzi wa pampu; na ujenzi wa chemba tatu (3). Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 75** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024. Kukamilika kwa mradi huo, kutawanufaisha wakazi wapatao 15,000 wa maeneo ya Mabokweni, Kibafuta, Chongoleani na Mleni.

95. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea na uboreshaji wa mfumo wa maji katika Mji wa Pangani kwa gharama ya **Shilingi 1,000,000,000**. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni uchimbaji wa kisima kirefu; ununuzi na ulazaji wa mabomba umbali wa kilomita 15; ununuzi na ufungaji wa pampu; ujenzi wa chemba; na ujenzi wa nguzo za alama. Hadi mwezi Aprili 2024, kazi zilizotekelezwa ni ununuzi na ulazaji wa mabomba umbali wa kilomita 10.5; na uchimbaji wa kisima kirefu. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 50** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024. Kukamilika kwa mradi huo, kutawanufaisha wakazi wapatao 16,000 wa Mji wa Pangani.

96. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea na utekelezaji wa mradi wa uboreshaji wa mfumo wa maji katika Mji wa Muheza kwa gharama ya **Shilingi 700,000,000**. Mradi huo unahusisha ununuzi na ulazaji wa mabomba umbali wa kilomita 7.5; ujenzi wa chemba 32; ujenzi wa *anchor block* 20; na ujenzi wa nguzo za alama 182. Hadi mwezi Aprili 2024, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na ununuzi na ulazaji wa mabomba umbali wa kilomita 7.47; na ujenzi wa nguzo za alama 182. utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 90 na** unatarajiwa

kukamilika mwezi Juni, 2024. Kukamilika kwa mradi huo kutawanufaisha wakazi wapatao 14,160 wa Mji wa Muheza.

***(e) Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Mkoa wa Dar es Salaam na Miji ya Kibaha, Kisarawe, Mkuranga, Chalinze na Bagamoyo katika Mkoa wa Pwani***

97. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imekamilisha kipande cha kwanza na cha pili cha mradi wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji kutoka katika visima virefu vya Kimbiji kwa gharama ya **Shilingi 21,278,706,991**. Kukamilika kwa mradi kumeimarisha hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa wakazi wapatao **250,000** wa Chanika, Luzando, Mpera, Chamazi, Kitunda, Kinyerezi, Temeke, Kisarawe, Kibada, Kimbiji, Kigamboni, Tuangoma, Mkuranga, Kongowe, Mbagala, Kurasini, Mtoni, Keko na Chang'ombe. Kazi zilizotekelezwa ni ujenzi wa tanki la **lita milioni 15** katika eneo la Kisarawe II; ujenzi wa kituo cha kusukuma maji katika eneo la Kimbiji; ulazaji wa bomba kuu umbali wa **kilomita 6.9** kutoka Kibada hadi Maweni kwa Mwingira; ulazaji wa bomba la kusafirisha maji umbali wa **kilomita 8** kutoka Kibada kupitia Daraja la Nyerere hadi bomba la kusambaza maji katika Jiji la Dar es Salaam; ulazaji wa bomba umbali wa **kilomita 6.3** kutoka kwenye visima kupeleka maji kwenye tanki; ufungaji wa pampu **10**; na ulazaji wa bomba la kusafirisha maji umbali wa **kilomita 15.8** kutoka kwenye visima hadi kwenye kituo cha kusukuma maji.

98. **Mheshimiwa Spika**, pia, Wizara inaendelea kutekeleza kipande cha tatu cha mradi kinachohusu ujenzi wa mfumo wa mabomba ya maji Kimbiji – Kigamboni kutoka kwenye tanki la Kimbiji kwa gharama ya **Shilingi 8,000,000,000**. Hadi mwezi Aprili 2024, kazi zilizotekelezwa ni ulazaji wa mabomba umbali wa kilomita 44 kati ya kilomita 65 zilizopangwa. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 75** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2024.

99. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeanza kutekeleza mradi wa ujenzi wa mtandao wa usambazaji maji na matanki ya kuhifadhi maji Kusini mwa Dar es Salaam kwa gharama ya

**Shilingi 35,149,404,125**. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa kituo cha kusukuma maji; ujenzi wa tanki la kukusanyia maji la lita 500,000; ulazaji wa bomba kuu la chuma umbali wa kilomita 10.8; ulazaji wa bomba za kusambaza maji umbali wa kilomita 108.15; na ujezi wa tanki la lita milioni 9. Hadi mwezi Aprili 2024, kazi zilizotekelezwa ni ulazaji wa bomba kuu umbali wa kilomita 1.164 na ujenzi wa tanki la lita milioni 9. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 19** na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba 2024. Mradi unatarajiwa kunufaisha wakazi wapatao 450,000 wa maeneo ya Bangulo, Mwanagati, Kitunda, Kipunguni, Majohe, Kivule, Magole, Msongola, Chanika na Chalambe.

100. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara inatekeleza kipande cha kwanza na cha pili cha mradi wa usambazaji maji katika maeneo yaliyo nje ya mtandao kwa gharama ya **Shilingi 22,079,079,033** na unatarajiwa kuwanufaisha wakazi wapatao 215,380. Hadi mwezi Aprili 2024, kazi zilizotekelezwa ni ujenzi wa mtandao wa usambazaji maji umbali wa kilomita 138.414 kati ya kilomita 138.446 zilizopangwa na utahudumia vitongoji 13 vya Kisewe, Magengeni, Dovya, Mwembebamia, Mianzini, Mwanamtoti, Butiama, Mgeule, Mgeule Juu, Upendo, Tungi, Magogoni na Ferry vilivyopo Kigamboni na Temeke; ujenzi wa mtandao wa usambazaji maji umbali wa kilomita 69.278 ambao utahudumia vitongoji sita (6) vya Nzasa A, Somelo, Kifurukwe, Kichangani, Yangeyange na Vumba vilivyopo Kigamboni na Ilala; na ujenzi wa tanki la lita milioni 2 katika eneo la Somelo. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 96** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2024.

#### *(f) Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Jiji la Mwanza na Maeneo ya Pembezoni*

101. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (*European Investment Bank-EIB*) pamoja na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*French Development Agency-AFD*) imekamilisha utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa chujio la Butimba kwa gharama ya **Euro 31,172,568.93**. Kukamilika kwa mradi huo kumeboresha hali ya upatikanaji

wa huduma ya maji kwa wakazi wapatao **450,000** katika Jiji la Mwanza.

102. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara inatekeleza mradi wa kuongeza mfumo wa usambazaji wa maji katika miji ya Magu na Misungwi kwa gharama ya **Shilingi 1,939,814,086.65**. Hadi mwezi Aprili 2024, kazi zinazoendelea kutekelezwa ni ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa kilomita 85.94 ambapo kilomita 40.24 zimelazwa; ujenzi wa vituo 10 vya kuchotea maji; ujenzi wa kituo cha kusukuma maji; ujenzi wa tanki la kukusanyia maji la lita 50,000; ujenzi wa matanki mawili (2) yenye uwezo wa lita 240,000; na ujenzi wa njia ya mfumo wa umeme. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 70** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024 na kunufaisha wakazi wapatao 33,000 wa miji ya Magu na Misungwi.

103. **Mheshimiwa Spika**, pia, Wizara inatekeleza mradi wa kuboresha mfumo wa usambazaji maji katika Jiji la Mwanza kwa gharama ya **Shilingi 4,624,246,101.32**. Hadi mwezi Aprili 2024, kazi zilizotekelezwa ni ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa kilomita 54.5 kati ya kilomita 71.3 zilizopangwa; na ujenzi wa chemba za valvu 40. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 70** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024 na utawanufaisha wakazi wapatao 33,000. Vilevile, Wizara inatekeleza mradi wa kuboresha mfumo wa usambazaji maji kwa gharama ya **Shilingi 405,640,707.20**. Kazi zinazoendelea kutekelezwa ni ulazaji wa bomba za kusambaza maji umbali wa kilomita 10.85 kati ya kilomita 18.263 zilizopangwa; ujenzi wa vituo 14 vya kuchotea maji; ujenzi wa chemba za valvu 9; na ujenzi wa ofisi ya mlinzi. Hadi mwezi Aprili 2024, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 70** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024 na kuwanufaisha wakazi wapatao 12,000 wa Mwanza.

***(g) Upanuzi wa Huduma ya Maji kupitia Mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Lindi***

104. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea na utekelezaji wa mradi wa usambazaji maji kutoka Lindi Mjini hadi Mchinga

unaogharimu **Shilingi 12,419,342,808.31**. Hadi mwezi Aprili 2024, kazi zilizotekelezwa ni uchimbaji wa visima vitatu (3); ujenzi wa vioski 20; ulazaji wa mabomba katika njia kuu umbali wa kilomita 30 na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa kilomita 80. Kazi zinazoendelea ni ujenzi wa tanki la lita 680,000; ujenzi wa uzio kuzunguka tanki; na ujenzi wa nyumba ya mlinzi. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 95** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024 na kuwanufaisha wakazi wapatao 40,000 wa maeneo ya Mchinga.

105. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara inaendelea kutekeleza mradi wa upanuzi wa mtandao wa maji katika eneo la Angaza kwa gharama ya **Shilingi 1,138,328,705.12**. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni ufungaji wa pampu; ujenzi wa tanki la lita 200,000; ulazaji wa mabomba katika njia kuu umbali wa kilomita 1.6; na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa kilomita 16.4. Hadi mwezi Aprili 2024, ujenzi wa tanki, ulazaji wa mabomba katika njia kuu na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umekamilika; na kazi iliyobaki ni ufungaji wa pampu. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 60** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024 na utawanufaisha wakazi wapatao 5,600 wa eneo la Angaza.

***(h) Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Manispaa ya Musoma na Maeneo ya Pembezoni***

106. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea na utekelezaji wa mradi wa upanuzi wa mtandao wa majisafi katika Mji wa Musoma kwa gharama ya **Shilingi 400,000,000**. Mradi huo unahusisha ununuzi na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji yenye jumla ya urefu wa kilomita 36.768. Hadi mwezi Aprili, 2024 kazi zilizotekelezwa ni ununuzi wa mabomba yenye urefu wa kilomita 29.759 na ulazaji wa mabomba kwenye mtandao wa maji umbali wa kilomita 11.9. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 40** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024. kukamilika kwa mradi kutawanufaisha wakazi wapatao 40,000.

107. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara inaendelea kutekeleza mradi wa maji Rorya – Tarime kwa gharama ya **Shilingi 134,398,706,754.46**. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa chanzo cha maji chenye uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 29; ujenzi wa chujio lenye uwezo wa kusafisha na kutibu maji lita milioni 28; ujenzi wa matanki matatu (3) yenye uwezo wa kuhifadhi maji lita milioni 10; ujenzi wa kituo cha kusukuma maji eneo la Gamasara - Tarime; ununuzi na ulazaji wa mabomba katika mtandao wa kusambaza maji umbali wa kilomita 20; na ununuzi na ulazaji wa mabomba katika njia kuu ya kusafirisha maji umbali wa kilomita 90. Hadi mwezi Aprili 2024, kazi zilizoanza kutekelezwa ni ujenzi wa matanki mawili (2) yenye uwezo wa kuhifadhi maji lita milioni 4 na ujenzi wa kituo cha kusukuma maji eneo la Gamasara. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 11** na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2025. Kukamilika kwa mradi kutawanufaisha wakati wapatao 487,533 wa miji ya Rorya na Tarime.

108. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea kutekeleza Mradi wa Maji wa Miji 28 katika Mji wa Mugumu kwa gharama ya **Shilingi 22,369,967,795**. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa chanzo cha maji chenye uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 15; ujenzi wa chujio lenye uwezo wa kusafisha na kutibu maji lita milioni 14.5; ujenzi wa tanki lenye uwezo wa kuhifadhi maji lita milioni 2; ununuzi na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa kilomita 31; na ununuzi na ulazaji wa mabomba katika njia kuu ya kusafirisha maji umbali wa kilomita 6.6. Hadi mwezi Aprili 2024, kazi zilizoanza kutekelezwa ni ujenzi wa tanki na ujenzi wa chujio. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 6** na unatarajiwa kukamilika mwezi Aprili, 2025. Kukamilika kwa mradi kutawanufaisha wakazi wapatao 166,960 wa Mji wa Mugumu.

***(i) Kuboresha Huduma ya Maji katika Mji wa Babati***

109. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea na utekelezaji wa mradi wa maji Dareda – Singu – Sigino - Bagara unaogharimu **Shilingi 12,724,407,807.85**. Mradi huo

unahusisha ujenzi wa matanki matano (5) ya kuhifadhi maji yenye jumla ya lita milioni 4.1; ulazaji wa mabomba usambazaji maji umbali wa kilomita 63.31; ujenzi wa bomba kuu la kusafirisha maji umbali wa kilomita 26.83; ujenzi wa vituo viwili (2) vya kusukuma maji; ununuzi na ufungaji wa pampu mbili (2) za kusukuma maji; ujenzi wa mtambo wa kusafisha na kutibu maji; na ujenzi wa chanzo. Hadi mwezi Aprili 2024, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa matanki matatu (3) ya kuhifadhi maji yenye ujazo wa lita milioni 2.45; ujenzi wa mtambo wa kusafisha na kutibu maji; ulazaji wa bomba kuu la kusafirisha maji umbali wa kilomita 20; na ujenzi wa chanzo. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 90**. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024 na utawanufaisha wakazi wapatao 60,000.

***(j) Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Jiji la Dodoma***

110. **Mheshimiwa Spika**, mahitaji ya maji kwa Jiji la Dodoma ni **lita milioni 149.5** ikilinganishwa na uzalishaji wa **lita milioni 79.1** kwa siku hivyo, kuwa na upungufu wa **lita milioni 70.4** kwa siku. Kutokana na hali hiyo, Wizara imeendelea kutekeleza mipango ya muda mfupi inayolenga kukabiliana na adha ya upatikanaji wa maji ambapo utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi wa ujenzi na uboreshaji wa mtandao wa majisafi Nzuguni umekamilika. Mradi huo unawanufaisha wakazi wapatao **75,968** wa maeneo ya Nzuguni, Ilazo, Swaswa na Kisasa. Aidha, Serikali imeanza kutekeleza awamu ya pili ya mradi wa ujenzi wa mtandao wa majisafi Nzuguni kwa gharama ya **Shilingi 5,509,671,097.11**. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni ufungaji wa pampu tano (5); ujenzi wa jengo la kuendeshea visima; ulazaji wa mabomba kutoka kwenye visima na kupeleka maji kwenye tanki umbali wa kilomita 4.3; kubadilisha mabomba ya kusambaza maji kwa kuweka yenye kipenyo kikubwa umbali wa kilomita 20; na ufungaji wa mfumo wa SCADA wa kuendeshea visima. Mradi upo kwenye hatua za awali za utekelezaji na unatarajiwa kukamilika mwezi Machi 2025 na kuwanufaisha wakazi wapatao 80,000 wa Jiji la Dodoma.

111. **Mheshimiwa Spika**, pia, Wizara inatekeleza mradi wa kupanua na kuboresha huduma ya majisafi kwenye maeneo ya Dodoma mjini na Chamwino kwa gharama ya **Shilingi 4,181,321,572.74**. Kazi zinazotekelezwa ni ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa kilomita 64.387 kati ya kilomita 146.437 zilizopangwa; ujenzi wa chemba 84; ujenzi nguzo 143 za alama katika njia ya bomba za maji; na ujenzi wa nguzo za kushikilia mabomba. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 40** na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba 2024 na kunufaisha wakazi wapatao 150,000 wa Dodoma na Chamwino.

***(k) Miradi ya Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Miji ya Vwawa – Mlowo***

112. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea kutekeleza mradi wa upanuzi wa mtandao wa maji katika Miji ya Vwawa na Mlowo unaogharimu **Shilingi 2,205,767,425.21**. Hadi mwezi Aprili 2024, kazi zilizotekelezwa ni uchimbaji wa kisima kirefu eneo la Hasanga; ujenzi wa tanki la kukusanya maji la lita 75,000; ujenzi wa tanki la kuhifadhi maji la lita 250,000 eneo la Ichenjezya; ujenzi wa uzio kuzunguka tanki; ununuzi na ulazaji wa mabomba katika njia kuu umbali wa kilomita 2.46; ulazaji wa mabomba ya mtandao wa kusambaza maji umbali wa kilomita 39.25 kati ya kilomita 48.7 zilizopangwa; na ujenzi wa nyumba ya pampu. Kazi zinazoendelea kutekelezwa ni pamoja na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa kilomita 9.45; uchimbaji, ununuzi na ufungaji wa pampu nne (4); ununuzi na ufungaji wa dira kubwa za maji 21 kwa ajili ya kupima maji; ununuzi wa gari na pikipiki sita (6); ununuzi na ufungaji wa jenereta na mashine ya kuunga mabomba; na uwekaji wa umeme kwenye chanzo. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 64** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024. Kukamilika kwa mradi huo kutawanufaisha wakazi wapatao 23,294.

113. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara inaendelea kutekeleza mradi wa ukarabati wa vyanzo vya maji vya Mwasanya na Mlowo kwa gharama ya **Shilingi 1,763,598,600**. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na ununuzi na ulazaji

wa mabomba ya kusafirisha maji umbali wa kilomita 17.35, ujenzi wa chemba 17, uwekaji wa alama za bomba *(marker post)*, ukarabati wa jengo la ofisi, ununuzi wa pikipiki tano (5), ununuzi wa kompyuta tatu (3) na ukarabati wa uzio kuzunguka chujio la maji lililopo Mlowo. Hadi mwezi Aprili, 2024 kazi iliyotekelezwa ni ununuzi na ulazaji wa mabomba ya kusafirisha maji umbali wa kilomita 15.442. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 85** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024 na kuwanufaisha wakazi wapatao **13,294**.

***(l) Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Manispaa ya Iringa na Maeneo ya Pembezoni***

114. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea kutekeleza mradi wa uboreshaji wa huduma ya maji katika Mji wa Kilolo unaogharimu **Shilingi 825,812,568.80**. Mradi huo unahusisha ujenzi wa chanzo cha maji ya mtiririko cha Mwosongela II chenye uwezo wa kuzalisha maji lita 691,000 kwa siku; na ulazaji wa bomba kuu la kusafirisha maji umbali wa kilomita 16.2 kutoka kwenye chanzo hadi kwenye tanki lililopo eneo la Luganga. Hadi mwezi Aprili, 2024 kazi iliyotekelezwa ni ujenzi na ulazaji wa bomba kuu la kusafirisha maji umbali wa kilomita 14.256. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 88** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024 na utawanufaisha wakazi wapatao 6,871.

115. **Mheshimiwa Spika**, aidha, Wizara imeendelea na uboreshaji wa huduma ya maji katika Mji wa Ilula na vijiji vya Imalutwa na Mazombe kwa gharama ya **Shilingi 445,739,445.15**. Hadi mwezi Aprili, 2024 kazi zilizotekelezwa ni ujenzi wa tanki la lita 75,000; ulazaji wa bomba la kusafirisha maji umbali wa kilomita 3.4; na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa kilomita 6.3. Kazi inayoendelea ni ujenzi wa vituo sita (6) vya kuchotea maji. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 95** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024 na utawanufaisha wakazi wapatao 7,455.

116. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara inaendelea na utekelezaji wa mradi wa maji Ismani - Kilolo kwa gharama ya **Shilingi 9,270,306,365**. Hadi mwezi Aprili, 2024, kazi zilizotekelezwa ni

pamoja na kuboresha chanzo cha maji Mgera; ununuzi na ufungaji wa pampu mbili (2); ujenzi wa bomba kuu la kusafirisha maji umbali wa kilomita 84 kati ya kilomita 111.8 zilizopangwa; ujenzi wa matanki nane (8) yenye uwezo wa kuhifadhi maji lita milioni 1.725; na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa kilomita 89.54 kati ya kilomita 106.99 zilizopangwa. Kazi zinazoendelea ni upanuzi wa mtambo wa kusafisha na kutibu maji Ndiuka, ukarabatia wa vituo 14 vya kuchotea maji na ufungaji wa dira za maji 1,000. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 95** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024 na utawanufaisha wakazi wapatao 58,821.

***(m) Kuboresha Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Manispaa ya Songea na Maeneo ya Pembezoni***

117. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imekamilisha mradi wa upanuzi wa mtandao wa majisafi eneo la Mwengemshindo kwa gharama ya **Shilingi 547,521,500.** Kazi zilizotekelezwa ni ununuzi na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa kilomita 26.5. Kukamilika kwa mradi huo, kumeimarisha huduma ya maji kwa wakazi wapatao **3,000** wa eneo hilo.

118. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara imekamilisha ujenzi wa mradi wa maji katika eneo la viwanda - Lilambo kwa gharama ya **Shilingi 415,980,885**. Kazi zilizotekelezwa ni ujenzi wa nyumba ya pampu; ununuzi na ufungaji wa pampu; ujenzi wa tanki la lita 100,000; ununuzi na ulazaji wa mabomba ya kusafirisha maji umbali wa kilomita 5; ununuzi na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa kilomita 8.1; ujenzi wa uzio kuzunguka tanki; na ujenzi wa mfumo wa kutibu maji. Kukamilika kwa mradi kumenufaisha viwanda **200** vilivyopo eneo la Lilambo.

119. **Mheshimiwa Spika**, aidha, Wizara inaendelea kutekeleza mradi wa maji katika eneo la Subira unaogharimu **Shilingi 1,168,863,390**. Mradi huo unahusisha ujenzi wa nyumba mbili (2) za pampu; ununuzi na ufungaji wa pampu mbili (2); ujenzi wa tanki la lita 200,000; ununuzi na ulazaji wa mabomba katika mtandao wa kusambaza maji umbali wa kilomita 42.5;

na ujenzi wa mfumo wa kutibu maji. Hadi mwezi Aprili 2024, kazi zilizotekelezwa ni ununuzi wa mabomba yenye jumla ya urefu wa kilomita 39.6 na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa kilomita 17. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 40** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024 na utawanufaisha wakazi wapatao 12,691.

***(n) Kuboresha Huduma ya Maji katika Manispaa ya Mtwara na Maeneo ya Pembezoni***

120. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imekamilisha utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa chujio la maji katika eneo la Mangamba kwa gharama ya **Shilingi 3,451,853,994**. Kazi zilizotekelezwa ni ujenzi wa tanki la maji kwa ajili ya huduma ya zimamoto; ununuzi na ufungaji wa mabomba na viungio; ujenzi wa jengo la pampu; ufungaji wa pampu; ukarabati wa karakana; na ujenzi wa mifumo ya usalama ya umeme. Kukamilika kwa mradi huo, kumewezesha wakazi wa Mji wa Mtwara kupata huduma ya maji yaliyosafishwa na kutibiwa kwa viwango vinavyokubalika.

121. **Mheshimiwa Spika**, aidha, Wizara inaendelea kutekeleza mradi wa uboreshaji wa huduma ya maji katika Mji wa Mtwara kwa gharama ya **Shilingi 20,361,599,950**. Mradi huo unatekelezwa katika awamu mbili ambapo awamu ya kwanza inahusisha ujenzi wa matanki mawili (2) yenye jumla ya ujazo wa lita milioni 7; pamoja na ukarabati wa mtandao wa bomba kuu. Awamu ya pili inahusisha ujenzi wa tanki la ujazo wa lita 500,000. Hadi mwezi Aprili 2024, utekelezaji wa awamu ya kwanza umefikia **asilimia 85** na awamu ya pili umefikia **asilimia 35**. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2024 na kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa wakazi 139,336 wa Mji wa Mtwara.

### 3.2.4.2. Miradi ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa

***(a) Miji ya Tinde na Shelui***

122. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya India kupitia Benki ya Exim - India imekamilisha utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi wa kuboresha huduma ya maji katika miji ya Tinde na Shelui kwa gharama ya **Shilingi 24,753,848,782**. Vilevile, katika kuhakikisha wananchi wengi zaidi wa miji hiyo wanafikiwa na huduma ya maji, Serikali inaendelea na upanuzi wa mradi huo ambapo hadi mwezi Aprili 2024, ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa kilomita 7.6 umekamilika kwa gharama ya **Shilingi 1,150,000,000**. Awamu ya pili ya mradi inahusisha upanuzi wa mtandao wa usambazaji maji katika miji ya Tinde na Shelui itakaogharimu kiasi cha **Dola za Marekani 6,000,000**. Taratibu za kupata kibali cha kuanza utekelezaji wa awamu hiyo kutoka Serikali ya India zinaendelea. Mradi huo utakapokamilika utawanufaisha wakazi wapatao **86,983** wa miji hiyo.

***(b) Mradi wa Kuboresha Huduma ya Maji katika Mji wa Turiani***

123. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa uboreshaji wa huduma ya maji katika Mji wa Turiani kwa gharama ya **Shilingi 3,905,699,196**. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa tanki la ujazo wa lita 150,000 na chujio katika Kijiji cha Luamba; ujenzi wa vyanzo vitatu (3) vya maji vya mserereko katika vijiji vya Luamba, Mlaguzi na Ubiri; ulazaji wa mabomba za kusafirisha na kusambaza maji umbali wa kilomita 70; na ujenzi wa vituo 15 vya kuchotea maji. Hadi mwezi Aprili 2024, kazi zilizoanza kutekelezwa ni ujenzi wa tanki, ujenzi wa vyanzo vya maji viwili (2) vya Luamba na Mlaguzi; na ulazaji wa bomba umbali wa kilomita 15. Kwa wastani utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 40** na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2024 na utawanufaisha wakazi wapatao 40,700.

### *(c) Uboreshaji wa Huduma ya Maji katika Mji wa Tunduma*

124. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imekamilisha awamu ya kwanza ya mradi wa uboreshaji wa miundombinu ya maji katika Mji wa Tunduma uliogharimu **Shilingi 818,237,830**. Kazi zilizotekelezwa ni ununuzi na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa kilomita 6.6; ujenzi wa vituo vitano (5) vya kuchotea maji; ununuzi wa dira za maji 100 na viungio vya maunganisho mapya; ujenzi wa uzio; na ununuzi wa pikipiki tatu (3). Mradi unatoa huduma kwa wananchi wapatao **15,562** wa mji huo.

125. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara inaendelea na utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi wa uboreshaji wa miundombinu ya maji katika Mji wa Tunduma kwa gharama ya **Shilingi 918,626,905.5**. Kazi zinazoendelea kutekelezwa ni ujenzi wa tanki la lita 50,000; ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa kilomita 14.5; utafiti wa waji chini ya ardhi katika maeneo 16; uchimbaji wa visima virefu sita (6); ununuzi wa transfoma 50KVA; ujenzi wa nyumba za mitambo mbili (2); uvutaji wa umeme wa njia tatu; ujenzi wa chemba 14 na ufungaji wa pampu nne (4). Hadi mwezi Aprili, 2024, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 60** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024 na kuwanufaisha wananchi 25,071 wa mji huo.

### *(d) Mradi wa Kitaifa wa HTM*

126. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeanza utekelezaji wa mradi wa kimkakati wa maji Segera-Kabuku ambao ni sehemu ya mradi wa kitaifa wa Handeni Trunk Main (HTM) kwa gharama ya **Shilingi 25,585,976,283.13**. Mradi huo unalenga kuwapatia huduma ya maji safi, salama na yenye kutosheleza wananchi wa vijiji 15 vya Kwamgwe, Chanika Kofi, Seza Kofi, Bondo, Kwadoya, Ngojoro, Kwedizinga, Ugweno, Taula, Kwedibago, Kabuku Nje, Kabuku Mjini, Komsanga, Kabuku Kaskazini na Kabuku Ndani pamoja na Kambi ya Jeshi Mgambo-Kabuku. Hadi mwezi Aprili 2024, kazi zilizoanza kutekelezwa ni ununuzi wa mabomba yenye jumla ya urefu wa kilomita 10 na ujenzi wa tanki lenye ujazo

wa lita milioni 2. Kazi nyingine za mradi zinahusisha ujenzi wa kidakio cha maji; ujenzi wa mtambo wa kusafisha na kutibu maji wenye uwezo wa kuzalisha lita milioni 6.27 kwa siku; ulazaji wa mabomba umbali wa kilomita 106; ujenzi wa jengo la mitambo; na jengo la maabara. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2024 na kuwanufaisha wananchi wapatao 120,000.

***(e) Mradi wa Maji Mugango – Kiabakari – Butiama***

127. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika *(BADEA)* na Mfuko wa Maendeleo wa Saudia *(Saudi Fund for Development – SFD)* inaendelea na utekelezaji wa mradi wa maji utakaohudumia maeneo ya Mugango, Kiabakari na Butiama kwa gharama ya **Dola za Marekani 30,690,000**. Kazi zinazoendelea kutekelezwa ni ujenzi wa choteo la maji katika Ziwa Victoria; ujenzi wa mtambo wa kusafisha na kutibu maji; pamoja na ujenzi wa mantaki manne (4) yenye jumla ya ujazo wa lita milioni 7 katika maeneo ya Kong, Kiabakari, Butiama Hill na Bumangi; ulazaji wa bomba kuu umbali wa kilomita 48 kutoka Mugango kwenda Kiabakari hadi Butiama; ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa kilomita 140; ujenzi wa ofisi na nyumba za wasimamizi wa mitambo; ukarabati wa matanki mawili (2) katika maeneo ya Kyatungwe na Bisarye; ujenzi wa vioski 40 vya maji na ununuzi wa dira za maji 2,000. Hadi mwezi Aprili 2024, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 98.5** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024. Mradi huo utawanufaisha zaidi ya wananchi 100,000 waliopo katika eneo la mradi; vijiji vilivyopo ndani ya kilomita 12 kutoka bomba kuu; na wananchi wa Kata ya Nyamswa yenye vijiji vya Nyamswa, Makongoro A, Makongoro B na Bukama ambao watanufaika na upanuzi wa mradi huo.

***(f) Mradi wa Maji Same – Mwanga – Korogwe***

128. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Mashirika ya BADEA, OPEC Fund na Kuwait Fund inaendelea kutekeleza mradi wa maji Same – Mwanga - Korogwe utakaohudumia

Miji ya Same na Mwanga pamoja na vijiji 38 kwenye Wilaya za Same na Mwanga na vijiji vitano (5) katika Wilaya ya Korogwe. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa chanzo; ujenzi wa kituo cha kupokea na kupoza umeme; ujenzi wa mtambo wa kusafisha na kutibu maji; ujenzi wa matanki 16 yenye ukubwa kuanzia lita laki 3 hadi lita milioni 9; ulazaji wa mabomba ya kusafirisha maji umbali wa kilomita 260; na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa kilomita 306. Hadi mwezi Aprili 2024, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa mtambo wa kuzalisha maji, ujenzi wa chanzo; ujenzi wa kituo cha kupokea na kupoza umeme; ulazaji wa bomba kuu umbali wa kilomita 81.7; ulazaji wa mabomba ya mtandao wa kusambaza maji umbali wa kilomita 207 katika Miji ya Same na Mwanga; ujenzi wa mtambo wa kusafisha na kutibu maji; na ujenzi wa matanki saba (7) ya kuhifadhi maji. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 86.7** na kwa sasa upo kwenye majaribio ya kutoa maji kutoka katika chanzo kuyapeleka kwenye chujio. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024 na utakuwa na uwezo wa kuhudumia wananchi **456,931** wa wilaya za Same, Mwanga na Korogwe.

***(g) Uboreshaji wa Huduma ya Maji katika Mji wa Sengerema***

129. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea na utekelezaji wa mradi wa maji Nyasigu – Lubungo – Ngoma kwa gharama ya **Shilingi 13,742,895,491.14**. Mradi huo unahusisha ujenzi wa jengo la mtambo wa kusukuma maji; ufungaji wa pampu; ujenzi wa mtambo wa kusafisha na kutibu maji wenye uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 12 kwa siku; ujenzi wa matanki matatu (3) yenye jumla ya ujazo wa lita milioni 2.6; ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa kilomita 108.4; ujenzi wa vituo 70 vya kuchotea maji; ununuzi wa gari na pikipiki saba (7); ujenzi wa chemba; ujenzi wa jengo la ofisi kuu na jengo la ofisi ya uendeshaji eneo la Ngoma; ujenzi wa njia ya umeme kutoka Nyasigu hadi katika chanzo cha Mabiru; na uunganishaji wa wateja wa majumbani. Hadi mwezi Aprili 2024, kazi zilizoanza

kutekelezwa ni ujenzi wa njia ya umeme kutoka Nyasigu hadi kwenye chanzo cha Mabiru; ujenzi wa jengo la mtambo wa kusukuma maji; ujenzi wa jengo la ofisi kuu na jengo la ofisi ya uendeshaji eneo la Ngoma. Kwa wastani, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 30** unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2024 na utawanufaisha wakazi wapatao 20,024 wa maeneo ya Nyasigu, Lubungo na Ngoma.

***(h) Uboreshaji wa Huduma ya Maji katika Mji wa Mafinga***

130. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeanza utekelezaji wa mradi wa uboreshaji wa huduma ya maji katika Mji wa Mafinga unaogharimu kiasi cha **Shilingi 866,957,377**. Mradi huo unahusisha ununuzi na ufungaji wa pampu; ukarabati wa banio la maji la Ikangafu, ukarabati wa tanki la kutibu maji; ukarabati wa nyumba ya kuendeshea mitambo; ukarabati wa mtambo wa kutibu maji; na ukarabati wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa kilomita 13.5. Hadi mwezi Aprili 2024, kazi zilizotekelezwa ni ukarabati wa nyumba ya kuendeshea mitambo na ununuzi wa mabomba yenye urefu wa kilomita 11.06. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 18** na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai 2024. Mradi huo utaboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa wakazi 48,807.

***(i) Uboreshaji wa Huduma ya Maji katika Mji wa Busega***

131. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imekamilisha mradi wa upanuzi wa mtandao wa majisafi katika kata za Nyashimo, Lamadi na Mkula uliogharimu **Shilingi 685,000,509**. Kazi zilizotekelezwa ni ulazaji wa mabomba katika njia kuu ya kusafirisha maji umbali wa kilomita 3 na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa kilomita 20. Mradi unatoa huduma kwa wananchi wapatao **8,290** wa kata hizo.

132. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara inaendelea na mradi wa kuboresha huduma ya maji katika maeneo ya Nyashimo, Mkula na Shule ya Sekondari Mwabayanda kwa gharama ya **Shilingi 639,772,790.70**. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni

ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa kilomita 23; ufungaji wa *surge tank*; na ufungaji wa pampu tatu (3). Hadi mwezi Aprili, 2024 kazi zilizotekelezwa ni ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa kilomita 17.4 na ufungaji wa pampu moja. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 18** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024. Kukamilika kwa mradi huo kutawanufaisha wananchi wapatao 7,103 wa maeneo hayo.

***(j) Mradi wa Uboreshaji wa Huduma ya Maji Ngara Mjini***

133. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inatekeleza mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Ngara kwa gharama ya **Shilingi 1,256,556,468.93**. Kazi zinazotekelezwa ni pamoja na ununuzi na ufungaji wa Pampu; ufungaji wa *control pannel*; ujenzi wa tanki la lita 200,000; ulazaji wa mabomba ya kusafirisha maji umbali wa kilomita 16.06; ukarabati wa jengo la mitambo; ujenzi wa uzio kuzunguka eneo la jengo la mitambo; na ufungaji wa miundombinu ya umeme kwenye jengo la mitambo. Hadi mwezi Aprili 2024, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 16** na unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba 2024 na kuwanufaisha wakazi wapatao 13,560 wa Mji wa Ngara.

***(k) Mradi wa Kuboresha Huduma ya Maji katika Miji 28***

134. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea na utekelezaji wa mradi wa uboreshaji wa huduma ya maji katika miji 28 ambapo miradi katika miji 24 inatekelezwa kupitia fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya India kupitia Benki ya Exim na miradi katika miji minne (4) inatekelezwa kwa fedha za ndani. Mradi unatekelezwa kwa utaratibu wa usanifu na ujenzi *(Design & Build)* na kwa mujibu wa Mkataba, mradi unatarajiwa kukamilika mwaka 2025/26. Aidha, misamaha ya kodi imepatikana na malipo ya awali yamefanyika kwa Wakandarasi wote wa miji 28. Hadi mwezi Aprili 2024, Wakandarasi wanaendelea na utekelezaji wa miradi na hatua zilizofikiwa ni kama ifuatavyo:-

135. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Kipande cha Kwanza kinachohusisha Miji ya Handeni, Korogwe, Muheza na Pangani umefikia **asilimia 30**; Kipande cha Pili chenye Miji ya Kilwa Masoko na Nanyumbu **(asilimia 28)**; Kipande cha Tatu chenye Miji ya Ifakara, Rujewa, Chunya, Njombe, Makambako na Wanging'ombe **(asilimia 9)**; Kipande cha Nne chenye Miji ya Kiomboi, Singida, Manyoni, Mugumu, Chemba na Chamwino **(asilimia 9)**; Kipande cha Tano chenye Miji ya Kasulu, Mpanda, Sikonge, Urambo na Kaliua **(asilimia 40)**; Kipande cha Sita chenye Miji ya Kayanga, Chato na Geita **(asilimia 10)**; Kipande cha Saba kinachohusisha mradi wa Makonde Plateau chenye Miji ya Newala, Nanyamba, Tandahimba na sehemu ya Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara **(asilimia 23.5)**; Kipande cha Nane chenye Mji wa Mafinga **(asilimia 16.5)**; Kipande cha Tisa chenye Miji ya Rorya na Tarime **(asilimia 13)**; na Kipande cha Kumi chenye Mji wa Songea, utekelezeji umefikia **asilimia 3**. Kwa mujibu wa Mkataba, mradi huo wa miji 28 unatarajiwa kukamilika mwaka 2025/26.

***(l) Mradi wa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Mkoa wa Simiyu***

136. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (*KfW*) na Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (*Green Climate Fund - GCF*) inatekeleza Mradi wa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi kwa gharama ya **Euro 171,000,000**. Mradi huo unatekelezwa kwenye wilaya tano (5) za Busega, Bariadi, Itilima, Maswa na Meatu katika Mkoa wa Simiyu. Utekelezaji wa mradi utahusisha ujenzi wa chanzo chenye uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 73.2 kwa siku; ulazaji wa mtandao wa bomba kuu la kusafirisha maji umbali wa kilomita 151; ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa kilomita 358.93; ujenzi wa matanki sita (6) yenye jumla ya ujazo wa lita milioni 39.5; ulazaji wa bomba umbali wa kilomita 1.1 ndani ya Ziwa Victoria; ujenzi wa kituo cha kusukuma maji ghafi; ulazaji wa bomba umbali wa kilomita 2.75 kutoka kituo cha kusukuma maji ghafi hadi kituo cha kusafisha maji; ufungaji wa *SCADA System*; ujenzi wa kituo cha kusafisha na

kutibu maji chenye ujazo wa lita milioni 69.5 kwa siku; ujenzi wa kituo cha kusukuma maji katika eneo la Nyangokolwa; ujenzi wa nyumba za wafanyakazi wa mitambo, nyumba ya mlinzi, jengo la ofisi na nyumba ya mtambo wa kusuma maji; na ununuzi wa dira za maji 2,800. Hadi mwezi Aprili 2024, kazi zinazoendelea ni maandalizi ya awali ya kuleta vifaa vya ujenzi na wataalam; na upimaji (*survey*) wa njia kuu yatakapopita mabomba pamoja na maeneo yanayotarajiwa kujengwa matanki. Mradi huo unatarajiwa kuwanufaisha wananchi wapatao **662,500** wa Wilaya hizo.

### 3.2.4.3. Miradi ya Usafi wa Mazingira

137. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuboresha huduma ya usafi wa mazingira katika maeneo mbalimbali ya mijini kwa kuwekeza kwenye miundombinu ya uondoshaji majitaka. Hadi mwezi Aprili 2024, mtandao wa majitaka mijini umefikia **kilomita 1,455.93** kutoka **kilomita 1,416.93** mwezi Aprili, 2023. Vilevile, maunganisho ya huduma ya uondoshaji majitaka yameongezeka kutoka wateja **56,923** mwezi Aprili, 2023 hadi wateja **58,650** mwezi Aprili, 2024. Miradi ya uondoshaji majitaka inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na:-

#### *(a) Kuboresha Huduma ya Uondoshaji Majitaka katika Jiji la Tanga*

138. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa miundombinu ya majitaka kutoka Duga hadi Makorora katika Jiji la Tanga unaogharimu **Shilingi 509,234,651**. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa nyumba ya pampu; ununuzi na ulazaji wa bomba umbali wa kilomita 3.2 na ujenzi wa chemba 30. Hadi mwezi Aprili 2024, mradi umefikia **asilimia 80** na kazi iliyotekelezwa ni ujenzi wa chemba 30. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024 na kuboresha huduma ya uondoshaji majitaka kwa wakazi wapatao 3,500 wa maeneo ya Duga na Makorora.

***(b) Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Majitaka katika Mji wa Muheza***

139. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa miundombinu ya majitaka katika Mji wa Muheza kwa gharama ya **Shilingi 1,013,234,000**. Utekelezaji wa mradi unahusisha ujenzi wa mtambo wa kutibu tope kinyesi; ujenzi wa mabwawa mawili (2) ya kukusanya majitaka; ununuzi wa gari la usimamizi wa mradi; ununuzi wa gari la uondoshaji wa majitaka; na ujenzi wa vyoo vitatu (3) katika maeneo ya stendi, choo kimoja (1) na shule vyoo viwili (2). Hadi mwezi Aprili 2024, utekelezaji wa mradi unaendelea na umefikia **asilimia 85.** Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2024 na kuimarisha huduma ya uondoshaji majitaka kwa wakazi wapatao 38,131.

***(c) Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Majitaka katika Mji wa Pangani***

140. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa miundombinu ya majitaka katika Mji wa Pangani kwa gharama ya **Shilingi 995,519,888**. Utekelezaji wa mradi unahusisha ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka; ununuzi wa gari la uondoshaji wa majitaka; ununuzi wa gari la usimamizi wa mradi na ujenzi wa vyoo vitatu (3) katika maeneo ya stendi, choo kimoja (1) na shule vyoo viwili (2). Hadi mwezi Aprili 2024, utekelezaji wa mradi unaendelea na umefikia **asilimia 90**. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2024 na kuimarisha huduma ya uondoshaji majitaka kwa wakazo wapatao 38,131.

***(c) Kuboresha Huduma ya Uondoshaji Majitaka katika Jiji la Mwanza***

141. **Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha huduma ya uondoshaji majitaka katika Jiji la Mwanza, Wizara imetekeleza na kukamilisha mradi wa upanuzi wa mabwawa ya kutibu majitaka kwenye Manispaa ya Ilemela kwa gharama ya **Shilingi 6,739,048,681.80**. Aidha, ujenzi wa mfumo rahisi wa uondoshaji majitaka uliogharimu **Shilingi**

**3,720,864,077.92** umekamilika katika maeneo ya Mabatini, Kilimahewa A, Kilimahewa B na Pasiansi. Vilevile, ujenzi wa mfumo rahisi wa uondoshaji majitaka uliogharimu **Shilingi 3,844,768,482.50** umekamilika kwenye sehemu za milimani katika maeneo ya Igogo – Sahara, Kabuhoro, Isamilo, na Ibungiro. Kukamilika kwa miradi hiyo kumeboresha huduma ya uondoshaji majitaka kwa wakazi wapatao **355,000** wa maeneo hayo.

***(d) Kuboresha Huduma ya Uondoshaji Majitaka katika Jiji la Dar es Salaam***

142. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea na utekelezaji wa mradi wa mfumo rahisi wa uondoshaji majitaka na mtambo wa kutibu majitaka katika Jiji la Dar es Salaam kwa gharama ya **Shilingi 9,022,243,047.85**. Mradi unahusisha ujenzi wa mtandao wa majitaka wenye urefu wa kilomita 54.5 na ujenzi wa mitambo minne (4) ya kutibu majitaka. Hadi mwezi Aprili 2024, utekelezaji umefikia **asilimia 12** na unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2024. Mradi utakapokamilika utaboresha huduma ya uondoshaji majitaka kwa wakazi wapatao 36,000 wa maeneo ya Kinyerezi, Kipawa, Buguruni - Kisiwani, Mivinjeni, Mikocheni, Faru na Kombo.

143. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara inaendelea na ujenzi wa mtandao wa uondoshaji majitaka na kituo cha kusukuma majitaka eneo la Mbezi Beach kwa gharama ya **Shilingi 52,407,401,646.15**. Kazi zinazotekelezwa ni ujenzi wa mtandao wa majitaka umbali wa kilomita 101 ambapo kilomita 53.1 zimejengwa; ujenzi wa vituo viwili (2) vya kusukuma majitaka; na ujenzi wa chemba za majitaka 2,383. Hadi mwezi Aprili 2024, utekelezaji umefikia **asilimia 44** na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2024. Mradi huo utaboresha huduma ya uondoshaji majitaka kwa wakazi wapatao 130,000 wa Mbezi Beach.

***(e) Mradi wa Ukarabati wa Mfumo wa Majitaka katika Maeneoya Area C na Area D katika Jiji la Dodoma***

144. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi wa ukarabati wa mfumo wa majitaka unaendelea katika maeneo ya Area C na Area D yaliyopo Jijini Dodoma. Mradi huo unatekelezwa kwa gharama ya **Shilingi 4,958,631,400** na unahusisha ujenzi wa chemba 962 za majitaka na ukarabati wa mabomba ya majitaka umbali wa kilomita 19. Hadi mwezi Aprili 2024, kazi zilizotekelezwa ni ujenzi wa chemba 936 za majitaka na ukarabati wa mabomba ya majitaka umbali wa kilomita 19. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 96** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024 na kuboresha huduma ya uondoshaji majitaka kwa wakazi 16,200 wa maeneo ya Area C na Area D.

145. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara inaendelea na ujenzi wa mtandao wa majitaka katika eneo la Chamwino – Ikulu kwa gharama ya **Shilingi 452,288,600**. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa chujio la majitaka; ujenzi wa chemba 30; ulazaji wa bomba za majitaka umbali wa mita 500; na ujenzi wa mabwawa mawili ya majitaka. Hadi mwezi Aprili 2024, utekelezaji wa kazi zilizopangwa unaendelea na umefikia **asilimia 50**. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2024 na kuboresha huduma ya uondoshaji majitaka kwa wakazi 300 wa maeneo ya Chamwino – Ikulu.

***(f) Mradi wa Upanuzi wa Mfumo wa Majitaka katika Maeneo ya Korongoni na Longuo "A" Manispaa ya Moshi***

146. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imekamilisha mradi wa kuboresha huduma ya uondoshaji wa majitaka katika Kata za Korongoni na Longuo "A" zilizopo katika Manispaa ya Moshi kwa gharama ya **Shilingi 1,000,000,000**. Mradi huo ulihusu upanuzi wa mfumo wa uondoshaji wa majitaka. Kukamilika kwa mradi kumeboresha huduma ya uondoshaji majitaka kwa wakazi wapatao **7,500** wa kata hizo.

147. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara imeanza utekelezaji wa mradi wa upanuzi wa mtandao wa majitaka kuunganisha

kiwanda cha kuchakata bidhaa za ngozi kwa gharama ya **Shilingi 2,118,431,709.38**. Mradi huo unahusu ujenzi wa mtandao wa majitaka wenye urefu wa kilomita 12.99. Hadi mwezi Aprili 2024, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 15** na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2024.

***(g) Kuboresha Huduma ya Uondoshaji Majitaka katika Jiji la Arusha***

148. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea na ujenzi wa mtandao wa majitaka kutoka eneo la Kisongo hadi Olasiti kwa gharama ya **Shilingi 2,515,456,580**. Kazi zinazoendelea kutekelezwa ni upimaji na usanifu wa njia mpya ya mtandao wa majitaka; ujenzi wa chemba 188 za majitaka; na ulazaji wa bomba za mtandao mpya wa majitaka umbali wa kilomita 9.21. Hadi mwezi Aprili 2024, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 36** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2025. Mradi utakapokamilika utaboresha huduma ya uondoshaji majitaka kwa wakazi wapatao 1,200.

***(h) Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Majitaka katika Mji wa Nzega***

149. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imekamilisha utekelezaji wa mradi wa kuboresha huduma ya uondoshaji wa majitaka katika Mji wa Nzega kwa gharama ya **Shilingi 1,586,916,242**. Mradi huo ulihusisha ujenzi wa chemba ya kupokea majitaka; ujenzi wa mabwawa ya *anaerobic* mawili (2) na *facultative* mawili (2); ujenzi wa jengo la mlinzi; ujenzi wa eneo oevu; ujenzi wa mfumo wa kukausha topekinyesi; uwekaji wa *geomembrane*; na ujenzi wa uzio kuzunguka eneo la mabwawa. Mradi unatoa huduma ya uondoshaji wa majitaka kwa wananchi wapatao **133,000** wa Mji huo.

***(i) Mradi wa Ujenzi wa Mabwawa ya Kutibu Majitaka katika Manispaa ya Singida***

150. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa miundombinu ya kusafisha na kutibu majitaka katika Manispaa ya Singida unaogharimu **Shilingi**

**1,764,606,000**. Utekelezaji wa mradi unahusisha ujenzi wa mabwawa ya kusafisha majitaka, ujenzi wa jengo la walinzi, eneo oevu, ujenzi wa maabara, ujenzi wa jengo la ofisi na ununuzi wa gari la uondoshaji wa majitaka. Hadi mwezi Aprili 2024, kazi inayoendelea ni ujenzi wa mabwawa ya kusafisha majitaka na utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 50**. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2024 na utaboresha huduma ya uondoshaji majitaka kwa wakazi 112,934.

***(j) Mradi wa Ujenzi wa Mabwawa ya Kutibu Majitaka Omurushaka/Kayanga***

151. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka Omurushaka/Kayanga unahusisha ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita 1.2 kutoka barabara kuu kwenda kwenye mabwawa; ujenzi wa mabwawa mawili (2) ya *anaerobic*; ujenzi wa mabwawa mawili (2) ya *Facultative*; ujenzi wa mabwawa matatu (3) ya *maturation*; ujenzi wa jengo la walinzi; ujenzi wa mfumo wa kukausha topekinyesi; ununuzi wa vifaa vya kupima ubora wa majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira; na ununuzi wa gari la uondoshaji wa majitaka. Mradi huo unatekelezwa kwa gharama ya **Shilingi 1,071,954,550.84**. Hadi mwezi Aprili 2024, utekelezaji umefikia **asilimia 70** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024. Mradi unatarajiwa kuboresha huduma ya uondoshaji majitaka kwa wakazi wapatao 45,000 wa eneo hilo.

***(k) Mradi wa Ujenzi wa Mabwawa ya Kutibu Majitaka Kyaka-Bunazi***

152. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka Kyaka – Bunazi unatekelezwa kwa gharama ya **Shilingi 970,355,684**. Mradi huo unahusisha ujenzi wa barabara yenye urefu wa mita 800 kutoka barabara kuu kwenda kwenye mabwawa; ujenzi wa mabwawa mawili (2) ya *anaerobic*; ujenzi wa mabwawa mawili (2) ya *Facultative*; ujenzi wa mabwawa matatu (3) ya *maturation*; ujenzi wa jengo la walinzi; ujenzi wa mfumo wa kukausha topekinyesi; ununuzi wa vifaa vya kupima ubora wa

majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira; na ununuzi wa gari la uondoshaji wa majitaka. Hadi mwezi Aprili 2024, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 15** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024 na utaboresha huduma ya uondoshaji majitaka kwa wakazi wapatao 35,000.

***(l) Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Majitaka katika Mji wa Chato***

153. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa ujenzi wa miundombinu ya majitaka katika Mji wa Chato unatekelezwa kwa gharama ya **Shilingi 1,594,256,565.** Mradi huo unahusu ujenzi wa mabwawa ya majitaka; ujenzi wa uzio kuzunguka eneo la mabwawa; na ununuzi wa magari mawili (2) ya uondoshaji majitaka. Hadi mwezi Aprili 2024, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 40** na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2024. Mradi huo utaboresha huduma ya uondoshaji majitaka kwa wakazi wapatao 16,000 wa mji huo.

***(m) Mradi wa Ujenzi wa Mabwawa ya Majitaka Eneo la Ngalanga katika Mji wa Njombe***

154. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa ujenzi wa mabwawa ya majitaka katika eneo la Ngalanga katika Mji wa Njombe unatekelezwa kwa gharama ya **Shilingi 1,240,186,800**. Mradi huo unahusisha ujenzi wa mabwawa ya *anaerobic* mawili (2) na mabwawa ya *facultative* mawili (2); ujenzi wa wetland; ujenzi wa uzio kuzunguka eneo la mabwawa; ujenzi wa maabara na jengo la walinzi; na ununuzi wa gari la uondoshaji majitaka. Hadi mwezi Aprili, 2024 kazi ya ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka inaendelea na utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 10**. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2024 na utaboresha huduma ya uondoshaji majitaka wa wakazi wapatao 90,353 wa eneo hilo.

***(n) Mradi wa Kuboresha Huduma ya Usafi wa Mazingira katika Kata ya Sinde Jijini Mbeya***

155. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imekamilisha utekelezaji wa mradi wa kuboresha huduma ya usafi wa mazingira katika Kata ya Sinde Jijini Mbeya kwa gharama ya **Shilingi milioni 167.07**. Kazi zilizotekelezwa ni ulazaji wa bomba umbali wa kilomita 1.5; ujenzi wa chemba 71 za majitaka; ukarabati wa bomba umbali wa mita 220; na ukarabati wa chemba 12. Kukamilika kwa mradi huo kumeboresha huduma ya uondoshaji majitaka kwa wakazi wapatao **5,800** wa Kata hiyo.

***(o) Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Majitaka katika Manispaa ya Musoma***

156. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa ujenzi wa miundombinu ya uondoshaji wa majitaka katika Manispaa ya Musoma unatekelezwa na Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*AFD*) kwa gharama ya **Shilingi 30,812,999,179.47**. Mradi huo unahusisha ujenzi wa miundombinu ya kukusanya majitaka katika kata za Kitaji, Iringo, Mwigobero, Mwisenge na Mkendo; ujenzi wa vituo vinne (4) vya kusukuma majitaka; ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka katika Kata ya Makoko; na ujenzi wa vyoo 60 katika shule za msingi na vyoo vitano (5) kwa ajili ya masoko na machinjio. Hadi mwezi Aprili 2024, kazi inayoendelea ni ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka na utekelezaji umefikia **asilimia 48**. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2024 na utaboresha huduma ya uondoshaji majitaka kwa wakazi wapatao 12,209.

***(p) Mradi wa Ujenzi wa Mabwawa ya Kutibu Majitaka katika Manispaa ya Tabora***

157. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa ujenzi wa mabwawa ya majitaka katika Manispaa ya Tabora unatekelezwa kwa gharama ya **Shilingi 1,613,830,289.76**. Mradi huo unahusisha ujenzi wa mabwawa mawili (2) ya *anaerobic*, ujenzi wa mabwawa mawili (2) ya *Facultative*, ujenzi wa

*wetland*, ujenzi wa mfumo wa kukausha topekinyesi, ujenzi wa uzio, ujenzi wa *incinerator*, matengenezo ya barabara kwenda kwenye mabwawa ya majitaka na ujenzi wa mtaro wa kuondosha maji yaliyotibiwa. Hadi mwezi Aprili 2024, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 35** na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2024. Mradi huo utaboresha huduma ya uondoshaji majitaka kwa wakazi wapatao 16,353.

***(q) Mradi wa Ujenzi wa Mabwawa ya Majitaka katika Mji wa Babati***

158. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka katika Mji wa Babati unatekelezwa kwa gharama ya **Shilingi 6,900,000,000**. Mradi huo unahusisha ujenzi wa mabwawa mawili (2) ya *anaerobic*, ujenzi wa bwawa la *Facultative*, ujenzi wa bwawa la *maturation*, ujenzi wa mfumo wa kukausha topekinyesi na ujenzi wa mtaro wa kuondosha maji yaliyotibiwa. Hadi mwezi Aprili 2024, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 67** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024. Kukamilika kwa mradi huo kutaboresha huduma ya uondoshaji majitaka kwa wakazi wapatao 389,000.

**3.2.5. Gridi ya Taifa ya Maji**

159. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea na maandalizi ya Gridi ya Taifa ya Maji na kwa sasa hatua iliyofikiwa ni ya kuajiri Mtaalam Mshauri atakayefanya upembuzi yakinifu wa mpango huo. Aidha, Wizara imeanza kutumia vyanzo vikubwa vya maji vya uhakika ikiwemo maziwa, mito mikubwa na mabwawa kwa ajili ya kusambaza huduma ya maji kwenye maeneo ambayo hayana vyanzo vya uhakika vya maji. Kwa mfano; mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria ambao umenufaisha Miji ya Kahama, Shinyanga, Tinde, Nzega, Tabora, Igunga na Shelui. Vilevile, taratibu za manunuzi za kumpata mtaalam mshauri wa kutoa maji Ziwa Tanganyika na kuyapeleka katika mikoa ya Katavi, Rukwa mpaka Kigoma zimeanza. Pia, Wizara imesaini Mkataba na Mtaalam Mshauri atakaefanya upembuzi

yakinifu na usanifu wa kina wa mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria na kuyapeleka Dodoma.

### 3.2.6. Mpango Kabambe wa Taifa wa Maji (*National Water Master Plan*)

160. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeanza zoezi la uandaaji wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Maji katika mikoa ya Rukwa, Njombe na Dodoma. Kupitia mpango huo miradi yote itabainishwa na kuanza kusanifiwa kulingana na vipaumbele vya mikoa na wilaya husika. Mpango huo utaainisha vyanzo vya maji katika maeneo husika, aina ya miundombinu inayofaa kutumika katika maeneo hayo, teknolojia ya usambazaji maji inayofaa kwa eneo husika, teknolojia inayofaa ya kusafisha na kutibu maji, na kama hakuna chanzo cha uhakika mpango utabainisha vyanzo vitakavyotumika kupeleka maji kwenye maeneo yasiyo na vyanzo na hatimaye kujua kiwango cha uwekezaji kinachohitajika. Katika mwaka 2024/25 zoezi hilo litaendelea katika mikoa mingine iliyobaki.

### 3.2.7. Matumizi ya Dira za Maji za Malipo Kabla

161. **Mheshimiwa Spika**, matumizi ya dira za maji za malipo kabla (*pre-paid water meters*) yana manufaa makubwa ikilinganishwa na dira za kawaida (*post-paid water meters*) ikiwemo kukusanya madeni na kuimarisha ufanisi katika makusanyo ya maduhuli; kuongeza ufanisi wa matumizi ya maji pamoja na kudhibiti mivujo inayosababisha hasara kwa mteja. Kwa kutambua umuhimu wa dira hizo, Wizara kupitia Mamlaka za Maji na CBWSOs zimeendelea kuwafungia wateja ambapo hadi mwezi Aprili 2024, wateja **13,526** wamefungiwa dira kati ya wateja **2,019,951** wa vijijini na mijini. Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira zilizowafungia wateja dira hizo ni pamoja na Iringa ambayo imefunga dira **6,544**, Dodoma **(1,085)**, Tanga **(627)**; na kwa upande wa vijijini, RUWASA imefunga jumla ya dira **1,986** kwenye mikoa mbalimbali.

162. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na ufanisi ulioonekana kwenye matumizi ya dira za maji za malipo kabla ikiwemo kupunguza malalamiko ya wateja kwenye ankara za maji, mnamo tarehe 4 Machi, 2024, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan** aliielekeza Wizara ya Maji kuongeza kasi ya ufungaji wa dira za maji za malipo kabla ili kuwafikia wananchi wote nchini. Katika kutekeleza agizo hilo, Wizara imeandaa Mkakati wa Kuongeza Kasi ya Ufungaji wa Dira za Maji za Malipo Kabla ambapo kupitia Mkakati huo asilimia 50 ya wateja wa maji vijijini na mijini watafungiwa dira hizo ifikapo Desemba 2025. Utekelezaji wa Mkakati huo umezingatia masuala muhimu yakiwemo kuandaa mpango wa pamoja wa ununuzi wa dira ili kurahisisha upatikanaji wake na kwa bei nafuu; kuunda mfumo jumuishi wa TEHAMA wa dira za maji za malipo kabla ili kuondoa utegemezi wa mifumo ya Wazabuni; kuhamasisha wadau wa maendeleo na sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa dira hizo; na kujenga uelewa kwa wananchi kuhusu umuhimu wa matumizi ya dira hizo.

### 3.2.8. Udhibiti wa Huduma ya Maji Mijini

163. **Mheshimiwa Spika**, huduma za maji mijini zinadhibitiwa na EWURA kupitia Kifungu Na. 414 cha Sheria Na.11 ya *EWURA* ya mwaka 2001. Sheria hiyo inaitaka *EWURA* kudhibiti utoaji wa huduma kwenye Sekta za Maji na Nishati katika maeneo ya maji na usafi wa mazingira, umeme, mafuta ya petroli pamoja na gesi asilia. Majukumu ya *EWURA* ni pamoja na kutoa leseni, kusimamia utekelezaji wa masharti ya leseni, kudhibiti ubora na ufanisi wa utoaji huduma, kutathmini na kupitisha bei za huduma na kutatua migogoro baina ya watoa huduma na wateja wao.

164. **Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Aprili 2024, EWURA ilitoa leseni nne (4) za kutoa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira kwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira za Miji ya Rombo, KyelaKasumulu, Njombe na Busega. Aidha, EWURA ilitathmini na kuidhinisha bei mpya za huduma ya maji kwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa

Mazingira saba (7) ambazo ni Dodoma, Makonde, Sumbawanga, Orkesumet, Mombo, Bariadi na Lindi. Vilevile, katika kipindi hicho, EWURA ilifanya mapitio ya mipangobiashara ya mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira 11 na kuidhinisha mikataba sita (6) ya huduma kwa mteja kwa mamlaka za Musoma, Liwale, Makambako, Lindi, Biharamulo na Geita.

165. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2022/23, EWURA ilitoa Taarifa ya Utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira. Taarifa hiyo inaainisha utendaji wa mamlaka za maji nchini na kuweza kusaidia Wizara pamoja na wadau wa sekta ya maji katika kuandaa na kutekeleza mipango mbalimbali ya kuimarisha na kuboresha huduma za majisafi na usafi wa mazingira. Taarifa hiyo, imebainisha kuwepo kwa mafanikio katika ongezeko la uzalishaji wa maji kwa **lita bilioni 7** sawa na **asilimia 1.78**, kuongezeka kwa uwezo wa miundombinu ya kuzalisha maji kwa **lita bilioni 126** sawa na **asilimia 16.94** na kuongezeka kwa idadi ya wateja wanaopata huduma ya maji kwa **asilimia 11**. Aidha, taarifa imebainisha changamoto zinazokabili mamlaka za maji zikiwemo: kuongezeka kwa upotevu wa maji ambao umefikia **asilimia 37**, upungufu wa miundombinu ya huduma ya usafi wa mazingira; na uwiano usioridhisha wa ongezeko la mahitaji ya maji ikilinganishwa na uzalishaji wa maji.

### 3.3. Taasisi zilizo Chini ya Wizara

#### 3.3.1. Mfuko wa Taifa wa Maji

166. **Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Taifa wa Maji ulianzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 44 cha Sheria Na. 12 ya mwaka 2009 ya Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira. Kwa sasa Mfuko unatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Na. 5 ya Huduma za majisafi na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019. Mfuko ni Taasisi yenye dhamana ya kutafuta na kutoa rasilimali fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji nchini. Lengo kuu la kuanzishwa kwa Mfuko ni kuwa na rasilimali fedha ya uhakika kwa ajili ya kusaidia

kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya maji nchini pamoja na kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa vyanzo vya maji. Chanzo cha mapato cha Mfuko kwa sasa ni tozo ya Shilingi 50 kwa kila lita ya mafuta ya diseli na petroli. Fedha hizo hutumika kutekeleza miradi ya maji inayosimamiwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini na Bodi za Maji za Mabonde.

167. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2023/24, Mfuko uliidhinishiwa **Shilingi 175,912,837,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji. Hadi mwezi Aprili, 2024, kiasi cha fedha kilichopokelewa ni **Shilingi 102,657,068,560.15** sawa na **asilimia 58.4**. Fedha hizo zimetumika kutekeleza miradi ya maji kwenye maeneo mbalimbali nchini na kipaumbele kimetolewa kwa miradi inayoendelea na iliyo kwenye hatua za mwisho kukamilika ili wananchi wengi zaidi wanufaike na huduma ya maji kwa wakati. Jumla ya miradi **165** kati ya miradi **332** iliyopangwa kutekelezwa katika bajeti imepokea fedha ambapo miradi **46** imekamilika na inatoa huduma. Vilevile, Mfuko wa Taifa wa Maji umetoa fedha kwa ajili ya kuhifadhi vyanzo vya maji ambapo takribani vyanzo **40** vimelindwa na kutunzwa kwa kuwekewa mipaka, kupanda miti na kuzuia shughuli za kibinadamu katika maeneo ya vyanzo.

168. **Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za kuongeza wigo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji nchini, Mfuko umeanza rasmi kutumia dirisha lake la mikopo ya riba nafuu lililozinduliwa mwezi Aprili, 2023. Hadi mwezi Aprili 2024, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bunda imenufaika na dirisha hilo na Mamlaka nyingine 12 zimewasilisha maombi ya kupata mkopo. Aidha, Mfuko umeendelea kuzijengea uwezo taasisi zinazotekeleza miradi ya maji nchini kwa kutoa mafunzo ya uandaaji wa maandiko ya miradi (*Bankable Project Proposals*) kwa ajili ya kutafuta fedha za uwekezaji katika sekta ya maji. Hadi mwezi Aprili 2024, maandiko ya miradi mitatu (3) kutoka Mamlaka za Maji za Mafinga, Makambako na Morogoro yameandaliwa.

### 3.3.2. Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA)

169. **Mheshimiwa Spika**, Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) ni Taasisi iliyoanzishwa kwa Kifungu cha 42 cha Sheria Na. 5 ya Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019. Taasisi hiyo imepewa jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira vijijini. Vilevile, Taasisi hiyo ina jukumu la kudhibiti bei za maji zinazotozwa na CBWSOs kwenye maeneo ya vijijni.

170. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuijengea uwezo RUWASA ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira vijijini. Katika mwaka 2023/24, Serikali imenunua jumla ya magari **15** na pikipiki **395** kwa ajili ya kuimarisha usimamizi, ufuatiliaji na uendeshaji wa miradi ya maji vijijini. Magari hayo yamepelekwa katika mikoa **13** ya Tanga, Arusha, Njombe, Dodoma, Mtwara, Ruvuma, Rukwa, Kagera, Morogoro, Shinyanga, Mara, Tabora na Iringa na magari **mawili (2)** yamebaki RUWASA makao makuu. Pikipiki zilizonunuliwa zimepelekwa katika ofisi za RUWASA Wilaya na kwenye Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii.

### 3.3.3. Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira

171. **Mheshimiwa Spika**, Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira zimeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Na. 5 ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019. Mamlaka hizo zina jukumu la kutoa huduma ya maji safi na usafi wa mazingira kwenye maeneo ya mijini. Utendaji kazi wa Mamlaka unasimamiwa na Bodi za Wakurugenzi zinazoteuliwa na Waziri mwenye dhamana na Maji. Hadi sasa, kuna jumla ya mamlaka za maji 90 zinazojumuisha mamlaka 25 za miji mikuu ya mikoa, miradi ya kitaifa nane (8), miji mikuu ya wilaya (51) na miji midogo, mamlaka sita (6). Mamlaka hizo zimegawanywa kwenye madaraja kulingana na uwezo wa kujiendesha ambapo kuna mamlaka za madaraja AA, A, B na C. Mamlaka za Daraja

AA ni zile zinazoweza kumudu gharama zote za uendeshaji, matengenezo na uwekezaji wa miundombinu ya maji; Mamlaka za daraja A ni zile zenye uwezo wa kumudu gharama zote za uendeshaji na matengenezo ikiwa ni pamoja na gharama za uchakavu wa mali; Mamlaka za daraja B ni zile zenye uwezo wa kumudu gharama za uendeshaji na matengenezo bila gharama za uchakavu wa mali; na Mamlaka za daraja C zina uwezo wa kumudu sehemu ya gharama za uendeshaji na matengenezo ambapo hupata ruzuku kutoka Serikalini kwa ajili kusaidia gharama za uendeshaji.

172. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha ufanisi wa utoaji wa huduma na kupunguza utegemezi kwa Serikali, katika mwaka 2023/24, Wizara ilifanya tathmini kubaini uwezo wa kujiendesha kwa mamlaka za maji. Matokeo ya tathmini hiyo ilizipandisha hadhi ya madaraja baadhi ya mamlaka ambapo mamlaka sita (6) zilitoka A kwenda AA; nne (4) kutoka daraja B kwenda A; tisa (9) kutoka daraja C kwenda B na mamlaka nne (4) ambazo hazikuwa daraja maalum kwenda daraja C. Kupandishwa kwa hadhi kwa mamlaka hizo kunaziongezea motisha katika kutoa huduma bora, kukusanya mapato, kupunguza utegemezi kwenye ruzuku na kuhimili gharama za uendeshaji.

173. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na jitihada za kuimarisha ufanisi wa utoaji wa huduma kwa mamlaka za maji, bado kumekuwa na changamoto mbalimbali zikiwemo, upotevu wa maji, malalamiko ya bili za maji, migawo ya maji, wateja kuchelewa kuunganishiwa huduma na utegemezi kwenye ruzuku. Katika kukabiliana na changamoto hizo, mamlaka za maji zimeelekezwa kufunga dira za maji kwa wateja wote, kufunga dira za maji za malipo kabla kwa wateja wa majumbani na taasisi pamoja na kuhakikisha wateja wanaunganishiwa huduma kwa wakati kulingana na mkataba wa huduma kwa mteja *(client service charter)*.

174. **Mheshimiwa Spika**, aidha, katika kupunguza utegemezi wa ruzuku, mamlaka za maji zimeelekezwa kutafuta vyanzo mbadala vya fedha za uwekezaji ambapo hadi sasa

mamlaka **13** zimekopa fedha za uwekezaji kutoka kwenye taasisi za fedha. Mamlaka hizo ni Arusha, Iringa, Moshi, Singida, Kahama, Dar es Salaam, Bunda, Tanga, Tabora, Songea, Mtwara, Mwanza na Shinyanga. Vilevile, mamlaka zimetakiwa kutumia fursa zilizopo katika soko la hisa ili kupata mitaji ya uwekezaji kwenye ujenzi wa miundombinu ya majisafi na majitaka. Katika kutekeleza maelekezo hayo, Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Tanga, imekuwa mamlaka ya kwanza kuzindua uuzaji wa hati fungani ya kijani yenye thamani ya **Shilingi 53,120,000,000**, fedha ambazo zitatumika kuboresha huduma ya maji kwenye maeneo yanayohudumiwa na mamlaka hiyo.

175. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara imeendelea kuzijengea uwezo Mamlaka za maji kwa kujenga ofisi katika Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira ambapo jengo la ofisi la mamlaka ya Maji Arusha limekamilika; na ujenzi wa majengo unaendelea na umefikia hatua mbalimbali za utekelezaji katika mamlaka ya Maswa **(asilimia 98)**, Sengerema **(asilimia 75)**, MugangoKiabakari **(asilimia 95)**, Kondoa **(asilimia 95)** na Biharamulo **(100)**. Vilevile, Wizara imezipatia magari **sita (6)** Mamlaka za Maji za Kigoma, Kasulu, Kibondo, Ushirombo, Ngara na Biharamulo kwa ajili ya shughuli za uendeshaji na matengenezo.

### 3.3.4. Bodi za Maji za Mabonde

176. **Mheshimiwa Spika**, Bodi za Maji za Mabonde *(Basin Water Boards - BWBs)* ni Taasisi zinazotekeleza majukumu yake kupitia Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, Sura 331. Nchi yetu imegawanyika katika mabonde tisa (9) ambapo mgawanyo wake unatokana na mipaka ya kihaidrolojia. Mabonde hayo ni Pangani, Rufiji, Wami-Ruvu, Ruvuma na Pwani ya Kusini, Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, Ziwa Rukwa na Bonde la Kati. Katika mwaka 2023/24, Bodi za Maji za Mabonde ziliendelea kutekeleza majukumu yake ikiwemo kufanya ufuatiliaji na tathmini ya rasilimali za maji nchini; kugawa na kudhibiti matumizi ya maji ili kuondoa migogoro; kuhifadhi na kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji; na kuandaa na kutekeleza Mipango

Shirikishi ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji. Katika kuziimarisha Bodi za Maji za Mabonde, Wizara imeendelea kuzijengea uwezo kwa kuzipatia ofisi, watumishi na vitendea kazi.

### 3.3.5. Chuo cha Maji

177. **Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Maji ni taasisi yenye jukumu la kuandaa wataalam wa maji, kutoa ushauri wa kitaalam pamoja na kufanya tafiti mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya maji. Chuo kinatoa mafunzo katika ngazi ya Astashahada, Stashahada, Shahada na Shahada ya Uzamili (yaani *Masters*). Mafunzo yanayotolewa katika ngazi za Astashahada na Stashahada ni Uhandisi wa Maji na Usafi wa Mazingira (*Water Supply and Sanitation Engineering*); Uhandisi wa Umwagiliaji (*Irrigation Engineering*); Haidrojiolojia na Uchimbaji wa Visima (*Hydrogeology and Water Well Drilling*); Haidrolojia na Hali ya Hewa (*Hydrology and Meteorology*); Uhandisi wa Usafi wa Mazingira (*Sanitation Engineering*) pamoja na Teknolojia ya Maabara na Ubora wa Maji (*Water Quality Laboratory Technology*).

178. **Mheshimiwa Spika**, katika ngazi ya Shahada mafunzo yanatolewa katika fani za Uhandisi wa Rasilimali za Maji na Umwagiliaji (*Bachelor Degree in Water Resources and Irrigation Engineering*); Uhandisi wa Usafi wa Mazingira (*Bachelor Degree in Sanitation Engineering*); Maendeleo ya Jamii na Uhandisi wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira (*Community Development for Water Supply and Sanitation Engineering*); Haidrojiolojia na Uchimbaji (*Hydrogeology and Drilling*) na Uhandisi wa Haidrolojia (*Engineering Hydrology*). Aidha, katika ngazi ya Shahada ya Uzamili, mafunzo yanatolewa katika fani za Uhandisi wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira (*Master in Water Supply and Sanitation Engineering*) na Rasilimali Maji na Usimamizi wa Huduma (*Master in Water Resources and Utility Management*). Vilevile, Chuo kinaendesha kozi mbalimbali za muda mfupi katika sekta za maji na umwagiliaji.

179. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2023/24, jumla ya wanafunzi **1,785** wa Astashahada, Stashahada, Shahada na Shahada ya Uzamili wamedahiliwa ambapo wanafunzi **1,619** wamedahiliwa Kampasi ya Ubungo na **166** Kampasi ya Singida. Hadi mwezi Aprili, 2024, Chuo kina jumla ya wanafunzi **3,546** ikilinganishwa na wanafunzi **2,835** katika mwaka 2022/23 ikiwa ni ongezeko la **asilimia 25**. Aidha, katika mahafali ya mwezi Novemba 2023, jumla ya wanafunzi **682** walihitimu mafunzo yao ambapo wanafunzi **230** ni wa Shahada, **423** ni Stashahada na wanafunzi **29** wa ngazi ya Astashahada. Uhitimu huo umeongezeka kwa **asilimia 47** ikilinganishwa na wahitimu **464** wa mwezi Novemba, 2022.

180. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha taaluma bora inatolewa, Chuo kimeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake katika ngazi za Shahada ya kwanza, Uzamili na Uzamivu. Hadi mwezi Aprili, 2024, watumishi **12** wanaendelea na mafunzo ya Shahada ya Uzamivu (*PhD*); Watumishi watano **(5)** Shahada ya Uzamili (*Masters*); watumishi Watatu **(3)** Shahada ya kwanza na watumishi **25** walipatiwa mafunzo ya muda mfupi. Vilevile, Chuo kimeendelea kuongeza idadi ya watumishi ambapo katika mwaka 2023/24, Chuo kimeajiri watumishi **17** na hivyo kuwa na jumla ya watumishi **99**. Mahitaji ya watumishi kwa sasa ni **180**, na Chuo kipo katika hatua za kuajiri watumishi wengine **33** wa kada mbalimbali ambapo usaili umekamilika na watumishi hao watakuwa wamepatikana mwezi Juni, 2024. Aidha, Chuo kinaendelea na ujenzi wa jengo la maktaba na ukarabati mkubwa wa majengo, ikiwa ni pamoja na kuongeza *floors* (*vertical extension*) kwa gharama ya **Shilingi 5,094,843,455.** Hadi mwezi Aprili, 2024 kazi ya ujenzi na ukarabati wa jengo la maktaba imefikia **asilimia 75**, na inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024.

### 3.4. Masuala Mtambuka

#### 3.4.1. Rasilimali Watu katika Sekta ya Maji

181. **Mheshimiwa Spika**, mahitaji halisi ya rasilimali watu katika sekta ya maji kwa kada mbalimbali ni watumishi **10,640**. Kwa sasa sekta ina watumishi **9,293** hivyo, kuwa na upungufu wa watumishi **1,347**. Serikali imeendelea kuajiri watumishi wa kada mbalimbali ili kukidhi mahitaji ya sekta ambapo katika mwaka 2023/24, jumla ya watumishi **420** wameajiriwa ikihusisha kada za Wahandisi, wahaidrolojia, wahaidrojiolojia, Wakemia na Kada Saidizi. Katika kutatua upungufu uliopo, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - UTUMISHI itaendelea kuajiri wataalam wa kada mbalimbali ili kufikia malengo ya sekta ya kuwahudumia wananchi.

182. **Mheshimiwa Spika**, aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ndani na nje ya nchi. Hadi mwezi Aprili 2024, jumla ya watumishi **1,487** walipatiwa mafunzo ambapo watumishi **1,390** walipatiwa mafunzo ya muda mfupi na watumishi **97** walipatiwa mafunzo ya muda mrefu. Aidha, katika kukuza taaluma na weledi kwa wahandisi wa maji, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo wahandisi hao kwenye fani zao ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wamesajiliwa na Bodi ya Usajili ya Wahandisi nchini (*Engineers Registration Board - ERB*). Vilevile, wahandisi **77** wamesajiliwa na *ERB* kama wahandisi wataalam na wahandisi **85** wapo kwenye hatua mbalimbali za kusajiliwa.

#### 3.4.2. Sheria

183. **Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa Sheria Na. 5 ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019, Wizara imetayarisha Notisi **mbili (2)** kwa ajili ya kuongeza maeneo ya huduma kwa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira ya *Handeni Trunk* Main (HTM) kupitia Tangazo la Serikali Na. 774 la tarehe 03/11/2023 na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Tabora kupitia Tangazo la Serikali Na. 771

la tarehe 13/11/2023. Vilevile, Wizara imetayarisha Notisi **mbili (2)** kwa ajili ya kuanzisha Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mkwajuni kupitia Tangazo la Serikali Na. 173 la tarehe 03/11/2023 na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Kakonko kupitia Tangazo la Serikali Na. 754 la tarehe 20/10/2023.

184. **Mheshimiwa Spika**, aidha, Wizara imeandaa Notisi za kupandisha madaraja ya Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira **23**, ambapo Mamlaka za Maji **sita (6)** za Dar es Salaam, Iringa, Kahama, Moshi, Mwanza na Tanga zimepandishwa kutoka daraja A kwenda daraja AA kupitia Tangazo la Serikali Na. 473 la tarehe 14/7/2023; Mamlaka za Maji **nne (4)** za Bukoba, Kahama – Shinyanga, Igunga na Nzega zimepandishwa kutoka daraja B kwenda daraja A kupitia Tangazo la Serikali Na. 472 la tarehe 14/7/2023; Mamlaka za Maji **tisa (9)** za Babati, Bunda, Geita, Mafinga, Makambako, Masasi – Nachingwea, Mpanda, Lindi na Njombe zimepandishwa kutoka daraja C kwenda daraja B kupitia Tangazo Na. 471 la tarehe 14/07/2023; na Mamlaka za Maji **nne (4)** za Busega, Kyela – Kasumulu, Rombo na Same – Mwanga kupandishwa kutoka daraja lisilo maalum kwenda daraja C kupitia Tangazo la Serikali Na 474.

### 3.4.3. Jinsia

185. **Mheshimiwa Spika**, uwiano wa jinsia ni muhimu katika vyombo vya maamuzi, usimamizi, uendeshaji na utekelezaji wa miradi ya maji nchini. Katika kutimiza azma hiyo, Wizara imeendelea kuhamasisha na kuhakikisha uwepo wa uwiano wa jinsia kwenye taasisi zilizopo chini ya Wizara katika ngazi mbalimbali za utekelezaji na utoaji maamuzi. Taasisi zilizopo chini ya Wizara ni Bodi za Maji za Mabonde, Mamlaka za Maji, Wakala wa Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, Mfuko wa Taifa wa Maji na Chuo cha Maji. Hadi mwezi Aprili 2024, idadi ya watumishi wanawake ni **5,663** sawa na asilimia **60** na wanaume **3,642** sawa na **asilimia 40**. Vilevile kwa upande wa utawala ngazi ya Wizara na Taasisi, kati ya viongozi wa ngazi mbalimbali waliopo, wanawake ni **201** sawa na

**asilimia 24** na wanaume ni **622** sawa na **asilimia 76**. Aidha, Wizara imeweka miongozo ya uundaji wa Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii inayozingatia masuala ya jinsia ili kuleta usawa kwenye maamuzi. Vilevile, uteuzi wa kamati na vikosi kazi mbalimbali huzingatia uwiano wa jinsia ili kuhakikisha watumishi wote wanashiriki kikamilifu katika kutekeleza majukumu na pia, kufanya maamuzi bila kujali jinsia zao.

### 3.4.4. Mapambano Dhidi ya Rushwa

186. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea na juhudi za kuzuia na kupambana na rushwa kwa kutekeleza na kusimamia Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji wa Awamu ya Nne *(National Anti-Corruption Strategy and Action Plan - NACSAP IV)*. Aidha, Wizara inatekeleza Mkataba wa Huduma kwa Mteja wa mwaka 2003 ambao unalenga kuhakikisha wananchi wanatambua haki na wajibu wao katika kupokea huduma mbalimbali zinazotolewa na Wizara na Taasisi zake. Vilevile, Kamati za Maadili zilizoundwa ngazi ya Wizara na Taasisi zake zimeendelea kusimamia masuala ya maadili mahali pa kazi ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo yanayohusu maadili na mapambano dhidi ya rushwa. Kwa ujumla, hali ya mapambano dhidi ya rushwa imeendelea kuimarika na hivyo, kupunguza viashiria vya rushwa kwenye maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na masuala yanayohusu ununuzi wa wakandarasi, wataalam washauri na huduma nyingine zinazotolewa.

### 3.4.5. UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza

187. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutoa elimu kuhusu afya hususan kujikinga dhidi ya maambukizi ya UKIMWI na magonjwa yasiyoambukiza kwa watumishi wake pamoja na Taasisi zake. Hadi mwezi Aprili 2024, jumla ya watumishi **3,283** walipata mafunzo maalum kuhusu kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza na yanayoambukiza ikiwa ni pamoja na kufanya vipimo ili kujua afya zao. Aidha, posho kwa ajili ya kununua lishe bora na usafiri kwa watumishi **tisa**

**(9)** wanaoishi na virusi vya UKIMWI imeendelea kutolewa. Vilevile, Wizara imeendelea kuhamasisha watumishi wake kufanya mazoezi na kuzingatia lishe bora ili kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza.

### 3.4.6. Ujenzi wa Majengo ya Wizara na Taasisi Zake

188. **Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa watumishi, Serikali inaendelea kujenga majengo ya ofisi kwenye maeneo mbalimbali nchini. Hadi mwezi Aprili 2024, Serikali imekamilisha ujenzi wa jengo la Makao Makuu Mtumba, Dodoma kwa gharama ya **Shilingi 22,957,343,341.80**. Aidha, ujenzi wa jengo la ofisi ya RUWASA Makao Makuu umeanza na ujenzi wa majengo **matano (5)** ya ofisi za RUWASA Mkoa katika mikoa ya Njombe, Geita, Manyara, Morogoro na Mara unaendelea na upo kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji. Vilevile, ujenzi wa jengo la Kituo Mahili cha Rasilimali za Maji (*Water Resource Centre of Execellence*) unaendelea na umefikia **asilimia 80**. Pia, Wizara imekamilisha ujenzi wa Ofisi ya Bodi ya Maji Bonde la Rufiji.

### 3.4.7. Kuimarisha Mifumo ya TEHAMA

189. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuongeza jitihada katika matumizi ya TEHAMA ili kuboresha huduma zinazotolewa na sekta. Katika mwaka 2023/24, Wizara imeendelea kujenga na kuboresha Mifumo ya Pamoja katika Sekta ya Maji kama ifuatavyo:-

***(a) Mfumo wa Pamoja wa Ankara za Maji (Unified Maji Billing System)***

190. **Mheshimiwa Spika**, Mfumo wa Pamoja wa Ankara za Maji umetengenezwa kwa ajili ya kusimamia ankara za maji zinazotolewa na Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira pamoja na Bodi za Maji za Mabonde. Pia, mfumo umelenga kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato yatokanayo na mauzo ya maji. Hadi sasa, mamlaka za maji **87** sawa na **asilimia 96.7** ya mamlaka

zote za maji na Bodi za Maji za Mabonde yote **tisa (9)** zinatumia mfumo huo. Aidha, mfumo huo umeboreshwa kwa kujumuisha Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii ambapo hadi mwezi Aprili 2024, CBWSOs **524** kwenye mikoa **14** ya Manyara, Kilimanjaro, Arusha, Iringa, Mwanza, Shinyanga, Katavi, Morogoro, Simiyu, Kagera, Mara, Geita, Singida na Tabora zimeanza kutumia mfumo huo.

***(b) Mfumo wa Kusimamia Shughuli za Taasisi (Enterprise Resource Management Suite)***

191. **Mheshimiwa Spika**, Mfumo wa Kusimamia Shughuli za Taasisi umeundwa kwa lengo la kuziwezesha Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira kutekeleza majukumu yake kwa njia ya kidijitali katika uchakataji wa masuala ya fedha, uhasibu, utumishi, ununuzi, usafiri na likizo. Hadi mwezi Aprili 2024, mamlaka za maji **36** sawa na **asilimia 40** ya mamlaka zote zimeanza kutumia mfumo huo.

***(c) Mfumo wa Kusimamia Shughuli za Maabara za Maji (Water Laboratory Information System - LIMS)***

192. **Mheshimiwa Spika**, Mfumo wa Kusimamia Shughuli za Maabara za Maji umeundwa kwa lengo la kuziwezesha maabara kutekeleza majukumu yake kidijitali. Hadi mwezi Aprili 2024, mfumo huo umefungwa kwa majaribio katika maabara **tano (5)** za Mwanza, Kigoma, Musoma, Dodoma, na Dar es Salaam. Baada ya majaribio kukamilika, mfumo utafungwa kwenye maabara zote 17 za maji.

***(d) Water Resources Operational Decision Support System (ODSS)***

193. **Mheshimiwa Spika**, *Water Resources Operational Decision Support System (ODSS)* ni mfumo ulioundwa kwa ajili ya kuzisaidia Bodi za Maji za Mabonde kufanya maamuzi ya rasilimali za maji kupitia huduma za kihaidrolojia na hali ya hewa. Hadi mwezi Aprili 2024, mfumo huo umefungwa kwa

majaribio katika Bodi za Maji za Mabonde **matatu (3)** ambazo ni Pangani, Rufiji na Wami Ruvu. Majaribio yatakapokamilika, mfumo utafungwa kwenye bodi zote tisa (9) za maji za mabonde.

## 4. MAFANIKIO YA SEKTA YA MAJI KATIKA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2023/24

194. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2023/24 chini ya uongozi mahiri wa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,** sekta ya maji imepata mafanikio makubwa ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kuongezeka kwa hali ya upatikanaji wa huduma ya maji vijijini kutoka wastani wa **asilimia 77** mwezi Desemba 2022 hadi **asilimia 79.6** mwezi Desemba, 2023 na mijini kutoka wastani wa **asilimia 88** mwezi Desemba, 2022 hadi **asilimia 90** mwezi Desemba, 2023.

(ii) Kupatikana kwa chanzo kipya cha fedha za utekelezaji wa miradi ya maji kupitia Hati Fungani ambapo Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga imekuwa mamlaka ya kwanza kuzindua uuzaji wa Hati Fungani ya Kijani yenye thamani ya **Shilingi bilioni 53.12**. Hadi mwezi Februari 2024, **Shilingi bilioni 54.72** sawa na **asilimia 103** zimekusanywa. Fedha hizo zitatumika kuboresha miundombinu ya usambazaji maji na utunzaji wa mazingira Jijini Tanga pamoja na miji ya Muheza, Pangani na Mkinga.

(iii) Kufikiwa kwa malengo ya programu ya PforR kwa muda uliopangwa ikiwa ni pamoja na kuvuka lengo la idadi ya wanufaika kutoka watu **milioni 3** hadi **milioni 4.07**. Hali hiyo imeifanya Benki ya Dunia kuitambua nchi ya Tanzania kuwa ya kwanza kati ya nchi zaidi ya 50 duniani kufanya vizuri katika utekelezaji wa Programu hiyo kwa

kipindi cha miaka miwili mfululizo. Mafaniko hayo yamesaidia kuongezeka kwa fedha za utekelezaji wa programu kutoka **Dola za Marekani milioni 350** hadi **Dola** za **Marekani milioni 654** na kuongeza mikoa inayonufaika kutoka **17** hadi **25** na Halmashauri kutoka **86** hadi **137.**

(iv) Kukamilika kwa miradi mikubwa na ya kimkakati ikiwemo mradi wa maji Arusha ambao umeongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 40** hadi **lita milioni 200** kwa siku na muda wa upatikanaji wa huduma ya maji kutoka **saa 12** hadi **saa 24** kwa siku; na kukamilika kwa mradi wa maji wa Butimba unaonufaisha wakazi wapatao **450,000** katika Jiji la Mwanza.

(v) Kuanzishwa kwa *Consultancy Bureau* katika Chuo cha Maji inayosaidia kutoa huduma za ushauri elekezi kwenye sekta ya maji na sekta nyinginezo ikiwa ni pamoja na uandaaji na usimamizi wa miradi; kuwajengea uwezo vijana wanaohitimu masomo na kusaidia kuongeza mapato ya taasisi.

(vi) Kuanza kwa utekelezaji wa mkakati wa kuwa na Gridi ya Taifa ya Maji kwa kutumia vyanzo vikubwa vya maji vya uhakika ikiwemo maziwa, mito na mabwawa kwa ajili ya kupeleka maji kwenye maeneo ambayo hayana vyanzo vya uhakika. Kwa mfano; mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria ambao umenufaisha miji ya Kahama, Shinyanga, Tinde, Nzega, Tabora, Igunga na Shelui pamoja na vijiji vilivyopo ndani ya kilomita 12 kutoka kwenye bomba kuu. Pia, mradi wa kutoa maji Ziwa Tanganyika kupeleka kwenye mikoa ya Kigoma, Rukwa na Katavi, ambao upo kwenye hatua za kumpata Mtaalam Mshauri atakayefanya usanifu wa mradi.

(vii) Kuanza kwa utekelezaji wa miradi ya maji ya kimkakati ikiwemo mabwawa ya Kidunda na Farkwa pamoja na Mradi wa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi – Simiyu.

(viii) Kukwamuliwa kwa miradi **157** kati ya miradi **177** ya maji vijijini iliyokuwa na changamoto ya kutokukamilika kwa muda mrefu.

(ix) Kuimarika kwa mazingira ya kazi kutokana na kukamilika na kuanza kutumika kwa jengo jipya la ofisi za Wizara lililopo Mtumba pamoja na ununuzi wa vitendea kazi ikiwemo magari, pikipiki na kompyuta.

(x) Kuendelea na ujenzi wa miradi ya maji katika miji 28 ambapo utekelezaji upo katika hatua mbalimbali.

(xi) Kukamilika kwa ujenzi wa mabwawa **12** ya ukubwa wa kati na madogo ya kuvuna maji ya mvua kwenye maeneo mbalimbali nchini yenye uwezo wa kuhifadhi maji **lita bilioni 1.86**. Uwepo wa mabwawa hayo unaongeza uhakika wa maji nchini *(water security)*.

(xii) Kukamilika kwa uchimbaji wa visima **283** na kuendelea na ujenzi wa mabwawa **12** kwa kutumia seti 25 za mitambo ya kuchimba visima na seti tano (5) za mitambo ya ujenzi wa mabwawa iliyonunuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**. Pia, mitambo hiyo imesaidia kukabiliana na janga la maafa la Hanang' mkoani Manyara kwa kuchimba visima **nane (8)** na kurejesha huduma ya maji kwa wananchi; na kuchimba visima **6** vinavyohudumia wananchi waliohama kutoka Ngorongoro kwenda Msomera.

(xiii) Kuimarika kwa usimamizi wa CBWSOs ambapo kwa mara ya kwanza katika mwaka 2022/23, Wizara kupitia RUWASA imeziwezesha CBWSOS **136** kuandaa Vitabu vya Hesabu (*Financial Statements*) za mwaka 2023/24 na kukaguliwa na CAG. Kati ya hizo, CBWSOs **133** sawa na **asilimia 98** zimepata Hati safi. Vilevile, katika kuimarisha udhibiti wa mapato ya fedha za umma, CBWSOs **661** zimejiunga katika Mfumo wa GePG na kuanza kukusanya mapato ya mauzo ya maji kupitia mfumo huo.

## 5. CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA NA HATUA ZINAZOCHUKULIWA

195. **Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2023/24, Wizara imekabiliana na changamoto mbalimbali. Miongoni mwa changamoto zilizojitokeza na hatua zinazochukuliwa ni kama ifuatavyo:-

### 5.1. Uchafuzi, Uharibifu na Uvamizi wa Vyanzo vya Maji

196. **Mheshimiwa Spika**, rasilimali za maji nchini zimeendelea kuathiriwa kutokana na uchafuzi, uharibifu na uvamizi wa vyanzo vya maji. Hali hiyo inatokana na ongezeko la watu linaloenda sambamba na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kijamii. Pamoja na hayo, uelewa mdogo wa jamii juu ya utunzaji wa vyanzo vya maji umechangia kwa kiwango kikubwa kuwepo kwa changamoto hizo katika rasilimali za maji.

197. **Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuimarisha usimamizi na uendelevu wa rasilimali za maji. Vilevile, Wizara imeendelea kuimarisha uhifadhi wa vyanzo vya maji kwa kuviwekea mipaka na kuvitangaza kwenye gazeti la Serikali. Aidha, elimu kuhusu sheria, kanuni na miongozo ya usimamizi wa rasilimali za maji pamoja na umuhimu wa kutunza vyanzo vya maji imeendelea kutolewa kwa jamii kupitia vyombo mbalimbali vya habari na mitandao ya kijamii.

## 5.2. Mahitaji Makubwa ya Fedha kwa ajili ya Uwekezaji wa Miradi Mikubwa ya Maji

198. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inakabiliwa na changamoto ya mahitaji makubwa ya fedha za uwekezaji kwa ajili ya kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati inayohusisha uvunaji wa maji ya mvua kwa kujenga mabwawa makubwa na ya ukubwa wa kati pamoja na ujenzi wa miundombinu ya kutoa maji kwenye maeneo yenye vyanzo vya maji vya uhakika kama maziwa na mito kwenda kwenye maeneo yenye uhaba wa maji.

199. **Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali imeendelea kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutumia fedha za ndani kutekeleza miradi hiyo mikubwa. Jitihada hizo zimewezesha kupatikana kwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa bwawa la Kidunda; kuendelea kwa kazi ya mapitio ya usanifu wa mradi wa bwawa la Farkwa pamoja na kuanza kwa utekelezaji wa mradi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika Mkoa wa Simiyu. Serikali itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati ambayo ni muhimu katika kuchangia uchumi wa nchi yetu.

## 5.3. Mabadiliko ya Tabianchi

200. **Mheshimiwa Spika**, mabadiliko ya tabianchi yameendelea kuathiri nchi yetu kwa kusababisha mafuriko, ukame wa muda mrefu na kupata mvua zisizotabirika. Athari za mabadiliko ya tabianchi zimechangia kupungua au kukauka kwa vyanzo vya maji, kupungua kwa uzalishaji wa maji na kusababisha kuongezeka kwa migao ya maji pamoja na kuharibika kwa miundombinu ya maji kutokana na mafuriko. Katika kipindi cha hivi karibuni nchi yetu imeshuhudia uwepo wa mvua kubwa za El-nino kwenye maeneo mbalimbali. Mvua hizo zimesababisha mafuriko, uharibifu wa miundombinu na vyanzo vya maji.

201. **Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali imeendelea na jitihada za ujenzi wa mabwawa ya kuvuna maji ya mvua kwa lengo la kuhifadhi maji na kudhibiti mafuriko. Vilevile, Wizara inaendelea kuhakikisha miundombinu ya maji inayojengwa inakuwa himilivu ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Aidha, Wizara inaendelea kuandaa maandiko mbalimbali kwa ajili ya kuibua miradi itakayosaidia katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

### 5.4. Uendelevu wa Miradi ya Maji Vijijini

202. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na jitihada za Serikali katika kuimarisha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji vijijini, uendelevu wa miradi umeendelea kuwa changamoto katika baadhi ya maeneo ya vijijini. Hali hiyo imetokana na kukauka kwa vyanzo vya maji, wananchi kushindwa kumudu gharama za uendeshaji na matengenezo, makusanyo hafifu ya mauzo ya maji pamoja na uharibifu wa miundombinu ya maji.

203. **Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto hizo, RUWASA imeendelea kuviimarisha kwa kuvijengea uwezo Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii ili viweze kusimamia na kuendesha skimu za maji kwa ufanisi; kufanya matengenezo makubwa ya miradi; kuboresha usimamizi wa mauzo ya maji na makusanyo kwa kufunga dira za malipo kabla ya matumizi, kuweka mfumo wa pamoja wa ankara (*Unified Maji Billing System*) na kujiunga kwenye mfumo wa makusanyo ya fedha za umma (*GePG*); kuendelea kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kuchangia gharama za huduma ya maji pamoja na kujenga miradi inayotumia vyanzo vya maji vya uhakika. Vilevile, katika kupunguza gharama za uendeshaji, Serikali imeendelea kufanya jitihada za kubadili matumizi ya nishati ya dizeli kwenda kwenye matumizi ya umeme jua na umeme wa gridi.

## 6. VIPAUMBELE NA MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2024/25

### 6.1. Vipaumbele vya Sekta

204. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeweka vipaumbele mbalimbali ambavyo vimezingatiwa katika mpango na bajeti ya mwaka 2024/25; lengo ni kuwapatia huduma ya maji safi na salama kwa zaidi ya asilimia 85 ya wananchi wa vijijini na zaidi ya asilimia 95 ya wakazi wa mijini. Utekelezaji wa vipaumbele, utazingatia majukumu ya Wizara yakiwemo kuimarisha usimamizi, uendelezaji, uhifadhi na utunzaji wa vyanzo vya maji pamoja na kuimarisha na kusimamia huduma za ubora wa maji. Vipaumbele hivyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kukamilisha utekelezaji wa miradi inayoendelea na kuendelea na ujenzi wa miradi mikubwa.

(ii) Kuongeza kasi ya uvunaji wa maji ya mvua kwa kujenga mabwawa ya ukubwa wa kati na mabwawa ya kimkakati.

(iii) Kufikisha huduma ya maji kwenye vijiji ambavyo havina huduma.

(iv) Kukamilisha uandaaji wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Maji *(Water Master Plan),* Mtandao wa Taifa wa Kusambaza Maji *(National Water Grid)* na mapitio ya Sera ya Taifa ya maji.

(v) Kupunguza upotevu wa maji.

(vi) Kuongeza kasi ya ufungaji wa dira za malipo kabla ya matumizi ya maji *(pre-paid water meters)*.

(vii) Kuongeza kasi ya uwekezaji kwenye usafi wa mazingira.

(viii) Kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika uwekezaji na uendeshaji wa skimu za maji.

## 6.2. Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2024/25

205. **Mheshimiwa Spika**, mpango na bajeti kwa mwaka 2024/25 umezingatia vipaumbele vya sekta pamoja na masuala ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji; usimamizi wa huduma za ubora wa maji; huduma ya majisafi na usafi wa mazingira vijijini; huduma ya majisafi na usafi wa mazingira mijini; na kujenga uwezo wa Wizara na Taasisi zake. Maelezo ya kina kuhusu mpango wa utekelezaji ni kama ifuatavyo:-

### 6.2.1. Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

***(a) Usimamizi wa Rasilimali za Maji***

206. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2024/25, Wizara itaendelea kuimarisha mfumo wa kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji ikiwemo ukarabati wa vituo **100** vya usimamizi wa rasilimali za maji; kutoa vibali **600** vya matumizi ya maji; kuunda jumuiya **18** za watumia maji na kuunda kamati **tisa (9)** za vidakio vya maji. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji shirikishi; kuendesha majukwaa ya wadau wa sekta mtambuka wa rasilimali za maji; kufanya tathmini ya rasilimali za maji; na kufanya ukaguzi wa vyanzo vya maji katika Bodi za Maji za Mabonde.

207. **Mheshimiwa Spika**, vilevile Wizara imepanga kuimarisha uhifadhi na utunzaji wa vyanzo vya maji kwa kutambua vyanzo vya maji juu ya ardhi na maeneo yenye hifadhi ya maji chini ya ardhi. Kwa upande wa maji chini ardhi, utafiti wa kina utafanyika ili kubaini maeneo yenye maji na kuyafanya kuwa maeneo tengefu. Vilevile, Wizara itaendelea kutambua, kupima, kuweka mipaka na kutangaza vyanzo vya maji kuwa maeneo tengefu katika gazeti la Serikali. Aidha, Wizara imepanga kuimarisha mifumo ya ugawaji maji kwa kutoa vibali vya matumizi pamoja na kuimarisha uhifadhi na udhibiti wa uchafuzi wa vyanzo vya maji.

### *(b) Uendelezaji wa Rasilimali za Maji*

208. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2024/25, Wizara imepanga kuendeleza rasilimali za maji kwa kutumia maji chini ya ardhi na juu ya ardhi kwa lengo la kuhakikisha usalama wa maji unakuwepo. Miradi iliyopangwa kutekelezwa ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa mabwawa ya kimkakati ikiwemo bwawa la Kidunda na kukamilisha maandalizi ya ujenzi wa mradi wa bwawa la Farkwa; kuanza ujenzi wa mabwawa **22** pamoja na kuendelea na ujenzi wa mabwawa **26** ya ukubwa wa kati na madogo; na kufanya usanifu wa mabwawa **45**. Aidha, Wizara itakamilisha maandalizi ya Mpango Kabambe wa Taifa wa Maji (*National Water Master Plan*) na Gridi ya Taifa ya Maji (*National Water Grid*) pamoja na kuendelea kusimamia uchimbaji wa visima virefu vya maji. ***Kiambatisho Na. 4*** kinaonesha mabwawa yaliyopangwa kutekelezwa katika mwaka 2024/25.

### 6.2.2. Usimamizi wa Huduma ya Ubora wa Maji

209. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2024/25, Wizara itaendelea kufanya tathmini na ufuatiliaji wa ubora wa maji katika vyanzo vya maji **2,200**, mifumo ya usambazaji maji **8,245** vijijini na mijini, na mifumo **150** ya majitaka. Vilevile, Wizara imepanga kuweka mifumo ya ukusanyaji na utunzaji wa takwimu na taarifa za ubora wa maji; kuendelea na utekelezaji wa mkakati wa kupunguza madini ya *flouride* kwenye maji ya kunywa na ya kupikia; na kuwezesha uandaaji na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mipango ya usalama wa maji katika mamlaka za maji **40** na *CBWSOs* **120**. Vilevile, Wizara itaendelea kuziboresha maabara za maji kwa kuzipatia vitendea kazi na kuziwezesha kupata na kudumisha hadhi ya ithibati katika viwango vya kimataifa.

### 6.2.3. Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini

210. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2024/25, Wizara imepanga kuendelea kutekeleza jumla ya miradi **1,095** (***Kiambatisho Na. 5***) ya usambazaji maji vijijini katika maeneo mbalimbali

nchini ikiwemo maeneo yanayozunguka vyanzo vya Bwawa la Kidunda na vijiji vilivyopitiwa na mradi wa Same - Mwanga. Aidha, kwa vijiji ambavyo havijafikiwa na huduma ya maji, Serikali imepanga kuchimba visima **vitano (5)** katika kila jimbo la uchaguzi kwenye maeneo ya vijijini na kwa kuanzia, Wizara itaanza na uchimbaji wa visima **900**. Utekelezaji wa miradi hiyo utaongeza hali ya upatikanaji wa huduma ya maji vijijini kutoka wastani wa **asilimia 79.6** hadi zaidi ya wastani wa **asilimia 85** ifikapo mwaka 2025.

211. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha uendelevu wa huduma ya maji vijijini, Wizara itaendelea kubadili mitambo inayotumia dizeli na kuweka umeme wa gridi ya taifa au nishati ya jua ili kupunguza gharama za uendeshaji wa skimu za maji; kuimarisha usimamizi wa mauzo ya maji na makusanyo kwenye *CBWSOs* kwa kufunga dira za malipo kabla ya matumizi *(pre-paid water meters)*; kuweka mfumo wa pamoja wa ankara za maji *(Unified Maji Billing System)*; na kujiunga kwenye mfumo wa makusanyo ya fedha za umma *(GePG)*. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika utoaji wa huduma ya maji, kuzijengea uwezo *CBWSOs* **1,382** na kuendelea kuziunganisha *CBWSOs* ili kuimarisha uwezo wa kujiendesha.

### 6.2.4. Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini

212. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2024/25, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo pamoja na sekta binafsi imepanga kutekeleza jumla ya miradi **247** ya maji mijini. Lengo ni kuhakikisha zaidi ya **asilimia 95** ya wakazi wa mijini wanapata huduma ya maji safi na salama ifikapo mwaka 2025. Miradi itakayotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya maji kutoka Mto Kiwira kupeleka Jiji la Mbeya; mradi wa kutoa maji Mto Ruvuma kupeleka Mtwara; mradi wa kutoa maji Mto Momba kwenda Tunduma; kutoa maji kutoka tanki la Bisarye mradi wa kutoa maji Mto Rufiji kwenda mikoa ya Dar es Salaam na Lindi; kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miradi ya maji kupitia mradi wa miji 28; mradi wa maji na usafi wa mazingira Vwawa – Tunduma; utekelezaji wa miradi ya uondoshaji majitaka katika miji

mikuu ya mikoa, miji mikuu ya wilaya na miji midogo; kuendelea kuimarisha usimamizi wa utoaji huduma, uendeshaji na matengenezo ya skimu za maji; na kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ikiwa ni hatua za awali za maandalizi ya miradi ya maji katika maeneo mbalimbali ikiwemo mradi wa kutoa maji Mto Rufiji kupeleka katika mikoa ya Dar es Salaam na Lindi. Miradi ya maji na usafi wa mazingira mijini itakayotekelezwa katika mwaka 2024/25 imeoneshwa kwenye ***Kiambatisho Na. 6***.

213. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Jiji la Dodoma, Wizara imepanga kuboresha huduma ya maji kwa kutekeleza mipango ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. Mpango wa muda mfupi ni kuendelea na utekelezaji wa miradi ya majisafi maeneo ya Jiji la Dodoma na Chamwino, DTC Nala, Nala ITRACOM, Njedengwa National Housing hadi UDOM, Zuzu-Nala na mradi wa maji Nzuguni Awamu ya Pili. Vilevile, Wizara itajenga mtandao wa majisafi na kuchimba visima katika Mji wa Serikali ikiwa ni pamoja na maeneo ya pembezoni mwa Jiji. Katika mpango wa muda wa kati, Wizara itaanza ujenzi wa mradi wa bwawa la Farkwa; na mpango wa muda mrefu ni kutekeleza mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda Jiji la Dodoma kupitia Singida.

### 6.2.5. Kupunguza Upotevu wa Maji

214. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2024/25, Wizara imepanga kufanya ukarabati wa miradi ya maji na kudhibiti wizi wa maji ili kupunguza kiwango cha maji yanayopotea ambacho hadi sasa kimefikia wastani wa **asilimia 35.3** ya maji yanayozalishwa. Kiwango hicho ni kikubwa kikilinganishwa na kiwango kinachokubalika kimataifa cha **asilimia 20**. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na ukarabati wa miundombinu ya maji iliyochakaa; kufunga dira za maji ya jumla (*bulk meters*); kufunga dira za maji kwa wateja wote; kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kulinda miundombinu ya maji; na kushirikisha viongozi wa mikoa, Jeshi la Polisi na wananchi katika kuwabaini na kuwachulia hatua stahiki

wanaojihusisha na wizi wa maji na uharibifu wa miundombinu ya maji.

### 6.2.6. Kuimarisha Utoaji wa Huduma ya Maji

215. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2024/25, Wizara itaendelea kuimarisha utoaji wa huduma bora ya maji kwa lengo la kuinua hali ya maisha ya wananchi, kudhibiti bei za maji, kuondoa migao ya maji, kuunganisha huduma kwa wakati na kupunguza malalamiko yatokanayo na huduma ya maji. Katika kuhakikisha azma hiyo inatimia, Wizara itasimamia ufungaji wa dira za maji za malipo kabla (*prepaid metres*); kutumia na kuendelea kuboresha mfumo wa pamoja wa ankara za maji (*Unified Maji Billing System*); na kuhakikisha wateja wanaunganishiwa huduma ya maji kwa wakati.

### 6.2.7. Kujenga Uwezo wa Kitaasisi

216. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2024/25, Wizara itakamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Maji ya Mwaka 2002; kuendelea kujenga uwezo wa kitaasisi wa sekta ya maji ikiwa ni pamoja na watumishi na kukiwezesha Chuo cha Maji kuendelea kutoa wataalam kulingana na mahitaji. Aidha, Wizara itaendelea kuujengea uwezo Mfuko wa Taifa wa Maji ili uweze kupata ithibati kwa ajili ya kupata fedha za Mifuko ya Mabadiliko ya Tabianchi. Vilevile, Wizara itaendelea kuimarisha mifumo ya TEHAMA; na ufuatiliaji na tathmini ili kuongeza ufanisi.

## 7. SHUKRANI

217. **Mheshimiwa Spika**, kipekee napenda kutumia fursa hii kuwashukuru wananchi pamoja na wadau mbalimbali kwa ushrikiano wao katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu kwa mwaka 2023/24. Maandalizi ya bajeti hii ya wizara yamezingatia michango, maoni na mapendekezo yaliyotolewa na wadau katika kuweka vipaumbele vinavyolenga kuboresha utoaji wa huduma za

maji na usafi wa mazingira. Ushirikishwaji wa wadau na makundi mbalimbali ya jamii unadhihirisha umuhimu wao katika kuhakikisha tunakuwa na bajeti inayokidhi matarajio ya wananchi na maendeleo ya Sekta ya Maji.

218. **Mheshimiwa Spika**, kwa dhati ya moyo wangu, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru wewe Spika na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa mnayoifanya katika kuhakikisha sekta yetu ya maji inafikia azma ya Serikali ya kuwapatia wananchi wote maji safi, salama na ya kutosheleza. Ninaomba Mwenyezi Mungu awabariki sana.

219. **Mheshimiwa Spika**, napenda pia, kutoa shukrani zangu kwa Nchi Rafiki, Washirika wa Maendeleo, Mashirika ya Misaada ya Kimataifa, Sekta Binafsi, Taasisi Zisizo za Kiserikali, Mashirika ya Kidini na Wadau Wengine kwa ushirikiano wanaoutoa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu.

220. **Mheshimiwa Spika**, kipekee ninapenda kuzishukuru nchi rafiki tunazoshirikiana nazo zikiwemo Uingereza, Ujerumani, India, Marekani, Korea Kusini, Uholanzi, Hispania, Misri, Ufaransa, Kuwait, Ubelgiji, Italia na Saudi Arabia. Vilevile, ninayashukuru Mashirika ya Maendeleo na Taasisi za Kimataifa kwa misaada ya kitaalam na kifedha katika kuiwezesha Sekta ya Maji kutekeleza majukumu yake. Mashirika na Taasisi hizo ni pamoja na Benki ya Dunia (*World Bank - WB*), Benki ya Maendeleo ya Africa (*AfDB*), Benki ya Maendeleo ya Ujerumani *(KfW),* Benki ya Uwekezaji ya Umoja wa Ulaya *(EIB)*, Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika *(BADEA)*, Mfuko wa Maendeleo wa Nchi zinazozalisha Mafuta *(OPEC Fund for International DevelopmentOFID)*, Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait *(Kuwait Fund)*, Mfuko wa Maendeleo wa Saudia (*SFD), Foreign Commonwealth and Development Office (FCDO),* Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*), Shirika la Maendeleo la Ujerumani *(GiZ),* Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*AFD*), *Global Environment Facility (GEF), Green Climate Fund (GCF),* Shirika la Afya Duniani *(WHO),* Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (*UNICEF),* Shirika la

Maendeleo la Ubelgiji *(BTC),* Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (*UNDP)* na Shirika la Misaada la Marekani (*USAID)*.

221. **Mheshimiwa Spika**, viongozi na waumini wa dini mbalimbali wamekuwa na mchango muhimu katika kudumisha amani na utulivu wa nchi yetu. Kwa namna ya pekee ninawashukuru kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuliombea Taifa na ninawaomba waendelee kuliombea Taifa letu na viongozi wetu. Vilevile, ninayashukuru Mashirika na Taasisi za Kidini ambazo zimeendelea kusaidia Sekta ya Maji katika kufikia malengo yake. Mashirika na Taasisi hizo ni pamoja na *Catholic Agency for Overseas Aid and Development (CARITAS)*, *Adventist Development Relief Agency (ADRA), Norwegian Church Aid, Livingwater International, World Islamic League,* Shirika la *Ahmadiya Muslim Jamaat Tanzania, Islamic Foundation,* Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA), Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Kanisa Katoliki Tanzania na Kanisa la Anglikana Tanzania.

222. **Mheshimiwa Spika**, napenda pia kuzishukuru Taasisi zisizo za Kiserikali ambazo zimekuwa na mchango muhimu katika maendeleo ya sekta ya maji nchini. Taasisi hizo ni pamoja na *Association of Tanzanian Water Suppliers (ATAWAS), OIKOS, Tanzania Water and Sanitation Network (TAWASANET),* Wahamasishaji wa Maji, Maendeleo na Afya *(WAMMA), World Vision*; *Worldwide Fund for Nature (WWF*), *Netherlands Volunteers Services (SNV), Plan International*, *Concern Worldwide*, WaterAid Tanzania, *Water Mission* (T), Shirika la Kimataifa la Kuhifadhi Uasili na Maliasili (*IUCN*), Shahidi wa Maji na Mashirika mengine mbalimbali.

223. **Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee kabisa naomba nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Naibu Waziri wa Maji **Mheshimiwa Mhandisi Kundo Andrea Mathew (Mb)** ambaye kwa kipindi kifupi tangu kuteuliwa kwake, tumeshirikiana naye katika kuendeleza kazi kubwa ya kuhakikisha Sekta ya Maji inasonga mbele na wananchi wengi zaidi wanafikiwa na huduma ya maji. Vilevile,

naomba kuwapongeza **Mhandisi Mwajuma Waziri** kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji na **Bibi Agnes Kisaka Meena** kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji. Imani na dhamana waliyopewa na Mheshimiwa Rais ni kubwa na ninaamini katika utendaji wao tutafanya mageuzi makubwa katika kuongeza kasi ya maendeleo katika Sekta ya Maji. Aidha, kipekee napenda kuwashukuru Viongozi wa Taasisi, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, na Watumishi wote wa Wizara ya Maji na Taasisi zake kwa ushirikiano wanaonipatia pamoja na kujituma kwao kwa kusimamia utekelezaji wa majukumu yao kwenye Sekta ya Maji kwa kiwango cha hali ya juu.

224. **Mheshimiwa Spika**, naomba nieleze kuwa ninayo furaha kubwa kuendelea kuishukuru familia yangu na wananchi wa Jimbo la Pangani kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Napenda kuwaahidi kuwa nitatumia weledi, maarifa na uwezo wangu wote niliojaliwa na Mwenyezi Mungu katika kulijenga jimbo letu na Taifa kwa ujumla.

## 8. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2024/2025

225. **Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, ninaomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 627,778,338,000** kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2024/25, ambapo **Shilingi 69,662,959,000** ni fedha za matumizi ya kawaida na **Shilingi 558,115,379,000** ni fedha za maendeleo.

226. **Mheshimiwa Spika**, kati ya fedha za matumizi ya kawaida, **Shilingi 17,542,812,000** ni kwa ajili ya kugharamia matumizi mengineyo (*OC*) na **Shilingi 52,120,147,000** ni kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi (*PE*) wa Wizara, RUWASA, Mfuko wa Taifa wa Maji na Chuo cha Maji. Kwa upande wa fedha za maendeleo, **Shilingi 340,463,656,000** sawa na **asilimia 61** ni fedha za ndani na **Shilingi 217,651,723,000** sawa na **asilimia 39** ni fedha za nje.

227. **Mheshimiwa Spika**, ninaomba tena kutoa shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara *www.maji.go.tz*

228. **Mheshimiwa Spika**, ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Sasa namuita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira. Mheshimiwa Jackson Kiswaga, aje awasilishe Maoni ya Kamati.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuleta Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2023/2024, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo, kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, Utangulizi. Naomba taarifa hii yote iingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na uhai na kuweza kuiona siku hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii imegawanyika katika Sehemu Kuu Tatu, kama zinavyoonekana katika Taarifa ya Kamati. Taarifa hii inakusudia kuliwezesha Bunge lako Tukufu, kwa niaba ya wananchi, kujadili Hotuba ya Waziri wa Maji aliyoiwasilisha mapema hii leo.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 inaweka masharti yanayozingatiwa na Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta ikiwemo Kamati hii, kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha unaoisha. Aidha, Masharti ya Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge yanaitaka Kamati kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, ili kulinganisha na Makadirio ya Matumizi ya Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, Matokeo ya Uchambuzi wa Miradi ya Maendeleo; Kamati ilizingatia Masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 ya kutembelea na kukagua Miradi 6 ya Maendeleo iliyotekelezwa na Wizara ya Maji iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 katika Mikoa ya Iringa, Njombe na Ruvuma kuanzia tarehe 12 mpaka 18 Machi, 2024. Miradi iliyotembelewa ni pamoja na:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji, Itagutwa, Mkoani Iringa; Mradi huu unatekelezwa kwa gharama ya Shilingi 322,000,067,025 ambazo ni Fedha za Mfuko wa Maji na Fedha kutoka Benki ya Dunia kupitia Programu ya Malipo kwa Matokeo *(Program for Results (PforR)*. Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya shilingi 320,935,960 zililipwa na utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 98, ambapo wananchi wapatao 4,215 watanufaika katika huduma ya maji kwa majaribio. Kamati inaipongeza Serikali kwa utekelezaji wa mradi huu ambao kwa kiasi kikubwa unawezesha wananchi, hususan akinamama, kushiriki katika shughuli za maendeleo badala ya kutumia muda wao mwingi katika utafutaji wa maji.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji, Nyamlenge II, Mkoani Iringa; Mradi huu unatekelezwa katika Wilaya ya Iringa kwa gharama ya shilingi 1,170,174,638. Katika Mwaka wa Fedha

2023/2024 kiasi cha shilingi 675,485,709 kilitengwa, kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huu. Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya Shilingi 1,017,270,639 zililipwa huku utekelezaji wake ukifikia asilimia 98.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Bwawa la Masaka; ujenzi wa Bwawa lenye ukubwa wa lita za ujazo 439,803 umekamilika na umegharimu kiasi cha Shilingi 1,698,159,182.41.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Igongwi (*Lot 1*,2,3 na 4). Mradi huu unatekelezwa katika Halmashauri ya Njombe Mji, Mkoani Njombe, ambapo utekelezaji wake upo katika vipande *(lots)* vinne, kama inavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji Ngumbo Awamu ya Pili. Mradi huu unatekelezwa na Mkandarasi mzawa katika Wilaya ya Nyasa, Mkoani Ruvuma kwa gharama ya shilingi 2,030,668,500. Hadi kufikia Mwezi Machi, 2024 utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 60.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji wa Malungu. Mradi huu unatekelezwa katika Wilaya ya Nyasa Mkoani Ruvuma kwa gharama ya shilingi 1,222,759,056.69 kwa Fedha za Mfuko wa Maji na Fedha za Mfuko wa Serikali Kuu. Mradi haujatekelezwa kwa wakati kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo, kutopelekwa kwa mabomba kwa wakati. Maelezo ya kina kuhusu miradi hii yanapatikana katika Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kamati iliridhishwa na utekelezaji wa miradi hii. Kamati inampongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutoa fedha nyingi katika Miradi ya Maji inayotekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati. Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo 11. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, kwa kiasi kikubwa Maoni na Ushauri wa Kamati umezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, mfano wa ushauri ambao umezingatiwa unahusu Wizara kuweka utaratibu wa watalaam katika Sekta ya

Maji kutembeleana na kubadilishana uzoefu, ili kuleta ufanisi katika Miradi ya Maji. Utekelezaji huo ulioripotiwa unaonesha kuwa, Wizara imeandaa Mwongozo wa Usimamizi kwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira, unaoendelea katika mamlaka zenye uwezo na zilizofanikiwa kuzijengea uwezo mamlaka changa na zenye uwezo mdogo.

Mheshimiwa Spika, vilevile viongozi na watalaamu wa Wizara za Maji wa pande zote mbili za Muungano wamekuwa wakikutana ili kubadilishana uzoefu katika maeneo mbalimbali ikiwemo utunzaji wa vyanzo vya maji na ujenzi wa miradi ya maji. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia sehemu kubwa ya ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi ni rai ya Kamati kwamba, Serikali iendelee kutekeleza kikamilifu na kwa haraka maeneo ambayo utekelezaji wake umefanyika kwa kiwango cha chini. Mfano, ushauri huu ni kwa Serikali kuongeza juhudi za kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kutekeleza Mwongozo wa Uvunaji wa Maji ya Mvua.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa ukusanyaji wa maduhuli; kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Maji iliidhinishiwa kukusanya jumla ya shilingi 1,200,001,000. Hadi mwezi Februari 2024, Wizara ilikusanya kiasi cha shilingi 983,669,897 sawa na 82% ya lengo. Mchanganuo wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli na kiasi kilichokusanywa hadi Februari 2024 yanaonekana katika Kielelezo Na. 1 katika Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati unaonesha kuwa, mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa Wizara ya Maji hadi Februari 2024, ni 82% ya lengo. Hali hii ni dalili nzuri kwamba Wizara itaweza kufikia lengo la ukusanyaji wa maduhuli kutokana na vyanzo hivyo ifikapo mwezi Juni, 2024.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mipango na majukumu ya Wizara ya Maji; bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, ililenga kufanikisha utekelezaji wa mipango na majukumu ya Wizara ya Maji na taasisi zilizo chini ya Wizara. Hivyo katika maeneo ya matano ya sekta ya maji kama

yanavyoonekana katika Taarifa ya Kamati. Mafanikio yaliyopatikana kutokana katika sekta ya maji ni kama yanavyoonekana katika Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati inampongeza kwa dhati Mheshimiwa Jumaa Aweso (Mbunge), Waziri wa Maji pamoja na Watendaji Wakuu wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Mhandisi Mwajuma Waziri kwa usimamizi mahiri na madhubuti.

Mheshimiwa Spika, changamoto; pamoja na mafanikio yaliyopatikana kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati ilibaini changamoto zifuatazo: -

(i) Mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mikubwa ya maji ya kimkakati kama vile ujenzi wa Mabwawa ya Kidunda, Farkwa, Ndembela – Lugoda;

(ii) Uchafuzi, uvamizi na uharibifu wa vyazo vya maji unaotokana na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kijamii kandokando ya vyanzo vya maji;

(iii) Kukauka kwa vyanzo vya maji na kuharibika kwa miundombinu ya maji unaotokana na athari za mabadiliko ya tabianchi ikiwemo ukame wa muda mrefu na mafuriko.

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo; hadi kufikia Februari 2024, Wizara ya Maji ilipokea 81% ya Bajeti ya Miradi ya Maendeleo. Kiwango hicho cha upatikanaji wa fedha kinaendana na hali halisi ya utekelezaji wa bajeti. Kiasi kilichopatikana ni shilingi 563,398,121,378.53 kati ya shilingi 695,829,632,000 zilizoidhinishwa na Bunge kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 2 katika Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi wa Kamati yanaonesha kuwa, upatikanaji wa fedha kwa ajili kugharamia miradi ya maendeleo yanalenga kuimarisha upatikanaji wa huduma za maji safi na salama uliofikia 81% ya bajeti

iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili hiyo. Mwenendo wa upatikanaji wa fedha za maendeleo kwa wakati ni kiashiria kwamba, miradi ya maendeleo iliyopangwa kutekelezwa itakamilika kama ilivyokusudiwa ifikapo Juni, 2024. Upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni 87.6% ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili hiyo. Hali hii inaonesha dhamira nzuri ya Serikali ya kushirikiana na Washirika wa Maendeleo katika kuhakikisha kuwa wananchi wananufaika na miradi hii ili kuondokana na kero za kukosa maji.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha za Washirika wa Maendeleo kutoka nje upatikanaji wake ni 71.5% ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili hiyo. Hali hii inaonesha kwamba, bajeti iliyopangwa ni halisia na inaonesha ushirikiano wa dhati kati Washirika wa Maendeleo wa kutoka nje. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha za maendeleo kwa wakati na hivyo kuongeza kasi ya kutekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020-2025. Ni maoni ya Kamati kwamba, nchi inaendelea kuwa na usalama wa maji na kuimarisha huduma za maji safi na salama na kuwafikia wananchi kama ilivyoelezwa katika Ilani hiyo. Ni rai ya Kamati kwamba, kiasi cha fedha kilichobaki kitatolewa mapema kabla ya mwezi Juni ili miradi iweze kukamilika kwa 100%.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; hadi kufikia Februari 2024, Wizara ya ilipokea 61.3% ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kiwango hicho cha upatikanaji wa fedha hakiendani na hali halisi ya utekelezaji wa bajeti. Kiasi kilichopatikana ni shilingi 37,048,093,833.83 kati ya shilingi 60,375,474,000 zilizoidhinishwa na Bunge kama inavyoonekana katika Kielelezo Na.3 katika Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya maduhuli yatakayokusanywa; kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Maji inatarajia kukusanya jumla ya shilingi 1,200,001,000 kutokana na vyanzo vya mauzo ya nyaraka na zabuni, leseni za kampuni za utafiti na uchimbaji wa visima vya maji, tozo mbalimbali kwa wateja wanaopata huduma za Maabara za Ubora wa Maji na vibali vya matumizi ya maji katika mabonde.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2024/2025; kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Maji inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 627,778,338,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 69,662,959,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 558,115,379,000 sawa na 89% ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo za maendeleo shilingi 340,463,656,000 sawa na 61% ni fedha za ndani na shilingi 217,651,723,000 sawa na 39% ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati unaonesha kuwa, makadirio ya Bajeti yote ya Wizara ya Maji yamepungua kwa 17% ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Makadirio ya matumizi kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo yamepungua kwa kiasi cha shilingi 137,714,253,000 sawa na 18.4%, ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Ni mtazamo wa Kamati kwamba, kupungua kwa kiasi hiki cha bajeti ya maendeleo kutaathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyopangwa kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati haijaridhishwa na bajeti hii kwani haijazingatia ipasavyo maelekezo ya Serikali yaliyomo kwenye Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi wa Mwaka 2025. Ilani ya CCM iliahidi kuimarishwa kwa huduma ya maji safi na salama ifikapo mwaka 2025 kwa 85% kwa wananchi waishio vijijini na 95% kwa wakazi waishio mijini, wawe wamefikiwa na huduma hiyo ya maji. Msisitizo wa Kamati kwa Serikali ni kuhakikisha kwamba Bajeti ya Wizara ya Maji angalau inaongezwa kiasi cha shilingi 137,714,253,000 ili angalau ibakie kama ilivyokuwa mwaka uliopita wa fedha wa 2023/2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Maji dhidi ya Bajeti Kuu ya Serikali; Kamati imefanya ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Maji dhidi ya Bajeti Kuu ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ili kubaini ongezeko au upungufu wa Bajeti ya Wizara ya Maji dhidi ya Bajeti Kuu ya Serikali. Ulinganisho huo unaonekana kwenye Kielelezo Na. 6 katika Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa ulinganisho huo unaonesha kuwa, Bajeti ya Wizara ya Maji ya Mwaka wa Fedha 2024/2025 ni 1.3% ya Bajeti Kuu ya Serikali. Hali hii inaonesha kwamba, Bajeti ya Wizara ya Maji imepungua kwa 0.4% ukilinganisha na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Maendeleo ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ni 1.1% ya Bajeti Kuu ya Serikali ya Maendeleo ambayo ni 32%. Uchambuzi huo unaonesha kuwa Wizara ya Maji kwa mwaka huu haijawa kipaumbele kikubwa cha Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maelezo ya jumla; lengo la taarifa hii ni kubainisha maoni na ushauri wa Kamati ili kuwezesha Majadiliano ya Bunge. Pamoja na majadiliano kuhusu hoja hii, upo umuhimu wa kuzingatia maoni na ushauri unaotolewa katika taarifa hii kwa lengo la kuboresha utendaji wa Serikali ili kuwezesha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama nchini.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati; baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, naomba kubainisha maoni ya Kamati ambayo yamezingatia changamoto zinazoikabili sekta ya maji kama ifuatavyo:-

(i) Kupungua kwa Bajeti ya Maendeleo ya Wizara ya Maji kunaweza kuathiri utekelezaji bora wa miradi ya maendeleo na miradi hiyo kukosa tija iliyokusudiwa kwa wananchi.

(ii) Utekelezaji wa miradi mikubwa ya maji kama vile ujenzi wa Mabwawa ya Kidunda, Furkwa na Ndembela au Lugoda unahitaji dhamira ya dhati ya Serikali ya kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili hiyo. *(Makofi)*

(iii) Kuchelewa kukamilika kwa baadhi ya miradi kutokana na malimbikizo ya madeni ya wakandarasi kuna athiri utoaji wa huduma ya maji kwa wananchi na kuongeza gharama na kuathiri maslahi ya wakandarasi. *(Makofi)*

(iv) Uharibifu wa vyanzo vya maji unachangiwa kwa kiasi kikubwa na shughuli za kibinadamu zinazofanyika kandokando ya vyanzo vya Maji. Utekelezaji wa Mwongozo wa Uvunaji wa Maji ya Mvua umekosa msukumo wa kutosha wa Serikali. Hivyo, kusababisha upotevu mkubwa wa maji.

(v) Mabadiliko ya tabianchi yana athari kubwa kwa vyanzo vya maji na miundombinu ya maji. Migogoro baina ya wananchi na hujuma ya miundombinu ya maji maeneo ambayo miradi ya maji inapita, inayosababishwa kwa kasi kikubwa na wananchi hao kutopatiwa huduma ya maji.

(vi) Kutosambaza maji kwa wananchi maeneo ambayo uchimbaji wa visima umekamilika kunaondoa tija ya miradi hiyo na hasara kwa Serikali. Vituo vya kuchotea maji katika baadhi ya maeneo kuwa mbali na makazi ya watu ni kinyume cha Sera ya Maji ya Mwaka 2002 inayotaka wananchi kupata maji katika umbali usiozidi meta 400.

(vii) Gharama kubwa ya maunganisho mapya ya maji inawanyima wananchi wa hali ya chini hasa wa vijijini kupata haki ya huduma ya maji. Wataalamu wa maunganisho mapya ya maji kuwa mbali kunapelekea upotevu mkubwa wa maji pale mivujo inapotokea.

(viii) Kutokutumika ipasavyo kwa mitambo iliyonunuliwa na Serikali kwa ajili ya kuchimbia visima nchini, kunaondoa tija iliyokusudiwa na Serikali ya kuwapa wananchi maji safi na salama. Ushirikishwaji mdogo wa wananchi katika uandaaji wa miradi ya maji unachangia uwepo wa migogoro inayoharibu miundombinu ya maji.

(ix) Madai ya fidia kwa wananchi wanaopisha miradi ya maji hayalipwi kwa wakati kama Sheria ya Fidia inavyopendekeza na maji katika baadhi ya miradi hayana ubora.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Kamati; kutokana na maoni yaliyobainishwa hapo juu, naomba kutoa ushauri wa Kamati kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali iongeze Bajeti ya Maendeleo ya Wizara ya Maji kwa kiasi cha shilingi 137,714,253,000 ili Wizara iweze kukamilisha miradi ya maji na hivyo kutimiza ahadi ya Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu ya Mwaka 2020 – 2025, inayoelekeza Serikali kuimarisha huduma za maji safi na salama kwa wananchi, kufikia 85% kwa wananchi wa vijijini na 95% kwa mijini ifikapo mwaka 2025. Aidha, ongezeko hilo la bajeti litaiwezesha Serikali kutekeleza azma yake na azma ya Mheshimiwa Rais ya kuvipatia huduma ya maji safi vijiji 2,581 ambavyo havijafikiwa na huduma hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kusisitiza hapa kwamba Kamati itaunga mkono hoja hii leo lakini tunashauri kwamba, kiasi hiki ambacho kimepungua cha shilingi bilioni 137 kwa kadiri tunavyoendelea kutekeleza bajeti hii kati ya Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali ione chanzo kingine chochote ambacho kinaweza kusaidia hizi fedha zipatikane ili hii miradi iweze kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ione umuhimu wa kuongeza fedha katika mfuko wa maji ili kukamilisha miradi mikubwa ya kimkakati kwa wakati. Tunaiomba Serikali iongeze fedha kutoka shilingi 50 iliyotolewa sasa kwa lita ya diseli na petroli, hadi kufikia shilingi 100. Kwa nini tunasema hivyo? Tumesema kwamba miradi mingi ya kimkakati ambayo tunataka kuitekeleza na Mheshimiwa Waziri amezungumza hapa habari ya kuanza sasa kutekeleza Gridi ya Taifa na tukiwa na hiki chanzo cha uhakika cha Mfuko wa Maji kwa kuongeza shilingi 100, itaisaidia sana Serikali kutekeleza miradi yake mikubwa. Kwa hiyo, tunashauri hiyo shilingi 50 iongezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutafuta vyanzo vingine vya fedha kama vile Hati Fungani. Kwa hapa ninapenda sana kuipingeza Wizara, walikaribisha watu wajitokeze walivyouza Hati Fungani pale Tanga na walitamani wapate shilingi bilioni 53 lakini mpaka sasa wamepata shilingi bilioni 54, wamepata shilingi bilioni moja zai.

Kwa hiyo, hii inawezekana kwa hizi Hati Fungani na vyanzo vingine. Kuandaa maandiko ya kupata fedha katika Mifuko ya Fedha ya Kimataifa *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ihakikishe inalipa malimbikizo ya madeni yote ya wakandarasi kabla ya tarehe 30 Juni, 2024 ili miradi ya maji ikamilike na kuwanufaisha wananchi. Katika eneo hili pia napenda kutoa msisitizo wa Kamati kwamba, tulivyofanya kutembelea miradi mingi tumegundua kwamba wakandarasi wengi, aidha wengine wameacha kuendelea kufanya utekelezaji wa miradi kwa sababu fedha zimechelewa. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali katika kuwalipa hawa wakandarasi hasa wa ndani katika Miradi ya *RUWASA*, wazingatie na kama tulivyokubaliana ifikapo Juni 2024 wawe wamelipa *certificates* zote ambazo ziko mezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali iendelee kuelimisha wananchi kutofanya shughuli za kiuchumi na kijamii kando kando ya vyanzo vya maji. Aidha, Serikali iwatafutie wananchi hao shughuli mbadala za kiuchumi na nishati mbadala ili kujikimu kimaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali iweke msukumo wa kutosha wa utekelezaji wa Mwongozo wa Kuvuna Maji ya Mvua kuanzia ngazi ya kaya, taasisi za Umma pamoja na binafsi. Ili kukabiliana na mafuriko na ukame yanayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi, Serikali kwa kutumia taarifa za Utabiri wa Hali ya Hewa iandae mkakati mahsusi wa kukabiliana na hali hiyo kwa kuchimba mabwawa, visima na kupanda miti rafiki ya mazingira ili kulinda vyanzo vya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali iwashirikishe wananchi kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi ya maji ili kusaidia kuondoa migogoro baina ya Serikali na wananchi wa eneo husika lakini pia itasaidia kuleta tija iliyokusudiwa na kuwawezesha kuilinda, kuitunza na kusimamia na kufanya miradi hiyo kuwa endelevu. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, Serikali kupitia Wizara ihakikishe inasambaza maji kwa wananchi kwenye maeneo ambayo

uchimbaji wa visima umekamilika ili kuleta tija iliyokusudiwa. Serikali iongeze vituo vya kuchotea maji na vituo hivyo vijengwe karibu na makazi ya watu, hususan vijijini ili kwendana na Sera ya Maji inayoelekeza kwamba mwananchi asiende kupata huduma ya maji zaidi ya meta 400. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie upya bei za maunganisho ya maji hasa kwa wateja wapya maeneo ya vijijini ili ziendane na hali halisi ya uwezo wa wananchi. Aidha, kuwepo na utaratibu wa kuwaunganishia na kuwapatia maji makundi maalum, hasusan wazee na watu wenye ulemavu ambao kimsingi hawana uwezo wa kugharimia na kupata huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali iandae mpango wa utoaji huduma za matengenezo ya mabomba kwa haraka, pale inapotokea kuna mivujo ya maji kutokana na kupasuka kwa mabomba ili kuepusha hasara inayotokana na uvujaji wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali iweke utaratibu mzuri wa matumizi ya mitambo iliyonunuliwa kwa ajili ya kuchimba visima nchini, kwa kuelekeza mitambo hiyo kwenye maeneo yenye uhitaji zaidi wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali itekeleze sera ya maji ya mwaka 2002 inayotaka wananchi wanaopitiwa na miradi ya maji kuwa wanufaika wa kwanza wa huduma hiyo hali hii itaondoa migongano baina ya wananchi na itasaidia miundombinu ya maji kutoharibika.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipe fidia kwa wananchi wanaopisha miradi ya maji kabla ya miradi hiyo kuanza kutekelezwa ili kuepusha migogoro. Serikali ihakikishe maji yanayosambazwa yanakuwa na ubora unaohitajika kwa matumizi ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Kwa niaba ya Kamati kwa mara nyingine napenda kukupongeza tena kwa uongozi wako madhubuti, Kamati yangu inakuahidi ushirikiano wa hali ya juu na

kukuombea afya njema, maisha marefu na mafanikio katika kutekeleza majukumu yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru na kumpongeza Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kukusaidia katika kuliwezesha Bunge kutekeleza wajibu wake na kuisimamia na kuishauri Serikali kwa ustawi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, kipekee nawashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati hususani wakati wa uchambuzi wa bajeti. Hali hiyo ni ushahidi tosha kwamba Wajumbe wa Kamati hii wapo tayari kulitumikia Bunge, Taifa na wananchi wakati wowote.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua na kuthamini umuhimu wa Wajumbe wa Kamati ningetamani kuwatambua kwa kuwataja majina yao, hata hivyo kwa kuzingatia ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso, Mbunge na Naibu Waziri wake *Engineer* Andrea Mathew Kundo Mbunge, Katibu Mkuu, Mhandisi Mwajuma Waziri pamoja na wataalam wote wa Wizara ya Maji kwa ushirikiano wanaonesha wakati wa kuchambua na kujadili bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi, Mbunge, Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa ushirikiano wake kwa kamati kwa kipindi alichokuwa Naibu Waziri wa Maji. Nampongeza pia kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa umahiri wake katika kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu na bila mkwamo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuhidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, Muundo wa Taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 142 kuhusu muundo wa Taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni. Kwa msingi huo, Taarifa ninayoiwasilisha imegawanyika katika Sehemu Kuu Tatu zifuatazo: -

(i) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla na kuonesha Msingi na Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;

(ii) Sehemu ya Pili inabainisha Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2023/2024 na

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025; na

(iii) Sehemu ya Tatu inabainisha Maoni na Ushauri wa Kamati na kumalizia kwa hitimisho.

## 1.2 Msingi wa Uchambuzi wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 6(6) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Maji na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira. Kwa madhumuni ya taarifa hii, Wizara ya Maji **(Fungu 49)** inahusika**.** Aidha, Masharti ya Kanuni ya 118 (4) ikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 yanazitaka Kamati za Kisekta ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuchambua Taarifa za Bajeti kabla ya kujadiliwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi masharti hayo, tarehe 22 Machi, 2024, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Maji kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

## 1.3 Mawanda (Scope) ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji ina Fungu Moja **(Fungu 49).**

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI

## 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Madhumuni ya Taarifa hii ni kuliwezesha Bunge kujadili Hotuba ya Waziri wa Maji aliyoiwasilisha mapema leo hii. Ili kuliwezesha Bunge kufanya kazi hiyo inavyostahili, Taarifa hii inabainisha uchambuzi katika maeneo yafuatayo: -

(i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;

(ii) Hatua iliyofikiwa katika uzingatiaji wa Ushauri uliotolewa na Kamati kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(iii) Hali ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa fedha kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(iv) Hali ya Upatikanaji wa Fedha za Matumizi hadi kufikia Mwezi Februari, 2024;

(v) Hatua iliyofikiwa katika Utekelezaji wa mipango iliyowekwa kwa Mwaka wa fedha 2023/2024; na

(vi) Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ikilinganishwa na utekelezaji kwa mwaka wa fedha unaoisha.

## 2.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilizingatia Masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 kwa kutembelea na kukagua Miradi **Sita (6**) ya Maendeleo inayotekelezwa na Wizara ya Maji iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2023/2024 katika Mikoa ya Iringa, Njombe, na Ruvuma kuanzia tarehe 12 hadi 18 Machi, 2024. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu matokeo ya Ukaguzi wa Miradi hiyo kama ifuatavyo: -

### (a) Mradi wa Maji – Itagutwa Mkoani Iringa

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unatekelezwa kwa gharama ya **Shilingi 322,067,025/=** ambazo ni fedha za Mfuko wa Maji na fedha kutoka Benki ya Dunia kupitia Program ya Malipo kwa Matokeo (*Program for Results* PforR).

**Mheshimiwa Spika,** hadi Machi, 2024 jumla ya **Shilingi 320,935,960/=** zimelipwa na utekelezaji wa Mradi umefikia **asilimia 98.** Aidha, Wananchi **4,215** wamenufaika katika huduma yaMaji kwa majaribio. Kamati inaipongeza Serikali kwa utekelezaji wa Mradi huu ambao kwa kiasi kikubwa umewezesha Wananchi hususan akina Mama, kushiriki katika shughuli za maendeleo badala ya kutumia muda mwingi katika utafutaji wa maji.

**(b) Mradi wa Maji –Nyamlenge II Mkoani Iringa**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unatekelezwa katika Wilaya ya Iringa kwa gharama ya **Shilingi 1,170,174,638/=.** Katika mwaka wa fedha 2023/2024 kiasi cha **Shilingi 675,485,709/=** kilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huu.

**Mheshimiwa Spika,** hadi Machi, 2024 jumla ya **Shilingi 1,017,270,639/=** zimelipwa huku utekelezaji wa mradi ukifikia **asilimia 98.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Wizara kwa kukamilisha mradi huu kabla ya muda wa Mkataba**,** hivyo kuwezesha Wananchi **5,692** wa Vijiji vya Nyabula na Mlanda kuanza kunufaika na huduma ya majisafi na salama**.**

**(c) Ujenzi wa Bwawa la Masaka**

**Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa Bwawa hili umekamilika na umegharimu kiasi cha **Shilingi 1,698,159,182.41**. Bwawa lina ukubwa wa mita za **Ujazo 439,803** likiwa na tuta lenye kimo cha **Mita 14**.

**Mheshimiwa Spika,** Bwawa hili lina uwezo wa kuhudumia Wananchi wapatao **9,682** wa Kata ya Masaka, Mifugo **7,780**, Kilimo cha umwagiliaji zaidi ya ekari **400** na Shughuli za uvuvi ambapo Vifaranga **19,000** vimepandikizwa kwenye Bwawa hilo. Aidha, Bwawa hili litapunguza shughuli za kibinadamu zilizokuwa zikifanyika kwenye vyanzo vya Maji na kufanya kuwe na uendelevu wa upatikanaji wa Maji yanayotegemewa chini ya

kidakio kwa ajili ya uzalishaji wa Nishati ya Umeme kwenye Bwawa la Mtera, Kidatu na Julius Nyerere.

**(d) Mradi wa Igongwi (Lot 1,2,3 na 4)**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unatekelezwa katika Halmashauri ya Njombe Mji Mkoani Njombe ambapo unatekelezwa katika vipande (lots) Vinne: -

(i) Kipande cha Kwanza (Lot 1) kinahusisha ujenzi wa vyanzo Vinne (*intakes*) vya Maji na ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa **Kilomita 51.1** kwa gharama ya **Shilingi 4,307,798,502.56.** Utekelezaji wa kipande hicho umefikia **asilimia 99** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2024. Hadi mwezi Machi,2024 Mkandarasi amelipwa kiasi cha **Shilingi 3,438,511,347.78** sawa na **asilimia 80** ya gharama zote.

(ii) Kipande cha Pili (Lot 2), utekelezaji wa kipande hicho ulipangwa kufanyika katika Vijiji vya Madope na Luvuyo kwa kutumia vyanzo vya maji vya Igongwi. Hata hivyo kutokana na uchache wa maji kwenye vyanzo hivyo ililazimika kuondolewa kwenye mradi wa Igongwi na kutafutiwa vyanzo vingine kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji kama ifuatavyo:-

- ☞ Mradi wa maji Madope – Mradi huu unahusisha ujenzi wa tanki la maji lenye ujazo wa **Lita 150,000,** ujenzi wa **Vituo 16** vya kuchotea maji na mtandao wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa **Kilomita 12**. Mradi huu umekamilika na Wananchi wanafaidika na huduma ya maji.

- ☞ Mradi wa Maji Luvunyo- Mradi huu unahusisha ujenzi wa chanzo, ujenzi wa tanki la **Lita 50,000,** ujenzi wa **Vituo 20** vya kuchotea maji, ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa **Kilomita 6**, ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa **Kilomita 8.7.** Mradi huu unatekelezwa kwa kutumia Watalaam wa ndani kwa gharama ya **Shilingi 1,151,203,621/=.** Hadi Machi,2024 utekelezaji wa Mradi umefikia **asilimia 71** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024.

(iii) Kipande cha Tatu (Lot 3) – Kipande hiki kinatekelezwa katika Vjiji vya Kitulila na Madobole kwa gharama ya **Shilingi 480,299,111.78**. Kazi zinazotekelezwa ni pamoja na ulazaji wa Mabomba ya Usambazaji maji umbali wa **Kilomita 13.8,** Ujenzi wa **Vituo 28** vya kuchotea maji na ujenzi wa matenki mawili yenye ujazo wa **Lita 75,000.** Hadi Mwezi Machi, 2024 Mkandarasi amelipwa **Shilingi 222,594,099** sawa na **asilimia 46.3** na Utekelezaji wake umefikia **asilimia 97** ambapo unatarajiwa kukamilika Mwezi Juni, 2024.

(iv) Kipande cha Nne (Lot 4)- Kipande hiki kinatekelezwa katika Vjiji vya Luponde na Njoomlole kwa gharama ya **Shilingi 828,931,576.** Kazi zinazotekelezwa ni pamoja na ulazaji wa Mabomba ya Usambazaji maji umbali wa **Kilomita 21.8**, Ujenzi wa **Vituo 42** vya kuchotea maji na ujenzi wa matenki mawili yenye ujazo wa **Lita 250,000**. Hadi Mwezi Machi, 2024 Mkandarasi amelipwa **Shilingi 448,525,980/=** sawa na **asilimia 54** ya malipo yote na Utekelezaji wake umefikia **asilimia 72.** Hata hivyo, utekelezaji wa kipande hiki umepangwa kukamilishwa kwa kutumia mafundi wazawa kutokana na Mkandarasi kutokuwa tayari kuendelea na kazi baada ya kuwa na madai ya muda mrefu.

**(e) Mradi wa Maji Ngumbo Awamu ya Pili**

Mradi huu unatekelezwa na Mkandarasi mzawa katika Wilaya ya Nyasa Mkoani Ruvuma kwa gharama ya **Shilingi 2,030,668,500**. Shughuli zinazotekelezwa katika Mradi huu, ni pamoja na uchimbaji wa mtaro, ulazaji na ufukiaji wa bomba lenye urefu wa **Kilomita 29.5**, ujenzi wa **vituo 30** vya kuchotea maji na ujenzi wa Ofisi ya chombo cha watoa huduma ngazi ya Jamii. Hadi mwezi Machi, 2024 utekelezaji wa mradi huu umefikia **asilimia 60.**

Jumla ya madai yaliyowasilishwa na Mkandarasi hadi Machi, 2024 ni **Shilingi 1,202,421,285/=** ambapo hadi Machi, 2024 Mkandarasi amelipwa kiasi cha **Shilingi 304,600,275.00** sawa na **asilimia 25.3** ya madai yaliyowasilishwa. Baada ya kukamilika kwa Mradi huu Wananchi wapatao **11,080** watanufaika na huduma ya majisafi katika Vijiji vya Ngumbo, Mbuli, Mkili, Liwundi na Yola.

**(f) Mradi wa Maji wa Malungu**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unatekelezwa katika Wilaya ya Nyasa Mkoani Ruvuma kwa gharama ya **Shilingi 1,222,759,056.67** kwa fedha za Mfuko wa Taifa wa Maji na Fedha za Serikali kuu. Mradi haukutekelezwa kwa wakati kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kutopelekwa kwa mabomba kwa wakati. Mradi umepangwa kukamilika tarehe 01Juni, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu ukikamilika utanufaisha Wananchi wapatao **9,659** kutoka Vijiji vya Malungu na Tingi. Aidha, katika madai ya Mkandarasi ya **Shilingi 361,717,380.00,** Mkandarasi amelipwa kiasi cha **Shilingi 149,491,980** sawa na **asilimia 41.3** ya madai.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliridhishwa na Utekelezaji wa Miradi hii. Kamati inampongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha nyingi katika Miradi ya Maji inayotekelezwa.

**2.2.1 Yaliyobainika kwenye Miradi ya Maendeleo iliyotembelewa na kukaguliwa na Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya Ukaguzi wa Miradi hiyo yamebainisha mambo yafuatayo: -

(a) Kwa ujumla hatua iliyofikiwa katika Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyopangwa kutekelezwa na Wizara ya Maji kwa mujibu wa Mpango kazi ni ya kuridhisha;

(b) Kuchelewa kutolewa kwa fedha za utekelezaji wa Miradi ya Maji;

(c) Uwepo wa malimbikizo ya madeni kwa Wakandarasi;

(d) Ushirikishwaji mdogo wa Wananchi katika uandaaji wa Miradi ya maji.

(e) Baadhi ya Wananchi wanaopitiwa na Miradi ya Maji kutopata maji;

(f) Gharama kubwa ya maunganisho ya Maji Vijijini hivyo kuwafanya baadhi ya Wananchi kushindwa kumudu gharama hizo;

(g) Uwepo wa Vituo vichache vya kuchota maji na Vituo vingine kuwa mbali na makazi ya Wananchi tofauti na Sera ya Maji inavyoelekeza;

(h) Bado Wananchi wengi hawajui umuhimu wa kutunza na kulinda vyanzo vya maji;

(i) Wataalamu wa maunganisho mapya ya Maji kuwa mbali hali inayosababisha upotevu mkubwa wa maji pale mivujo inapotokea;

(j) Shughuli za Kilimo kuendelea pembezoni mwa vyanzo vya Maji;

(k) Madai ya fidia kwa Wananchi wanaopisha Miradi ya Maji;

(l) Uwepo wa Visima vilivyochimbwa ambavyo havijakamilika hali inayosababisha kukosekana kwa tija ya fedha zilizotumika kugharimia uchimbaji wa visima hivyo;

(m) Kukwama kwa utekelezaji wa Miradi ya Maji kutokana na Mvua na;

(n) Maji katika baadhi ya Miradi kutokuwa na ubora.

### 2.2.2 Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilizingatia Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 na kufanya Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, tarehe 22 Machi, 2024. Uchambuzi katika sehemu hii umejikita kwenye maeneo yafuatayo: -

(a) Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri uliotolewa na Kamati katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024;

(b) Ukusanyaji wa Maduhuli;

(c) Utekelezaji wa Mipango na Majukumu ya Wizara ya Maji na;

(d) Hali ya Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika**, Lengo la Uchambuzi wa Kamati ni kuliwezesha Bunge kupata ulinganisho utakaosaidia katika mjadala wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja. Ulinganisho huo unafanyika kwa njia ya asilimia, na Vielelezo, ili kubainisha taswira ya mlingano uliopo.

**2.2.3 Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Kamati ilitoa Maoni na Ushauri katika maeneo Kumi na Moja (11). Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa Maoni na Ushauri wa Kamati umezingatiwa.

**Mfano** wa Ushauri uliozingatiwa unahusu Wizara kuweka utaratibu wa Watalaam katika Sekta ya Maji kutembeleana na kubadilishana uzoefu ili kuleta ufanisi katika Miradi ya Maji. Utekelezaji ulioripotiwa unaonesha kuwa Wizara imeandaa Mwongozo wa Usimamizi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira unaoelekeza Mamlaka zenye uwezo na zilizofanikiwa kuzijengea uwezo Mamlaka changa na zenye uwezo mdogo. Vile vile Viongozi na Watalaam wa Wizara za Maji wa pande zote mbili za Muungano wamekuwa wakikutana ili kubadilishana uzoefu katika maeneo mbalimbali ikiwemo utunzaji wa vyanzo vya Maji na ujenzi wa Miradi ya Maji. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia sehemu kubwa ya Ushauri uliotolewa na Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na pongezi hizo, ni rai ya Kamati kwamba Serikali iendelee kutekeleza kikamilifu na kwa haraka maeneo ambayo utekelezaji wake umefanyika kwa kiwango cha

chini. Mfano wa Ushauri huo ni Serikali kuongeza juhudi za kuwaelimisha Wananchi kuhusu umuhimu wa kutekeleza Mwongozo wa uvunaji wa maji ya mvua.

### 2.2.4 Uchambuzi wa Ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Maji **(Fungu 49)** iliidhinishiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 1,200,001,000.00** kutokana na mauzo ya Nyaraka za Zabuni, Leseni kwa Makampuni ya Utafiti na Uchimbaji wa Visima vya Maji na Ada kwa huduma za Maabara za Ubora wa Maji. Hadi mwezi Februari 2024, Wizara ilikusanya kiasi cha **Shilingi 983,669,897.00** sawa na **asilimia 82** ya lengo. Mchanganuo wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli na kiasi kilichokusanywa hadi Februari, 2024 ni kama unavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 1**

**Kielelezo Na.1 Mchanganuo wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli na kiasi kilichokusanywa hadi Februari, 2024**

| CHANZO | MAKADIRIO YA MAKUSANYO 2023/2024 | MAKUSANYO HADI FEBRUARI,2024 | ASILIMIA YA LENGO |
|---|---|---|---|
| Mauzo ya Nyaraka | 1,000 | 800,000.00 | 80,000 |
| Malipo ya Leseni kwa Kampuni za Utafiti na Uchimbaji wa Visima vya Maji | 250,000,000 | 230,974,062 | 92 |
| Ada kwa huduma za Maabara. | 950,000,000 | 751,895,835 | 79 |
| **JUMLA** | **1,200,001,000.00** | **983,669,897** | **82** |

**Chanzo: Randama ya Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati unaonesha kuwa: -

(a) Mwenendo wa ukusanyaji wa Maduhuli kwa Wizara ya Maji kwa kipindi cha robo ya tatu ya utekelezaji wa Bajeti **ni asilimia 82** ya lengo la ukusanyaji kwa mwaka. Hali hii ni dalili nzuri kwamba Wizara itaweza kufikia lengo la ukusanyaji wa Maduhuli kutokana na vyanzo hivyo ifikapo mwezi Juni, 2024.

(b) Makadirio ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2024/2025 umezingatia hali halisi ya ukusanyaji wa Maduhuli katika mwaka wa fedha unaoisha.

**Mheshimiwa Spika**, kwa Uchambuzi huo, Kamati ina maoni kuwa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli yalipangwa kulingana na uhalisia wake. Aidha, Uwekezaji wa kutosha katika Leseni za Kampuni za Utafiti na Uchimbaji wa Visima vya Maji pamoja na uboreshaji na usimamizi wa huduma za Maabara za ubora wa maji unaweza kuongeza Mapato ya Serikali, na hivyo kuleta tija iliyokusudiwa kwa Wananchi.

**2.2.5 Utekelezaji wa Mipango na Majukumu ya Wizara ya Maji**

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ililenga kufanikisha utekelezaji wa Mipango na majukumu ya Wizara ya Maji na Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo. Ili kujiridhisha na mwenendo wa Matumizi unaoakisi madhumuni ya kuidhinishwa kwa Bajeti hiyo, Kamati ilidadisi utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika maeneo Makuu matano ya Sekta ya Maji. Maeneo hayo ni: -

(a) Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji;

(b) Huduma ya Ubora wa Maji;

(c) Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini;

(d) Huduma za Usambazaji wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini na;

(e) Uratibu wa Masuala Mtambuka

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa kazi katika Sekta ya Maji ni pamoja na: -

(i) Kukamilika kwa Miradi ya maji **659** ambapo Miradi **589** ni ya Vijijini na Miradi **70** ni ya Mijini;

(ii) Kuongezeka kwa huduma ya Maji kutoka **asilimia 77** Disemba 2022 Vijijini na **asilimia 88** Mijini hadi **asilimia 79.6** Vijijini na **asilimia 90** Mijini mwezi Disemba,2023;

(iii) Kukamilika kwa Mabwawa ya ukubwa wa kati **Tisa (9);**

(iv) Kutatuliwa kwa migogoro **23** ya matumizi ya maji;

(v) Kupanda miti rafiki kwa mazingira **649,356** kwenye vyanzo vya Maji katika Mabonde yote **Tisa (9)** na;

(vi) Kukamilika kwa utekelezaji wa Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira katika Jiji la Arusha

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na utekelezaji huo, Kamati inampongeza kwa dhati Mhe. Juma Aweso (Mb), Waziri wa Maji pamoja na Watendaji Wakuu wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Mhandisi Mwajuma Waziri kwa usimamizi mahiri na madhubuti.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana wakati wa utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Changamoto zifuatazo ziliathiri utekelezaji bora wa shughuli za Wizara: -

(a) **Mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi mikubwa ya Maji ya Kimkakati**

Utekelezaji wa Miradi mikubwa kama vile Ujenzi wa Mabwawa ya Kidunda, Farkwa na Ndembera/ Lugoda umechukua muda mrefu kuanza kutekelezwa kutokana na kuhitaji fedha nyingi kwa wakati mmoja wakati upatikanaji wa fedha hizo umekuwa si kwa kasi iliyokusudiwa;

(b) **Uchafuzi, uvamizi na uharibifu wa vyazo vya Maji**

Uchafuzi, uvamizi na uharibifu wa vyanzo vya Maji unaotokana na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na Kijamii unaathiri kwa kiasi kikubwa uendelevu wa Rasilimali za Maji nchini;

(c) **Mabadiliko ya Tabianchi**

Athari za mabadiliko ya tabianchi zikiwemo ukame wa muda mrefu na mafuriko zinachangia kukauka kwa vyanzo vya Maji na kuharibika kwa miundombinu ya maji.

**2.2.6 Hali ya Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika**, Upatikanaji wa fedha ni hatua muhimu katika utekelezaji wa Bajeti. Aidha, uzoefu wa kiwango cha fedha kinachopatikana kwa mwaka wa fedha unaoisha ni muhimu katika uamuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka unaofuata. Kwa msingi huo, Kamati ilifanya uchambuzi wa hali ya upatikanaji wa fedha kwa mwaka wa Fedha 2023/2024. Naomba kulijulisha Bunge kuwa matokeo ya uchambuzi yameonesha mambo yafuatayo: -

**(a) Hali ya Upatikanaji wa Fedha kwa ajili ya kugharimia Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika,** hadi Februari, 2024, Wizara ya Maji ilipokea **asilimia 81** ya Bajeti ya Miradi ya Maendeleo. Kiwango hicho cha upatikanaji wa fedha kinaendana na hali halisi ya utekelezaji wa Bajeti. Kiasi kilichopatikana ni **Shilingi 563,398,121,378.53** kati ya **Shilingi 695,829,632,000.00** zilizoidhinishwa na Bunge kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na.2**

**Kielelezo Na. 2Mchanganuo wa Bajeti na kiasi cha fedha kilichopokelewa kwa Matumizi ya Maendeleo hadi Februari, 2024**

| BAJETI ILIYOIDHINISHWA 2023/2024 | | FEDHA ILIYOPOKELEWA HADI FEBRUARI, 2024 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| **FEDHA ZA NDANI** | 407,064,860,000 | 356,910,567,637.62 | 87.6 |
| **FEDHA ZA NJE** | 288,764,772,000 | 206,487,553,740.91 | 71.5 |
| **JUMLA** | **695,829,632,000.00** | **563,398,121,378.53** | **81** |

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya Uchambuzi yanaonesha kuwa:-

(i) Upatikanaji wa fedha kwa ajili kugharimia Miradi ya Maendeleo inayolenga kuimarisha upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama ulifikia **asilimia 81** ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili hiyo. Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za Maendeleo kwa wakati ni kiashiria kwamba Miradi ya Maendeleo iliyopangwa kutekelezwa itakamilika kama ilivyokusudiwa ifikapo Juni, 2024;

(ii) Upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni **asilimia 87.6** ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili hiyo. Hali hii inaonesha dhamira nzuri ya Serikali ya kushirikiana na Washirika wa Maendeleo katika kuhakikisha kuwa Wananchi wananufaika na Miradi hii na kuondokana na kero za kukosa maji.

(iii) Kwa upande wa fedha za Washirika wa Maendeleo kutoka nje upatikanaji wake ni **asilimia 71.5** ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili hiyo. Hali hii inaonesha kwamba Bajeti iliyopangwa ni halisia na inaonesha ushirikiano wa dhati wa Washirika wa Maendeleo wa kutoka nje.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kusimamia Upatikanaji wa fedha za Maendeleo kwa wakati na hivyo kuongeza kasi ya kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka

2020-2025. Ni maoni ya Kamati kwamba nchi inaendelea kuwa na usalama wa maji na kuimarisha huduma ya Majisafi na Salama na kuwafikia Wananchi kama ilivyoelezwa katika Ilani hiyo. Ni Rai ya Kamati kwamba kiasi cha fedha kilichobaki kitatolewa mapema kabla ya mwezi Juni ili Miradi iweze kukamilika kwa asilimia 100.

Aidha, ni matarajio ya Kamati kuwa uzoefu uliopatikana katika mwaka wa fedha 2023/2024 utafaa kutumika katika upatikanaji wa fedha za Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2024/2025, ili Miradi iliyopangwa kutekelezwa ikamilike kwa wakati.

**(b) Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida kwa mwaka wa fedha 2023/2024**

**Mheshimiwa Spika,** hadi Februari, 2024, Wizara ya Maji ilipokea **asilimia 61.3** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kiwango hicho cha upatikanaji wa fedha hakiendani na hali halisi ya utekelezaji wa Bajeti. Kiasi kilichopatikana ni **Shilingi 37,048,093,833.87** kati ya **Shilingi 60,375,474,000.00** zilizoidhinishwa na Bunge kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na.3**

**Kielelezo Na. 3Mchanganuo wa Fedha za Matumizi ya Kawaida zilizoidhinishwa na kupokelewa hadi Februari, 2024**

| BAJETI ILIYOIDHINISHWA 2023/2024 | | FEDHA ILIYOPOKELEWA HADI FEBRUARI, 2024 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| **FEDHA ZA MISHAHARA** | 42,339,913,000.00 | 29,052,227,510.00 | **68.6** |
| **FEDHA ZA OC** | 18,035,561,000.00 | 7,995,866,323.87 | **44.3** |
| **JUMLA** | **60,375,474,000.00** | **37,048,093,833.87** | **61.3** |

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi unaonesha kuwa utolewaji wa fedha za Matumizi ya Kawaidi ambazo zinakusudiwa kutumika katika uendeshaji wa shughuli za uimarishaji wa huduma za Maji Mijini na Vijijini hadi Februari 2024, ni **asilimia 61.3** ya Bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili hiyo. Upatikanaji huo wa fedha uko chini

ikilinganishwa na kiasi kilichopaswa kufikiwa kwa kipindi kama hiki ambao ni **asilimia 66.6.**

## 2.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

### 2.3.1 Maelezo ya jumla

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwa Malengo na vipaumbele vilivyoainishwa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, vinaendana na majukumu ya Msingi ya Wizara ya Maji, ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025; Awamu ya Nne ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano mwaka 2021/22 – 2025/26; Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 - 2025; Malengo ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2030; na ahadi mbalimbali za Viongozi wa Kitaifa.

Aidha, Wizara inaendelea kutekeleza Miradi ya Maji kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002, Sheria ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya Mwaka 2009 na maboresho yake ya mwaka 2022; Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya mwaka 2019 pamoja na Kanuni zinazoelekeza utekelezaji wa Sheria hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji ulifanyika kwa kuzingatia kazi zilizopangwa kutekelezwa katika maeneo yafuatayo: -

(a) Kuimarisha Usimamizi, Uendelezaji, Uhifadhi na Utunzaji wa Vyanzo vya Maji;

(b) Kuimarisha Huduma ya Usimamizi wa ubora wa maji nchini;

(c) Kuboresha Huduma ya Maji katika Maeneo ya Mijini;

(d) Kuboresha Huduma ya Maji Vijijini; na (e) Kuimarisha Uwezo wa Kitaasisi.

### 2.3.2 Makadirio ya Maduhuli yatakayokusanywa

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Maji (**Fungu 49**) inatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 1,200,001,000,** kutokana na vyanzo vya mauzo ya Nyaraka za Zabuni, Leseni kwa Kampuni za Utafiti na Uchimbaji wa Visima vya Maji, Tozo mbalimbali kwa wateja wanaopata huduma ya Maabara za Ubora wa Maji na Vibali vya Matumizi ya Maji katika Mabonde.

**Mheshimiwa Spika,** Ulinganisho wa Maduhuli yaliyokusanywa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 yanaoneshwa katika Kielelezo **Na. 04**

**Kielelezo Na. 4: Ulinganisho wa Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

| CHANZO | MAKADIRIO YA MADUHULI 2023/2024 | MAKADIRIO YA MADUHULI 2024/2025 | % ONGEZEKO/ PUNGUFU |
|---|---|---|---|
| **Mauzo ya Nyaraka za Zabuni** | 1,000.00 | 1,000.00 | **0** |
| **Leseni za Kampuni za Utafiti** | 250,000,000.00 | 250,000,000.00 | **0** |
| **Ada - Huduma za Maabara** | 950,000,000.00 | 950,000,000.00 | **0** |
| **JUMLA** | **1,200,001,000.00** | **1,200,001,000.00** | **0** |

**Chanzo: Randama ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2024/2025**

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya Uchambuzi yanaonesha kuwa Lengo la ukusanyaji wa Maduhuli kwa mwaka 2024/2025 halijaongezeka, kiasi kilichopangwa kukusanywa mwaka wa fedha unaoisha ndio kilichokadiriwa kukusanywa kwa mwaka huu wa fedha. Hali hii inaonesha kuwa makadirio ya Maduhuli yamezingatia hali halisi ya makusanyo yaliyopatikana kwa mwaka wa fedha unaoisha.

**2.3.3 Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2024/2025,**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Maji (**Fungu 49)** inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 627,778,338,000.00**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 69,662,959,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 558,115,379,000** sawa na **asilimia 89** ni kwa ajili ya kugharimia Miradi ya Maendeleo, kati ya fedha hizo za Maendeleo **Shilingi 340,463,656,000** sawa na **asilimia 61** ni fedha za ndani na **Shilingi 217,651,723,000** sawa na **asilimia 39** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia uzoefu uliopatikana katika Utekelezaji wa Bajeti inayoisha, Kamati ilifanya ulinganisho kati ya Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,** ulinganisho huo unaonekana katika **Kielelezo Na. 5.**

**Kielelezo Na. 5Ulinganisho wa Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2023/2024 na mwaka wa Fedha 2024/2025**

| AINA YA MATUMIZI | CHANZO CHA FEDHA | FEDHA ILIYOIDHINISHWA 2023/2024 | KIASI CHA FEDHA KINACHOOMBWA 2024/2025 | ONGEZEKO/ PUNGUFU | ASILIMIA ONGEZEKO/ PUNGUFU |
|---|---|---|---|---|---|
| **MATUMIZI YA MAENDELEO** | **Fedha za ndani** | 407,064,860,000.00 | 340,463,656,000.00 | -66,601,204,000.00 | **-9** |
| | **Fedha za nje** | 288,764,772,000.00 | 217,651,723,000.00 | -71,113,049,000.00 | **-9.4** |
| **JUMLA NDOGO** | | **695,829,632,000.00** | **558,115,379,000.00** | **-137,714,253,000.00** | **-18.4** |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **MATUMIZI YA KAWAIDA** | **OC** | 18,035,561,000.00 | 17,542,812,000 | -492,749,000.00 | **-0.1** |
| | **Mishahara** | 42,339,913,000.00 | 52,120,147,000 | 9,780,234,000.00 | **1.3** |
| **JUMLA NDOGO** | | **60,375,474,000.00** | **69,662,959,000** | **9,287,485,000** | **1.2** |
| **JUMLA KUU** | | **756,205,106,000.00** | **627,778,338,000.00** | **128,426,768,000.00** | **-17** |

**Chanzo:** Randama ya Wizara ya Maji (**Fungu 49)** kwa mwaka wa fedha

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi umeonesha kuwa: -

(i) Makadirio ya Bajeti yote ya Wizara ya Maji yamepungua kwa **asilimia 17** ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(ii) Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya kugharimia Miradi ya Maendeleo yamepungua kwa kiasi cha **Shilingi 137,714,253,000.00** sawa na **asilimia 18.4** ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Ni mtazamo wa Kamati kwamba kupungua kwa kiasi hiki cha Bajeti ya Maendeleo kutaathiri Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

(iii) Makadirio ya Matumizi ya Kawaida yameongezeka kwa kiasi cha Shilingi **9,287,485,000** sawa na **asilimia 1.2** ya Bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haijaridhishwa na Bajeti hii kwani haijazingatia ipasavyo maelekezo kwa Serikali yaliyomo kwenye Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020-2025. Ilani ya CCM imeahidi kuimarishwa kwa huduma ya Majisafi na salama ili ifikapo mwaka 2025 Wakazi asilimia 85 waishio Vijijini na asilimia 95 ya Wakazi waishio Mjini wawe wamefikiwa na huduma hiyo. Msisitizo wa Kamati kwa Serikali ni kuhakikisha kuwa Bajeti ya Wizara ya Maji inaongezwa kwa **Shilingi 137,714,253,000.00** ili angalau ibaki kama ilivyokuwa mwaka wa fedha 2023/2024.

## 2.4 Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Maji dhidi ya Bajeti Kuu ya Serikali

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Maji dhidi ya Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ili kubaini ongezeko/ pungufu la Bajeti ya Wizara ya Maji dhidi ya Bajeti Kuu ya Serikali. Ulinganisho huo unaonekana kwenye **Kielelezo Na.6**

**Kielelezo Na. 6 Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Maji dhidi ya Bajeti Kuu ya Serikali 2024/2025**

| MCHANGANUO | BAJETI KUU YA SERIKALI | | BAJETI YA WIZARA YA MAJI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| **MATUMIZI YA KAWAIDA** | **33,556,566,000,000.00** | | **69,662,959,000** | **0.2** |
| | Fedha za Ndani | 12,148,283,000,000.00 | 340,463,656,000.00 | **0.7** |
| | Fedha za Nje | 3,640,838,000,000.00 | 217,651,723,000.00 | **0.4** |
| **JUMLA FEDHA ZA MAENDELEO** | | **15,789,122,000,000.0 0** | **558,115,379,000.00** | **1.1** |
| **JUMLA MATUMIZI YOTE** | **49,345,688,000,000.00** | | **627,778,338,000.00.** | **1.3** |

**Chanzo:** Mapendekezo ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/2025 na Randama ya Wizara ya Maji 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Ulinganisho huo unaonesha kuwa: -

(a) Bajeti ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ni **asilimia 1.3** ya Bajeti Kuu ya Serikali. Hali hii inaonesha kwamba Bajeti ya Wizara ya Maji imepungua kwa **asilimia 0.4** ikilinganishwa na Bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024;

(b) Bajeti ya Maendeleo ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ni **asilimia 1.1** ya Bajeti Kuu ya Serikali ya Maendeleo ambayo ni **asilima 32**. Uchambuzi huo unaonesha kuwa Wizara ya Maji siyo miongoni mwa Vipaumbele vya Serikali kwa mwaka huu wa fedha.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la Taarifa hii ni kubainisha Maoni na Ushauri wa Kamati ili kuwezesha majadiliano ya Bunge. Pamoja na majadiliano kuhusu hoja hii, upo umuhimu wa kuzingatia Maoni na Ushauri unaotolewa katika Taarifa hii kwa lengo la kuboresha utendaji wa Serikali ili kuwezesha upatikanaji wa Huduma ya Majisafi na Salama nchini.

### 3.2 Maoni ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Uchambuzi wa kina kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji –**Fungu 49** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025, naomba kubainisha Maoni ya Kamati ambayo yamezingatia changamoto zinazoikabili Sekta ya maji kama ifuatavyo: -

(a) Kupungua kwa Bajeti ya Maendeleo ya Wizara ya Maji kunaweza kuathiri utekelezaji bora wa Miradi ya Maendeleo na Miradi hiyo kukosa tija iliyokusudiwa kwa Wananchi;

(b) Utekelezaji wa Miradi mikubwa ya Maji kama vile Ujenzi wa Mabwawa ya Kidunda, Furkwa na Ndembera/ Lugoda unahitaji dhamira ya dhati ya Serikali ya kutenga Bajeti ya kutosha kwa ajili hiyo;

(c) Kuchelewa kukamilika kwa baadhi ya Miradi kutokana na malimbikizo ya madeni ya Wakandarasi kunaathiri utoaji wa huduma ya maji kwa Wananchi, kuongeza gharama na kuathiri maslahi ya Wakandarasi;

(d) Uharibifu wa Vyanzo vya Maji unachangiwa kwa kiasi kikubwa na shughuli za Binadamu zinazofanyika kando kando ya vyanzo vya Maji;

(e) Utekelezaji wa Mwongozo wa uvunaji wa Maji ya mvua umekosa msukumo wa kutosha wa Serikali, hali inayosababisha mpotevu mkubwa wa maji;

(f) Mabadiliko ya Tabianchi yana athari kubwa kwa Vyanzo vya Maji na Miundombinu ya Maji;

(g) Migogoro baina ya Wananchi na hujuma ya miundombinu ya maji maeneo ambayo Miradi ya Maji imepita inasababishwa kwa kiasi kikubwa na Wananchi hao kutopatiwa huduma ya Maji;

(h) Kutosambaza Maji kwa Wananchi maeneo ambayo uchimbaji wa Visima umekamilika kunaondoa tija ya Miradi hiyo na hasara kwa Serikali;

(i) Vituo vya kuchotea maji katika baadhi ya maeneo kuwa mbali na makazi ya watu ni kinyume na Sera ya Maji ya mwaka 2002 inayotaka Wananchi kupata Maji katika umbali usiozidi Mita 400;

(j) Gharama kubwa ya maunganisho mapya ya Maji inawanyima Wananchi wa hali ya chini Hasa wa Vijijini kupata haki ya huduma ya Maji;

(k) Wataalamu wa maunganisho mapya ya Maji kuwa mbali kunapelekea upotevu mkubwa wa maji pale mivujo inapotokea;

(l) Kutokutumika ipasavyo kwa Mitambo iliyonunuliwa na Serikali kwa ajili ya kuchimba Visima nchini kunaondoa tija iliyokusudiwa na Serikali ya kuwapatia Wananchi majisafi na salama.

(m) Ushirikishwaji mdogo wa Wananchi katika uandaaji wa Miradi ya maji kunachangia uwepo wa migogoro na uharibifu wa Miundombinu ya maji;

(n) Madai ya fidia kwa Wananchi wanaopisha Miradi ya Maji hayalipwi kwa wakati kama Sheria ya fidia inavyoelekeza na;

(o) Maji katika baadhi ya Miradi hayana ubora.

### 3.3 Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na Maoni yaliyobainishwa hapo juu naomba kutoa Ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

(a) Serikali iongeze Bajeti ya Maendeleo ya Wizara ya Maji kiasi cha **Shilingi 137,714,253,000.00** ili Wizara iweze kukamilisha Miradi ya Maji na hivyo kutimiza ahadi ya Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu ya Mwaka 2020-2025 inayoelekeza Serikali kuimarisha huduma ya majisafi na salama kwa Wananchi na kuwafikia wakazi **asilimia 85** kwa Vijijini na **asilima 95** kwa Mijini ifikapo mwaka 2025. Aidha, ongezeko hilo la bajeti litawezesha Serikali kutekeleza azma ya Mhe. Rais ya kuvipatia huduma ya Maji Vijiji **2581** ambavyo havijafikiwa na huduma hiyo;

(b) Serikali ione umuhimu wa kuongeza fedha katika Mfuko wa Taifa wa Maji ili kukamilisha Miradi Mikubwa ya Kimkakati kwa wakati kwa;

   (i) Kungeza fedha kutoka **Shilingi 50** inayotolewa sasa kwa kila Lita ya Diseli na Petroli hadi kufikia **Shilingi 100**;

   (ii) Kutafuta vyanzo vingine vya fedha kama hati fungani na;

   (iii) Kuandaa maandiko ya kupata fedha katika mifuko ya fedha ya Kimataifa;

(c) Serikali ihakikishe inalipa malimbikizo ya madeni yote ya Wakandarasi kabla ya tarehe 30 Juni, 2024 ili miradi ya maji ikamilike na kuwanufaisha Wananchi;

(d) Serikali iendelee kuelimisha Wananchi kutofanya shughuli za kiuchumi na kijamii kando kando ya Vyanzo vya Maji. Aidha, Serikali iwatafutie Wananchi hao shughuli mbadala za kiuchumi na nishati mbadala ili kujikimu kimaisha;

(e) Serikali iweke msukumo wa kutosha wa utekelezaji wa Mwongozo wa kuvuna maji ya mvua kuanzia ngazi ya Kaya, Taasisi za Umma na Binafsi;

(f) Ili kukabiliana na mafuriko na ukame vinavyosababishwa na Mabadiliko ya Tabianchi, Serikali kwa kutumia taarifa za Utabiri wa Hali ya Hewa, iandae Mkakati mahsusi wa kukabiliana na hali hiyo kwa kuchimba Mabwawa/Visima na kupanda miti rafiki kwa mazingira ili kulinda vyanzo vya maji;

(g) Serikali iwashirikishe Wananchi kabla ya kuanza utekelezaji wa Miradi ya Maji. Hii itasaidia kuondoa migogoro baina ya Serikali na Wananchi wa eneo husika, lakini pia itasaidia kuleta tija iliyokusudiwa na kuwawezesha kuilinda, kuitunza, kuisimamia na kuifanya kuwa endelevu.

(h) Serikali kupita Wizara ihakikishe inasambaza Maji kwa Wananchi kwenye Maeneo ambayo uchimbaji wa Visima umekamilika ili kuleta tija iliyokusidiwa;

(i) Serikali iongeze Vituo vya kuchotea Maji, na vituo hivyo vijengwe karibu na makazi ya Watu hasusan Vijijini ili kuendana na Sera ya Maji inavyoelekeza kwamba Mwananchi asiende kupata huduma ya Maji zaidi ya Mita 400;

(j) Serikali iangalie upya bei za maunganisho mapya ya Maji kwa wateja wapya hasa wa Vijijini ili ziendane na hali halisi ya uwezo wa Wananchi. Aidha, kuwepo na utaratibu wa kuwaunganishia na kuwapatia maji makundi maalum hasusan Wazee na Watu wenye ulemavu ambao kimsingi hawana uwezo wa kugharimia kupata huduma hiyo;

(k) Serikali iandae Mpango wa utoaji huduma za matengenezo ya mabomba kwa haraka pale inapotokea kuna uvujaji wa

maji kutokana na kupasuka kwa mabomba ili kuepusha hasara inayotokana na uvujaji wa maji;

(l) Serikali iweke utaratibu mzuri wa matumizi ya Mitambo iliyonunuliwa kwa ajili ya kuchimba Visima nchini kwa kuelekeza mitambo hiyo kwenye maeneo yenye uhitaji zaidi wa Maji;

(m) Serikali itekeleze Sera ya Maji ya mwaka 2002 inayotaka Wananchi wanaopitiwa na Miradi ya Maji kuwa Wanufaika wa kwanza na Huduma hiyo. Hali hii itaondoa migogoro baina ya Wananchi na itasaidia Miundombinu ya Maji kutoharibiwa;

(n) Serikali ilipe fidia kwa Wananchi wanaopisha Miradi ya Maji kabla ya Miradi hiyo kuanza kutekelezwa ili kuepusha migogoro;

(o) Serikali ihakikikshe maji yanayosambazwa yanakuwa na ubora unaohitajika kwa matumizi ya Wananchi.

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa kina pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati, naomba kuhitimisha hoja ya Kamati kama ifuatavyo: -

### 4.2 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati kwa mara nyingine napenda kukupongeza tena kwa uongozi wako madhubuti. Kamati yangu inakuahidi ushirikiano wa hali ya juu na tunakuombea afya njema, Maisha marefu na mafanikio katika utekelezaji wa majukumu yako.

**Mheshimiwa Spika,** namshukuru na kumpongeza Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kukusaidia katika

kuliwezesha Bunge kutekeleza wajibu wake wa kuisimamia na kuishauri Serikali kwa ustadi wa hali ya juu.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee nawashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati hususan wakati wa Uchambuzi wa Bajeti. Hali hiyo ni ushahidi tosha kwamba, Wajumbe wa Kamati hii wako tayari kulitumikia Bunge, Taifa na Wananchi wakati wowote.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua na kuthamini umuhimu wa Wajumbe wa Kamati ningetamani kuwatambua kwa kuwataja majina yao. Hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*). Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo: -

1. Mhe. Jackson Gedion Kiswaga, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb - **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Asya Sharif Omar, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Prof. Shukrani Elisha Manya, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Bashiru Ally Kakurwa, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Kasalali E. Mageni, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Robert Maboto, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Juma Usonge Hamad, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Ritta Kabati Enespher, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Haji Makame Mlenge, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Asya Mwadini Mohammed, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Kavejuru Eliadory Felix, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Regina Ndege Qwaray, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Agnes Elias Hokororo, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Emmanuel Peter Cherehani, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Charles John Mwijage, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Deo Kasenyanda Sanga, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Mohammed Jumah Soud, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Keneth Nollo, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Suleiman Omar Mohamed, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Maji Mhe. Jumah Aweso, (Mb) na Naibu Waziri Mhe. Kundo Andrew Mathew (Mb), Katibu Mkuu Mhandisi Mwajuma Waziri

pamoja na Wataalamu wote wa Wizara ya Maji kwa ushirikiano walioonesha wakati wa kuchambua na kujadili Bajeti ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb), Naibu Waziri wa Mawasiliano kwa ushirikiano wake kwa Kamati kwa kipindi alichokuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maji nampongeza pia kwa kuteuliwa Kuwa Naibu Waziri wa Mawasiliano.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc,* kwa umahiri wake katika kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu bila kukwama.

**4.3 Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Jackson Gedion Kiswaga, (Mb)
**MWENYEKITI,**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA.**
09 MEI, 2024.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa maoni hayo ya Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni ambao wameingi baada ya tangazo letu la awali la wageni tutaanza na wageni waliokaa jukwaa la Spika.

Yupo Mheshimiwa Narender Kumar ambaye ni Balozi Mdogo wa India Nchini Tanzania, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo ndugu Reginald Baynit ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Uthamini wa Mikopo Mikubwa *NMB*, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Jumaa Aweso, Waziri wa Maji, hawa ni Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Maji, wasimame wote kwa pamoja, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia Wakurugenzi Watendaji waliopo chini ya Wizara ya Maji, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia Wakuu wa Wilaya, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Wakuu wa Wilaya wote, Mheshimiwa Ngollo Ng'waniduhu Malenya, Wakuu wa Wilaya, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia Washirika wa Maendeleo, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao Wahariri wa Vyombo vya Habari, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao viongozi wa Chama cha Mapinduzi kutoka Wilaya ya Pangani Mkoa wa Tanga na wapiga kura wake kutoka Pangani, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 33 wa Mheshimiwa Jackson Kiswaga ambao ni Wenyeviti wa Kata, Makatibu Kata na Makatibu wa Mbunge kutoka Kalenga Mkoa wa Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wa wili wa Mheshimiwa Priscus Tarimo, ambao ni Watumishi wa Shirika lisilo la Kiserikali la *Miinjeni Women Organization*. Shirika hili linajishughuli na kupambana na umaskini Tanzania, karibuni sana wanatoka Mkoa wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo la wageni sasa tutaanza uchangiaji na kama nilivyokuwa nimesema awali majina ni mengi kuliko muda tuliyonao. Wabunge watatu watachangia kwa dakika 10, Wabunge wote watakaosalia watachangia kwa dakika saba na Wabunge wanaochangia kwa

dakika 10 ni kwamba hawajachangia kwenye Wizara nyingine, hiyo ndiyo sababu ya kugawa huo muda. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine Mheshimiwa Waziri wa Maji alipomaliza kusoma sikusema hili, wakati akisoma hotuba yake yapo maneno ambayo amezungumza nje ya ile hotuba lakini yapo pia maneno ambayo ni ya msingi sana na ameyasema ila hayapo kwenye ile taarifa aliyotuletea kama Bunge. Kwa hivyo taarifa zetu Rasmi za Bunge zitakaa na ile ambayo ametukabidhi, kwa hivyo wanasimba niliwaona wanasikitika humu ndani msiwe na wasiwasi, maneno aliyoyasema kuhusu Yanga hayamo kwenye taarifa yake rasmi ya Bunge, kwa hiyo msiwe na wasiwasi. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Mheshimiwa Vuma Augustine Holle, atafuatiwa na Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, ajiandae.

**MHE. VUMA A. HOLLE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kupewa nafasi hii ya kufungua pazia kwenye Wizara hii muhimu sana kwa ajili ya Wizara ya Maji. Awali ya yote kabisa nimshukuru kwanza, ninaishukuru Serikali chini ya Mheshimiwa Rais, Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kweli kwa kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Rais, anaenda kufanya kwenye Wizara hii ya Maji nchi nzima lakini hususani Kasulu Vijijini.

Mheshimiwa Spika, Kasulu Vijijini tumepokea miradi mingi sana kwenye mwaka wa fedha uliyopita, kwa kutaja tu kidogo, tumepata mradi wa maji kwenye Kata ya Titye, Rusesa, Nyamnyusi, Kagera Nkanda na Mvugwe. Hii miradi inaenda kunufaisha watu zaidi ya 72,000 na gharama yake ni zaidi ya shilingi karibia bilioni tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kusema Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya hasa ambayo yeye mwenyewe aliamua kuifanya kwa kuanza na kuasisi ile kauli mbiu kwamba ya kumtua mama ndoo kichwani, naamini kabisa Taifa hili litaendelea kumkumbuka Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia kupitia sekta hii ya maji. Mheshimiwa Aweso ninakushukuru sana kwa namna ambavyo umekuwa unasaidia kutafasili maono ya

Mheshimiwa Rais. umezunguka nchi nzima lakini na Kasulu Vijijini ulifika, nakumbuka ulifika pale mwaka jana na kwa kweli ukawatua wakina mama wa Kata ya Makele ndoo kichwani, tunakushukuru sana, wewe ni mtu mnyenyekevu, mfuatiliaji, mchapakazi lakini ni mtu ambaye unaweza kufanya maamuzi, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naamini hata ndugu yangu, kaka yangu Kundo, amepata mtu sahihi wa kuweza kumwelekeza kazi vizuri na atafanya kazi vizuri kwa sababu na yeye ni mchapakazi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nitaanza na Mfuko wa Maji. Mfuko wa Maji ni nyenzo muhimu sana ambayo inapaswa kutumika kusaidia sana kutatua kero za shida ya maji lakini zipo changamoto. Mfuko wa Maji hauna fedha za kutosha lazima Serikali iumize kichwa, lazima Serikali itafute vyanzo mbadala au vyanzo vingine vya kuhakikisha kwamba mfuko wa maji unakuwa na pesa ya kutosha. Kwa sababu kama mfuko wa maji hauna fedha za kutosha maana yake nini? Maana yake tija yake inakuwa siyo kubwa sana, lazima tumekaa nao kama Kamati mara kadhaa, moja ya changamoto yao kubwa ni kukosekana kwa fedha za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanayo miradi mingi ambayo wanapaswa ku-*finance* lakini hela ni kidogo. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri naamini umekuwa unapambana na Mheshimiwa Rais, amekutuma sehemu mbalimbali kwa ajili ya kutafuta fedha za maendeleo, wapeni mfuko wa maji hela za kutosha ili waweze kutekeleza miradi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapo hapo kwenye Mfuko wa Maji. Kwenye mfuko wa maji wanadirisha la mikopo, kwa maana kwamba zile mamlaka kubwa za maji zinaweza kwenda kukopa pale kwenye mfuko wa maji, sasa tunaomba utaratibu wa utoaji wa mikopo usimamiwe vizuri na uimarishwe, maana yake zipo bado taasisi ambazo zinazo uwezo kabisa wa kwenda kukopa na kujiendesha kibiashara, bado wanaenda kuomba fedha za ruzuku kitu ambacho siyo kweli siyo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha za ruzuku zinapaswa kwenda vijijini, Kasulu Vijijini kule, Kibondo, Buhigwe, Pangani, siyo kwenda kufadhiri miradi ya taasisi kubwa kama *DUWASA, DAWASA* hawa wakubwa hawa, hawa nadhani wanapaswa waende kwa maana ya kwenda kukopa kwa utaratibu ambao umewekwa ili waweze kurudisha, hela za ruzuku ziende vijijini kwa ajili ya kusaidia kule kwa sababu taasisi za kule hazina uwezo wa kujiendesha kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nizungumze kuhusu suala la mradi wa maji wa Ziwa Tanganyika. Kwanza, Mheshimiwa Waziri tunakushukuru sana kwa sababu imekuwa ni kiu na wimbo wetu mkubwa wa siku zote, mradi huu unaenda kunufaisha Mkoa wa Kigoma, Katavi pamoja na Rukwa. Tumeusubiri kwa hamu sana, na tunashukuru hata kwa angalau sasa tumeambiwa mwaka huu wa fedha mnaenda kutafuta mshauri elekezi. Tunaomba sana kwa kweli mradi huu uharakishwe kwa sababu wananchi wanahitaji maji ya uhakika kwenye Mikoa hii mitatu. Mimi nasema huu mradi ukikamilika Mheshimiwa Aweso, Mikoa hii itamkumbuka sana Mheshimiwa Rais, kupitia mradi huu na wewe mwenyewe kama Waziri wa Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kuhusu suala la hati fungani *(green bond)*. Kwetu Tanzania ni kama jambo jipya lakini ni jambo ambalo ni muhimu sana kama *alternative source of financing* ya miradi. Kwa sababu ukiangalia mahitaji ya maji katika nchi hii ni makubwa yaani miradi ipo mikubwa ambayo inahitaji pesa na wakati mwingine inazidi hata uwezo wa Serikali kuigharamikia yote kwa Pamoja, lakini kupitia hati fungani tumeona inawezekana kupitia Tanga *UWASA*.

Mheshimiwa Spika, Tanga *UWASA* wame-*issue bond,* mwaka jana walikuwa wana-*target* ya kukusanya shilingi bilioni 53 imeenda zaidi na sasa hivi wamekusanya shilingi bilioni 54, kwa hiyo sasa wanaweza wakafanya miradi yao vizuri, watu wamewekeza pale. Wapo watu wanahitaji kuwekeza, wapo watu ndani ya nchi na nje ya nchi wanahitaji kutoa fedha zao kwa ajili ya kuwekeza kupitia miradi ya maji na miradi ya maji ikisimamiwa vizuri, ikiwa *designed* vizuri na ikisimama vizuri ni uwekezaji mzuri ambao hauna shida yoyote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, kama *Tanga UWASA* imewezekana tunaamini hata taasisi zingine za maji hizi kubwakubwa ambazo vitabu vyao vya hesabu vipo vizuri wanao uwezo wa kwenda huko, kuliko kuanza kulialia kwamba wapewe ruzuku, wanaweza pia kuanzisha huu utaratibu wa hati fungani wakapata fedha watu wakawekeza. Kwa hiyo naomba sana Mheshimiwa Aweso hili ulifanyie kazi ni *alternative way* ya kupata fedha kwa ajili ya ku-*finance* miradi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali Mheshimiwa Aweso, tarehe 18 Julai, mwaka jana ulikuja kwangu Jimboni Kasulu Vijijini. Kwanza nakushukuru kwa sababu ya utendaji kazi mzuri uliyotukuka wa aliyekuwa Kaimu Meneja wa *RUWASA* Wilaya ya Kasulu ulimsimika pale pale kwamba awe *full* na kweli tunashukuru, kijana ulimpa morali kubwa ameshathibitishwa sasa ni Meneja kamili na kazi anachapa kweli kweli, pia niseme wazi tu Mheshimiwa Aweso, kwamba ile ahadi ambayo ulisema utatusaidia ya gari kwa ajili ya Meneja wa *RUWASA* ili aendelee kuchapa kazi vizuri bado naendelea kukumbusha kwamba haijafika. Nakuomba sana Kaka yangu najua wewe ni msikivu hilo halikushindi lipo ndani ya uwezo wako utusaidie gari ili Meneja wa *RUWASA* Wilaya ya Kasulu aweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nishukuru kwenye hotuba yako umesema unaenda kutoa visima vitano kwenye kila Jimbo na naamini Kasulu Vijijini, tutapata na mimi kwa sababu huwa silazi damu ulivyosema tu hapa nilimpigia simu Meneja huyo huyo wa *RUWASA* tumepanga tayari, visima vitano tunachimba Kijiji cha Malalo, Kazage, Chekenya, Kabulanzwili na Mkiheta. Hapa nimesema wazi na wananchi wamesikia kwa hiyo tunasubiri visima vitano tukawachimbie wananchi wapate maji ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, atafuatiwa na Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia Wizara hii muhimu ya Maji. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Jumaa Aweso na Naibu wake na Watendaji wote wa Wizara hii ya Maji kwa kazi kubwa wanayofanya kuhakikisha Watanzania wanaenda kutatuliwa kero zao za maji kama siyo kuisha kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita itaacha historia ya aina yake katika utekelezaji wa miradi ya huduma za kijamii ikiwemo katika sekta hii ya maji. Wananchi wa Arusha hatuna budi kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunaona ni jinsi gani Dkt. Samia anaendelea kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, kweli Dkt. Samia yupo kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna hii *slogan* ya kusema kuwa "Kumtua Mama Ndoo Kichwani" tukumbuke kuwa *slogan* hii haijaanza leo wala jana, aliianzisha Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, akiwa Makamu wa Rais na tumeona nia dhahiri ya Dkt. Samia, kuhakikisha anamtua mama ndoo kichwani na alisema mama kwa sababu kina mama wengi ndiyo wamekuwa wakipitia changamoto ya maji kutafuta maji katika mazingira ya hatari, kuamka usiku mama kwa ajili ya kwenda kutafuta maji. Kwa hiyo, tunaona lengo rasmi na nia ya Dkt. Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais katika kipindi kifupi cha utawala wake ameweza kutekeleza miradi 47 yenye thamani ya shilingi bilioni 20 na kuwezesha upatikanaji wa maji katika vijiji 35, amepandisha upatikanaji wa maji kutoka 69.4% hadi wastani wa 73.5%, idadi ya vijiji vinavyopata huduma imeongezeka kutoka vijiji 304 hadi vijiji 339 sawa na 87% ya vijiji kwa Mkoa wote wa Arusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kukamilisha ujenzi wa mradi mkubwa wa maji katika Jiji la Arusha, nadhani wote mnaelewa jiji la Arusha tulipata mradi wenyethamani ya shilingi bilioni tano na 20 ambao ni karibu bajeti ya Wizara nzima, sisi ni nani tusiishukuru Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Dkt. Samia. Mradi huu umekuwa chanzo kikubwa cha maji kwa Wilaya hata zilizo za Jirani zisizo na vyanzo vya uhakika vya maji ambapo Serikali imeanza utekelezaji wa mradi wa kimkakati kutoka mradi

mkubwa wa Jiji la Arusha kwenda Monduli katika vijiji 13 katika Wilaya ya Monduli Mjini, gharama ambayo ni shilingi bilioni 20.3 ambapo itahudumia jumla ya watu 34,000.

Mheshimiwa Spika, sambamba na mradi huu Serikali imeendelea na mradi wa vijiji vinne ambavyo ni Makuyuni, Naiti, Mbuyuni na Loosimingor wa shilingi bilioni saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kumekuwa na malalamiko ya wakazi wa Jiji la Arusha kuwa bili zinakuwa kubwa sana za maji lakini tatizo kubwa siyo katika Mamlaka ya Maji ya Jiji la Arusha, tatizo kubwa lipo katika Wizara ya Nishati. Kwa sababu maji yale yanasukumwa kwa *pump,* bili inayokuja katika Mamlaka ya Maji ya Jiji la Arusha inakuwa kubwa sana. Kwa hiyo, naomba Serikali waangalie Wizara ya Nishati ni jinsi gani watawapunguzia gharama za umeme Mamlaka ya Jiji la Arusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nitakuwa mchoyo wa shukrani nisipomshukuru Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maji Arusha *(AUWSA)* Ndugu Lujoba pamoja na Meneja Mkuu wa Mamlaka ya Maji ya Mkoa wa Arusha Ndugu Makaidi, wamekuwa wakifanya kazi vizuri, wamekuwa wakishirikiana katika kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kuhakikisha wakazi wa mji wa Arusha wanapata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna ule mradi wa Mlangarini wa shilingi bilioni 3.7, mradi huu tuliambiwa unakamilika Disemba. Disemba imebaki miezi michache sana, Mheshimiwa Waziri naomba sana mradi huu ukamilike kwa wakati. Kuna mradi wa Enguik Monduli wa shilingi bilioni mbili, utekelezaji wake umefikia asilimia 67, Mheshimiwa Waziri mlisema unakamilika mwezi Juni, bado wiki tatu tu tufike mwezi Juni, ninaimani Mheshimiwa Waziri mwezi ujao wana-Monduli wanaenda kufurahia maji haya ambayo Mama Samia aliweka *slogan* yake ya kumtua mama ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina imani Mheshimiwa Waziri, mwezi ujao wana Monduli wanaenda kufurahia maji haya ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliweka *slogan* yake ya kumtua mama ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mradi wa Imbaseni upo Arumeru wa shilingi bilioni moja na mwenyewe waliahidi watakamilisha mwezi Juni, mwezi Juni bado wiki tatu. Mheshimiwa Waziri, najua kabla hatujaondoka kwenye Bunge hili atatukabidhi miradi yetu miwili ya Imbaseni, Arumeru na miradi ya Monduli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mradi wa Oldonyosambu wa shilingi bilioni sita, tuliambiwa unakamilika mwezi Juni, 2025; hapa bado una muda. Changamoto kubwa ya wakazi wa Oldonyosambu ni *Fluoride* ambayo kina mama wengi walikuwa wanapata shida wanapobeba ujauzito wanajifungua watoto wenye matatizo ya meno na mifupa.

Mheshimiwa Spika, kimekuwa kilio cha muda mrefu sana. Tunaishukuru sana Serikali hii sikivu ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuna wataalamu wapo pale, kwa ajili ya kuchunguza na kurekebisha hili tatizo. Tunategemea matokeo mazuri na sasa kina mama wataenda kubeba ujauzito, watajifungua watoto wazima kama ambavyo inatakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mradi wa Mageri, Ngorongoro mradi wa shilingi bilioni sita. Utekelezaji wake umekamilika asilimia 52, wametuambia mpaka mwezi Juni, mwaka kesho mradi huu utakamilika. Mheshimiwa Waziri miradi hii nitaifuatilia kwa karibu sana kwenye Mkoa wa Arusha. Tunataka miradi hii ikamilike kwa wakati ili wananchi wa Arusha, waendelee kuwa na imani na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, na ikifika 2025, wampe Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kura za kishindo. Sasa miradi hii msipoikamilisha itakuwa hamna nia nzuri na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa sababu kashatenga bajeti. Tunataka miradi ikamilike wananchi wa Arusha wakapate maji ya kutosha, maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mradi wa *Seed Farm* wa Nanja wa shilingi bilioni 27 ambao utatiririshwa maji yake kutoka katika huu mradi mkubwa Jiji la Arusha ambao utasafiri kutoka *Seed Farm* Ngaramtoni hadi Nanja. Watu wa Monduli Mjini, Engutoto, Monduli Juu, Lashaine hadi Nanja watafaidika na maji haya. Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri tukafanye kama ambavyo tumepanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipindi cha mafuriko kutokana na mvua kubwa inayoendelea kunyesha tulipata hasara ya uharibifu wa miundombinu katika Bwawa la Nanja, lililopo Monduli linalohudumia zaidi ya Kata saba. Tunashukuru Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tulipewa shilingi milioni 354, Bwawa likakarabatiwa na kudhibiti maji yaliyokuwa hatarini kupotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna hii programu ya visima 900, ambayo wamesema kuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametoa kila jimbo visima vitano. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunaamini utendaji wake. Tunajua mama yupo kazini na mama halali amekuwa akihangaika usiku na mchana kuhakikisha kero zetu Watanzania wote zinatatuliwa. Hakuna kama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba visima hivi vikachimbwe kwa wakati. Waheshimiwa Wabunge wa majimbo wakitoka humu ndani, waende moja kwa moja kwenye majimbo yao wakaanze kuchimba visima kwa ajili ya wananchi ili wananchi wapokee zawadi hii iliyotoka kwa mpendwa wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba niishie hapa kwa leo na ninaunga mkono hoja asilimia 100, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula atafuatiwa na Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo ajiandae.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana na mimi kupata nafasi ya kuchangia kwa siku ya leo kwenye hii Wizara ya Maji. Tunamshukuru sana Mungu kwa kuendelea kutupa afya na nafasi ya kuwatumikia wananchi ndani ya nyumba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kwamba, maji ni muhimu sana kwa wananchi wetu na Watanzania kwa ujumla. Bila maji tafsiri yake ni kwamba hakuna kinachoweza kufanyika. Nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu

Hassan, kwa kuwa kocha mzuri na ukocha mzuri unatokana na namna alivyoamua kupanga wachezaji wake toka mwanzo kwenye kila namba na namna wachezaji wake walivyoamua kucheza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Aweso kwa kuwa mchezaji mzuri sana kwenye Sekta ya Maji. Yeye mimi ninamchukua ni kama namba tisa bora kabisa kuwahi kutokea kwenye Sekta hii kwa sababu ya aina ya utendaji wake wa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, takwimu zozote zile ndizo zinatufanya sisi kama Waheshimiwa Wabunge tuweze kufahamu kazi kubwa ambayo anaifanya Mheshimiwa Aweso na Sekta yake na Watumishi wenzake wote kwenye Wizara ya Maji. Utakubaliana na mimi kwamba katika moja ya jambo kubwa ambalo Mheshimiwa Waziri ameweza kulifanya leo hii, ukitafuta kila Mheshimiwa Mbunge mwenye mradi wa maji humu ndani na yeye amekuwa ni kama sehemu ya *engineers* wanaotekeleza ule mradi. Hii yote ni kwa sababu ya ushirikishwaji mkubwa. Hii namna ameisambaza mpaka kwa Watendaji wake wa chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwapongeza sana watu wa Mamlaka ya Maji na Wizara nzima kwa ujumla na taasisi zake zote wakiwemo hata wale *RUWASA,* ambao wanashughulika na maji maeneo ya vijijini. Ukiangalia takwimu, kwa mfano; nilikuwa ninajaribu kumsikiliza Mheshimiwa Aweso pia nimesikiliza vizuri sana Hotuba ya Kamati. Upatikanaji wa maji umeongezeka. Kuongezeka kwa huduma ya upatikanaji wa maji vijijini na mijini kutoka asilimia 77 mpaka 79.6 vijijini na asilimia 88 mpaka 90 mjini. Hili ni jambo kubwa sana na hii inaenda sambamba na utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Jiji la Mwanza ukichukulia miradi mingi mikubwa ambayo imetekelezwa tumekuwa na chanzo cha maji kwa zaidi ya miaka 40, kikiwa na uwezo wa kuzalisha lita milioni 90 peke yake. Leo ndani ya miaka miwili peke yake na miaka mitatu ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Serikali imejenga chanzo kikubwa cha maji kilichokamilika kwa

asilimia 100 kwa zaidi ya shilingi bilioni 69, kikiwa na uwezo wa kuzalisha zaidi ya lita milioni 48 kwa siku. Haya ni mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wetu kwenye miji hii tunayo wawakilisha ilikuwa ni jambo la aibu sana mtu anaishi zaidi ya kilometa tano kutoka lilipo Ziwa Victoria, lakini hana uhakika wa maji safi na salama ya kunywa. Leo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, chini ya Mheshimiwa Aweso na timu yake nzima wamefanikisha ukamilishaji na ujenzi wa chanzo kikubwa cha maji na cha kipekee kinachokwenda kuwahudumia na kuwaondolea adha watu wa Mji wa Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, chanzo hiki kitahudumia zaidi ya watu 450,000. Nimetazama kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri pamoja na miradi mingine anaeleza namna ambavyo itahudumia Watanzania zaidi ya 4,000,000 kwa miradi yote ambayo imekamilika. Tafsiri yake ni nini? Kwamba, tunapozungumza tatizo la maji kwenye nchi hii ni lazima tuwe na mikakati ambayo italeta tija na kufanikisha kwenye miradi yote ambayo tumeitekeleza. Jambo hili Wizara ya Maji, kwa miaka hii miwili wamefanya kazi kubwa sana, kwa sababu shida iliyokuwepo kwa Watanzania ni miradi inapoanzishwa na kushindwa kukamilika kwa wakati na hivyo kushindwa kufikisha huduma kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunawapongeza sana Wizara ya Maji, kwa sababu wao katika miradi ambayo wameifanya kwa ubora zaidi ukiachana na ule mradi ambao Waheshimiwa wameshautaja wa Arusha, lakini Mradi wa Butimba ni kielelezo kikubwa kwenye nchi hii kwamba, Serikali ikiamua inaweza na pale inapoamua inaweza kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyozungumza sasa hivi tunatarajia na nikuombe sana Mheshimiwa Aweso. Katika kazi kubwa ambayo umeifanya, watu wa Mwanza wanayo matarajio na imani kubwa kwenye mradi ambao tutakwenda kusaini muda siyo mrefu wa usambazaji wa njia na bomba za maji, ujenzi wa matenki zaidi ya matano yatakayobeba zaidi ya lita milioni 31 kwenye Kata ya Kishili kule Fumagila, Nyamazobe kwenye Kata ya

Mkolani na kule Buhongwa. Hii itakwenda mpaka kule Usagara kwenye Wilaya ya Misungwi. Pia, itakwenda mpaka Kisesa kwa Mheshimiwa Kiswaga. Tafsiri yake watu wa Mwanza, Nyamagana na pembezoni kule Ilemela tatizo la maji linakwenda kuwa historia. Hii peke yake inatosha kusema hongereni sana Wizara ya Maji kwa kazi kubwa ambayo mmeifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliposema suala la ushirikishwaji na wewe ni shahidi tulikuona kwa mara ya kwanza kwenye uzinduzi wa ule mradi wa maji kule Kiwira tukasema kweli shughuli imepata mwenyewe. Mheshimiwa Aweso, amesema hapa utulie usiwe na presha kwa sababu majukumu uliyonayo ni makubwa na atahakikisha anakwenda Kiwira kila mara kama alivyofanya Butimba kuhakikisha ule mradi unakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kikubwa zaidi tunafahamu watu wetu wengi wanaamini kwa kuona na miradi mingi ambayo tunaitekeleza muda fulani hivi imekuwa haikamiliki kwa wakati. Kutokukamilika kwake kwa wakati tumeona hapa Kamati imesema vizuri sana. Tunapokuwa hatuna fedha za kutosha hatuwezi kukamilisha miradi hii kwa wakati. Miradi hii ili ikamilike kwa wakati ni lazima tuwe na fedha za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa anayoifanya Mheshimiwa Waziri wa Maji na timu yake, ni vyema sana tukafikiri kama Kamati walivyopendekeza turejeshe ile shilingi bilioni 137, ili Wizara iweze kufanya kazi vizuri. Wakandarasi wetu ambao hawalipwi kwa wakati siyo kwa sababu Wizara ya Fedha inazo hela imezikalia; hawalipwi kwa wakati kwa sababu Wizara haina fedha. Kwa hiyo, tuhakikishe fedha zinakwenda Wizarani na Wakandarasi walipwe ili miradi ikamilike kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukitazama vizuri Mheshimiwa Aweso, alipokuwa anasema Benki ya Dunia imetupa tena nafasi kwa mara ya pili mfululizo kwa kutuongezea idadi ya Halmashauri kutoka 80, mpaka 137 na Mikoa kutoka kumi na ngapi mpaka ishirini na ngapi. Haya ni matokeo makubwa ya uadilifu na uaminifu kwenye utendaji wa kazi za miradi ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tunasikia hapa miezi michache iliyopita Mheshimiwa Aweso na Wizara wanaongelea miradi kichefuchefu. Miradi hii ndiyo iliyokuwa inawafanya wananchi wachukie. Wananchi wanakichukia chama, wananchi wanawachukia hadi Wawakilishi wao. Ni kwa sababu fedha za kutekeleza haya hazipo.

Mheshimiwa Spika, miradi ya maji Kamati imesema ni miradi mikubwa inayohitaji fedha za kutosha. Haiwezekani kama tukitegemea hizi shilingi bilioni 600, hatuwezi kutatua changamoto za maji tulizo nazo. Kwa hiyo, Wizara na Serikali isisite kukopa kwa ajili ya miradi ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninarudia tusisite wala tusiogope kukopa kwa ajili ya miradi ya maji kwa sababu mwananchi aliyepo kule Fumagila, mwananchi aliyepo Kanenwa na mwananchi aliyepo kule Bulale ndani hawezi kujua chochote kwamba hatujakopa au tumekopa au hatuna hela; atakachojua yeye Serikali wamekuwa wazembe hawawezi kufanya kazi. Kwa hiyo, ni lazima tukubali kwamba Serikali ni lazima iingie kwenye mikopo ilete fedha itekeleze miradi mikubwa ya maji halafu mambo mengine haya yanaweza yakaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tuna Mheshimiwa Aweso hapa ni Mkemia. Jana Mheshimiwa Balozi Dkt. Bashiru, alieleza vizuri sana kuhusu ubora na namna ambavyo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimetoa matunda bora ukiwemo wewe. Hivi kama Mwalimu asingeamua kukopa kujenga Chuo cha Dar es Salaam, tungekuwa nacho Chuo cha Dar es Salaam, leo?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukope kwa tija na hivi ndivyo Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inavyofanya. Mradi wa Butimba wamekopa, umejengwa na umekamilika. Wananchi tunaanza ku-*enjoy* maji haya na miradi mingine tusiogope kwa sababu kwa kufanya hivyo ndivyo tutakavyotatua kero za wananchi. Nikuhakikishie nikimalizia mambo yote haya kwa wananchi ni maji, maji, maji. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo atafuatiwa na Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa ajiandae.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii muhimu, Wizara ya Maji inayoongozwa na ndugu yangu kaka yangu Mheshimiwa Aweso.

Mheshimiwa Spika, tumesikia hapa kwenye salamu za kutambulisha wageni wametambulisha uwepo wa wananchi wa Pangani pamoja na viongozi wetu wa Chama. Mawazo yangu ni kwamba kijana huyu Mheshimiwa Aweso, Waziri wetu wa Maji watu wa Pangani watambue ya kwamba tuna kazi naye sisi kama nchi hapa. Kwa hiyo, waendelee kumpa nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe shukurani za pekee sana kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Sisi kule Handeni tumekuwa na mradi mkubwa mara ya mwisho mwaka 1974. Hiyo ndiyo kusema kwamba miaka 50 imepita, Handeni hatukuwahi kuwa na mradi mkubwa wa maji. Amekuja Mheshimiwa Rais, mama shupavu, mama muungwana na mama anaye elewa shida za wanawake. Ametuletea Handeni fedha za miradi kiasi ambacho tunashindwa hata tuanzie wapi na tumalizie wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumepata shilingi 1,248,000,000 Mradi wa Kweinkambala ambao unapeleka maji kwenye mitaa yote mitano ya Kata ya Kweinkambala. Tumepata shilingi milioni 261 Kata ya Kwamagome, tumepata shilingi milioni 320 Kata ya Malezi, tumepata mradi wa Mabanda Mankinda shilingi milioni 761. Kana kwamba haitoshi tumepata shilingi bilioni 2.5 ujenzi wa Bwawa la Kweinkambala. Hivi ninavyozungumza, awamu ya tatu ya utoaji wa fedha shilingi milioni 900 zipo kwenye akaunti tunasubiri mvua zimalizike kazi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi funga kazi ambao Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametupa wana Handeni, mradi mkombozi kwa shida hii ya maji ambayo tumekuwa nayo kwa

miaka karibia 50 ni Mradi wa *HTM* (mradi wa Miji 28 shilingi bilioni 171).

Mheshimiwa Spika, mradi huu ni mradi wa Kitaifa. Tunajenga dakio la maji pale Mswaha, tutayasukuma maji kwa *pump* mpaka pale Tabora ambapo tutajenga *treatment plant*. Tutayatoa maji pale kwa *gravity* mpaka Kwamatuku, yakitoka Kwamatuku yatasukumwa kwenda Sindeni, yakitoka Sindeni yatasukumwa mpaka Mlima Mhandeni, mlima ambao panajengwa tenki kubwa la milioni mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi wana Handeni Mheshimiwa Waziri, ninaomba uelewe hili na ulichukue; tumekubaliana kwa pamoja kwenye mkutano wa hadhara tenki lile juu ya Mlima Mhandeni litaitwa Tenki la Ukombozi. Kwa hiyo, kwenye kumbukumbu zenu, kwenye takwimu zenu na maandishi yenu ya Wizara wakabadilishe badala ya kuliita Tenki la Vibaoni liitwe Tenki la Ukombozi. Ina maana kubwa sana hiyo. Mheshimiwa Rais, anakwenda kuwakomboa wananchi wa Handeni kutoka dhiki hiyo ya maji ambayo tumeipata kwa miaka mingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maji yatatiririka kutoka Mlima Mhandeni mpaka Kwedizando kule Kwediyamba, maji yatatiririka kutoka Mlima Mhandeni mpaka Bangu kule Kideleko, maji yatatiririka mpaka Kulukole kule Malezi kutoka Mlima Mhandeni. Kazi ya Mheshimiwa Rais. Dkt. Samia Suluhu Hassan, hiyo. Maji yatatiririka mpaka Lusanga, maji yatakwenda mpaka Kulukole, maji yatakwenda Komoza na maji yatakwenda kila kona ya Jimbo la Handeni Mjini kutoka Mlima Mhandeni. Ndiyo maana tunasema tenki lile liitwe Tenki la Ukombozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo mambo machache ambayo lazima tuyafanye kuboresha mradi wetu na kuufanya uende kwa haraka. Mradi huu wa *HTM* umekuwa *designed* kukamilika miaka miwili na miezi nane. Tumeshafanya kikao cha kwanza na Mkandarasi, tumekubalina kwamba, atafupisha muda na mradi ule ukamilike walau mwezi Machi, mwakani. Ombi langu kwako Mheshimiwa Waziri, tutakapomaliza Bunge hili, kwa sababu wewe ni kijana wetu wa nyumbani twende tukakae na Mkandarasi tuhakikishe kwamba, mradi huu unakamilika mapema, kwa

sababu fedha zipo na ni kazi tu ya kugawanya zile kandarasi ili washambulie wajenge kwa mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukakamilishe *distribution design* kwenye Kata zote 12 na ikaanze mapema kwa sasa, kwa sababu fedha zipo tusingoje muda. *Distribution design* ifanyike ili tujue wapi mabomba yanapita yale ya usambazaji. Vilevile, kama ambavyo nimekuwa nikisisitiza siku zote tukafanye *soft part engineering design* ya ule mradi wetu. Ni muhimu sana Mto Ruvu - Korogwe ambao ndiyo tunachukulia maji tukaulinde. Tukalinde mazingira, tukalinde vyanzo kwa kufanya hii kazi ambayo nimeisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtakumbuka kwamba pale Handeni tunao mradi wa Kitaifa wa Msomera, mradi ambao tumewapokea wenzetu kutoka Ngorongoro na tunaishi nao kule Handeni. Kwa kuongezeka kwa Mradi wa Msomera na kwa sababu Handeni tayari ina halmashauri mbili, watendaji wetu wanazidiwa. Tuhaitaji tuongezewe watendaji na vitendeakazi kama magari ili waweze kufanya kazi kwa urahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile *HTM* ile ya zamani twendeni tukaikarabati. Tusiiache ikawa mfu ili tuwe na *alternative sources* na *alternative distributions.* Twendeni tukaikarabati *HTM* ya zamani baada ya kuwa tumeshakamilisha mradi huu mpya tunaoendelea kuujenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Mkoa wa Tanga tumekubaliana kwamba mwaka 2025 kura zote za Mkoa wa Tanga zinakwenda kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, na sababu tunazo. Nitawatajia miradi michache iliyopo ndani ya Mkoa wetu wa Tanga. Mradi wa Maji wa Mkinga Holoholo shilingi bilioni 35, Mradi wa Maji Dibuluma Songe Kilindi shilingi bilioni 22, uboreshaji wa mradi kwenye Jiji la Tanga kwa dada yangu Mheshimiwa Ummy shilingi milioni 516, uboreshaji wa maji huko Mheshimiwa Waziri anakotokea shilingi bilioni moja, uboreshaji wa maji kwenye Mji wa Muheza ambako Mheshimiwa Mwana FA ndugu yangu Naibu Waziri anapotokea shilingi milioni 700. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya ninayoyataja ndiyo yanafanya mwaka 2025 watu wasihangaike. Kura za wana-Tanga zitakwenda kwa Mheshimwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo atafuatiwa na Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga ajiandae.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, mimi nitajielekeza kwenye mambo manne. Kwenye gharama za umeme kwa mamlaka za maji nchini, kwenye mita za *pre-paid,* changamoto ya maji taka kwenye majiji pamoja na fursa ya mradi mkubwa tulio nao kwenye Jiji letu la Arusha.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia mamlaka zetu za maji nchini, mamlaka kama ya maji Jiji la Arusha *(AUWSA)* wana deni la umeme kama la bilioni 4.95 kutoka kwa wenzetu *TANESCO*, Mamlaka ya Maji Jiji la Dar es salaam *(DAWASA)* wana deni kama la bilioni 36 na mamlaka ya Maji ya *KASHWASA* wana deni la bilioni 2.97.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa data tulizo nazo, ukiangalia kwenye taarifa hii moja inaonesha kuwa Mamlaka ya Maji Jiji la Arusha wao wanakusanya 2,325,000,000 kwa mwezi lakini umeme pekee wanalipa kiasi cha bilioni 1,100,0000,000 ambayo ni sawa na asilimia 47 ya wanachokikusanya. Mamlaka ya Maji ya Jiji la Dodoma *(DUWASA)* wao wanakusanya 2,200,000,000 lakini wanalipa umeme milioni 843 sawa na asilimia 38. Mamlaka ya Maji ya Mji wa Kahama *(KUWASA)* wao wanakusanya milioni 290 na umeme wanalipa milioni 140, sawa na asilimia 48. Nikimalizia na *KASHWASA* wao wanakusanya 1,325,000,000 wanalipa umeme milioni 666 sawa na asilimia 50.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye data za namna hiyo utagundua mengi. Kwa mfano kwenye taarifa niliyo nayo inaonesha kuwa *DAWASA* pamoja na kukusanya bilioni

2,600,000,000 lakini kwenye upande wa *KVA (kilo-volt-amperes)* pekee wanalipa kiasi cha shilingi milioni 288; na pia wanalipa pia *VAT* milioni 370.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka yetu ya Maji Safi na Maji Taka ya Jiji la Arusha wanalipia umeme kwa maana ya kwenye bili ya maji kwa mwezi kiasi cha shilingi bilioni 1,100,000,000 lakini kwa upande wa *KVA* ni milioni 94 na *VAT* ni milioni 150.

Mheshimiwa Spika, nimesema nisome data hizi ili tuone namna ambavyo wenzetu wa mamlaka za maji wanavyopata mzigo mkubwa wa kulipa bili za umeme ilhali mitambo yao inatumika kwa ajili ya kutoa huduma na wala si kwa kufanya biashara kama ya kupata faida kwa watu wengine. Kwa hiyo tulikuwa tunaomba; na nilikuwa ninateta pia asubuhi na Mheshimiwa Waziri Mkuu; kwamba kwa sababu jambo hili linahusisha Wizara tatu, linahusisha Wizara ya Maji, Wizara ya Nishati pamoja na Wizara ya Fedha; ni vizuri Wizara hizi zikakutanishwa ili wakatoa ahueni kwa Wizara ya Maji ili hatimaye mamlaka hizi ziendelee kupunguza mzigo kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ukiwaambia leo walipe *VAT* na wao hawachaji *VAT* kwa wananchi unawapa gharama kubwa za uendeshaji na baadaye wanalazimika kuongeza gharama zaidi kwa mwananchi; na hatimaye mabilioni haya yanayokwenda kwa Watanzania yatakuwa hayana tija sana. Kwa sababu wananchi watakuwa wanalalamika sana kubambikiwa bili, gharama kubwa za maji kutokana na mzigo mzito ambao wenzetu wa mamlaka za maji wanao. Kwa hiyo ombi langu la kwanza lilikuwa ni hilo. Kwamba tumwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu kama Kiongozi Mkuu wa Serikali katika suala la utendaji aweze kuzikutanisha wizara hizi ili tuweze kuangalia namna nzuri zaidi ya kukumbana na changamoto hii.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kuhusiana na mita za *pre-paid*. Nilimsikia Mheshimiwa Rais akitoa maelekezo kwa Wizara ya Maji kuhakikisha kwamba wanafunga mita za *pre-paid* ili kuendelea kupunguza malalamiko ya wananchi ya kubambikiwa bili za maji na kuwa na bili kubwa za maji. Tunafahamu kuwa Wizara ya Maji wameshaanza kufanya kazi hiyo kwenye maeneo

mbalimbali. Sisi watu wa Arusha ambao tuna wateja 123,204 mpaka sasa wameshaunganishiwa wateja 325 ambao ni sawa na asilimia 0.26. Hii ni ishara ya kwamba bado kazi kubwa inatakiwa ifanyike. Ninajua jambo hili Mheshimiwa Waziri analifahamu, na ninafahamu kuwa amefanya kazi kubwa ya kuhamasisha na kuelekeza lakini bado kazi ya ziada inatakiwa ifanyike ili wananchi wenzetu waweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ni kuhusiana na maji taka. Ukiangalia Taarifa ya Kamati ya Bunge ambayo waliisoma hapa Bungeni, ninakumbuka ilikuwa ni tarehe 9 Februari, 2024; Kamati ya Bunge ilisema kwamba "kwa kuwa miundombinu ya maji taka katika miji na majiji bado hairidhishi kwa kiwango kinachostahili; na kwa kuwa hali hii inaweza kusababisha mlipuko wa magonjwa kwa wananchi hali ambayo inaweza kuathiri shughuli za uzalishaji;" kwa hiyo inaonekana kabisa hii changamoto ya maji taka ni kubwa. Sisi Jiji la Arusha tumepata mradi mkubwa sana wa maji wa bilioni 520, na kabla ya mradi huo mtandao wa maji taka uliopatikana ulikuwa ni wa 7.66%.

Mheshimiwa Spika, uwepo wa mradi huu mkubwa umeweza kuitoa hiyo 7.6% kwenda hadi asilimia 30. Kwa hiyo unaweza ukaona kabisa kwamba asilimia 70 ya wananchi wa Jimbo la Arusha bado hawana uwezo wa kupata huduma za maji taka kutokana na uwezo mdogo wa fedha zilizopo. Kwa hiyo ningependa kumwomba Mheshimiwa Waziri, ninajua ametusaidia sana Jiji la Arusha tuna kiwanda chetu cha A to Z ambacho kimeajiri watu zaidi ya 10,000, kwa kile cha mjini na cha kule Olmoti; lakini kuna mtaro wa maji taka ambao una changamoto kubwa sana kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ninajua Mheshimiwa Waziri alishafika hapo na tayari kuna fedha zimekwishatolewa kama 1,152,000,000 na bado kuna mahitaji ya 1,362,000,000. Kwa hiyo tunaomba Mheshimiwa Waziri atumalizie fedha hizi ili tuondoe changamoto baina ya kiwanda, kwa maana ya mwekezaji na wananchi, hasa wa mitaa ya olmoti na Mtaa wa Olteves.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, ukienda Masklia kwenye Kata ya Telati tumejenga bwawa kubwa lenye uwezo wa

kuhifadhi lita milioni 22 za maji taka kwa siku. Changamoto iliyopo, wananchi wanaozunguka pale, wa Mtaa wa Masklia wanataka wafanye shughuli za kilimo na masuala mengine kwa kutumia maji yale, lakini hawajapelekewa miundombinu ya kufika kwenye mashamba yao.

Mheshimiwa Spika, ninakumbuka jana tulizungumza kwa pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Maji. Ninaomba jambo hili tulipe uzito unaostahili ili wananchi wenzetu waweze kutumia fursa ile ya maji taka kama mbolea na kwa hivyo waweze kufanya shughuli za kilimo vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya changamoto ya muda tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na kwa usimamizi wa Waziri Aweso na Naibu wake, Katibu Mkuu na timu nzima kwa namna ambavyo wametupatia mradi mkubwa wa maji wa bilioni 520.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia; kuna maeneo ambayo bado hayana maji, hasa kwenye maeneo ya pembezoni kama kwenye Kata ya Telati, kuna mitaa ya Bondeni, Olekolesi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga, Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza ajiandae.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Wizara yetu hii ya Maji.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya katika sekta zote na hasa katika sekta hii muhimu

amefanya makubwa sana nchini na katika Jimbo langu la Namtumbo kwa kuwatoa akina mama kutoka kwenda mwendo mrefu kufuata maji na kuleta majumbani na kumtua mama ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ninaomba nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Aweso, Waziri wa Maji, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, wataalamu wote na wakuu wa taasisi walio chini ya wizara hii. Ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa usimamizi mzuri sana na ushirikiano mkubwa anaotupa sisi Waheshimiwa Wabunge pamoja na watumishi wote katika wizara yake, wa juu mpaka wa chini. Ninakmwombea kila la kheri katika kazi hii anayoifanya, Mwenyezi Mungu aendelee kumpa hiyo busara na hekima katika kazi yake ya kulitumikia taifa hili. Hongera sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika wilaya yangu Mheshimiwa Waziri amefanya mambo makubwa sana. Nilipomwendea mara ya kwanza kumwambia kwamba nina maeneo ambayo yana shida ya maji aliniambia, rudi nenda kakae na DM na RM wako wa mkoa, kaorodheshe maeneo yote yaandaeni tuleteeni tutaanza kuweka kwenye bajeti. Kwa hiyo ninaomba nimshukuru leo mbele ya Bunge hili Tukufu. Tupeleka miradi mikubwa isiyopungua 15 na yote imefanyiwa kazi. Ninamshukru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna mradi wa maji ambao ulikuwa kama donda ndugu, ulikuwa kizungumkuti mradi wa Walitora-kumbala. Mradi huu ulisimama kwa muda wa miaka isiyopungua saba bila kufanya kazi. Tulipeleka taarifa za mradi ule na sasa leo hii watu wanakunywa maji katika Kata ya Litora na Kumbala. Pia tuna mradi wa maji Lingusanguse. Lingusanguse ni kijiji ambacho hakikuwa na maji kabisa, hawakuwahi kupata maji ya mtiririko lakini leo wanakunywa maji ya mtiririko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi wa tatu ni Mradi wa Ilumbahiro na Ikesi, nao ulilala ni wa miaka isiyopungua nane; lakini tulipompelekea taarifa za mradi huu walianza kutuwekea bajeti na unaendelea, ambapo sasa hivi wamefikia asilimia 80, na wanakunywa maji. Tuna Mradi wa Maji Mgombasi, kule Mgombasi hatujawahi kupata maji ya mtiririko; kulikuwa na maji

ya visima na akina mama walikuwa wanakwenda kuchota maji mabondeni, wanakwenda kwa mwendo mrefu. Leo wametupatia mradi huu wa 2,700,000,000. Mradi huu umejengwa lakini umebakia eneo kidogo tu ambalo ni kwa ajili ya mabomba ya nchi nane. Changamoto ambayo imebaki ni kwenye kupatikana kwa mabomba ya nchi nane ambayo inaonekana mkandarasi hajalipwa ili *PLASCO* waweze kutusambazia hayo maji kutoka kwenye tenki.

Mheshimiwa Spika, chanzo cha maji kimejengwa, tenki limejengwa, visambazio na mabomba madogo mpaka kwenye vituo vya maji vyote vimejengwa. Bomba la nchi nane kutoka kwenye tenki la maji kuleta chini kwenye visambazio na vituo vya maji kwa ajili watu waweze kuteka maji hayo ndiyo bado. Kwa hiyo tunaomba sana mradi huu ukamilike. Hilo bomba la *inchi* nane linunuliwe na kuletwa pale. Sio mita nyingi sana na si kilomita nyingi sana, ni chache, lakini ni hapo ndipo tulipokwama; hatuna bomba la inchi nane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna mradi mwingine wa maji wa Msisima ambao unaendelea katika Kata ya Msisima na Vijiji vya Mnalawi. Utekelezaji wake unaendelea, upo vizuri, ujenzi wa kichotea maji kile umeshakamilika, ujenzi wa tenki lita 200 umekamilika na kazi inaendelea. Kwa hiyo tunamshukuru sana na wananchi wa kule wanamshukuru sana. Mradi wa maji Mchomolo nao unaendelea vizuri sana, ujenzi wa chanzo cha maji umekamilika, ujenzi wa lita 300 nao umekamilika. Kwa hiyo tunaendelea vizuri na usambazaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji Misufini, kazi ya kwanza ya kuchimba visima ilifanyika kwa kutumia gari zile walizotuletea; tunashukuru sana. Sasa hivi tumeshatangaza ili kupata mkandarasi wa kuweka mabomba na kujenga matenki kwa ajili ya kusambaza maji. Kwa hiyo tunamshukuru sana kwa kazi hii nzuri ambayo ameifanya katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna Mradi wa Limamu ambao tumeshapitia, umekamilika na sasa hivi tunaomba kibali kwa ajili ya Mradi huo. Pia Mradi wa Maji Rumecha Mtakanini wa milioni 200, tulishachimba kisima na sasa hivi tupo katika hatua hizi za

usambazaji wa maji. Pia kuna Mradi wa Maji Hanga, mradi huu nao ni miongoni mwa ile miradi ambayo ni donda ndugu. Huu ninaomba waufanyie kazi. Kati ya ile miradi miwili iliyokuwa donda ndugu mmoja aliufanyia kazi na umekamilika lakini Mradi huu wa Hanga ambao sasa hivi upembuzi yakinifu ulishafanyika, sasa watu wamesubiri zaidi ya miaka nane lakini bado mradi huu haujaanza. Tunaomba sana tupate kibali cha kuanza mradi huu ili mradi uweze kuanza. Juzi nilikuwepo Kata ya Msindo na Kata ya Hanga. Kule malalamiko yao makubwa ni kwamba mradi huu umechukuwa miaka mingi na haujaanza; na wanaona maeneo mengine miradi inaendelea lakini katika Kata hii ya Msindo na Hanga mradi huu haufanyika. Kwa hiyo tunaomba sana mtusaidie.

Mheshimiwa Spika, pia kuhusu kuboresha maji Namtumbo Mjini; tunashukuru sana leo asubuhi Naibu Waziri amenijibu vizuri sana hapa. Pale Namtumbo Mjini mradi ule ulijengwa miaka ya 80, wakati huo kabla haujawa mji na wala haujawa Makao Makuu ya Wilaya, kilikuwa ni kijiji tu; kwa hiyo ni mradi wa siku nyingi. Miaka miwili ya nyuma walitusaidia, walitupatia bilioni 1.5…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili imeshagonga.

**Mhe. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba mtusaidie. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga atafuatiwa na Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mheshimiwa Saimon Songe Lusengekile ajiandae.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema maneno haya yafuatayo; Mheshimiwa Awezo Waziri wetu, mtu makini, Waziri wa viwango Mwenyezi Mungu amjalie kwa ibada hii kubwa ambayo

unaifanya ya kugawa maji kwa kila mwananchi wa hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sifa nyingi na kubwa zaidi zimwendee kipenzi chetu Mama, yetu Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye yeye alitanabaisha kwamba, moja kati ya jambo kubwa ambalo yeye atalifanya ni kuhakikisha kwamba anamtua mama ndoo kichwani. Tunaona na tunathibitisha *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na nikupongeze kwa maneno ambayo uliongea jana mbele ya Mheshimiwa Rais, kwamba wanaomuelewa ni wengi zaidi kuliko wale ambao hawamuelewi. Kwa hiyo tupo naye, mafanikio tunayaona, kazi kubwa ambayo anaifanya tumeiona. Tumeona fedha za *UVIKO* zilivyokwenda kwenye sekta hii ya maji, tumeona jinsi ambavyo wananchi wengi wamepata maji kuliko miaka ile ya nyuma ilivyokuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuna budi kumuombea Mheshimiwwa Rais wetu, kumuombea Mheshimiwa Waziri wetu, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa wizara kwa kazi hii kubwa ya ibada wanayoifanya. Juhudi hizi siyo sisi tu ambao tumeziona kama Watanzania au kama wananchi wa hapa Tanzania; Benki ya Dunia imethibitisha mwaka jana mwaka 2023 kwa kuona utendaji bora ambao umefanywa kwa mradi wa *P4R,* malipo kwa matokeo. Kutokana na faida hiyo na kazi kubwa ambayo Serikali yetu imeifanya hasa Wizara ya Maji, tunapata fedha kutoka bilioni 350 kwenda bilioni 654, na kwamba sasa mikoa itaongezeka kutoka mikoa 17 – 25; halmashauri kutoka mia moja themanini na sita, ukitoka themanini na sita hadi mia moja tfedhathini na saba.

Mheshimiwa Spika, hii ni kazi kubwa na mafanikio haya kwa kweli hatutaweza kupna kwa kipindi kifupi lakini huko mbele kunatia matumaini makubwa. Hongereni sana sana Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninaona kabisa kwamba kwa mafanikio haya fedha hizi zikija tukichanganya na fedha ambazo zitakuwa zimetoka kwenye mfuko wa maji nina uhakika acha zile changamoto ambazo zipo kwangu kule Kishapu zitashughulikiwa.

Ninasema hivyo kwa sababu kwangu kule Kishapu kuna miradi ambayo kidogo imekwamakwama, na changamoto kubwa imekuwa ni fedha; lakini sasa hivi kwa uwepo wa fedha hizi Mheshimiwa Waziri sitamwelewa kama kwenye miradi ile ambayo imekwama ya Igaga, Mwamashele, Lagana, Mwamandota kule Ngofira, Nwang'olo, Ngenze pale Mwadui, Masanga kwenda Ndoleleji, miradi ya visima virefu ya Idukilo hadi Kabila; kama ikikwama sitaelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sitaelewa miradi hii ikiendelea kukwama baada ya kipindi cha mwaka mmoja kama mambo yakiwa yamekaa sawa sawa, maana fedha watakuwa tayari wanazo.

Mheshimiwa Spika, nitoe angalizo moja, tunachangia hapa tunasema kwamba mfuko wa maji uongezewe fedha kutoka shilingi 50 mpaka shilingi 100, lakini mimi angalizo langu ninapenda kulitoa kwenye kanuni ya ugawaji wa fedha kwenye mfuko wa maji.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninaomba kanuni ya ugawaji wa fedha kwenye mfuko wa maji iwe sawa sawa na kanuni ya ugawaji wa maji kwenye mfuko wa barabara. Leo hii tuna Waziri ambaye ni mwelewa, ambaye ni mwema na mcha Mungu. Siku ikijakutokea Waziri ambaye anajijua mwenyewe akaja akawepo Wizara hii ya Maji, mgao ule anaweza mtu akaja akaamua akapeleka fedha nyingi zaidi huku na huku kwingine akaacha. Kitu ambacho kinaweza kikatuletea shida. Kwa hiyo walao tukijaribu kuangalia mfuko wa maji, kanuni zikaendana na mfuko wa barabara ambao wenyewe unasema kwamba asilimia kadhaa itakwenda huku, fulani atapata hiki na fulani atapata hiki lakini sasa hivi haifafanui. Haifafanui nani anapata nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa kulionge kwa msisitizo mkubwa sana, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri; mafanikio mengi ambayo tunayasema kwenye Wizara hii, na mafanikio mengi ambayo tunawasifu watendaji; nimpongeze sana mimi kwa kweli kwenye watendaji napenda sana kumpongeza Mkurugenzi Mkuu wa *RUWASA Eng.* Clement Kifegalo. Mwenyezi Mungu amjalie mema sana na aendelee kumuweka Mkurugenzi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ambacho mimi napenda kukisema ni kuhusu malipo ya wakandarasi, benki sasa hivi wamekaa wathamini kule juu ukikopa bilioni tatu sasa hivi unalipa milioni 500 kwa mwaka, *that is a lot of money. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi hii mikubwa ambayo tunaifanya na inafanywa, mimi ninaomba Serikali ijaribu kuwa makini sana. Tusiache mpaka watu... Watu sasa hivi wameanza kuuziwa nyumba na wameanza kupata *stress*. Hili jambo mafanikio haya yaende sambamba na mafanikio ya wale ambao wanafanya hizi sifa zipatikane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi hii bila kufanywa na hao watu wakandarasi ambao wamekuwa wakiifanya kwa roho moja, kazi ingekuwa ni ngumu sana na pengine leo lugha hii ambayo tunaizungumza isingekuwa namna hii. Ninaomba sana Wizara ijaribu kukaa na Wizara ya Fedha. Wizara ya Fedha huko hebu wa-*boost* kidogo maana na wenyewe kule wana mambo yao. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza. Atafutatiwa na Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile. Tutamalizia na Mheshimiwa Grace Victor Tendega. *(Makofi)*

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Spika, na mimi nashukuru kwa kupata nafasi lakini nianze kwanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Aweso kwa kazi nzuri anayofanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais katika ajenda yake ya kumtua mama mdoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja ya sifa kubwa ambayo Mheshimiwa Aweso amejaliwa ni usikivu, niliposimama hapa mwaka jana kuchangia bajeti ya maji, nilizungumza umuhimu wa Wizara kuangalia namna gani ambavyo wataongeza bajeti ili waweze kukarabati miundombinu ya maji ambayo imechakaa. Nikatolea

mfano wa Maeneo ya Mwenge Ichenjeze ambayo yanapatikana kwenye Mkoa wangu wa Songwe. Miundombinu ilikuwa ni mibovu lakini leo nimesimama hapa kumshukuru sana Mheshimiwa Aweso, ametuletea fedha bilioni moja 1.7 na sasa hivi mabomba yanatandazwa, ukienda kule Mloho na Vwawa, wananchi wanapata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, nampongeza Mheshimiwa Aweso, tulimshauri kuhusu mita zile za malipo ya kabla, jambo hili lilikuwa ni muhimu sana, wananchi walikuwa wanateseka kwa kubambikiziwa bili za maji. Leo sisi ni mashahidi, Mheshimiwa Aweso ameshaanza kulifanyia kazi na kwenye taarifa yake amesema kwamba ameanza kwenye mikoa mitano ukiwepo Mkoa Tanga, Arusha pamoja na mikoa mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme kitu kimoja, katika mchakato huo nimevutiwa zaidi na namna ulivyotoa nafasi kwa wataalam wetu wa ndani. Umeondoa ile kasumba kwamba kila kitu lazima tuagize nje. Mita hizo umezinunua humu humu ndani, zinazotengenezwa na wataalam wetu wa ndani katika vyuo vyetu, nikupongeze sana kwa hilo. Niombe vilevile taasisi zingine ziweze kuiga mfano huo ambalo ni jambo jema, kwa sababu kwanza linasaidia kukuza ujuzi ndani ya nchi yetu na kulinda thamani ya fedha ambazo tunazo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee zaidi nampongeza Mheshimiwa Rais wetu, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. Sisi Wanawake wa Mkoa wa Songwe tunasema kwamba ndiye balozi namba moja wa Ajenda ya Kumtua Ndoo Mwanamke Kichwani. Katika kipindi chake tumeshuhudia mapinduzi makubwa katika sekta ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii Mikoa yote ya Tanzania imepata mitambo ya kuchimba maji lakini sisi kwenye Mkoa wetu wa Songwe mtambo ule haujafika ukakaa tu, tunavyoongea sasa hivi tumeshachimba visima 65 ndani ya Mkoa wa Songwe, hili ni jambo jema, nimuombe Meneja wetu wa *RUWASA*, ameenda kwenye wilaya zote tatu, bado Wilaya moja ya Ileje, naamini kwamba atafika ili wananchi waweze kuondokana na kero ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wetu ameona kwamba haitoshi kwenye bajeti hii ametoa visima 900 kwenye majimbo yote 180. Hili ni jambo ambalo ni kubwa sana, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu kwa sababu anatekeleza kwa vitendo ajenda yake ya kumtua ndoo mwanamke kichwani. Sisi Wanawake wa Mkoa wa Songwe tuko pamoja naye na tunamuunga mkono sana. Tunasema kwamba mwaka 2025 kura zote ni kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tuna changamoto kubwa kwenye nchi yetu, kwamba fedha za miradi zinapelekwa lakini ukiangalia tija ya hizo fedha haionekani. Ndani ya miaka michache ya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, tumeshuhudia mapinduzi makubwa ya usimamizi wa fedha za miradi na *World Bank* wamekuwa ni mashahidi, wameonyesha namna gani ambavyo Tanzania sasa hivi tuko vizuri kwenye kusimamia fedha za miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi namuomba Mheshimiwa Waziri kitu kiimoja, umesema kwenye taarifa yako kwamba, kwa fedha hizo sasa mikoa imeongezeka kutoka mikoa 17 mpaka mikoa 25 na Mkoa wa Songwe uko ndani. Mimi naomba, tumekuwa tukisema miaka yote kwamba, ndani ya Mkoa wa Songwe, tunaishukuru sana Wizara tumepata miradi mingi lakini bado tulikuwa hatujapata miradi ya kimkakati. Tunao mradi wa kutoa maji Tunduma kwenda kuyasambaza kwenye Miji ya Mbozi, Tunduma, Vawa pamoja na Mji wa Mlowo, ni miji ambayo ina changamoto kubwa sana ya maji; Mheshimiwa Waziri tunaomba utusaidie kwa sababu mkandarasi ameshapatikana tunaomba sasa fedha hizo zije, mradi huo uweze kutekelezwa na usainiwe ndani ya Mkoa wa Songwe kama ambavyo juzi mmekuja kusaini ule mradi wa mafumbo ndani ya Wilaya ya Mbozi, Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala lingine ambalo ni muhimu sana, tunasema kwamba tunapozungumzia mafanikio yote ya Wizara ya Maji, hatuwezi kusahau kuwapongeza watu wa *RUWASA*, kwa kweli wanafanya kazi sana. Meneja wetu wa *RUWASA* Mkoa wa Songwe, anafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimuombe Mheshimiwa Waziri, tunasema kwamba unapomkamua ng'ombe maziwa ukumbuke vilevile kumlisha. Mimi nikuombe, mwaka jana nilisimama nikaongea, Mkoa wa Songwe mpaka sasa hivi hatuna gari la maji, tuna gari moja tu, yaani hilo gari anatumia Meneja wa RUWASA, wanatumia ma-*engineers* wa wilaya, hilo gari linaenda *site* na hilo gari linakuja Dodoma, hivi sasa leo yuko Dodoma, maana yake kule Songwe hakuna gari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Aweso ni msikivu lakini kwa hili naomba awe msikivu zaidi, utupatie magari ya kutosha ndani ya Mkoa wa Songwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, hukusu suala la maslahi ya watumishi, watumishi hawa wa *RUWASA* tangia walivyohamishwa kule kwenye halmashauri kwa kweli maslahi yao bado hayajaboreshwa. Wengine wa taasisi nyingine maslahi yao yaliboreshwa lakini hawa bado mpaka sasa hivi maslahi yao ni duni. Mheshimiwa Waziri, changamoto ni nini? Kama suala la kuthibitisha, tunaomba wathibitishwe ili maslahi yao yaweze kuboreshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu ni suala la ofis, juzi nilienda kumtembelea Meneja wa *RUWASA*, kwa kweli nilisikitika sana, amejibanza tu kwenye kachumba kamoja tu pale kwenye ofisi ya wilaya, hakuna ofisi kabisa. Ukimuona hapa Dodoma amevaa suti lakini hana ofisi, kwa hiyo, mimi naomba ujenge ofisi ili watu hawa wanavyofanya kazi nzuri, wafanye kazi kwenye mazingira ambayo ni mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kwenye Wilaya ya Momba pamoja na Songwe hawana ofisi. Naomba sana waweze kupatiwa ofisi, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, atafuatiwa na Mheshimiwa Grace Victor Tendega.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie Wizara ya Maji. Nikupongeze sana Mheshimiwa Aweso na timu yako kwa kazi kubwa

mnazofanya. Kwa kweli mnafanya kazi kubwa. Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamekupongza kwa usikivu wako na mimi nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu, *Engineer* Mwijuma, mnafanya kazi kubwa, Mheshimiwa Waziri kwa kweli tuna imani na timu yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kwa sababu mimi nanufaika na miradi ya maji vijiji, nampongeza sana Mkurugenzi Mkuu wa *RUWASA*, kaka yangu Clement, anafanya kazi kubwa sana kule vijiji na kuhakikisha kwamba maji yanapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa nimetunza pongezi za Mheshimiwa Rais, niziseme hapa sasa. Namshukuru sana na ninampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan. Sisi Wanamkoa wa Simiyu sasa hatuna deni naye, mwaka jana tarehe 10 Mwezi wa Tano, nilichangia hapa kwa uchungu sana; Mheshimiwa Aweso unakumbuka, mpaka nikataka nikata kushika shilingi yako. Mama yangu Mheshimiwa Esther alichangia hapa na Mheshimiwa Mpina alichangia hapa juu ya mradi mkubwa wa maji wa Ziwa Victoria. Sasa nitamke rasmi kwamba sasa ule mradi umeanza na mwezi wa pili ulikuwa na asilimia nne, kwa kweli tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kukubali kusaini mkataba wa bilioni 444 kwa ajili ya Mradi Mkubwa wa Maji wa Ziwa Victoria ambao unakwenda ku-*solve* matatizo yote ya Mkoa wa Simiyu, Busega, Itilima, Bariadi kwa kaka Kundo, Maswa pamoja na Meatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli peleka pongezi zetu kwa Mheshimiwa Rais, hatumdai kwenye mradi huu. Tunachokuomba Mheshimiwa Aweso, utakapokuwa unapeleka pongezi hizi na shukurani zetu kwa Mheshimiwa Rais, tunaomba sasa umuombe apande aje azingue rasmi mradi wetu, tumpe maua yake, aje Busega kwa sababu ndiyo kuna chanzo, ninajipendelea sana kwa sababu mimi ndiyo mchangiaji wa kwanza kwa Mkoa, basi aje Busega tuzindue ule mradi mkubwa wa Maji wa Ziwa Victoria ambao utakuwa unapeleka maji kwenye Mkoa wetu wa Simiyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tayari *clearance* za *site* pale Lwango kwa ajili ya kujenga *tank* kubwa la maji la ujazo wa lita milioni 5 umeshaanza na mimi nimeshuhudia pale. Nimeshaenda zaidi ya mara mbili, nimekutumia picha Mheshimiwa Aweso, umeona kazi inayofanyika pale ni Dhahiri tumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, umesema hapa habari ya visima, sisi pale na Meneja wangu wa *RUWASA* wa wilaya tuna *database* ya vijiji vyetu. Tunavipa *priority* kulingana na matatizo yaliyopo, sisi tumeshamaliza kuweka kwenye orodha; tunaanza na Malili, tunaenda Ngunga, Mwamgoba, Ngasamo tunamalizia Nasanga. Sisi vijiji vyetu vitano ndiyo hivyo tulishamaliza, kwa sababu tuna *data* ya vijiji vyote ambavyo bado vina changamoto ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, meneja wangu wa wilaya ni mzuri, ananisaidia vizuri sana, nimeshaleta taarifa zake kwako, yeye ndiye anayejua, Mheshimiwa Aweso huwa unasema, anayelala na mgonjwa ndiye anayejua mhemo wa mgonjwa. Kwa hiyo, mimi na meneja wangu wa *RUWASA* wa Wilaya ndiyo tunajua mihemo ya wananchi wetu. Kwa hiyo, hii tuliyokwambia ndiyo mihemo ya Wananchi wa Busega na ndiyo mahitaji ya kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi moja tu ambayo nimeshakuomba kijana wangu huyu Daniel Gagala, Meneja wetu wa wilaya amekaimu zaidi ya miaka miwili, mthibitishe, mimi binafsi nimeshamfanyia *vetting*, anatosha. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni malipo kwa wakandarasi, Waheshimiwa Wabunge hapa wameshachangia juu ya malipo kwa wakandarasi. Kwa kweli kuna wakandarasi wanadai fedha nyingi, wengine wanadai miezi saba na wengine wanadai mwaka na bado hawajalipwa. Tunaomba sana sasa ukae na Wizara ya Fedha, tuwalipe wakandarasi hasa wakandarasi wazawa. Kwa kweli wanateseka na hawa ni wazalendo sana, wakandarasi wazawa hawatozi riba wakicheleweshewa malipo yao, wanakuwa wazalendo. Mheshimiwa Aweso, tunaomba sana mkae na Mheshimiwa Waziri

wa Fedha tuweze kuwalipa hawa wakandarasi wazawa ili waweze kufanya kazi wakijua kwamba wana fedha zao. Kwa sababu wengine wana mikopo wanafirisiwa lakini mkiwalipa basi watapeleka mikopo yao na kurejesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule Usukumani tuna msemo mmoja unasema Ukiwa na wakulima wawili mazao yao yakaliwa, mkulima mmoja mazao yake yakaliwa na ng'ombe wa kwake na mkulima mwingine mazao yake yakaliwa na tembo, mwenye hasara zaidi ni yule ambaye mazao yake yameliwa na tembo. Kwa nini? Kwa sababu yeye hatafaidika popote pale lakini huyu ambaye mazao yake yameliwa na ng'ombe, jioni anaweza akakamua maziwa akapata *compensation* ya mazao yake waliyoliwa kwenye maziwa, namaanisha nini? Wasukuma hapa wanamaanisha kwamba mkandarasi mzawa tukimlipa fedha yake itazunguka hapa hapa Tanzania, ndiyo maana ya misemo hii ya Usukuma. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo, Mheshimiwa Waziri, tunaweza tukawalipa sasa hivi lakini ni lazima tutafute chanzo cha kudumu kwa ajili ya kupata fedha. Wenzangu wameshasema hapa juu ya chanzo, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha mzungumze, atakapokuwa analeta bajeti yake hapa mwezi wa sita basi aje na chanzo kitakachoiongezea fedha Wizara yetu ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna mfuko wa maji, huu mfuko wa maji unatakiwa uongezewe fedha ili kusudi ziende kwenye miradi yetu ya maji. Tunahitaji kuwa na maji na tunahitaji tupate maji kwenye vijiji vyetu hasa kwenye vijiji ambavyo bado havijapata maji. Wewe mwenyewe kwa kauli yako huwa unasema hamna mbadala wa maji na mimi naungana na wewe, hakuna mbadala wa maji, lazima leo tumalize tatizo la maji kwenye vijiji vyetu. Kwa hiyo, tutafute vyanzo tusiathiri wananchi,tuna vyanzo vya Serikali zingine, tunaweza kupunguza kidogo kidogo kwenye sekta zingine, tukaleta kwenye chanzo cha mfuko wa maji ili tuweze kupata fedha nyingi tuwapelekee Watanzania, wawe na maji kwa ajili ya matumizi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo...

*(Hapa kengele ililia kiashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Grace Victor Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Maji. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa fursa hii.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote, hongereni sana. Wanasema "Mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni." Mimi nakupongeza Mheshimiwa Waziri kwa sababu umefanya kazi kubwa ya kuhakikisha Watanzania wanapata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukianzia mkoani kwetu sisi, kwa kweli tumepata maji na kuna miradi ambayo inaendelea, ambayo wanakijiji walikuwa hawajawahi kuwa na maji lakini sasa hivi wanaanza kupata maji safi na salama, nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna vijiji ambavyo vilikuwa havijapata maji lakini miradi imekamilika na vingine ambavyo sasa hivi inaenda kukamilika. Kwa mifano, kuna vijiji vya Itagutwa, Nyamlenge, Wangama, Idodi, Ufyambe, Izazi, Makatapola, Magulilwa, Nabula, Kilambo, Mlanda na vingine vingi. Kwa kweli kazi kuwa imefanyika, nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, mimi nampongeza Mheshimiwa Waziri katika Wizara yake kuna ile *Program* ya *P4R*, wameshika nafasi ya kwanza kwa nchi 50, si kitu kirahisi, ni kitu ambacho ni sifa kwa nchi yetu na kinatuletea sifa kubwa sana. Kwa hiyo, kwa kufanya hivyo wametuletea pesa ambayo itasaidia kupeleka maji katika vijiji vile ambavyo havikutajwa katika taarifa yako. Kwa hiyo, ni mategemeo yangu sasa vile vijiji ambavyo tunavitaka

vipate maji, vitapata maji tena. Sisi tuna vijiji vingi kwetu, ningevitaja lakini kuna vijiji vingi ambavyo vipo vinatakiwa kupata maji, nitakuletea kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nianze kwa kuzungumzia madeni. Kumekuwa na changamoto kubwa saba ya taasisi za umma na mashirika mbalimbali kutokulipa maji katika mamlaka zetu. Hii inasababisha mamlaka kushindwa ufanya kazi yake ipasavyo, tunaona hivyo wakati Serikali ikiwa na sisi kama Bunge tukiwatengea *OC* humu ndani lakini hawpeleki hizo fedha kwa Mamlaka ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninaomba na ninatoa ushauri, ninaomba Wizara muende mfuatilie fedha hizo, lakini mna mradi wa zile *prepaid meters*. Ninaomba muende mkafunge hizo *prepaid meters* kwenye hizo taasisi na hayo mashirika ambayo hayawalipi pesa. Mkianza nao hizo pesa zitapatikana na tutaweza kuangalia Mamlaka yetu ya Maji itapata fedha. Kwa hiyo, mimi huo ni ushauri wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *prepaid meters* zianze kwenye taasisi hasa zile zenye madeni makubwa. Tunasoma taarifa za *CAG*, Taarifa za Kamati ya *PIC, LAAC* na *PAC* zote zinazungumza madeni makubwa ya Taasisi za Serikali. Sasa kama tunawatengea pesa hapa na hawawalipi mamlaka, mkafunge *prepaid meters* tuone watafanya nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye suala la upotevu wa maji, kumekuwa na upotevu mkubwa wa maji katika maeneo mengi tunayoishi. Maji yamekuwa yakipotea na tumekuwa tukitoa taarifa, wakati mwingine hakuna majibu ya haraka. Kwa hiyo, unakuta kwamba tunaona Serikali inapoteza Serikali inapoteza maji mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mmesema mna *system* ya ku-*detect* upotevu wa maji, lakini hata kama mna *system* ya ku-*detect* upotevu wa maji, wakati mwingine tumekuwa tukiona maji yanatiririka bila kudhibitiwa, sasa hapo inakuwaje, mnaona halafu ham-*respond* tu kwenda kufanya hivyo?

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo huwa napita, karibu na Nzuguni kuna eneo ambalo karibu mwezi mzima maji yametengeneza kama bwawa hapa Dodoma. Kuna maeneo ya Ilazo maji yanamwagika lakini hatuoni ile *response* ya wafanyakazi kwenda kufanya hivyo. Kwa hiyo, ushauri wangu mimi kila wakati muwe mnapanga *program* ya kwenda kuangalia jinsi mabomba mabomba yanavyoendelea hata kama mmeweka leo, *TARURA* inaweza ikaja ikatengeneza barabara wakafukua wakaharibu muundombinu. Kwa hiyo, mtengeneze hiyo *regular monitoring and evaluation* ya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine, kuna suala la uboreshaji wa huduma za maji wenzangu wamezungumza, tumekuwa na changamoto ya maji vijijini. Pamoja na zile asilimia mlizoweka kwamba mmefikia asilimia 79.6 lakini bado kuna changamoto ya maji vijijini kwa asilimia kubwa. Tunaona kwamba tulitoa ile shilingi 50 kwenda 100 lakini ile 50, asilimia 88 inatakiwa igawanywe kwa ile 50. Igawanywe kwa mabonde, maji vijijini na maji mjini lakini hakuna kiwango kinachosema, mijini wapewe maji asilimia hii, vijijini wapewe maji asilimia hii na mabonde wapewe asilimia hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nina ushauri, katika ile 50 kwenda 100, asilimia 60 wapewe *RUWASA*. Ambao ndiyo wanaoweza kutoa maji kwa wananchi vijijini. Hizi 20 wapewe mabonde na 20nyingine wapewe mijini kwa sababu mmeshafikisha asilimia 90 ambayo karibu mnamaliza. Hii itasaidia Watanzania wengi hasa wa vijijini waweze kupata maji. Mkiwapangia, Mheshimiwa Lucy alivyosema hapa kama wanavyofanya wenzetu huko *TANROADS*, unakuta kwamba asilimia 70 wanapewa *TANROADS* na asilimia 30 wanapewa *TARURA*; na huko muwawekee kiwango ili waweze kujua ni kiwango gani ambacho wanatakiwa kukipata wao kama wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa sababu kule *RUWASA* wazawa ndiyo ma-*engineer* wetu, wakandarasi wetu, sasa hawa wakandarasi hamuwalipi pesa, wana *raise certificate* kuanzia miezi sita mpaka miaka miwili hawapati pesa hata kidogo kwa sababu wao hawadai *interest,* lakini makampuni mengine ya nje

wanadai *interest* mnawalipa. Sasa mnawaonea hawa wazawa. muwape pesa na ndiyo maana tunaangalia katika bajeti asilimia ya pesa za maendeleo hazi…*(Makofi)*

*(Hapa Kengele Ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti, kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, katika fedha za maendeleo, hamjapewa hizo pesa. Tunaomba Serikali itoe fedha ili muweze kupeleka vijijini, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti, nimeona jina lako hapa, kwa hiyo, ulichotaka kumuambia utasema mwenyewe baadaye wakati wa muda wako wa kuchangia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa sehemu ya kwanza ya kukutana kwetu leo, nitaje baadhi ya majina ambayo tutaanza nayo mchana; Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea, Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki na wengine wataendelea kutajwa kadri muda utakavyokuwa unaenda. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo moja kutoka kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania, Mheshimiwa Shally Josepha Raymond anawatangazia Waheshimiwa Wabunge Wanawake wote kuwa leo tutakutana mara baada ya kuahirisha Kikao hiki cha Bunge katika Ukumbi wa Spika, Ghorofa ya Tano, tutakutana huko Wabunge wanawake wote.

Waheshimiwa wabunge baada ya tangazo hili nasitisha shughuli za Bunge mpaka leo saa 11.00 Jioni.

*(Saa 7.24 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

*Mwenyekiti (Mhe. Joseph K. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Kwa orodha niliyonayo tuna Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, atafuatia Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya na Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu ajiandae.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza jioni ya leo. Kwanza naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunipa afya njema na kusimama ndani ya Bunge kwa mara nyingine kujadili na kutoa maoni yangu kwenye Wizara hii, Wizara ya Maji, ambayo ndiyo uhai wa wananchi wetu wa maeneo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa nzuri ambayo ameendelea kuifanya. Kipekee kabisa nachukua nafasi hii kukuomba Mheshimiwa Waziri wa Maji tufikishie salamu sisi Wananchi wa Rorya, Tarime, tunamshukuru sana kwa Mradi mkubwa wa Maji wa Miji 28 unaoanzia Rorya kwenda Tarime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka wakati tunaanza mradi huu haukuwemo kwenye bajeti, lakini Mheshimiwa Waziri nilikufuata na ukaniahidi kwamba, acha nizungumze na Mheshimiwa Rais nimuombe miradi minne ambayo itaongezeka kupitia miradi 28, ili angalau na wewe mradi wako Mheshimiwa

Mbunge uwepo. Nakushukuru sana kwa sababu, ulitimiza ahadi hiyo na ulivyomuona Mheshimiwa Rais, leo tunajivunia sisi wananchi wa Rorya, Tarime. Mradi wa shilingi bilioni zaidi ya 134 unakwenda kutekelezwa kwenye eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee tufikishie salamu hizo, tunamshukuru sana Meshimiwa Rais kwa hiyo kazi kubwa nzuri unayoifanya. Pia, nachukua nafasi hii kukushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa, nzuri, unayoifanya *brother*. Wewe ni mtu mmoja ambaye kwa namna yoyote tukisema tuseme sifa zako ndani ya Bunge yawezekana tukajikuta tunamaliza dakika hizi zote saba tunakuelezea wewe, lakini tuendelee kukuomba endelea kuwa hivyohivyo, mnyenyekevu na namna ambavyo unashirikiana na Wabunge kutatua changamoto zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachua nafasi hii kukushukuru sana, Mheshimiwa Waziri, na kukupongeza kwa namna unavyoishi na kufanya kazi na watendaji wako wote wa Wizara. Kuanzia Katibu Mkuu, dada yangu *Eng.* Mwajuma, Mkurugenzi wa *RUWASA* na wengine wote kwa namna ya ushirikiano na unavyowaweka pamoja katika kutimiza lengo, dhamira na maono ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakika wewe umedhamiria kubeba maono ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunakupongeza sana kwa kazi kubwa na nzuri unayoendelea kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda mimi nina mambo mawili tu ya kushauri leo. Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yako ipo miradi ambayo umeitaja na hii ni miradi mikubwa. Pamoja na kwamba, haujaipa jina la miradi ya kimkakati, lakini kwa mtazamo wangu naiona kama ni miradi ya kimkakati. Mradi mmoja wapo ni huu niliousema wa Miji 28 kwa maana ya Rorya, Tarime, ni mradi mkubwa ambao una-*involve* zaidi ya shilingi bilioni 134, lakini, umesema kuna mradi mkubwa utakaotoa maji Ziwa Viktoria kuleta Dodoma. Kwa sasa wanafanya *feasibility study* na maana yake ni kwamba, na wenyewe unakwenda kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi umeuzungumzia ambao utatoa maji ziwa Tanganyika na kuyapeleka kwenye Mikoa ya pande hizo kwa maana ya Rukwa na Mikoa mingine. Vilevile kuna mradi wa Busega ambao ameuzungumza Mheshimiwa Mbunge aliyetoka kuchangia hapa asubuhi, lakini kuna Mradi wa Bwawa la Kidunda pamoja na miradi mingi mikubwa ambayo umeitaja kwenye bajeti yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii ni mikubwa ukijumlisha fedha zake inawezekana ikagharimu sio chini ya shilingi trilioni moja mpaka shilingi trilioni mbili kuhakikisha kwamba, miradi hii inatekelezwa. Hofu yangu na hapa, ningetamani sana tumsaidie Mheshimiwa Waziri pale ambapo anakuwa na miradi mikubwa, anabeba dhamira na maono ya Mheshimiwa Rais, lakini fedha anayopewa ni ndogo sana. Sasa wasiwasi wangu ni namna ambavyo, kama anakuwa na miradi mikubwa ya zaidi ya trilioni mbili, lakini ana bajeti ya shilingi bilioni 600, tunajiuliza anakwenda kutekelezaje miradi hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natamani kushauri mambo yafuatayo; la kwanza...

**MHE. BALOZI DKT. BASHIRU A. KAKURWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Almas Maige, Taarifa.

**MHE. BALOZI DKT. BASHIRU A. KAKURWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuongezea hapohapo, sekunde chache tu. Hata ukomo wa bajeti ya mwaka jana iliyopitishwa hapa, ya mwaka huu imeshuka kuliko ya mwaka jana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Samahani, nilimtamka Mheshimiwa Almas Maige, ni Mheshimiwa Kakurwa.

Naomba Mheshimiwa uendelee. Kwanza unaipokea hiyo Taarifa?

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea Taarifa hiyo. Nakushukuru sana Dokta kwa kunikumbusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichotamani kumshauri Mheshimiwa Waziri ni nini, ili twende sote kama Bunge na twende kwa maana ya kumshauri kwa dhamira hiyo ya kubeba maono ya Serikali, la kwanza ni, Mheshimiwa Waziri ipambanue hii miradi yote. Ni lazima ukubali kuanzisha kitu kinachoitwa Mpango wa Maji wa Taifa. Mpango huu, Mheshimiwa Waziri, nenda kaainishe miradi yote mikubwa ambayo ndiyo maono na dhamira ya Mheshimiwa Rais ambayo umeitaja kwenye bajeti yako iingie kama sehemu ya Mpango wa Maji wa Taifa, iainishwe, uisajili, uitengenezee urasimishaji, ili kama Taifa sisi Wabunge wote na wananchi kwa ujumla wake, kama Watanzania, tuwe tuna mipango tunayojua kwenye Sekta ya Maji ni miradi ipi mikubwa inayokwenda kutekelezwa kutatua changamoto yote ya maji nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii mikubwa hatuwezi kuiacha ikabaki kwenye bajeti ile ya shilingi bilioni 600 wakati miradi yenyewe ukiijumlisha inakwenda zaidi ya trilioni mbili. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri la kwanza kabisa tengeneza mpango kabambe wa maji wa Taifa, ili angalau wananchi wote, na sisi kama Wabunge, tutakuunga mkono kwa sababu, dhamira uliyonayo ni ya kumuunga mkono Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tumuombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha aone namna ya kumsaidia Mheshimiwa Waziri kwa kutafuta vyanzo vya mapato, ili kukidhi na kuratibu miradi hii mikubwa ya kimkakati ambayo Mheshimiwa Waziri ameiainisha. Mimi natamani niende moja kwa moja kupendekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ambalo ninapendekeza ni ningetamani kupitia tozo hii tunayokatwa kwenye mafuta Mheshimiwa Waziri wa Fedha aone namna ya kupunguza baadhi ya maeneo ampelekee Waziri wa Maji fedha hizi, ili aweze kuratibu na kukamilisha miradi hii mikubwa ya kimkakati. Tusisubiri tozo nyingine zaidi ya hii inayokatwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kwa kuwa, tayari alikuwa amekata fedha zaidi ya shilingi bilioni 137 kutoka kwenye bajeti ya mwaka jana ameipunguza kuja kwenye bajeti ya mwaka huu, naomba Waziri wa Fedha na Serikali kwa ujumla tumrudishie fedha huyu Waziri, ili aweze kutimiza haya maono na vipaumbele vya Mheshimiwa Rais. Ukipunguza fedha hizi huyu hawezi kutimiza haya malengo. Mwisho matokeo yake tutakuwa tuna miradi mikubwa ya maji ambayo itachukua miaka nenda rudi, wakati miradi hii inatakiwa itekelezwe ndani ya Mwaka 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa harakaharaka ninayo miradi ambayo Mheshimiwa Waziri ningetamani uishughulikie ndani ya Jimbo langu la Rorya. Tunao Mradi wa Bukura ambao unahudumia kata zaidi ya nne. Tulikwenda mimi na wewe Mheshimiwa Waziri tukaanzisha mradi huu, umesimama haufanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao Mradi wa Gabimoli, tunao Mradi wa Komuge, tunao Mradi wa Nyarombo, tunao Mradi wa Bugendi, tunao Mradi wa Ikoma na tunao Mradi wa Sakawa, juzi Jumapili, nilikuwepo pale nafanya mkutano na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri miradi hii unaijua. Mimi mwenyewe kwa upendo kabisa wa Wananchi wa Rorya nilikuchukua ukaenda ukaianzisha kwa kutoa fedha na miradi imeanza, lakini kwa sasa imesimama. Mheshimiwa Waziri nakuomba sana, wananchi hawa wapate fedha, ili miradi iweze kukamilika na kukimbia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni mimi sikitiko langu ni lilelile ambalo naona hawa watu wamepunguziwa zaidi ya shilingi bilioni 137 na wakati hapa walipo Wizara hii inadaiwa na Wakandarasi zaidi ya shilingi bilioni mia mbili *plus*. Yani leo ukienda kwa Mkurugenzi wa *RUWASA* ana *certificate* za malipo za Wakandarasi ambao ni wazawa wa nchi hii zaidi ya shilingi bilioni mia mbili *plus*. Sasa ukimpunguzia shilingi bilioni 137 bado anatakiwa alipe Wakandarasi ambao wamefanya kazi za wananchi huko chini. Wanatakiwa wakamilishe miradi, ili iweze kutoa maji. Tunakuwa hatumsaidii Waziri na tunakuwa hatuendani na maono ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana fedha hizi ambazo zimekatwa, hizi shilingi bilioni 137 zirudi, ili angalau hawa watu waweze kuwalipa wakandarasi waliotoa huduma kwenye maeneo mengine. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, atafuata Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu. Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea ajiandae.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Ninaunga mkono hoja ya Bajeti ya Wizara ya Maji ambayo imesheheni miradi ya kimkakati ya maji kila kona ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza moja kwa moja katika miradi 247 ya maji safi na usafi wa mazingira katika Mamlaka ya Mji wa Mwanuzi ambapo shilingi milioni 867.8 zimetengwa. Niliomba hii kwenye *item* ya ujenzi wa mabwawa ya majitaka na uboreshaji wa huduma ya maji katika Mji wa Mwanuzi, katika zile *component* mbili tupewe kipaumbele cha ujenzi wa ma-*tank* katika mji huu. Kwa sababu, tunavyo vyanzo viwili vya maji ya kutosha, lakini hatuna ma-*tank* ya kupokelea maji, ili yaweze kusogezwa kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda kwenye uendelezaji wa rasilimali za maji, hususan ujenzi na ukarabati wa mabwawa ya ukubwa wa kati na madogo, ili kuweza kukabiliana na maeneo yenye adha ya uhaba wa maji kutokana na ukame, mojawapo likiwa ni Jimbo la Meatu. Naipongeza Serikali kwa kutekeleza miradi 14 iliyokamilika nchi nzima, miradi mingine 26 inaendelea, lakini miradi 92 imepangwa katika bajeti tunayoiongea sasa hivi, ikiwemo Jimbo la Meatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunaomba kura za marudio ya Uchaguzi wa Udiwani, wananchi waliomba kile chanzo mlichojenga cha Lukale kitanuliwe, ili kiweze kupokea maji ya kutosha na niliwaahidi maombi haya nitayaleta. Nakushukuru Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Katibu Mkuu Wizara ya Maji ombi hili mmelipokea na

mmetutengea shilingi 1,117,000,000 za kutengeneza bwawa hili. Oneni namna mtakavyolijenga, ili muweze kusaidia pia, Kijiji cha Mwabagimu kwa sababu, eneo lile lina chumvi kutokana na *Lake Eyasi*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi, nimeangalia katika ukurasa wa 70, hongera kwa hatua hiyo na pia, hongera kwa kazi zilizoanzwa. Matamanio ya mradi huu ilikuwa ni kukabiliana na athari ya mabadiliko ya tabia-nchi ikiwepo upatikanaji wa maji ya umwagiliaji, maji kwa mifugo na maji kwa ajili ya binadamu ambapo kazi mlizoziainisha zimelenga katika majisafi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia ujenzi wa kituo cha kusukuma majighafi na ulazo wa bomba ambalo ni la kilomita 75 kutoka kituo cha kusukuma majighafi hadi kituo cha kusafisha maji inaonesha kwamba, *component* ya maji ya mifugo, *component* ya maji ya umwagiliaji haimo. Naomba basi hizi Wizara tatu, Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo mfanye kazi kwa *coordination,* kwa kushirikiana, na wa Wizara ya Maji, mkitekeleza tutapata maji ya binadamu, maji mkitekeleza tunapata mifugo na umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Wizara ya Kilimo katika fedha za *ECF* mmeweka usanifu wa maji na mnashirikiana. Kutokana na maelezo ya Waziri mtashirikiana, ili muweze kuweka bomba la maji ambayo hayajatibiwa, ili yawafikie wananchi kwa gharama ndogo waweze kumwagilia pamoja na mifugo iweze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie mwisho. Wizara imeandaa mwongozo na matumizi ya mitambo 25 ya uchimbaji wa visima na seti tano za mabwawa. Mmeweka mwongozo wa utaratibu wa muda wa ufanyaji kazi, muda wa matengenezo, kinga na matengenezo makubwa ya mitambo. Nataka kuuliza, je, gharama za uendeshaji wa hiyo mitambo kwa kila *RUWASA* mmeziainisha? Je, kuna mfuko unaozunguka au mtategemea asilimia 100 ya bajeti ya Serikali Kuu? Wakati mwingine tumekuwa tukifeli katika bajeti, maana yake ni tutafeli katika kuendesha ile mitambo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaomba kushauri muweke mfuko wa kuzunguka *(Revolving Fund),* ili wakati Serikali inapochelewa ninyi muendeleze mitambo. Je, mmetenga katika bajeti fedha za mafuta kuongeza hizo *RUWASA*? Kwa sababu, naona fedha zinaenda kununua mabomba na kusambaza, je, ruzuku ya mafuta tutapa kutoka Serikali Kuu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Jimbo la Meatu katika vile visima vitano vya kila jimbo liangaliwe kwa mtazamo wa malambo madogo kwa sababu, kwa miaka mitatu mfululizo miradi mikubwa imeshindwa kutekelezwa, muda wote tunatafuta vyanzo. Naomba muweke mtazamo wa kutengeneza malambo madogo madogo. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu atafuatia Mheshimiwa Jacqueline Kainja. Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki ajiandae.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi. Kwanza na mimi naanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa uhai na leo kupata nafasi ya kuweza kuchangia kwenye Hotuba ya Waziri wa Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya kwenye kutatua changamoto hii ya maji na upatikanaji wake nchini. Pia, nampongeza sana mdogo wangu, rafiki yangu, Mheshimiwa Waziri Aweso pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri Kundo, Katibu Mkuu wetu, dada yangu, Mwajuma Waziri pamoja na viongozi wote kwa maana mnaisimamia taasisi yenu na idara zake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siachi kuwapongeza sana watu wangu ninaofanya nao kazi kwa karibu kwa maana ya *DAWASA*, kaka yangu Kiula Kingu, Mkurugenzi Mtendaji wa *DAWASA,* na dada yangu Everlasting Lyaro ambaye ni Afisa Mahusiano wa *DAWASA*. Kwa kweli, umeweza kutuunganisha Wabunge wote wa Mkoa wa Dar es Salaam, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi zangu nyingi sana ni kwa Mheshimiwa Rais, nilisema juzi wakati nachangia kwa Waziri Mkuu, kwa sababu ya mambo makubwa ambayo ameyafanya, lakini kwa sababu ya muda nitasema tu kwa haraka kwa kutaja. Ndani ya muda huu wa miaka yake mitatu tayari tumeona ma-*tank* karibu mawili na jingine jipya linajengwa Tegeta A, lenye ujazo wa lita 6,000,000 ambalo linasaidia Goba yote na maeneo machache ya Mbezi, Mshikamano na Mbezi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, lipo *tank* la Kitopeni maeneo ya Mbezi, Makabe na sehemu ndogo ya Msumi A. Sasahivi linajengwa *tank* kubwa la ujazo wa lita 9,000,000 kule Bangulo, Ilala, ambalo litasaidia Kusini yote ya Dar es Salaam kwa hiyo, mimi napongeza sana juhudi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, niseme kidogo juu ya eneo la bajeti. Eneo hili limesemwa na wachangiaji wengi na mimi kwa fani yangu siwezi kupita bila kueleza jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni masikitiko sana, sijui kama miradi itakuja kutimia huko mbele, miradi ambayo imeainishwa humu ya zaidi ya trilioni 1.8 hadi mbili dhidi ya bajeti ya shilingi milioni 627 ambayo imepitishwa kwa Mwaka 2024/2025 tofauti na bajeti iliyopita ya Mwaka 2023/2024 ya shilingi bilioni 756.2. Tofauti yake ni shilingi bilioni 128.4 ambayo ni chini kwa asilimia 17, hii siyo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziada sitaki kusema mapungufu hayo kwenye fedha za *OC (Other Charges),* nizungumzie za maendeleo. Kwa Mwaka 2023/2024 zilitengwa shilingi bilioni 695.83, lakini sasa hivi kwa Mwaka 2024/2025 zimetengwa shilingi bilioni 558.1 tofauti ya shilingi bilioni 137.7, amesema Mwenyekiti wakati anaizungumzia Taarifa ya Kamati. Ipo chini kwa asilimia 18, hii ni hatari sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati kwa kukubaliana nayo imetoa mapendekezo na lugha yake imekuwa ngumu kidogo. Waheshimiwa Wabunge tunaweza tukajikuta tunashindwa kwenda kukubalina na hii bajeti katika kumsaidia Waziri wa Maji, ndugu yangu Mheshimiwa Aweso, lakini mimi nataka niseme au

kuchangia na kuchochea juu ya taarifa ya Kamati. Kupungua huku kwa shilingi bilioni 137 tunashangaa ni kwa nini dhidi ya mpango uliopo ambao ni mzuri kufikia ile asilimia 85 vijijini na asilimia 95 mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii haiendi bure, tunajua mpango huo pia, umeathiriwa sasa hivi na *El-Nino* na mvua nyingi. Tunashangaa, hapa palikuwa na maboresho makubwa ya miundombinu dhidi ya kupungua kwa fedha. Je, hiyo miundombinu itarudije? Siyo hivyo tu, ni vizuri tujue kuna faida au ushauri tupate wapi hizi fedha zilizoondoka shilingi bilioni 137?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyosema Kamati, ni vizuri, moja tunaweza tukaenda kwenye Hati Fungani, wala siyo jambo baya. Tunaweza tukajikuta Watanzania wengi wana fedha wakawekeza na kutapata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo limeshauriwa na kamati ni shilingi 50 ya Mfuko wa Maji ikaongezwa au ikabaki palepale, lakini kupunguza gharama nyingine kutoka kwenye zile ambazo tunazitoza sasa hivi, lakini ushauri wa ziada kwenye eneo hilo ni lazima ikumbukwe tuna madeni ya zaidi ya shilingi bilioni 300 ambayo yana-*exist* hadi sasa hivi na ni lazima yalipwe. Kwa hiyo, kwa kila hali tunatamani Waziri wa Fedha kesho uje na mawazo ya kutafuta fedha nyingine, ili tuzirudishe pale zile shilingi bilioni 137 zilizoondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kulizungumza hilo niseme kidogo katika uchimbaji wa visima. Nimefurahi, tungeweza kujiuliza ni kwa nini visima? Swali gumu lingekuwa tunaondoka kwenye majisafi na salama sasa tunarudi kwenye maji ya chumvi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni visima kwa sababu, kama nchi kuna wakati tunaingia kwenye vipindi vigumu vya ukame. Vile visima vinaweza vikatusaidia zile nyakati ambazo hatuna majisafi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwangu nimefurahia sana. Sasa hivi navitaka hivyo visima haraka hata kesho asubuhi vikachimbwe kule *Msumi Centre,* Msumi Darajani, Mpiji maeneo

ya kwa Mvungi, maeneo ya CCM ya zamani na maeneo ya Torino. Vilevile maeneo ya Msingwa Mpakani Kata ya Saranga, maeneo ya Msigani pale Manzese na kwa Mama Nipe ni muhimu sana. Sisi tunavitaka sasahivi visima hivi pamoja na hiyo miradi mizuri ambayo inakuja baada ya mwaka mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja la kumalizia ombi letu kwa sasa ambalo tuliliomba sana ni mabomba, *distribution* ya mabomba. Miradi hii tayari ina vifaa vya maji nakuomba sana Mheshimiwa Waziri ukija kujumuisha hapo naomba useme, nimeona kwenye bajeti yako fedha za ndani shilingi milioni 214 na za nje shilingi bilioni 6 kwenye eneo la kuendeleza miradi ya Dar es Salaam, utoe *commitment* hapa ili mabomba yapatikane ya aina zote wananchi wapate maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni Mradi wa Msumi ulieleza hapa swali langu la msingi juzi lilijibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri bilioni 13.9 zipo, nimeingia kwenye bajeti nakuta bilioni moja kuunganisha chanzo cha Ruvu Juu na Ruvu Chini ukija uniambie 13.9 zinapatikana wapi kwenye bajeti yako?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwisho ushauri nikuombe ukija hapa uniambie huu mradi unaondelea wa uuzwaji maji kwenye magari ambao nimeeleza humu ndani ni changamoto na ndiyo maana labda wananchi wanafikiri mabomba hatuletewi kukamilisha miradi aliyowekeza bilioni nyingi Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wetu wa Awamu ya Sita...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naunga mkono hoja ya taarifa hii au Hotuba wa Wizara ya Maji, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jacqueline Kainja, atafuatia Mheshimiwa Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele ajiandae.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi na mimi niweze kuchangia Wizara hii ya Maji pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa nafasi ambayo nimeweza kusimama hapa na kuweza kuchangia Hotuba ya Wizara ya Maji. Vilevile nichukue nafasi hii kuwapongeza sana, Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii ya Maji pamoja na Mheshimiwa Naibu wake kwa kazi kubwa na nzuri wanazozifanya, mmekuwa ni Mawaziri ambao mpo *busy site* na majibu na matokeo yanaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile niweze kuwapongeza watendaji wote wa Wizara kuanzia Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu. Vilevile niwapongeze sana watendaji wa *RUWASA* ambao ni Mamlaka ya Maji Safi vijijini pamoja na usafi wa mazingira, niwapongeze sana kwa kazi nzuri mnazofanya mkiongoza na Mkurugenzi wa *RUWASA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kupongeza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anazozifanya kuhakikisha anamtua mwanamama ndoo kichwani, kuhakikisha maji safi yanapatikana katika nchi yetu. Pamoja na kampeni hiyo ya kumtua mwanamama ndoo kichwani kwa Mkoa wetu wa Tabora, *TUWASA* wameamua kutuwekea maji ya Mradi wa Ziwa Victoria kwa wilaya zote saba na hivi sasa mkandarasi yupo *site* anapeleka maji Urambo, Kaliua na Sikonge na tumefika 36%. Ifikapo 2026 mradi huu unatakiwa ukamilike hivyo Wananchi wa Mkoa wetu wa Tabora waweze kuneemeka na maji safi ya Mradi wa Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mazuri hayo yanayoendelea kufanyika nimpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo ameweza kutoa magari ya kuchimbia visima vya maji kwa kila mkoa na Mkoa wa Tabora ikiwa ni mojawapo ambapo tumepata gari hilo. Vilevile kila jimbo visima vitano kwa ajili ya upatikanaji wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jambo hilo ambalo Mheshimiwa Rais ameona na ametuwezesha Wananchi wote wa Tanzania hususani pia Mkoa wangu wa Tabora, lakini vilevile nipongeze *RUWASA* Mkoa wa Tabora kwa kazi nzuri wanazofanya, Meneja wa *RUWASA* na timu nzima ya *RUWASA* ya Mkoa wangu

wa Tabora. Wao waliona waje na miradi ya mabwawa kwa ajili ya upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi wa Mkoa wa Tabora. Pamoja na miradi hiyo ambayo imeshaenda tuna changamoto kubwa sana ya miradi hii kutokukamilika kwa ukosefu wa pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Wilaya ya Urambo tuna Mradi wa Bwawa la Kalemela ambapo pesa zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya bwawa lile kwenye bajeti inayoishia 2023/2024 hakuna pesa iliyoenda mpaka sasa hiv**i.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile watendaji hawa wa *RUWASA* Mkoa wa Tabora waliona watumie pesa za *PforR* kuanza ujenzi wa mradi ule wa Bwawa la Kalemela. Kwa hiyo niiombe Serikali iweze kuona namna gani watendaji wetu wanawaza nje ya boksi kuhakikisha maji yanapatikana, kwa sababu Mkoa wa Tabora ni moja ya mikoa ambayo ina changamoto sana ya upatikanaji wa maji chini ya ardhi hasa kwa kuchimba visima, lakini wao wameenda mbali wakawaza zaidi kwa kuja na miradi ya mabwawa lakini bado inashindwa kutekelezeka. Kwa hiyo tatizo la maji kwa Mkoa wa Tabora bado linaendelea kuwa ni tatizo sugu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuna Mradi wa Bwawa la Ichemba ambapo mradi huu upo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2015/2020 na 2020/2025, lakini mpaka sasa hivi tunavyoongea kinachotekelezeka ni mkataba kusainiwa. Sasa tumebakiza mwaka mmoja au miezi nane kukamilisha awamu hii ya sita lakini bado Bwawa hili la Chemba halijakamilika. Niombe sana Serikali, pia niombe sana *RUWASA,* kwa magari haya ambayo Mheshimiwa Rais ametoa ambayo yanaenda kuchimba visima vitano kila jimbo hebu tuweze kuangalia majimbo ambayo hayana Miradi ya Maji ya Ziwa Victoria hasa kwa Mkoa wangu wa Tabora, mfano Jimbo la Ulyankulu, Jimbo la Urambo, Jimbo la Kaliua na Jimbo la Sikonge yaweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niwaombe pia watoe maelekezo mkoani, gari linapoenda jimbo moja lihakikishe linachimba visima vyote vitano ndipo lihamie wilaya nyingine. Kwa kufanya hivyo itakuwa imerahisishia majimbo ambayo

hayana mradi wa maji kuweza kupata maji na wakati wengine wanaendelea kupata maji na kuneemeka kwa maji Mradi wa Ziwa Victoria. *( Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umeisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema naomba niunge mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, atafuatia Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele na Mheshimiwa Neema William Mgaya ajiandae.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nami kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji jioni hii. Kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja, lakini pili ningependa niseme machache sana katika Wizara hii. Waswahili husema; "Chenye thamani hutunzwa na kulindwa." Nilichokuwa nataka kujua ni kipi chenye thamani zaidi kati ya fedha za kigeni, chakula na maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa kama Taifa tumekuwa na taratibu za kuhifadhi hela za kigeni ili kutakapotokea mtikisiko wa upungufu wa fedha za kigeni hizo, sisi kama Taifa tuwe nazo, lakini kwa upande wa chakula tukiwa kama Taifa tumekuwa na utaratibu wa kuhifadhi chakula ili baa la njaa linapoikabili Taifa au Mataifa mengine duniani sisi tuwe na chakula akiba hata kama ni cha miezi miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa chakula au upande wa dona si kila mtu ana uwezo wa kutumia dona, inatumiwa na watu wachache. Inawezekana Taifa hili linatumia chakula hiki au mtu huyu amepigwa marufuku kutumia chakula fulani, lakini hakuna daktari hata mmoja atakayekupiga marufuku katika utumiaji wa maji. Kwa maana gani, hakuna mtu anayetumia mafuta kama mbadala wa maji. Katika hili ningependa niweke sawa kidogo, kwanza fursa hii kuishukuru

sana hii Wizara kupitia kwa Mheshimiwa Waziri na Kamati yetu ya Bunge kwa kuona katika ripoti yao wameweka msisitizo juu ya umuhimu wa kuharakisha mchakato wa ujenzi wa Gridi ya Taifa ya Maji hongereni sana. Nini tufanye ili kuonesha sisi kama Taifa tunayathamini na kutoa mchango katika suala zima la maji? Nitakuwa na michango mitatu ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni lazima tufanye rejea ya Sera ya Maji, sera ambayo itaenda kuweza msisitizo juu ya elimu kwa umma kuhusiana na umuhimu wa kuhifadhi vyanzo vya maji. Inawezekana Serikali ipo katika mchakato wa kufanya mapitio au maboresho ya Sera ya Maji lakini ipo haja ya kuharakisha mchakato huo ili Sera hiyo izidi kuweka umuhimu kwa umma juu ya umuhimu wa maji. Umma ufahamu maji yana umuhimu gani. Lazima twende mbali zaidi kutokana na hali ya mabadiliko ya tabianchi tuliyokuwa nayo sasa hivi lazima sera iangalie na iboreshe namna gani miundombinu ya maji itakavyojengwa kwa kukabiliana na athari nzima za mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nalo ni la kisera; Sera yenyewe sasa itamke wazi kwamba maji ni uhai na maji ni usalama ya Taifa, kwa sababu Maisha yetu sote viumbe yanategemea maji. Viwanda vikubwa na vidogo uendeshaji wake unategemea maji, kilimo pamoja na mifugo vyote vinategemea maji. Hata hiyo nishati ya umeme kwa vyanzo vyake asilimia kubwa vinategemea maji. Sasa upungufu wa maji ukitokea basi tutaanza kushuhudia mtikisiko wa usalama katika nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano mdogo tu palipotokea upungufu wa vyanzo vya maji vinavyopeleka Dar es Salaam basi mtikisiko wa usalama ulianza kuonekana kwa baadhi ya maeneo. Maji yakipungua au ukame wa maji ukatokea basi mtikisiko katika sekta ya mifugo na viwanda au na kilimo lazima utatokea tu. Ndiyo maana nasema, nasisitiza maji ni usalama wa Taifa na hakuna mbadala wa maji. Maji si sehemu ya siasa ni sehemu ya Maisha ya Mtanzania na mwananchi yeyote wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ambalo litakuwa ni la mwisho katika mchango wangu ni lazima sasa Serikali iwekeze katika sekta nzima ya maji. Ni lazima Serikali iwekeze hasa kibajeti katika usimamizi wa rasilimali za maji, kuhusu njia sahihi na za kisasa pamoja na kuweka ushirikishwaji wa wananchi katika kulinda na kuhifadhi vyanzo vya maji hii ndiyo dawa tosha. Tusitarajie licha ya kwamba Serikali itawekeza huko lakini uwekezaji huo lazima uende mbali zaidi katika kujenga miundombinu ya kuhifadhi na kusambaza maji kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusitarajie kwamba...

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Anatropia.

**TAARIFA**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe Taarifa mzungumzaji pamoja na juhudi unazotaka Serikali ielimishe wananchi juu ya kuhifadhi maji, kuna halmashauri leo zimeweka Sheria kwamba yale maji yanayoifadhiwa pamoja na visima wanavyochimba kwa ajili ya kupata maji wawe wanalipia tozo hivyo visima.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Simai unapokea Taarifa?

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea, pamoja na yote hayo tusitarajie wala tusiruhusu sekta binafsi kwamba hiyo ndiyo iende ika-*control* uwekezaji katika masuala ya maji. Serikali haina jinsi lazima iwekeze kwa kiasi kikubwa katika changamoto hii. Tutakapoiruhusu sekta binafsi iingie huko maji yataenda kuwa bidhaa baada ya kuwa huduma na sisi tunachotaka maji yasimame kama ni huduma badala ya kuwa bidhaa hiyo itatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini chakusikitisha kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Bashiru kasema hapa kwamba bajeti sasa hivi

tumeanza kulega lega. Bajeti ya mwaka jana imekuwa ni kubwa ukilinganisha na bajeti ya mwaka huu, wakati ambapo ilitakiwa bajeti ya mwaka huu iwe ni kubwa zaidi maradufu kuliko bajeti ya mwaka jana. Kwa changamoto hizi ninazozisema na umuhimu ninaouona hakuna sababu ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo hususani katika suala la umwagiliaji iwe...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** ...ni kubwa halafu bajeti ya Wizara ya Maji iwe ndogo haiwezekani wakati Wizara ya Maji ndiyo inayo-*control* masuala na vyanzo vyote vya maji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, nakushukuru sana.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele, atafuatia Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala ajiandae.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uzima. Napenda kutoa pole kwa ndugu zangu na jamii yangu ya Mkoa wa Lindi kwa athari za Kimbuga kile cha Hidaya lakini Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan anafanya kazi kubwa vijana wake wanafanya kazi usiku na mchana na mawasiliano yanaenda kurejea muda si mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa dhamira yake ya dhati kwa ajili ya kumtua mama ndoo kichwani, tunashukuru sana. Pia, nampongeza Mheshimiwa Waziri Aweso, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Watendaji wote wa Wizara hii ya Maji na Mameneja wa *RUWASA*, Meneja wa *RUWASA* wa Mkoa wa Lindi na mameneja wote wa Wilaya zote za Mkoa wa Lindi, wanafanya

kazi nzuri sana kwa ajili ya kuwaletea Wananchi wa Mkoa wa Lindi maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wana-Lindi tunashukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ametupatia miradi ya maji mikubwa. Mradi wa kutoa maji kutoa Nyangao kupeleka Ruangwa – Nachingwea bilioni 119.5, si jambo rahisi ni jambo kubwa sana tunashukuru sana, vijiji 54 vinaenda kupata maji. Pia kuna mradi wa maji kutoka Ngapa kwenda Mchinga na sasa hivi tayari pale Mchinga wanapata maji ya bomba, maji safi na salama haijawahi kutokea na mradi ule unaenda mpaka Kilola Mbwani mpaka Kijiweni kwa kweli tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Aweso tunakushukuru sana kwa kutekeleza adhima ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Pia kuna maji ya kutoka Mto Mavuji bilioni 44 maji yanaenda kupelekwa Nangurukuru, Kivinje, Kilwa Masoko haijapata kutokea, huyo ndiye Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tumepokea milioni 400 pale Liwale kwa ajili ya kutoa maji kutoka chanzo cha Turuki kuja Liwale Mjini pamoja na vijiji vyake nalo hilo halijawahi kutokea ndiyo tunayaona sasa hivi kwa Serikali ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikienda kule Nachingwea naona kuna Mradi kule Naipanga wa bilioni 1.6 na ule pia nawahakikisha ndugu zangu wa Nachingwea kule Naipanga wanaenda kupata maji muda si mrefu, hata Juni, hii haitafika. Sisi Wana-Lindi tunafurahi sana tunashukuru sana kupata maji safi na salama. Naamini kabisa kwa bajeti hii mimi naiunga mkono kabisa ipite kwa asilimia zote ili kuhakikisha Nachingwea na Mkoa wa Lindi kwa ujumla tunapata. Mheshimiwa Aweso anakwenda kumalizia ile miradi ambayo ilikuwa bado haijaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa kupeleka maji Nachingwea, Meneja wa *RUWASA* ameomba shilingi milioni 670 ili Wananchi wa Ngunichile wapate maji safi ambayo wao tangu

misingi ya ulimwengu iumbwe wao wanakunywa maji ya kuokota okota. Tunaenda kushuhudia Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan anaenda kulimaliza hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia maji kutoka kwenye ardhi ya Mkoa wa Lindi hayana ubora ndiyo maana meneja wetu ameomba miradi ya mkakati ya kutoa maji kutoka Rufiji ili kuleta maji Kilwa, Lindi na Ruangwa na kutoa maji kutoka Mto Ruvuma kuleta Nachingwea, Ruangwa pamoja na Liwale. Tunaomba mikakati ya mradi huo Mheshimiwa Aweso itekelezeke kwa kipindi hiki tunachopoitsha bajeti hii, vinginevyo Wana-Lindi wale wataendelea kunywa maji yenye chumvi. Zaidi ya hayo wananchi wale wa Mkoa wa Lindi wanashukuru kwa miradi kama hii ambayo haijawahi kutokea hata kwa wakati mmoja kupata maji safi na salama ambapo mradi mwingine utaenda kulisha kule Kitomanga na Kilangala ambapo sasa hivi tanki kubwa linajengwa pale maeneo ya Mkwajuni. Hizi zote ni juhudi za Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan za kumtua mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakushukuru sana Mheshimiwa Aweso na timu yako yote, tunaomba mtuangalie bajeti hii tunaipitisha kwa asilimia zote ili miradi ile ikaendelee kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na Wana-Lindi wanaahidi kura zote kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, nashukuru ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Neema William Mgaya, atafuatia Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea ajiandae.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Maji. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na kuweza kusimama ndani ya Bunge hili Tukufu na kuweza kuchangia katika bajeti hii ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Jumaa Aweso pamoja na Naibu Waziri lakini

na Watendaji wote wa Wizarani katika Wizara ya Maji. Ninakiri kwamba Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake nzima wanafanya kazi nzuri katika kuhakikisha kwamba Rais Dkt. Samia anatimiza ile azma yake ya kuweza kumtua mwanamke ndoo kichwani. Pongezi sana kwa Mheshimiwa Waziri na timu yako.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nawapongeza? Naipongeza Serikali kwa sababu kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukiisikiliza ameonesha kabisa hali ya upatikanaji wa huduma ya maji ilivyoongezeka kutoka 77% Disemba, 2022 hadi kufika wastani wa 79.6% Disemba, 2023 kwa vijijini. Vilevile, tumeweza kuona ongezeko la hali ya upatikanaji wa maji mijini kutoka wastani wa asilimia 88 Disemba, 2022 hadi kufikia wastani wa 90% Disemba, 2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazidi kuamini kwamba Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ana nia ya dhati ya kumtua mwanamke ndoo kichwani kwa sababu hata kwenye hotuba ya Waziri pia imejidhihirisha, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia ametoa zawadi ya visima 900 ambavyo vitakwenda kwenye Majimbo 180 na kila Jimbo litakwenda kupata visima vitano. Waziri hapa wakati anawasilisha hotuba yake ametueleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada kubwa anazozifanya za kuhakikisha kwamba anataka kumaliza kero ya maji nchini kwetu Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sambamba na hilo niwashauri Wizara katika suala zima la *geothermically investigation.* Kipindi cha nyuma tuliona visima vilikuwa vinachimbwa lakini kipindi cha kiangazi havitoi maji. Kwa hiyo, Mheshimiwa Aweso na timu yako nakuomba sana muwe waangalifu sana katika suala zima la *geothermically investigation* ili vile visima ambavyo mnaenda kuchimba kwenye yale maeneo mliyokusudia kuchimba, mchimbe sehemu sahihi ili maji yaweze kupatikana ili azma ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kumtua mwanamke ndoo kichwani iweze kukamilika kwa ufanisi na ilete tija kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kusikiliza kilio cha wananchi katika changamoto za *bill* za maji. Wananchi wengi walikuwa wanalalamika kwamba wanabambikiwa *bill,* lakini kwenye hotuba ya Waziri ameeleza kabisa kwamba Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameelekeza Wizara kuongeza kasi ya ufungaji wa hizo dira za malipo ya kabla ya matumizi ya maji hizo *pre-paid meter* za maji ili wananchi waweze kutatua kero hizo za kubambikiziwa maji. Vilevile kwa kuweka *pre-paid meter* itatusaidia mashirika na zile taasisi za Serikali ambazo zilikuwa na madeni sugu, madeni makubwa, tunaamini kwamba hii itakwenda kuwa suluhisho la changamoto hizi, changamoto za wananchi kubambikiziwa *bill* za maji lakini pamoja na wale ambao walikuwa hawalipi maji kwa maksudi itakwenda kuwa mwarobaini wa changamoto hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila kwenye zuri hapakosi changamoto, napenda kuishauri Wizara muwe makini sana katika kuangalia ubora wa hizo *meter* ambazo zitakwenda kufungwa, kwa sababu kinyume cha hapo mtakuja kuiingizia Serikali hasara, na kama itakuwa na urahisi watu ku-*temper* nazo na kufanya ujanja ujanja mtu akatumia maji hata bila kulipa kabla ya matumizi ya maji. Tunajua Tanzania hii ina mambo mengi na wajanja ni wengi kwa hiyo muwe makini katika kuhakikisha kwamba mnapata *meter* au mna *supply meter* ambazo zina ubora na ambazo hazitaweza kuchezewa kwa urahisi na watu ambao hawana nia njema na nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nizungumzie changamoto za miradi ya maji Mkoa wa Njombe. Mkoa wa Njombe kuna mradi wa maji wa Mfumbi Wilaya ya Makete. Mradi huu wa Maji Mfumbi Wilaya ya Makete takribani sasa ni miaka miwili mradi huu haujaanza kufanya kazi. Wananchi wa Makete wanataka kujua nini tatizo? Na mkiangalia thamani ya mradi huu hauzidi hata milioni 700. Tunakuomba wananchi wa Makete uwamalizie kadhia hii ili nao waweze kufurahia matunda ya Chama Cha Mapinduzi kwa kupata maji bora, safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi wa maji Igando, Kijombe wenye thamani ya bilioni 10.8. Mradi huu wa maji wa Igando Kijombe uko ndani ya Jimbo la Wanging'ombe, mradi huu Mkandarasi amekabidhiwa kazi tangu Septemba, 2023 lakini mpaka ninavyozungumza hivi sasa bado Mkandarasi hajaanza kazi. Mheshimiwa Waziri tunaomba mzingatie pia Mkandarasi aanze kazi na wananchi wa Wilaya ya Wanging'ombe waweze kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi mwingine tena wa kujenga mtambo wa kusafisha maji chanzo cha Mbugwa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali iangalie namna ya mradi huu kuweza kuanza kufanya kazi kwa sababu Mkandarasi amepewa kazi tangu Oktoba, 2023.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ahsante.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti Yusuf Majala, atafuatia Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea, Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba ajiandae.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa muda na mimi niweze kuchangia hotuba ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa pongezi kwako Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara ya Maji. Naiona dhamira yenu kama Wizara na Watendaji wa Wizara hii kuhakikisha miradi yote mliyonayo na watanzania wote waweze kupata maji safi na salama ya kunywa.

Mheshimiwa Spika, tunakubaliana sote kwamba changamoto uliyonayo Mheshimiwa Aweso pamoja na dhamira hiyo uliyonayo hela hazipo, kwa kudhihirisha hilo ni kwamba safari hii badala ya Wizara kupanda ili tuende tukapate maji kwa watanzania na miradi mingi iweze kutekelezeka Wizara imepunguziwa bajeti na sasa hapa napata kizungumkuti, hii miradi iliyopo ambayo haikukamilika na miradi inayokuja tunakwenda kuikamilisha kwa namna gani kama bajeti inashuka? Serikali watanisaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, naomba nizungumzie suala la uhaba wa maji kwenye Mkoa wa Dodoma. Tumekuwa tukizungumza Ofisini, Bungeni, Katibu Mkuu na Watendaji wako. Mheshimiwa Waziri, tunaomba Dodoma muiangalie kwa jicho la kipekee, pamoja na ukame wake lakini bado tuna maji chini ya ardhi. Leo kati ya Mikoa ambayo ipo chini kwenye suala zima la maji ni Mkoa wa Dodoma na kwa Mkoa wa Dodoma, watu ambao wako chini kwenye suala la upatikanaji wa maji ambao na wewe ulifika ni Wilaya ya Chemba. Mheshimiwa Waziri umeenda kwenye vijiji viwili wamama wakakulilia wakakwambia Mheshimiwa Waziri tusaidieni maji, tunaombeni maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi na wanawake ambao ni mama zetu, dada zetu, shangazi zetu na bibi zetu wa Wilaya ya Chemba tunafukua maji kwenye mito ya mchanga, leo mvua ikiisha mwezi wa tisa wa kumi yale maji yamekauka pale ardhini kwenye mito hawa watu hawapati maji. Mmekuwa mkitupa miradi ambayo haitekelezeki Mheshimiwa Waziri. Kuna visima kumi mlitupa 2022 imepita kavu, 2023 imepita kavu. Tunashukuru tumeona sasa hivi umetuingiza *P4R - pay for results*. Tunashukuru mmetupa, lakini umetupa miradi saba tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba utuangalie Wilaya ya Chemba hali ya ukame ni ngumu. Mheshimiwa Waziri, nikuombe kutoka hiyo miradi saba uliyotupa tunakushukuru na wewe una msemo kwamba asiyeshukuru kwa kidogo hata kikubwa hawezi kushukuru. Sisi hicho kidogo tunakushukuru, ahsante lakini tunaomba utuongezee miradi hali ni ngumu. Tegemeo letu ilikuwa ni mradi wa Farkwa. Mradi wa Farkwa haueleweki Mheshimiwa

Waziri hata wewe mwenyewe kwenye hotuba yako umesema maneno mengi, lakini hitimisho lako Mkandarasi atakapopatikana, lini? Lini tunampata Mheshimiwa Waziri? Kwa hiyo, nikuombe miradi ya *P4R* ambayo tunaamini inaweza kutuokoa tusaidie tuongezee miradi angalau tufike hata 20, tunakuomba angalau ifike 20 na ukija hapa uwaambie wananchi wa Chemba angalau tutawapa hiyo miradi kutoka hiyo saba ifike 20. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunashukuru mradi wa miji 28 sisi pia ni wanufaika na ulisema. Pia kumekuwa na changamoto kidogo, walikuwa wanasuasua tunashukuru sasa hivi mkandarasi yuko *site* na kazi anafanya. Nina ushauri kwenye huu mradi, kulikuwa na uchimbaji wa visima kwenye maeno mbalimbali ili tuweze kuchimba kisima kujenga tenki na kusambaza kwenye eneo husika, lakini wameenda pale Chambalo wamechimba kisima kimedumbukia, lakini wameenda pale Paranga mpaka sasa wameshachimba visima viwili ambavyo vina maji mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninachotamani kushauri kwenye mradi huu, niombe yule mkandarasi waendelee kuchimba maji pale kama yanaweza kupatikana, tupate hata visima vinne tujenge tenki kubwa pale Chemba Mjini ili sasa maji yale yasambazwe kwenda Chambalo, yasambazwe na kwenda Gwandi badala ya kwenda kuchimba hivyo visima kwenye kila Kijiji. Kwa hiyo, ninaomba muone ni namna gani mkandarasi mnampa maelekezo ili aweze kufanya hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilikuwa natamani kulisema ni suala zima la mitambo ambayo tuko nayo. Tunaomba ile mitambo mitano iliyokuja ya uchimbaji wa mabwawa lakini na mitambo ya kuchimba visima, RUWASA Mkoa wa Dodoma, tunaomba hilo gari lianze kwa Wilaya ya Chemba hali ni mbaya, maisha ya wanawake wa Wilaya ya Chemba, wakina mama ikifika mwezi wa tisa wanafukuzana kwenye milima kwenda kutafuta maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine Mheshimiwa Waziri ni suala zima la wakandarasi wetu. Wakandarasi wetu wa ndani

wanafanya kazi kubwa sana na ndiyo wasaidizi na waokozi ndani ya Taifa letu, lakini kumekuwa na changamoto ya malipo yao. Kwa nini hao watu wanafanya kazi hamtaki kuwalipa? Serikali kuna shida gani? Awali mlisema fedha zinatumiwa vibaya kwa hiyo mkandarasi afanye a-*raise certificate* ipelekwe, wamepeleka *certificate,* watu wana miezi sita, watu wana miaka miwili, wengine wanauziwa nyumba, watu wanakufa, watu wanafanyaje, tunaomba hela za wakandarasi zilipwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kibaya zaidi hawa watu hawadai hata ile fedha ya kucheleweshewa miradi yao, wakidai mnawaambia sio wazalendo na wakiomba miradi mnawanyima eti kwa sababu wamedai *fee charge* ya ucheleweshaji wa kulipwa fedha, lakini tukiangalia wakandarasi wa nje mnawalipa, sasa kwa nini watu hawa tunawafanyia namna hiyo? Hawa ni wa kwetu hawa watu fedha yao, na ukiangalia Mheshimiwa Waziri wakandarasi wa nje wanaokuja kufanya kazi hapa nchini kwetu tunawapenda na tunatamani watufanyie kazi, wakija kwenye mikataba yetu tunasaini mikataba mafundi wao kila kitu ni cha kwao mpaka mabomba na kila kitu wanaleta wao, wanachochukua kwetu ni vibarua tu ambao wanawalipa shilingi elfu tatu kwa siku, lakini huyu mkandarasi wa hapa kila kitu atanunua hapa ndani, tutakusanya kodi kwa wakandarasi wetu lakini kwa nini tunawafanyia haya yote? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba uwasaidie wakandarasi wetu ambao wame-*raise certificate* ziko Wizarani kwenu ama ziko Wizara ya Fedha, tunaomba muwasaidie wapate hizo fedha ili waweze kukamilisha miradi wananchi wetu wapate maji safi na salama, pili kodi iweze kulipwa kwa wakati nchi yetu iweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea atafuatia Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla ajiandae.

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuku kwa nafasi hii na mimi kuchangia kwenye Wizara hii ya

Maji. Pia nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya na uzima na kwamba tunaweza kuwatumikia wananchi hasa wananchi wa Jimbo la Korogwe Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa adhma yake ya kumtua mama ndoo kichwani. Hii siyo kazi ndogo, tumeona ripoti sasa hivi tunafikia upatikanaji wa maji wa asilimia 79.6 kwa watu wa vijijini na asilimia zaidi ya 90 kwa watu wa mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kazi kubwa ambayo ameifanya, ninaamini kwa miradi mingi ambayo bado inaendelea iko kwenye hatua mbalimbali, baada ya kukamilika ni imani yangu kabisa kabla ya uchaguzi wa mwakani, mama atakuwa amefikisha ile asilimia ambayo imeahidiwa kwenye Ilani ya chama chetu, 85% vijijini na 95% mjini, hiyo ni imani yangu, miradi mingi mikubwa imetekelezwa tunampongeza sana Rais wetu kwa kazi kubwa ambayo ameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi siwezi kuelezea miradi yote. Kila Mbunge kwenye Mikoa yao na Wilaya zao watakuwa wanaelezea miradi huko angalau mimi nitaje michache kwenye Mkoa wangu lakini hasa kwenye Jimbo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tuna miradi yetu mikubwa miwili, hii ilikuwa kichefuchefu muda mrefu, lakini tumshukuru Rais wetu wa Awamu ya Sita, kipindi chake ameweza kuikwamua miradi hii miwili mikubwa. Nikizungumzia mradi mkubwa ule wa Mwanga, Same na Korogwe lakini mradi wa miji 28. Miradi hii ilikuwa kero kubwa Watanzania walikuwa wakipigia kelele lakini tunamshukuru Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweza kufanikisha kuleta fedha na miradi ile sasa hivi iko kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji. Kwa hiyo, ninampongeza Rais wangu Mama Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia pia nitumie fursa hii niwapongeze ndugu zangu viongozi wa Wizara hii. Moja, Kaka yangu Jumaa Hamid Aweso kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. Ndugu huyu ni

msikivu, mchapakazi lakini ni mcha Mungu na anashirikiana kwa asilimia kubwa sana na Wabunge ndiyo maana anaendelea kufanikiwa siku hadi siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumpongeza aliyekuwa Naibu Waziri dada yetu *Engineer* MaryPrisca Mahundi kwa kazi kubwa ambayo ameifanya, nimshukuru na kumpongeza *Engineer* Kundo amepokea kijiti na anakimbia nacho kwa *speed* kubwa sana. Kwa hiyo, nimpongeze kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya. Kipekee kabisa nimpongeze Katibu Mkuu Eng. Mwajuma Waziri, wakati akiwa Naibu Katibu Mkuu kafanya kazi kubwa, sasa hivi ni Katibu Mkuu anaendelea kupambana kuhakikisha anaendelea kumsaidia Mama Samia Suluhu Hassan ili kumtua Mama ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye Jimbo langu, wakati nachukua nafasi hii ya Ubunge upatikanaji wa maji kwenye Jimbo langu ulikuwa ni chini ya 43%, ilikuwa kila nikiongea Bungeni ilikuwa ni kulia kulalamika kumuomba Waziri Aweso aniokoe kwenye Jimbo la Korogwe Mjini, lakini namshukuru Mungu nimshukuru Rais pamoja na Waziri wangu Jumaa Hamid Aweso, Sasa hivi upatikanaji wa maji kwenye Jimbo langu la Korogwe Mjini ni zaidi ya 84%. Hebu chukulia kuanzia 43% sasa hivi ni 84% kwa hiyo ninakupongeza sana na ninakushukuru Kaka yangu kwa kunitendea mambo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nisiache kuwapongeza *MD* wetu wa Idara ya Maji kule Korogwe, Ndugu yangu Yohana Mgaza, Meneja wa *HTM* lakini na Wiliam Tupa Meneja wa *RUWASA* kwa namna wanavyoendelea kutupa ushirikiano kutusaidia kwenye kutatua changamoto ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kabisa kwa miradi ambayo inaendelea kwenye Jimbo langu la Korogwe Mjini baada ya mwaka huu upatikanaji wa maji utakuwa ni zaidi ya asilimia mia moja kwenye Jimbo la Korogwe Mjini kwa sababu tunao mradi wa miji 28 pia mradi wangu mkubwa unaitwa Mradi wa Ndemaa. Hii miradi ikikamilika nina uhakika kabisa upatikanaji wa maji kwenye Jimbo la Korogwe Mjini utakuwa ni zaidi ya

asilimia mia moja. Hivyo namshukuru sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maombi machache ninadhani muda wangu bado, ombi la kwanza, hatuna *treatment plant* kabisa kwenye Mji wetu wa Korogwe Mjini, wakati wa mvua maji yakichafuka kwenye vyanzo yanakuja nyumbani jinsi yalivyo. Tunashukuru umetutendea mambo makubwa sana. Upatikanaji wa maji umekuwa mkubwa sana, lakini tunaomba utusaidie tupate *treatment plant* ili maji yanayoingia majumbani yawe maji mazuri.

Mheshimiwa Waziri, kwenye Kata za pembezoni mwa Jimbo langu la Korogwe Mjini bado miundombinu, *network* za mabomba bado haijafika kwenye Kata za Mtonga, Kilole na baadhi ya Kata ambazo ziko pembezoni, miundombinu bado haijafika. Kwa hiyo tunaomba utusaidie kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo tenki letu dogo kwenye Kata ya Mgombezi kwenye Kijiji cha Mgambo, tenki hilo limejengwa miaka mitatu iliyopita lakini hadi sasa hivi hatujapatiwa *pump* ya kuweza kuchukua maji kuyapeleka kwenye tenki hilo. Naamini meneja wetu wa *HTM* analimudu hili ni kumpigia tu simu apelike ile *pump.* Juzi nilikuwa kwenye ziara katika Kijiji hicho, wakatuomba sana, nimeona niliongee hili, ninaamini watalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nitumie fursa hii kukushukuru sana na kuunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla, Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, ajiandae.

**MHE. SANTIEL E. KIRUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote ningependa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo amepambana kwa kipindi chote tangu alipokuwa Makamu mpaka amekuwa Rais kwa *agenda* hii ya kumtua mama ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameweza na amewekeza kwenye Sekta ya Maji kwa kiasi kikubwa sana. Mpaka sasa tunavyoongea takribani wakazi milioni nne Tanzania nzima wanapata maji safi na salama. Hili halikuwezekana katika kipindi cha nyuma lakini chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, maji yameweza kufika kwa haraka na amekuwa akitia jitihada za haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi wenyewe mnaelewa *agenda* ya kumtua mama ndoo kichwani ni kitu kikubwa sana na muhimu sana. Kwa sababu gani? Mwanamke anaweza akatumia masaa matatu hadi manne anakwenda kutafuta maji, shughuli za kiuchumi kwake zinakwama. Pia, hata wale watoto wetu wadogo wa kike waliokuwa wanakwenda kuchota maji walikuwa wanapitia ukatili wa kijinsia, wanabakwa na wengine kupelekea kupata mimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii *agenda* ya kumtua mwanamke ndoo kichwani ni *agenda* kubwa sana kwa Mheshimiwa Rais. Pia, anapokwenda kuitekeleza kwa namna moja au nyingine inakwenda hata kupunguza ukatili wa kijinsia kwenye Mkoa wetu wa Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine nipende kumpongeza Meneja wa *RUWASA* Mkoa wa Shinyanga, Dada Juliet. Mheshimiwa Waziri nakuomba unapokaa na unapofanya mambo yako huyu dada mtazame kwa jicho lingine. Huyu dada anaendana na kasi ya Mheshimiwa Rais. Kwenye bajeti iliyopita mlimuwekea hela takribani shilingi bilioni 28. Dada huyu aliweza kujenga visima, matenki na pesa zikaweza kubaki. Huyu ni mfano mmoja wa meneja ambaye anaendana na kasi ya Mheshimiwa Rais. Vilevile, kazi zake nyingi zimekuwa zikienda na kuisha kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nipende kuwapongeza Wizara, Mheshimiwa Jumaa Aweso na timu nzima kwa kuweza kupata tuzo duniani kwa mara ya pili mfululizo kwa kuweza kufikisha maji vijijini. Pia, hiyo imewapelekea hata *World Bank* kuwaongezea pesa za *PforR* kutoka dola milioni 330 mpaka milioni 650. Hii kwa namna moja ama nyingine Serikali hii imekuwa ikitekeleza Ilani ya

Chama Cha Mapinduzi kwa kishindo na imekuwa ikionekana kama mfano kwa nchi nyingine duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi 50 Nchi ya Tanzania ndiyo imeweza kupata tuzo kwa miaka miwili mfululizo na hii yote imekuwa ni chini ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nipende kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa namna anavyoendelea kufanya kazi kwa kuweza kutuletea maji ya Ziwa Victoria. Maji ya Ziwa Victoria yalikuwa ni *story* kila siku na wapinzani ndiyo walikuwa wanaitumia kama *agenda* kwamba, tuna maziwa lakini maji hayafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa Mkoa wangu wa Shinyanga, tumeweza kupata maji ya Ziwa Victoria. Ule Mradi mkubwa wa Tinde ambao unapelekea maji Tabora – Shelui na mwisho yale maji yatakuja kufika Dodoma. Ule Mradi ni baadhi ya miradi mikubwa sana kwa *East Africa* ambao umetekelezwa kwa takribani shilingi bilioni 640. Sisi kwa Mkoa wa Shinyanga Kata ya Tinde ni wanufaika wa ule Mradi mkubwa wa Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ule Mradi kwa Tinde tu umeweza kukidhi vijiji 23. Licha ya hivyo, kwa mwaka wa fedha uliopita Mheshimiwa Aweso amejitahidi sana kututendea haki. Tumeweza kupata maji ya Ziwa Victoria kutoka Nduku – Busangi ambao umetekelezwa kwa shilingi bilioni tano. Vilevile tumeweza kupata katika Kijiji kingine cha Igaga – Lagana shilingi bilioni sita, Zongombela – Kahama tumepata shilingi bilioni 1.5, Tinde – Tabora – Shelui ambao huo ndio Mradi mkubwa wa shilingi bilioni 640. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ambayo mpaka sasa hivi tunaongelea na nina imani kwenye hii bajeti yako Mheshimiwa Aweso umetenga fedha ambayo bado inaendelea na inakuhitaji sana kwa sababu kwetu hii bado ni changamoto kubwa sana. Kuna Chona – Ubabwe ambayo umeiahidi kwenye bajeti hii utaikamilisha, Seseko, Masengwa na Kagongwa. Hizo ni sehemu ambazo ni kubwa na zina mkusanyiko mkubwa wa watu lakini

zina changamoto ya maji. Mheshimiwa Aweso, nakuomba sana hii ukaitekeleze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashukuru kwa ambavyo mmeweza kutupatia mabwawa ambayo yanapatikana Shinyanya na Ngofila- Kishapu. Mheshimiwa Aweso, nikupongeze kwa jinsi ambavyo unafanya kazi na timu yako nzima na yule Dada yangu Katibu Mkuu ambaye amechaguliwa binti mdogo. Hii yote inaonesha Mheshimiwa Rais ana imani na vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine cha mwisho, napenda tena kuwapongeza kwa kutuletea visima kwenye kila jimbo kwa Mkoa wa Shinyanga. Majimbo yetu sita yameweza kupata visima vitano vitano. Hii inaonesha Mheshimiwa Rais ana nia ya dhati ya kila Mbunge aweze kurudi. Ni wakati wetu sisi kujitoa na kwenda *site* ili kuhakikisha kuwa utekelezaji huu unawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu haya maneno ya pesa za UVIKO yalisemwa sana lakini sasa hivi unaona kwa jinsi gani zile fedha za UVIKO mpaka sasa zimeendelea kutumika na ndiyo zimeweza kuleta mitambo hii. Kwa hiyo, nipende kumpongeza Mheshimiwa Rais, Wizara nzima na kila mtu pamoja na timu nzima ya Wizara ya maji. Mheshimiwa Aweso unaonesha utulivu wa hali ya juu. Hiyo inaonesha wewe balozi mzuri wa afya ya akili. Ukianzia nyumbani umekuja na timu nzima ya familia yako. Wewe inaonesha kwamba umetulia kuanzia nyumbani, unapata utulivu hadi kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla, atafuatiwa na Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa na Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai ajiandae.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa fursa hii ya kuchangia kwenye Hotuba ya Waziri wa Maji mdogo wangu Mheshimiwa Aweso. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai na fursa ya kutukutanisha hapa siku ya leo tukiwa wazima wa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nitumie fursa hii kwa namna ya Kipekee kabisa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya kwa kila sekta hususan kwenye Sekta hii ya Maji. Alipokuwa Makamu wa Rais alidhamiria na akaweka wazi dhamira yake ya kumtua ndoo mama kichwani. Ikawa neema Rais akawa ndiyo yeye na ameisimamia azma yake ya kumtua ndoo ya maji mama kutoka kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wetu alipopata fursa ya kuongoza Taifa letu, upatikanaji wa maji kwa wastani kwa sisi wenye majimbo ya vijijini haukuzidi 45%. Kwa Jimbo langu mahususi upatikanaji wa maji ulikuwa ni wa wastani wa 43%. Hata hivyo leo nasimama hapa kuongea, Jimbo la Nzega Vijijini tunapata maji kwa kiwango cha 79%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nimepata fursa ya kuwa Mbunge kwa mara ya kwanza mwaka 2010, upatikanaji wa maji katika Jimbo lote la Nzega ukichanganya na Nzega mjini ya sasa ulikuwa ni wastani wa 23%. Nilifika kwenye Kijiji kimoja kinaitwa Kabale pake kwenye Kata ya Nata, wananchi wakati wa kampeni waliniletea chupa ya maji wanayotumia yenye rangi kama juice ya *watermelon* (*juice* ya tikiti maji). Leo hii watu wa Kabale wanakunywa maji safi na salama kutoka Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ninapozungumza hapa watu wa Kabale wanapata maji yanayotiririka kutoka bombani wala siyo maji ya kisima. Watu wa Kabale wapo kilometa takribani tatu kutoka kwenye Mradi mkubwa uchimbaji wa dhahabu uliokuwepo pale Nzega maarufu kama *The Golden Pride Project.* Hata hivyo, pamoja na kuwa kwenye rasilimali kubwa ya namna hiyo, hawakuwa hata na maji ya kutumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii dhahabu imeondoka yamebaki mashimo lakini ameingia Rais mwenye nia thabiti ya kuleta maendeleo na ustawi wa watu. Watu wa Kabale wanapata maji safi na salama yanayotiririka kutoka bombani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana mdogo wangu Mheshimiwa Aweso kwa kazi nzuri na kubwa anayoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais wetu. Maana Mheshimiwa Rais anahitaji *paratroopers* kama Mheshimiwa Aweso ili azma yake ya kumtua mama ndoo ya maji kichwani iweze kutimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, japokuwa jukumu hili naona linachukua nguvu na nafasi ya ujana wa Mheshimiwa Aweso lakini hakuna namna ni lazima usimame imara uende ukaitende. Mheshimiwa Aweso ulikuja hapa Bungeni ulikuwa kijana mdogo *handsome* mwembamba. Leo hii una kipara, mvi na unazeeka kwa sababu ya kutatua kero za maji na kwa sababu ya kumsaidia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kutimiza azma yake. Kwa kweli kwa pamoja wewe Mheshimiwa Aweso na viongozi wote akiwemo Katibu Mkuu wetu mpya Bi. Mwajuma Waziri, tunawapongeza sana kwa kazi nzuri mnayoendelea kuifanya. Hatuna malalamiko mengi, tuna shukrani zaidi lakini tunawaombea dua pamoja na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanazunguka huko wanamsema vibaya sana Mheshimiwa Rais, amenyamaza kimya na hawajibu. Hata hivyo, mimi napenda leo kumuombea dua Mheshimiwa Rais na ninafahamu wananchi wa Kata ya Kigandwa ambao hawakuwa na maji wakati anapita na wewe Mheshimiwa Aweso ukaahidi na ukapeleka mradi wa shilingi bilioni mbili leo hii wanapata maji, wanamuombea dua Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakina mama wa Kabale ambao hawakuwa na maji walikuwa wanakunywa maji yenye rangi ya *watermelon* wanamuombea dua Mheshimiwa Rais, wanakuombea dua wewe Mheshimiwa Aweso, wanawaombea dua viongozi wote wa Wizara yetu ya Maji. Pia, hao hawana malalamiko na wala hawasikilizi kelele na vurugu zinazofanywa na viongozi wapuuzi wanaozunguka huko kumtukana na kumlaumu Mheshimiwa Rais wetu. Tunataka mpate nguvu na mjue sisi tuko nyuma yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwakani mwaka 2025 tunamuombea dua Mheshimiwa Rais wetu aweze kupita kwa

kura nyingi za kishindo. Kwa sababu kwa hili la maji, sadaka aliyoitoa ni kubwa sana na akina mama wataendelea kumuombea dua, watamsimamia, watampigania na sisi tutakuwa nyuma ya akina mama ambao amewatua ndoo ya maji kichwani, kwenda kumuombea dua na kumpigania ili kuhakikisha anapata ushindi wa kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimeona watu wa Pangani wako hapa. Mheshimiwa Aweso, watu wa Pangani kama wananisikiliza, wakulinde, wakulee, wakupiganie na wakatae mchwa wanaopita kwenye Jimbo lako wakupe kura za kishindo mwakani ili uendelee kutimiza majukumu yako. Mimi ninaamini Mheshimiwa Rais hatokutoa kwenye Wizara hii. Ninakuombea dua ubaki hapo uendelee kutufanyia kazi njema ambayo unaifanya. Vilevile, namuombea mdogo wangu Mheshimiwa *Engineer* Kundo katika msafara huo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda ni mdogo sana lakini namshukuru sana Mheshimiwa Aweso na viongozi wote wa Wizara kwa kuitikia maombi yetu tuliyomuomba Mheshimiwa Rais katika ziara yake aliyopita mwezi Oktoba mwaka 2023 kwenye maeneo matatu tu ambayo yalikuwa yamebaki hayana mradi wowote ule wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nasimama hapa kuzungumza maeneo hayo yote yana miradi. Mradi wa Kigandu unatekelezwa na juzi *engineer* wangu wa maji Ndugu Ntulo, amepeleka mradi kwenye eneo lingine na leo kwenye bajeti hii kuna kisima kirefu kwenye Kata ya Mwasala ambazo hazikuwa na maji.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ahsante kwa nafasi hii.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tunao wageni hapa, itakuwa hekima kuwaruhusu kama watahitaji

kuendelea na majukumu mengine. Kwa hiyo, nikaona niwatambulishe kwanza.

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni wanafunzi 42 wa Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini kutoka Jiji la Dodoma. Naomba msimame, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Sasa atafuatia Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa na baadaye atafuata Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai na Mheshimiwa Robert Chacha Maboto ajiandae.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi nianze moja kwa moja kwa kuunga mkono hoja. Vilevile, mimi naunga pale pale kwa Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla kwamba, niwaombe sana wapigakura au wajumbe wa Mheshimiwa Waziri Aweso basi muangalieni kwa huruma na kwake ninyi muwe watu wazuri ili tusiseme wajumbe noma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu, niseme tu nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Aweso kwa sababu ni kijana mdogo sana lakini mchapakazi sana. Kule kwetu Mkoa wa Mara tunamwita Chacha. Ukija kule Mkoa wa Mara ukisikia Waziri Chacha ujue ni Mheshimiwa Waziri Aweso kwa sababu wanaume wa Mkoa wa Mara ni wachapakazi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema hivi kwa sababu, mpe mtu maua yake akiwa bado yuko hai. Mheshimiwa Aweso ametuheshimisha sana vijana wa Kitanzania na anafanya kazi zinazozidi umri wake. Hii ni jinsi gani inaonesha kwamba Mheshimiwa Rais aliona vema na ataendelea kutuangalia vijana kutokana na vijana wenzetu ambao mmetuheshimisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze sana *Engineer* Mwakalukwa Meneja wa Mkoa wa Mara kwa kazi nzuri anazozifanya. Ni meneja ambaye ka kweli ni mchapakazi, halali, hatulii na haki ofisini; yeye anafanyia kazi *site*. Ombi langu kwa Serikali ni vizuri sasa miradi hii mnayowapatia hawa mameneja

wetu, nikimuangalia Mwakalukwa alikuja akiwa *handsome* lakini sasa hivi amezeeka zeeka hivi. Anafanya kazi sana lakini pesa kidogo ndiyo inakuwa shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi niiombe sana Serikali basi muwe mnawapa pesa kwa haraka mameneja hawa ili waweze kufanya kazi zao kwa urahisi. Vilevile, nimpongeze sana mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri na kubwa anayoifanya. Hili jambo alilolianzisha la kumtua mwanamke ndoo kichwani, kwetu sisi Mkoa wa Mara tunasema Mama Samia anastahili mitano tena kwa sababu ametuepusha na hatari nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndoa nyingi za wakina mama wa Mkoa wa Mara zilikuwa zinavunjika kwa sababu ya kufuata maji mbali lakini sasa tuna maji ya kutosha. Ukija pale kwetu Msoma Mjini, ukifika mpaka mabomba yanapasuka kwa kuwa tu na maji mengi sana ya kupitiliza. Vilevile, Mama Samia amefanya miradi isiyowezekana na sasa imewezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kuna Mradi wa Mugumu – Serengeti. Mradi huu ulikuwa ni Mradi chechefu na sugu lakini sasa umewezekana. Hata hivyo, hii yote ilikuwa ni kutokana na kwamba hata wawakilishi wake ambao ni wachapakazi majembe kama alivyo Waziri wetu Mheshimiwa Aweso anavyofanya kazi usiku na mchana, anapomtuma anatumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana sisi kwetu Mkoa wa Mara wanawake wote tunasema hatuna Rais mwingine, hatumfikirii mtu mwingine na anayewaza kuja kugombea na Mama Samia ajue amechelewa. Yeye asubiri bado sana. Sisi tuna Mama Samia mpaka kieleweke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe sana Wizara ya Maji. Ombi langu kwenu, visima vilivyotolewa na Mama Samia iwe baraka kwa Watanzania. Hata hivyo, ni vema mkavipeleka katika taasisi muhimu kama vile hospitali pamoja na shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kuna shule ambazo mimi niliwahi kutembelea kama vile Shule ya Tagota Tarime lakini pia Shule ya Nyandoto na Nkongore ni shule ambazo wana shida sana. Kwa hiyo, watakapopelekewa visima wakati tunasubiria yale maji mengine ambayo yanaendelea kuunganishwa basi itakuwa ni vizuri. Kwa hiyo, mimi niseme kwamba tuangalie sana kwenye taasisi hizi muhimu ili kusudi kuwakwamua watoto hawa na madhila ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze sana Waziri wangu Mheshimiwa Aweso kwa kazi nzuri na kubwa anayoifanya ya kusimamia kazi anazopewa na Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa mfano, kuna huu Mradi ambao umefanyika wa Mugango – Butiama. Mradi huu kwetu sisi umekwisha na sasa wana-*test* mitambo. Muda si mrefu watu watapata faida ya maji yanayoitwa Maji ya Mama Samia. Kwa hiyo, mimi niseme naishukuru sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri wanazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe wanawake wote wa Kitanzania. Ninyi ni mashahidi, tulikuwa tunafuata maji kwa shida sana lakini Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, amekuja kututua ndoo kichwani na ndiyo maana tunasema Mama Samia mitano tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai atatufatia mheshimiwa Robert Chacha Maboto na Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, ajiandae.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Bajeti ya Wizara ya Maji. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri na timu nzima ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi nipende sana kumshukuru Mheshimiwa Waziri. Kwenye Bajeti ya mwaka jana nilimwomba atupatie gari kwa ajili ya watumishi wa *RUWASA* Wilaya ya

Ngorongoro. Nimshukuru kwamba tumepata gari kwa jili ya watumishi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze Meneja wa *RUWASA* Wilaya ya Ngorongoro, wanafanya kazi kubwa sana. Pamoja na wilaya yetu kuwa kubwa lakini wanafanya kazi kubwa usiku na mchana kwa ajili ya kuwahudumia wananchi wa Wilaya ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi yangu leo ni shukurani lakini pia nina maombi. Tunashukuru kwa sababu mradi wa Oldonyosambu - Masusu wananchi wa Oldonyosambu pamoja na Masusu hawakuwahi kupata maji lakini sasa hivi wanatumia maji, akina mama wanatembea mita 500 wanapata maji ilhali walikuwa wanatembea zaidi ya kilomita 10 kufuata maji mtoni. Kwa hiyo nashukuru sana. Tunashukuru pia kwa mradi wa *quick win* wa Wasso. Awali wananchi walikuwa hawapati maji ya kutosha lakini kwa sasa hivi wanapata maji ya kutosha; pamoja na maeneo mengine ya Oloirien na Lopoluni kwenye mradi ule wa *Covid,* maeneo yale pia wamepata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wilaya zetu za wafugaji sisi tunahitaji maji kwa ajili ya binadamu pamoja na mifugo. Leo ukienda Wilaya ya Longido ukiwawekea wananchi maji bila mifugo ule mradi hautakuwa na maana kwao. Kwa hiyo nikuombe sana ninyi pamoja na Waziri wa Mifugo muweze kufanya *coordination,* ikiwezekana kama wewe una milioni 500 na yeye aongeze milioni 500 angalau tuwe na miradi ambayo ina *impact* kubwa kwa wananchi wale. Kwa sababu unaweza ukawapa wananchi lakini baadae watalazimisha mifugo yao kunywa. Kwa hiyo ni vizuri sana mkiweza kufanya *coordination.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Simanjiro, ukienda Kiteto, Longido na maeneo mengine kama Shinyanga na Mwanza mfanyae *coordination;* mifugo ikipata maji na binadamu wao ndio wanajisikia vizuri, lakini ukiwawekea wao koki na mifugo yao hawajapata maji kidogo ni tatizo kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri kuna mradi wake wa Mageli Vijiji Nane. Tunashukuru kwa

sababu ule mradi kwa sasa umekwishafika asilimia 54. Tulikuwa tunahitaji zaidi ya bilioni sita kwa sasa hivi mmetupa bilioni tatu. Hatua ambayo mradi umefika sasa hivi ni kwenye ujenzi wa tenki la lita 1,000,000, lakini bado kuna matenki mengine nane ambayo bado hayajajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri hizi bilioni tatu zilizobaki. Mradi huo umeanza mwaka 2017, mpaka sasa hivi ni miaka saba. Wananchi zaidi ya 54,000 ambao wanategemea mradi huo wanahitaji kupata maji, kwa sababu wananchi wa kata zaidi ya nne na vijije nane wanategemea mradi ule. Kwa hiyo nikuombe sana Mheshimiwa Waziri utuangalie katika suala hili na na angalau kuongea na wataalam wangu wa wilaya tuone namna ya kupanua yale maeneo kwa sababu kuna vichotea maji zaidi ya 60. Na vichotea ma 11 vimetengwa kwa ajili ya mifugo kupata maji huko Mbautu. Ni muhimu sana sasa tukaongeza kwa ajili ya kufanya mifugo kutorundikana katika eneo moja. Kwa hiyo nikoumbe sana Mheshimiwa Waziri atuangalie katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, kuna mradi wa visima 14 kwenye Pori Tengefu la Loliondo. Unajua aliienda na akawaahidi wananchi kwamba watakwenda kuchimba visima. Ni kweli kwamba visima vimechimbwa, lakini mpaka sasa hivi ni visima viwili ndivyo vinavyotoa maji, visima vingine vyote 12 hakuna. Visima hivyo ni kwa ajili ya Ngobereti, Arash, Losoito, Soitsambu, Loswashi, Orkuyane, Oloipiri, Ormanie kwa maana ya Oldovanioiti, Orkanda, Sukenya na Mondorosi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hawa walikuwa wanategemea maji kutoka kwenye eneo la Pori Tengefu, sasa hivi hawapati maji. Sasa ni vizuri sana wizara waangalie namna hawa wananchi sasa vile visima vichimbwe pamoja na kuweka miundombinu ya wananchi kupata maji ya mifugo pamoja na binadamu. Ni muhimu sana wakatekeleza hilo lakini kwenye visima hivi, na mkandarasi aliyechimba baadhi ya visima mpaka sasa bado anadai shilingi milioni 342 ya awamu ya kwanza lakini bado anadai awamu ya pili *advance payment* ya shilingi milioni 710 ni vizuri mkawalipa angalau kazi ifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine wakati huo pia waliahidi kwamba wizara watachimba mabwawa kwenye eneo la Pori Tengefu la Loliondo. Kulikuwa kuna mabwawa ya awali walisema 35, lakini baadaye Wizara ilipata fedha ya kufanya usanifu kwa mabwawa 18. Mpaka sasa hivi wameshafanya usanifu lakini mabwawa mengine 17 hayajafanyiwa usanifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalam wangu wameomba shilingi bilioni nne kwa ajili ya mabwawa sita ya awali. sasa mimi nimuombe Mheshimiwa Waziri, hawa wananchi walikuwa wanategemea kwamba kwenye mvua za mwaka huu tungeweza kupata maji mengi, na huu ndio ulikuwa mwaka wa fursa na kwamba wananchi wangepata maji mengi kulingana na mvua zilizonyesha, hatuwezi kujua mwakani. Mimi niombe, haya mabwawa yalikuwa kwenye kata zetu zaidi ya 17, kata ya Oldonyosambu ilikuwa ni bwawa moja, Engaresero moja, Malambo mabwa mawili Enguserosambu moja, Nam moja, Soitisambu moja, Ololosokwani moja, Samunge moja, Digodigo moja, Pinyinyi moja, Piaya, Arash, Ormanie, Losoito, Kirtalo Oloipiri na Loswash. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ni muhimu sana Mheshimiwa Waziri waangalie namna ya wananchi hawa. Wilaya yangu hadi sasa hivi upatikanaji wa maji ni 74%. Tukiweza kuchimba mabwawa haya pamoja na kutengeneza visima hivi wananchi watapata maji ya kutosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baada ya kusema hayanaimba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Robert Chacha Maboto atafuatia Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, ajiandae.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kupata fursa hii. Pia napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa nafasi hii ya jioni hii ya leo kupata nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi katika Wizara hii ni Mjumbe wa Kamati, kwa hiyo moja kwa moja ninaunga mkono hoja ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya hasa kwenye upatikanaji wa maji kwenye maeneo yetu. Mwaka 2022 Mheshimiwa Rais alikuja kuweka jiwe la msingi kwenye Halmashauri yetu ya Mji wa Bunda kwenye mradi mkubwa wa thamani ya shilingi bilioni 10.6 na leo mradi huu umeshakamilika kwa 100%. Kwa hiyo kilichobaki ni kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji, ndugu yangu Aweso kumwalika Mheshimiwa Rais aje kuzindua mradi ule kwa sababu umekamilika. Fedha zile ambazo tulipewa katika utekelezaji wa mradi ule zilitumika vizuri zikabaki tukanunua na gari yenye *crane* kwa ajili ya kusaidia kubeba mabomba katika mradi huo. Kwa hiyo tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya hasa katika Jimbo la Bunda Mjini kwenye suala la upatikanaji wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mradi mkubwa mwingine wa usambazaji wa maji Misisi Zanzibar ambao juzi Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja kuweka jiwe la msingi na hiyo kazi inaendelea. Tuna mradi mkubwa pia wa usambazaji wa maji Manyamanyama na Mgaja na kazi inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kumshukuru wewe Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake kwa ujumla kwa kazi kubwa ambayo mnaendelea kuifanya katika Halmashauri yetu ya Mji wa Bunda kwa suala la upatikanaji wa maji. Kwa hiyo kazi kubwa imefanyika kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mimi naingia kwenye nafasi yangu mwaka 2021 mwanzoni upatikanaji wa maji kwenye Halmashauri ya Mji wa Bunda ilikuwa ni kiasi cha chini sana, na maji yaliyokuwa yanapatikana pale yalikuwa ni maji ambayo hayakuwa katika kiwango ambacho kinatakiwa; lakini leo wananchi wa Bunda Mjini wanapata maji safi, salama na yenye uhakika. Kwa hiyo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ana

kila sababu ya kuja kuuzindua mradi ule kwa sababu umekamilika na wananchi wanapata maji vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati kwenye Wizara hii. Wizara ya Maji inashughulika na maji lakini Wizara ya Mifugo pia nayo katika bajeti unakuta kuna maji mle ndani kwa sababu inaweza ikatengeneza mabwawa kwa ajili ya wafugaji kunywesha mifugo yao. Wizara ya Kilimo pia nayo kwenye bajeti yake utakuta inatengeneza bajeti ikiwa inatarajia kuchimba Malambo kwa ajili ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama mbunge nikasema kwamba wizara hizi tatu zikiunganisha bajeti hizi za mabwawa, bwawa lile ambalo wamelenga Kwenda kulichimba katika Halmashauri ya Mji wa Bunda. Wizara ya Maji inachimba, Wizara ya Kilimo inachimba, Wizara ya Mifugo inachimba kwenye eno hilohilo, likaunganishwa bwawa hilo likawa bwawa moja, bwawa kubwa toshelezi ambalo likichimbwa likawekwa vizuri litakidhi mahitaji yote ya Wizara hizo zote tatu, wafugaji watanywesha, wakulima watafanya kilimo cha umwagiliaji na wananchi watatumia maji kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mimi nakua nilikuta kuna lambo moja tu kubwa ambalo lipo kwenye Kijiji cha Bitalaburu ambalo lilikuwa linaweza kubeba maji kwa kiasi kikubwa na likuwa linatumika katika mahitaji haya yote matatu na wananchi wakawa wanatumia vizuri na kwa muda mrefu. Leo ukija kuangalia mabwawa yetu yanayochimbwa madogo halafu hayatoshelezi, wakati mwingine unakuta ndani ya muda mfupi yale mabwawa yamekauka. Niliona lile Bwawa la Bitalabulu lilikuwa linaweza kuchukua muda mrefu sana; na katika umri wangu mimi nilifikiri kwamba ni ziwa, kumbe ni lambo tu limechimbwa katika viwango ambavyo vinatakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ya Maji kwa sababu inashughulika na maji, Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo wakiunganisha jambo hili kwenye eneo moja watatatua changamoto zote za wananchi kwenye maeneo hayo. Wizara ya Maji katika kuhudumia wananchi wake inaweza kutatua maji kwa kupeleka usambazaji wa maji kwa mabomba, pale ambapo

mabomba hayafiki Wizara inachimba visima na pale ambapo visima haviwezekani Wizara inachimba Malambo. Hiyo yote ni Wizara ya Maji inatatua changamoto za maji kwa wananchi wetu. Kwa hiyo mimi kama Mjumbe wa Kamati kwenye Kamati hii nilikuwa napenda kushauri hili, kwamba Wizara ilifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wao kama Mawaziri kwenye Wizara hizi, na wote ni Mawaziri vijana wanaweza wakakaa, wakakubaliana kutengeneza kitu kimoja chenye mvuto mkubwa na manufaa makubwa kwa wananchi. Kwa sababu wakichimba lambo ambalo litakidhi mahitaji yote hayo kwa wakati mmoja wanachi watalifurahia kwa sababu ni vitu ambavyo vimekuwapo huko nyuma tukiviona vinafanyika na vinawasaidia wananchi kwa muda mrefu. Kwa hiyo nimuombe sana Waheshimiwa Mawaziri wa wizara hizi washirikiane ili wakubaliane nalo vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nje na hapo tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya, kwa sababu hata kwenye mradi wetu ule wa Lubana, Mwizani wananchi wetu wa kwenda kule Mihale watapata maji kwa sababu shughuli inaendelea. Pia tuna mradi mkubwa pale wa maji taka na maji safi ambao bado unaendelea na kazi inafanyika. Kwa hiyo nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimuombe sana, kwamba yule Mkurugenzi wangu wa maji aliyeko pale asimtoe kwa sasa, amwache ili kwamba hiki alichokianzisha akikamilishe. Kwa taratibu ambazo mimi nimewahi kuziona wakati mwingine mtu mwingine akija akakuta mwenzake alikuwa ameshafanya vizuri akiingia pale yeye anaona apeleke njia nyingine, kwa hiyo inaweza kusababisha ile miradi mikubwa ambayo sasa hivi tunaitekeleza akaja mtu mwingine miradi hii ikaishia njiani kabla ya kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe Mheshimiwa Waziri alifanyie kazi jambo hili ili tufanye kazi na yule mama kwenye eneo lile ili tuendelee kutatua changamoto kubwa ya wananchi wetu wa Jimbo la Bunda Mjini kwenye changamoto zetu hizi za maji. Kwa kipindi hiki ambacho bado tupo naye, na

Mheshimiwa Waziri mwenyewe akiwepo kwenye Wizara hii naamini kwamba tatizo kubwa la maji katika Halmashauri ya Mji wa Bunda litapungua kama ambavyo amekuja yeye mwenyewe akashuhudia kipindi kile ambacho amekuja kuzindua Mradi ule wa Misisi Zanzibar Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru kwa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, atafuatia Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, ajiandae.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mezani ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia rehema, lakini pili nianze kwa kutumia nafasi hii kumpogeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ni kwa nini? Ni kwa sababu kila Mbunge aliyesimama hapa anakiri kwamba Mheshimiwa Rais ametekeleza kwa vitendo nia yake ya kumtua mama ndoo kichwani. Kwa hiyo na mimi nina kila sababu ya kumpongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi tunatambua mwaka jana alivyoona kuna adha sana ya maji vijijini Mheshimiwa Rais alinunua mitambo akapeleka mikoani kwa ajili ya kuchimba visima na mabwawa. Tuliona kwamba kuna visima 283 vilichimbwa na mabwawa 12 na hiyo kazi inaendelea. Kwa hiyo naomba nimpongeze na Watanzania wote tuna kila sababu ya kumpongeza. Nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri wa Maji kaka yangu Aweso. Sasa kwa vile anajuaga mihemo ya wagonjwa sasa sijui atakuwa daktari, lakini pamoja na timu yake yote kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijielekeze kwenye bajeti. Pamoja na kazi nzuri ya kaka yangu Mheshimiwa Waziri ukiangalia

bajeti aliyoiwasilisha leo, ukifanya ulinganisho bajeti ya mwaka 2022/2023 aliomba bilioni 709.4, mwaka 2023/2024 bilioni 695.8 mwaka huu ametuletea maomba ya bilioni 627.7 ambayo kila Mbunge hapa ameona kuna upungufu wa bilioni 137.7

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi najielekeza kwenye baadhi ya kazi alizoziainisha kwa mwaka huu wa fedha. Kwenye kazi alizoziainisha kwa mwaka 2024/2025 kwenye ukurasa wa 53 amesema Wizara pamoja na mambo mengine itafanya kazi ya kukamilisha utekelezaji wa miradi inayoendelea na ujenzi wa miradi mikubwa, lakini kazi nyingine ni kupeleka huduma ya maji kwenye vijiji. Sasa hapa ndipo ninapoona mzigo mzito alionao Mheshimiwa Waziri. Kwa nini? Kwa sababu pamoja na kwamba Wabunge wamesema hapa miradi imetekelezwa lakini kuna madeni ambayo yanapaswa kulipwa na Serikali ili Wizara iweze kutekeleza kazi ilizojipangia kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda wala sitakuwa ninakwenda maeneo mengi, lakini niombe hili, kwamba Serikali iiwezeshe Wizara ya Maji kulipa madeni takribani bilioni 300, ama ninaweza kusema bilioni 300 na zaidi ambayo wakandarasi mbalimbali wamewasilisha hati ama kwa kizungu mnasema *certificate* sjui. Hizo ambazo zimeshawasilishwa ni vema zikalipwa kabla mwaka huu wa fedha uliopo sasa hatujaumaliza ili kuiwezesha Wizara kwa fedha milioni 627 ambayo imeombwa pungufu ya mwaka jana kutekeleza kazi zake ilizojipangia. Vinginevyo hizi fedha zitakwenda kulipa madeni haya ya nyuma na sjui watalipa kwa vifungu gani, kwa sababu madeni kama wana bilioni 300 na zaidi na hapa kuna miradi ameionyesha itatekelezwa atalipaje. Kwa hiyo mimi niiombe Serikali ilipe haya madeni ya nyuma ili kuiwezesha Wizara itekeleze kazi zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wala sipaswi kufanya rejea majimbo mengine ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kule kwetu Mtwara tulibahatika kupata miradi mikubwa. Mradi wa Makonde wenye thamani ya bilioni 84.7 una hati mbili umewasilisha, moja bilioni moja lakini mwingine bilioni mbili na hela, kadhaa jumla ni bilioni 3.5. Hizo hazijalipwa hata senti. Pia kuna miradi ya *RUWASA*, pamoja na utendaji mzuri wa Meneja wa

*RUWASA* Mkoa na mameneja wa wilaya una-*certificate* takribani bilioni nne hazijalipwa hata senti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mradi wa pale Mtwara Mjini wa kuboresha miundombinu wenye thamani ya shilingi bilioni 19.7; umepelekwa hati lakini haujalipwa. Tuna mradi wa Mnyawi, Mtwara Vijijini bilioni 5.6, *certificate* imepelekwa miezi tisa iliyopita lakini haijalipwa hata *advance payment*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi niwaombe Waheshimiwa Wabunge, na kwa kweli nisipopata majibu ya kuridhisha, na hapa wala siamini kama Mheshimiwa Aweso anaweza akanijibu kwa sababu yeye ndiye anayeomba watu walipwe; kwa hiyo, yeye hana hela.

Naiomba Serikali na nilikuwa naangalia nadhani Wizara sahihi ya kutuletea hizi fedha ni Wizara ya Fedha, ilipe hizi fedha na mimi nitashika shilingi, nitaanza na Wizara ya Maji lakini nitaendelea na Wizara ya Fedha kama sitapata majibu ya kuridhisha kuhusiana na madeni mbalimbali ambayo Wizara ya Maji inadai ili tupate ahueni kwa utekelezaji wa miradi iliyopangwa kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kuanza kutekeleza mkakati wa Gridi ya Taifa ya Maji ambapo Kamati imekuwa ikilisema kila wakati lakini nimeona kwenye hotuba na nimesikiliza pia kwamba mmeanza kutekeleza huu mkakati. Tumeona maji ya kutoka Ziwa Victoria kuja huku ukanda wa kati lakini naomba sana Wizara iharakishe utekelezaji wa hii Gridi ya Taifa ya Maji kwa kuyapata maji kutoka Mto Ruvuma kwenda Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ule mradi wa shilingi bilioni 38 wa Mto Ruvuma kwenda Mangaka umeanza lakini ndiyo hizo *certificate* haziijalipwa, naomba mharakishe. Lakini pia kuyatoa maji kutoka Ziwa Nyasa kwenda Mkoa wa Lindi, Mtwara pamoja na Ruvuma yenyewe lakini kuyatoa maji Mto Rufiji na maeneo mengine ambayo mmeyaainisha kwenye hotuba. Hili kwa kweli tutaomba uharakishe ili kutekeleza hilo agizo la kamati na maoni

ya Wabunge wengi ili tuwe na Gridi ya Taifa ya Maji, ni kengele ya pili?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. AGNES E. HOKORORO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, basi naomba niombe niunge mkono hoja lakini niseme kabisa nia yangu ya kushika shilingi iwapo Serikali haitatueleza kwa kinaga ubaga kwamba italipaje madeni ya maji ili sasa Mheshimiwa Waziri wa Maji aweze kutekeleza miradi aliyoipanga. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa atafuatia Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo na Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga ajiandae.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani mashine zilikuwa zimekataa. Nashukuru sana kwa kupata fursa ya kuchangia Wizara ya Maji jioni hii, waswahili wanasema, "Kushukuru ni bkuomba tena." Nitajitahidi kutumia muda kushukuru na kueleza miradi yangu ambayo Serikali yetu imetufanyia kwa muda mfupi lakini ndiyo nitakuwa natumia gia hiyo pia kuomba katika kuhakikisha tunakamilisha miradi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa *commitment* kubwa aliyoifanya katika uwekezaji wa miradi ya maji mpaka Taifa letu limefikia kuwa kinara katika ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Jangwa la Sahara, hii ni *commitment* kubwa sana katika *rank* za *World Bank,* tunampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu; kwa lugha nyepesi Mheshimiwa Rais pamoja na Waziri wake wanaingia kwenye rekodi nyingine mpya ya kutekeleza miradi ya maji mingi sana nchini; tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nakupongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yako na Naibu Waziri kaka yangu Nsumba Ntale Mheshimiwa Kundo ambaye amehamishiwa Wizara hii na Mheshimiwa Rais. Nimpongeze Katibu Mkuu wenu na wasaidizi

wake wote pale Wizarani pamoja na Katibu wako Gibson ambaye amekuwa akitupa ushirikiano mkubwa sana; tunawashukuru *PR* yenu ni nzuri katika kuhakikisha mnatusikiliza na kupeleka miradi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Meneja wa *RUWASA* wa Mkoa wa Tabora, *Engineer* Kapufi, Meneja wa *RUWASA* Wilaya ya igunga na *Engineer* Humphrey Mkurugenzi wa Maji Igunga - *IGUWASA* pamoja na Bodi yake na watumishi wote; kiukweli wanatutekelezea kwa hatua kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Igunga na *specific* Jimbo la Igunga ilikuwa ni miongozni mwa Majimbo kame sana lakini sisi Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi imetupatia mradi mkubwa wa maji wa shilingi bilioni 600 kutoka maji ya Ziwa Victoria. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais pamoja na chama chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni takribani kilomita 400 kutoka Mwanza mpaka Igunga na sasa hivi sisi tunatumia maji ya Ziwa Victoria na ndiyo maana unaona hata mimi Mbunge wao ukiniangalia kipara kinawaka kwa sababu ya maji ya Ziwa Victoria, nashukuru sana chama chetu. Sasa tumeendelea kupewa fedha kwa ajili ya upanuzi wa miradi na changamoto kubwa kama ambavyo wamesema Wabunge wengi *cashflow* imekuwa siyo nzuri sana. Pamoja na hayo tunaendelea kushukuru; kiukweli mmetufanyia mambo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kusema mambo mawili matatu; jambo la kwanza, pale kwetu Mheshimiwa Waziri sisi tuna mradi mkubwa wa kupeleka maji katika kata saba vijiji 16 imefikia 60%. Unatoka sehemu inaitwa Bulenya ambapo limejengwa tenki kubwa lenye uwezo wa kubeba maji lita milioni 1, unakwenda Kata ya Mwamashiga, Kata ya Mbutu, Isakamaliwa, Kining'la, Mwamashimba, Mwamakona, Igurubi na Kinungu, tunaomba sana mumsimamie makandarasi ama mumfanyie *extension* ya muda. Tunaamini mpaka kufika mwezi wa 12 mwaka huu atakuwa amemaliza; kwa ufanisi na uwezo wenu wa kazi naamini mtalikamilisha linakwenda kwenye maeneo mengi ya wapiga kura wengi wa Chama cha Mapinduzi ambao ni wapiga kura wangu, Mheshimiwa Rais pamoja na

Waheshimiwa Madiwani wetu wa Chama cha Mapinduzi, lakini pia ni moja ya miradi ambayo itatusaidia kwenye kampeni zetu za uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa kuwa tunamtua mama ndoo kichwani kwa vitengo nashukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa mradi huu ambao mlitupatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, pale Igunga tuna mradi tunahudumiwa na mamlaka mbili, Mamlka ya vijijini *(RUWASA)* na mamlaka ya Mji *(IGUWASA)*. Nishukuru sana *IGUWASA* kwa kweli kwa mamlaka ya mji, mimi ni mmoja ya mamlaka za mji ambazo kiukweli tunasema tumefikiwa na maji kwa 100% pale mjini. Tunakushukuru sana kwa jitihada ambazo umetusaidia na sasa umetupatia fedha kwa ajili ya mradi wa maji taka. Mkandarasi bado yuko *site* anajenga yale mabwawa, *cashflow* imekuwa siyo nzuri tunaomba utusaidie ili yale mabwawa yaweze kukamilika katika mwaka huu wa fedha kwa ajili ya kuweza kuhudumia wakazi wa Igunga mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tuna maji kutoka Igunga Mjini, Makomelo kwenda Mgongolo ambao ni wa shilingi milioni 800 pia tunawashukuru Mheshimiwa Waziri ulitupatia huu mradi kwa ajili ya kufanya maboresho kutoa laini ya zamani kuweka laini mpya, tunaomba pia utusaidie huu mradi uweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, niipongeze bodi yangu ya Mamlaka ya Maji Mjini *IGUWASA* walibuni chanzo kipya cha maji. Wakatengeneza laini ya pili ambayo inaenda kuisaidia laini ya Ziwa Victoria, kutoka Igogo kwenda tenki kubwa pale la Mwamaganga ambalo linabeba maji lita 1,500,000. Sasa kuna fedha ambazo walikuwa wameomba Wizarani na tunashukuru Wizara yako mmetupitishia, basi tunaomba Serikali itupatie fedha na sisi utukumbuke katika kutengeneza hii laini. Lakini pia ndiyo mwenendo wa kuhakikisha kwamba tunaipunguzia presha KASHWASA. Tutakapokuwa na laini ya pili itakuwa inapa *back up,* hata inapotokea changamoto maji yanakosekana KASHWASA wananchi wa Igunga wanaendelea kupata maji kutoka kwenye hii laini yetu ya Igogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *point* nyingine ambayo ningependa kuchangia kwa jioni hii, kuna suala la uchimbaji wa

visima 900, mradi wa Mheshimiwa Rais; tunamshukuru sana kwa kuliona hili na mimi nimepata visima vitano, Ibole, Igurubi, Nguvumoja, Kityelo, Imenya, Lugubu na Mgazi – Lugubu. Lakini kabla ya hapo pia Mamlaka ya Maji Vijijini *(RUWASA)* walikuwa wameanza *programme* ya visima vingine vitano ambavyo vipo Mwajinjama Mtunguru, Mwajilunga Kinungu, Kining'inila, Isakamaliwa na Chagana, naishukuru sana Wizara, kwa hiyo, kwa ujumla nina visima 10 ambavyo viumeshaanza na kwa kuwa ile mitambo ilikuwa imeshafika kwenye jimbo langu, sasa wataunganisha na hivi visima vitano vya Mheshimiwa Rais. Naamini kufika mwezi wa 12 kama mlivyotuahidi kwamba mtatukabidhi visima basi tunawatakia kila la heri mkamilishe visima hivi ili tuendelee kumtua mama ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo ningependa kulichangia jioni hii kama ambavyo wamechangia Wabunge wengine ni vyanzo vya mapato ambavyo mnatumia kupata fedha kwa ajili ya kwenda ku-*finance* miradi hii. Ukifuatilia kwa haraka nchi nyingi za wahisani haziwekezi fedha nyingi sana kwenye maji maeneo ya vijijini wanakwenda sana mijini. Sasa kama Taifa inabidi tuamue ili angalau tuangalie namna ya ku-*finance* miradi ya maji ambayo inakwenda vijijini, na Wabunge wengi wametoa mawazo na mimi ningependa kuungana nao tuangalie *structure* mpya ya tozo za kwenye mafuta ambapo baadhi ya maeneo tunaweza tukahamisha kwa sasa wanapata kwa kila lita shilingi 50 angalau wapate hata shilingi 100 au 150 na waunde mgawanyo watengeneze *structure RUWASA* ipate fedha, maji mijini wapate fedha lakini pia na rasilimali maji wapate fedha ili tuweze kutatua kwa kiwango kikubwa matatizo ya maji yaliyoko vijijini kwa kuwa utafiti unasema katika Dunia hii ukiacha hewa jambo la pili linalofuata kwa umuhimu ni maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo atafuatiwa na Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga na Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah ajiandae.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji. Kwanza, niunge mkono hoja, pia namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Aweso na timu yote ya Wizara Naibu, Katibu Mkuu pamoja na Meneja wa Maji Mkoa wa Rukwa Ndg. Boaz pamoja na Wilaya ya Nkasi kwa sababu wanatupa ushirikiano mkubwa sana; nasema hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ya uboreshaji wa miundombinu ya maji nchini ikiwa ni pamoja na Jimbo la Nkasi kusini. Kwanza, nitumie nafasi hii kuwapa pole wananchi wa Jimbo la Nkasi Kusini kwa kupatwa na mafuriko Kata nne; Kata ya Wampembe, Kata ya Ninde, Kata ya Kizumbi na Kata ya Kala, timu ya wataalam ukijumlisha Mkuu wa Wilaya na viongozi wote wa wilaya wanaenda kutathmini tuone namna ya kuwasaidia walioathirika na mafuriko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitoe nafasi hii kuwatoa hofu wavuvi wa Jimbo la Nkasi Kusini na Mkoa wa Rukwa hasa suala la kupumzisha ziwa, wenyewe wanajua mtu yeyote haruhusiwi kuingia. Hata mvuvi yule wa ndoano wanaona kama hata kitoweo cha familia watakikosa lakini uvuvi wa ndoano kitoweo cha kwenda kula na familia unaruhusiwa, hii ni Serikali Sikivu ya Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Nkasi Kusini lina changamoto kubwa sana ya maji hasa baadhi ya miradi iliyokuwepo imesuasua kwa muda mrefu. Ukianza na mradi wa Isale ambao una miaka 11 toka uanze lakini mpaka sasa hivi haujaisha. Mheshimiwa Waziri nikuombe utakapokuja kuhitimisha Hotuba yako ya Bajeti ya Wizara ya Maji uwahakikishie wananchi wa Jimbo la Nkasi Kusini huu mradi wa Isale ambao utanufaisha Kijiji cha Mkata, Nkukwe, Temba, China, Kitosi, Ifundwa, Ntuchi na Chenje unakwisha lini? Huu mradi wameusubiri kwa muda mrefu. Vijiji vimeteseka sana kwa kukosa maji. Mabomba yamewekwa pale lakini matumaini ya maji hawayaoni kwa sababu kulikuwa na changamoto ya mkandarasi nadhani kesi imeshaisha., tumeshapata taarifa na tumekufata ofisini na mimi mwenyewe

nimekufata ofisini umenihakikishia mradi huu wa maji unaenda kwisha. Kutokana na umahiri wako na usikivu wako kama ulivyofanya katika Kijiji cha Kasu ulikuja nikakuomba shilingi milioni 400, wananchi wa Kijiji wameshapata maji na wanakushukuru sana, tupelekee salamu kwa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Katibu Mkuu Dkt. Nchimbi alikpokuwa niliwasilisha changamoto ya maji Wilaya ya Nkasi. Ulipigiwa simu palepale ukatupatia shilingi milioni 400, zimeshafika na ukarabati wa mabwawa Wilaya ya Nkasi kutatua changamoto ya maji kama dharura umeshaanza; tunakushukuru sana wananchi wa Wilaya ya Nkasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nje ya hapo Wilaya ya Nkasi ina changamoto kubwa, suluhu ya kutatua hii changamoto ya maji ni kutoa maji Ziwa Tanganyika, tumemfata Mheshimiwa Waziri ofisini ametuhakikishia upembuzi yakinifu umeshaanza. Nikushukuru sana Naibu Waziri ameshafika Wampembe kwa sababu mradi huu wa maji kutoa Ziwa Tanganyika unaanzia Jimbo la Nkasi Kusini Kata ya Kizumbi Tarafa ya Wampembe, tenki kubwa linajengwa Kijiji cha Kantawa, baada ya Kantawa maji yanaenda wilayani; tunasema ahsanteni sana, mradi huu ukamilika mapema ili wananchi waweze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia vijiji vinavyopita katika mradi huu viweze kupata maji na wananchi pamoja na vijana wengi wa Jimbo la Nkasi Kusini wapate ajira kupitia mradi huu mkubwa wa maji. Pia, upo mradi wa Kizumbi kwenda Wampembe, tarafa nzima hii haina mradi wa maji. Nikuombe mradi huu ni wa muda mrefu, Kata ya Kizumbi kwenda Wampembe kuna changamoto tarafa nzima haina mradi wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshmiwa Waziri, utakapokuja kuhitimisha hotuba yako uje na majibu ya namna ya kutatua changamoto ya mafundi wa pampu kwa sababu pampu ikiharibika wanasema inakaa muda mrefu, wananchi wanasubiria. Tuandae mafundi mahalia kama ni wilayani na kama ni kijijini tuwa-*train* ili pampu ya maji inapoharibika awepo fundi mara moja anaenda anatengeneza na wananchi wanaendelea kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bili za maji zimeongelewa humu, hizi bili za maji ziendane na vipato vya wananchi. Kuna wananchi wa *TASSAF* wengine hali duni vipato viko chini. Kwa hiyo, bili walau tukae chini muone namna ya wananchi watavyolipa kulingana na vipato vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga atafuatia Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi ajiandae.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitoe shukrani kwa kupata nafasi hii ya kuchangia Wizara hii ya Maji. Niungane na wenzangu kumshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Rais mpendwa wa Tanzania lakini Rais ambaye amekuja kuleta matokeo ya Watanzania nini kinafanyika kwenye kumtua mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nirejee kumpongeza Waziri wetu wa Maji na Naibu wake lakini Katibu Mkuu wa Maji na watumishi wote wa Wizara ya Maji. Wakati tunaingia 2020 hasa nikizungumzia kwenye jimbo langu nilikuta tunakinga maji kwenye mabomba yenye rangi ya njano. Tulipata kura Jimbo la Mtwara Mjini watu walikuwa wanatoa kura lakini kwa masikitiko. Hawaelewi kwamba kura wanazokipa Chama cha Mapinduzi faida yake ni nini? Hususan kwenye suala la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini namshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nilivyokutana na Mheshimiwa Aweso nikamweleza juu ya halihalisi ya maji ya Mtwara akanambia kaka usipige kelele suala hili nalibeba nakwenda kumweleza Rais. Nakushukuru sana Mheshimiwa Aweso ulitupatia fedha shilingi bilioni tatu na kujenga chujio ambalo kwa sasa hivi linasaidia kwa 80%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukuishia hapo tu, baada ya chujio lile kukamilika bado maji yalikuwa yana rangi. Nikarudi tena kwa Waziri wa Maji nikamweleza bwana tayari tiba tumeipata

lakini kuna matatizo madogo madogo ya maji, akanambia kaka Rais wetu ni msikivu sana ngoja nilibebe Mheshimiwa Aweso nakushukuru sana mlituletea fedha shilingi bilioni 19 ambazo tumeanza sasa kuyaondoa mabomba yaliyowekwa mwaka 51 ambayo yana kutu na yalikuwa yanapitisha maji pale chini; Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunae *Engineer* wetu wa maji, *Engineer* Reja; kwa kweli huyu mtu mzima na kama itakapofika muda wa kustaafu Mheshimiwa Waziri muongezee tena kwenye mkataba aendelee kuwatumikia watu wa Mtwara kwa sababu ndiyo suluhisho la watu wa Mtwara kufika mahala sisi tukajivunia kwamba tuna mtendaji ambaye anawajibika kwa malengo ya kuwasaidia wananchi wa Jimbo la Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee tena kuipongeza Serikali na kumpongeza Rais, eneo la Mtawanya Mheshimiwa Waziri wamepita Marais zaidi ya wanne lakini eneo lile lilikuwa bado halijalipwa fidia ulivyokuja Mtwara nikakueleza wananchi wanavyopata shida ambapo wanadai fidia takriban ya shilingi milioni 700. Mheshimiwa Aweso uliniahidi kwamba unakwenda kwa Rais, peleka salamu zetu kwa Rais kwamba watu wale tayari wamelipwa shilingi milioni 700 za fidia ya takriban miaka 20 iliyopita, kwa hiyo, tunatanguliza shukran kwake na hatuna cha kumpa lakini atatuona mwaka 2025 kura zitakavyojaa kwenye sanduku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Aweso leo sitaki kuzungumza sana lakini nina jambo moja nataka nikueleze kaka yangu. Tuna mradi wa Mto Ruvuma, suluhisho la Mtwara ni kuleta maji ya Mto Ruvuma na *brother* nilikuwa nakusudia nije hapa leo nikamate mshahara wako lakini kila nikikuangalia na sura yako na jinsi ulivyo siku ya leo unanigeukia mara mbilimbili njoo na majibu utueleze kwamba mradi ule *package* yake inaanza lini ya kutuletea maji ya Mto Ruvuma kuja pale Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nichukue fursa hii kukuomba kaka yangu na ndugu yangu umenisaidia sana kwenye Jimbo la Mtwara Mjini usichoke kutusaidia, hili nina imani unaliweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuunga mkono hoja na Mungu akubariki sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah atafuatia Mheshimiwa Dkt. Frorence George Samizi, Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa ajiandae.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Maji. Naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso, pamoja na timu nzima ya Wizara yake kwa namna ambavyo wametuheshimisha katika majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepunguza changamoto kwa kiasi kikubwa sana, leo sisi Wana-Lindi tuna maji mengi ya kutosha kwa hiyo, tunakushukuru sana Mheshimiwa Jumaa Aweso. Mheshimiwa Rais anakutegemea sana kwa sababu, umekuwa msaidizi mwema wa kutusogeza mbele kuhakikisha kwamba, Watanzania tunaendelea kupata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwa ukweli kabisa kwamba, katika miaka mitatu ya Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania changamoto kubwa ya maji imepungua katika maeneo yetu kwa zaidi ya 60%. Pale Lindi Manispaa wakati naanza kuwa Mbunge tulikuwa na changamoto kubwa ya maji. Ilikuwa ni kazi kubwa kuomba kura na tukaaminiwa na wananchi, lakini leo maji yako mengi ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna haki ya kumpongeza Mheshimiwa Rais, kuendelea kumtia moyo na kuhakikisha kwamba 2025/2030 kazi iendelee. Katika eneo la Manispaa ya Lindi tuna miradi ambayo tulitakiwa tuitekeleze katika kipindi cha Mwaka huu wa 2023/2024. Sasa tumebakiwa na robo moja ya kutekeleza miradi hii kufikia mwaka mpya wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba sana Mheshimiwa Jumaa Aweso, tuna Mradi wa Upanuzi wa Maji wa Hangaza

Sekondari ambao tumeshajenga tanki. Mradi ule ulikuwa wa gharama ya shilingi 1,100,000,000 fedha ambazo zimetoka ni shilingi 400,000,000 na fedha ambazo zimebaki ni shilingi 731,000,000. Mheshimiwa Jumaa Aweso nakuomba sana uhakikishe kwamba, tunapata fedha hizi, ili kufanya mtandao wa maji uweze kuwafikia wananchi na waendelee kupata huduma ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tuna Mradi wa Maji Mkundi. Nikisema Mkundi, imesemwa na Waheshimiwa Wabunge wengi, inawezekana majina ya maeneo yanafanana, lakini Mkundi ambayo ninaizungumzia Mheshimiwa Jumaa Aweso ni upande wa pili wa bahari ambako na wewe umeshawahi kufika. Tulitengewa fedha kiasi cha shilingi 934,000,000 pale wananchi hawajawahi kuona maji ya bomba, katika Mwaka huu wa Fedha kati ya kiasi hiki cha shilingi 934,000,000 tulizotengewa hatujaletewa hata shilingi moja. Tunakuomba utupatie fedha, ili twende kutekeleza mradi huu wa maji kwa sababu, matanki yapo, bado kwenda kuendelea kusambaza mtandao wa maji, ili kuhakikisha kwamba maji yanawafikia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Jumaa Aweso tulikueleza changamoto kubwa ambayo tunayo Lindi Mjini. Maji tunayo ya kutosha, matenki tumejenga kwa gharama kubwa, lakini changamoto tuliyonayo ni juu ya kuyasambaza na kuwasogezea wananchi miundombinu, ili waweze kuvuta maji majumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika eneo hili tuna changamoto kubwa. Mheshimiwa Aweso ulituahidi shilingi 500,000,000 mbele ya Mheshimiwa Rais. Tunaomba utekeleze kabla hujamaliza mwaka huu wa fedha ili kuhakikisha kwamba, wananchi wa Lindi wanasogezewa maji. Shilingi 500,000,000 tunataka kuielekeza katika kata ya Ng'apa, Tandangongoro, ambako kuna mradi mkubwa wa maji ambayo ndio tunatumia Wananchi wa Manispaa ya Lindi na mengine tunawapelekea majirani zetu wa Mchinga, lakini wananchi wa Ng'apa wenyewe wanakosa maji kwa sababu, hakuna miundombinu ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamuomba sana Mheshimiwa Jumaa Aweso ahakikishe kwamba, anatuongezea shilingi 500,000,000 ili kwenda kusogeza miundombinu ya maji. Tuna wananchi karibu 12,498 pale wanahitaji huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tunayo miradi mipya tunashukuru kwamba, tuna Mradi wa Kujenga Tenki Kiduni kwa fedha za *Covid-19*, shilingi 600,000,000 na mradi umekamilika. Sasa tunataka kuongeza miundombinu ya maji kuhakikisha kwamba, Wananchi wa Ruaha, Mnazi Mmoja, wanapata maji safi na salama. Tunakuomba Mheshimiwa Waziri utupatie fedha, hizi shilingi 1,229,000,000, ili tuweze kukamilisha wananchi wetu wapate huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna Mradi wa Upanuzi wa Maji kule Kitunda, upande wa pili wa bahari. Tanki tumejenga, lakini bado tunahitiaji kusambaza miundombinu ya maji, ili kuwafikia wananchi wa Kitunda, Mnali na Sinde. Mradi huu una gharama ya shilingi 1,500,000,000, tuna wananchi wengi wanaishi kule hawajawahi kuona maji safi na salama. Wamezoea kuokoteza maji huko mashimoni, mabondeni kwa hiyo, tunamuomba sana Mheshimiwa Jumaa Aweso ahakikishe kwamba, tunapatiwa hizi fedha, ili mambo yetu Lindi Mjini yawe supa. Tuhakikishe kwamba, mwaka huu uchaguzi tunaumaliza salama, mwaka kesho tunaendelea vizuri, tuendelee kurudi tena hapa mjengoni, tuendelee kuchapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, muda wako umeisha.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umeisha?

**MWENYEKITI:** Muda umeisha, ahsante.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Jumaa Aweso kwa kutuunganisha Wabunge wote pamoja na Wizara yake. Ushahidi tosha tumeuona kwamba, hata mwenyewe ameweza kuiunganisha familia yake. Tumeona wadada wazuri warembo walikuwa hapa wote wawili hawana mgogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, atafuatia Mheshimiwa Engineer Ezra John Chiwelesa na Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya maji, Wizara muhimu kabisa kwa maisha ya wananchi wetu. Mimi pia, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jinsi ambavyo anafanya kazi kwa bidii kuhakikisha kwamba, azma yake ya kumtua mwanamke ndoo kichwani inatimia. Wote ni mashahidi, tumeona ni jinsi gani pesa zimemiminika kwenye majimbo yetu, ili kutekeleza azma hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Muhambwe limepokea takriban shilingi bilioni 8.5 ili kutekeleza miradi ya maji mijini na vijijini. Hii imetusababisha kutoka kwenye upatikanaji wa maji vijijini kutoka 54% mpaka 77% na kwa upande wa maji mijini kutoka 37% mpaka 67%, hizi ni jitihada kubwa sana. Tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu, ameibeba ajenda hii akiwa bado ni Makamu wa Rais na ameenda kuitimiza kwa kishindo ambapo amekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pongezi nyingi zimuendee na waswahili wanasema tunampa maua na bustani yake kwa sababu, amefanya kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Jumaa Aweso, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii. Nampongeza *Engineer* Mwajuma kwa kazi nzuri anayoifanya, tumeona jinsi anavyofanya akiwa Naibu Katibu Mkuu na sasa anatekeleza kwa kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapongeza watendaji wa maji wa Mkoa wa Kigoma, *Engineer* Mwenda, *Engineer* Aida na Almas wa Kibondo kwa jinsi ambavyo wananifanya niweze kutekeleza kazi za Wizara hii ya Maji katika jimbo langu kwa urahisi. Hongereni sana watendaji wote wa Wizara ya Maji kwa jinsi mnavyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Aweso kipekee nakushukuru kwa heshima uliyonipa ya kufika Jimboni kwangu Muhambwe. Umekuja ukajionea mambo yanavyokwenda, kwa kweli tunamshukuru sana, Wana-Muhambwe wanakushukuru sana. Nachukua nafasi hii kusema tunakushukuru kwa sababu, ahadi ulizoziahidi zimekwishatekelezeka. Tumepokea gari moja kama ulivyotuahidi, tumepokea pikipiki nane na tumepokea guta la tani tatu katika Jimbo letu la Muhambwe. Tunakupongeza sana na ninakushukuru kwa niaba ya Wananchi wa Muhambwe, Mwenyezi Mungu akubariki sana ndugu yangu Mheshimiwa Aweso. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba, tumepiga hatua kubwa sana kwenye miradi ya maji. Wote wameongelea, sina sababu ya kurejea, lakini hizi pongezi ambazo mpaka Kimataifa na kidunia mnakwenda kushika nafasi ya pili kwa miaka miwili mfululizo sasa ndizo ambazo zimefanya tuweze kutekeleza miradi ya maji. Tumeona kwa kufanya kwenu vizuri, badala ya kuwapelekea huduma ya maji watu milioni tatu, mmepeleka kwa watu milioni nne, mmesababisha muaminiwe na mpewe pesa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona miradi ya *P4R* sasa itakwenda kupokea Dola za Marekani milioni 654 kutoka milioni 350. Hizi ni jitihada kubwa na wananchi wa Muhambwe wamefaidika. Kile kiasi cha shilingi bilioni 1.3 uliyonipatia kutoka *P4R* basi wananchi wa Rukaya wanakunywa maji, wananchi wa Magarama wanakunywa maji na wananchi wa Mikoko wanakunywa maji. Kwa hiyo, ni jitihada kubwa, tunakupongeza na tunaamini tutaendelea kupata pesa zaidi, ili miradi katika majimbo yetu iweze kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi nzuri hizi ambazo tunaendelea kumpatia, bado zipo changamoto ndogo ndogo ambazo tunaamini Serikali yetu inaziweza. Kwanza kabisa Wananchi wa Mkoa wa Kigoma leo wamefurahi sana kusikia kwamba na sisi tunaenda kuingia kwenye historia ya kupata maji kutoka kwenye Ziwa Tanganyika. Hiki kilikuwa ni kilio chetu na leo tumekusikia kwamba, mshauri anaendelea kufanya kazi, tunaamini atakuja na matokeo chanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, mimi jimbo langu lina Mto Malagarasi, kutoka Mto Malagarasi mpaka kata yangu ya kwanza ya Busunzu ni kilomita nane. Wananchi wa Nyalulanga na Busunzu hawana maji ilhali wako katika Mto Malagarasi, lakini sijakuona kuandika Mto Malagarasi kwenye *grid* yako. Mheshimiwa Waziri nakuomba uuingize Mto Malagarasi kwa sababu uko karibu sana na jimbo langu na utakwenda kutatua changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni Jimbo la Muhambwe tumefanya vizuri sana. Kwa sasa tunapata maji lita milioni tatu kwa siku, lakini mahitaji ni lita milioni 6.8 kwa siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Neema ya Mwenyezi Mungu, kupitia mitambo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, moja ya kisima tulichochimba katika Kata ya Lusohoko kimetufanyia maajabu kwa sababu, kimeleta maji mengi sana. Wanasema inawezekana ni katika mkoa mzima kisima kile kinatoa lita laki tatu na nusu kwa saa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Waziri Aweso kwa sababu, kisima hiki kimeleta hayo maji hatuna tena sababu ya kwenda kutoa maji Nduta kwa ajili ya maji ya mamlaka ya mji kwa maana ya Kata tatu za Kibondo Mjini, Biturana na Kumwambo. Tunachotakiwa kufanya, nakuomba Mheshimiwa Aweso, tumeshakuletea andiko ambalo linagharimu shilingi bilioni 4.5, hili tunakwenda kuweka tanki tu pale kwenye Mlima wetu wa Muyaga pale Kitahana na maji tunatoa Lusohoko badala ya kuhangaika na Mto Nduta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Aweso nakuomba unavyokuja kuhitimisha unihakikishie umeuweka mradi wangu huu mpya wa maji kutoka katika kisima hiki cha maji ambacho kimeonyesha maajabu katika Mkoa wa Kigoma, ili Wananchi wa Jimbo la Muhambwe waweze kupata maji. Kwa kufanya hivi, nina uhakika tutakwenda kutimiza matakwa ya Ilani yetu ambayo yanatutaka tufike 85% kwa 95% ya maji mijini na vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo mradi mwingine wa Nyamkokoma ambapo ni Kata ya Kumwambu, wananchi hawa hawana maji kabisa. Mradi ule umeshaanza japo kwa kununua mabomba tulipopata shilingi milioni 300, lakini mradi huu unahitaji shilingi bilioni moja. Naomba Serikali inisaidie niweze kupata hii pesa kwa ajili ya kuweza kutekeleza huu mradi wa Nyamkokoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia tuna vijiji sita ambavyo havijapata miradi. Mimi naishukuru Serikali kwa sababu, naamini vijiji hivi sasa vya Kumkuyu, Kasana, Nyarugusu, Kumhama, Nyarulanga na Kigina vitafaidika na hivi visima 900 ambavyo Mheshimiwa Rais ametoa. Kwa niaba ya Wananchi wa Muhambwe ninaishukuru sana Serikali kwa sababu, sasa tutakwenda kupata miradi ya maji katika vijiji vyote vya Jimbo la Muhambwe, ili Wananchi wa Muhambwe waweze kuendelea kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi niungane na wenzangu kuunga mkono hoja ya bajeti hii ya Wizara ya Maji kwa sababu, kwa kweli imetupa heshima katika majimbo yetu. Mwenyezi Mungu ambariki sana Rais wetu na Waziri wa Maji. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, atafuata Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris na Mheshimiwa Deus Clement Sangu ajiandae.

**MHE. ENG. EZRA J. CHILEWESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niwe mmoja wa wachangiaji katika hotuba ya Wizara ya Maji. Kipekee, namshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi

kubwa anayoifanya, hasa kwa visima hivi ambavyo vimeletwa kwenye majimbo yetu. Pia pongezi kwa msaidizi wake wa karibu anayemuwakilisha katika sekta ya maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso, na wasaidizi wako wote katika Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya sana mimi misemo ya pwani siijui, ningeweza kuchomekea kama ya kwako ile, lakini siijui. Kwa hiyo, mimi ninaenda hivyo hivyo na unielewe hivyo hivyo, lakini nasema tu wewe ni mtu rahimu sana. Ulikuja Biharamulo, mambo uliyoyakuta na ukaahidi, yote yameshatekelezwa mkuu. Kwa hiyo, mimi nakushukuru sana, tumepata gari, pesa na vitu vingine vyote tulivyokuwa tunavihitaji. Miradi hii miwili ya Usambazaji wa Maji Biharamulo Mjini na Nyarukongogo inaendelea, mmoja una 20% na mwingine una asilimia 65. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia bajeti yako Mheshimiwa Waziri, iko vizuri, miradi yangu mingi inayoendelea na hii mipya ambayo imewekwa, ninakushukuru sana, naamini utekelezaji wake unaenda kufanyika. Ninaomba *item 58* kwenye Mamlaka ya Maji Mijini, najua ndipo, nimeambiwa fungu hili ni kwa ajili ya mradi wa Ziwa Victoria. Mheshimiwa Rais alikuja Biharamulo na ahadi ikatolewa kwa hiyo, ninaomba utakaposimama Mheshimiwa Waziri, utakapokuwa unahitimisha, Wananchi wa Biharamulo wanakusikiliza na ninajua umekuwa ukinipa majibu, ningependa wananchi wa Biharamulo wajue kwa sababu, ni ahadi ya Rais, ni nini kinaendelea juu ya ule Mradi wa Maji wa Ziwa Viktoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya, mimi nina wazo tu. Ajenda ya maji ni ajenda ya Mheshimiwa Rais, maana ajenda zote ni zake, lakini ya maji ni yake zaidi. Ni yake zaidi kwa sababu, ni ajenda aliyoanza nayo tangu mwanzo na siku analihuitubia Bunge humu, Waziri aliyepewa maelekezo *specific* ni Mheshimiwa Aweso. Sasa bajeti ya maji inaporudi nyuma kwa kiasi kile, tunaifanya ajenda ya Rais au tunamrudisha wapi? *(Makofi)*

Mheshomiwa Mwenyekiti, kwa sababu Mheshimiwa Aweso nimemtaja kwamba, ni mtu rahimu. Mheshimiwa Aweso huyu

ukimpigia simu muda wowote ukamuambia jimboni, kesho ataonekana, kesho kutwa ataonekana, ndiyo maana maisha yake yeye na Wabunge ndani ya Bunge hili huwezi kusikia amegombana na Mbunge yeyote. Ni kwa sababu, ni mtu anajinyenyekeza kupita kiasi na anawasikiliza Wabunge wote, lakini usikilizaji wake kama hapewi pesa hauna maana, unamuangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba kama inawezekana, tuone jinsi ya kufanya pesa hizi, Kamati ya Bajeti wako hapa, kwa maelekezo ya Kiti chako, waende wakaangalie jinsi ya kumuongezea pesa huyu bwana afanye kazi hii. Maji ni ajenda ya Rais, sasa msipompa pesa inaonekana kaiangusha wakati yeye na maisha yake na Wabunge humu ndani kila kitu anaenda nao vizuri. Tuombe Kiti chako kione jinsi ya kufanya, hatuwezi kuona bajeti ya maji mwaka jana imeenda juu, sasa hivi tunarudi nyuma, hicho kitu hakikubaliki. Naomba niweke hivyo, Kiti kiangalie tujue jinsi ya kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa na ushauri pia kwa Mheshimiwa Waziri. Wabunge wengi hapa tunatoka vijijini ndiyo maana mliunda *RUWASA*, ili wananchi wa vijijini waweze kupelekewa maji. Walau mjini unaona asilimia iko juu, lakini sisi huku tunaozunguka vijijini akina mama bado wanabeba ndoo na kuhangaika. Mijini kuna baadhi ya watu wana uwezo wa kuwa na visima, wana maboza na nini wanasaidiana, lakini vijijini *facilities* kama hizo hazipo na baadhi ya maeneo bado. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ninaomba, ili uweze kuwa na mpango mzuri ni lazima ujipange pia katika utekelezaji na jinsi ambavyo watu wana-*project cash flow* yao. Ninaomba, pesa ya mfuko wa maji kama tunaweza tukaigawanya tukafanya kama wanavyofanya upande wa *TANROADS;* inajulikana kabisa kwamba, hapa ni vijijini *TARURA,* hapa ni *TANROADS.* Inakuwa inajulikana kwenye ile *road fund*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakuwa ni rahisi zaidi hata mtu anapokuwa anapanga, anakuwa anajua kabisa mwezi huu, kuna bilioni hizi, mwezi huu kuna bilioni hizi. Hata unapo-*project* na hawa wakandarasi wa kusaidia kufanya miradi, *it's very easy,*

hata wewe ukawa unajua unawajibu nini. *Sometimes* tunakuwa tunakuonea huruma Mheshimiwa Waziri, atakuja mtu wa Maji Mjini, hujui unamjibu nini, atakuja mtu wa *RUWASA,* hujui unamjibu nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuone kama mtafanya *projection*, *let say 60 percent,* ikaenda *RUWASA,* labda *25 percent,* ikaenda Mamlaka ya Maji Mijini, labda nyingine ndiyo iende kwenye mabonde; itakusaidia hata wewe unakuwa unajua kabisa kila mwezi nina *20 billion* au nina *30 billion* inaenda sehemu fulani. Kwa hiyo, hata wewe *projection* yako inaweza ikakaa vizuri ukaweza kuwasaidia wakandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri lazima ukubali wakandarasi wamekubeba. Wakandarasi wa Kitanzania ni lazima tuwapongeze kwenye hili, maana hakuna Mkandarasi wa Kitanzania anayedai riba mpaka sasa, lakini pesa zao zaidi ya shilingi bilioni 200 unaelewa ziko zinadaiwa, lakini kwa sababu wewe ni mtu rahimu ukiwaambia wanakusikiliza, wanaenda kukopa wanaendelea kufanya hii miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuiombe Wizara ya Fedha ikusaidie pia, usije ukapoteza ule uaminifu ambao umekuwanao, watu wanakusikiliza wanafanya, hatimaye sasa kesho wakaondoka *site* mambo yakaharibika. Kura za CCM na heshima ya Mheshimiwa Rais iko kwenye maji kwa sababu, ni ajenda yake. Sasa tuombe mjipange vizuri huko muweze kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala la mita za *pre-paid*, hili suala nimelisema juzi, naomba kulirudia tena hapa, *am talking of this as a professional*, suala la mita za maji za kulipia kabla, mimi naliunga mkono *100 percent*, sikatai, lakini ushauri wangu niliosema juzi, twende kwanza kwenye Mamlaka zenu za Serikali, Mamlaka za Serikali ndiyo zimekuwa hazilipi. Hayo madeni makubwa mnayoyasema yawekeni huko kwanza, kwa sababu *experience* yangu katika nchi nyingi ambazo nimefuatilia na kampuni nyingi kubwa ya mita duniani, hakuna kampuni inayozalisha hizo mita. Mita zimetokea China ingawa zimekuwa hazitumiki, tuone jinsi ya ku-*rectify*…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** …ili ziweze kutusaidia baadaye tusiingie mgogoro na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashukuru kwa ajili ya hilo, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, atafuatiwa na Mheshimiwa Deus Clement Sangu.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu ya Wizara ya Maji, Wizara ambayo kwa uhakika imebeba maisha ya Watanzania. Nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika kumtua mwanamke ndoo. Hii ilikuwa ni *agenda* yake toka alipoingia akiwa Makamu wa Rais lakini sasa hivi akiwa kama Rais, ameisimamia kwa dhati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Ndugu yangu Mheshimiwa Aweso, Naibu wake Mheshimiwa *Engineer* Kundo pamoja na watendaji wakiongozwa na Katibu Mkuu *Engineer* Mwajuma, kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Vilevile nitumie nafasi hii kumpongeza kwa dhati ya moyo wangu *Engineer* Mmasi, Meneja wa Bonde Ruvu, lakini *Engineer* wa Mkoa wa *RUWASA* pamoja na *Engineer* wa Wilaya yangu ya Morogoro Vijijini kwa kazi kubwa ambayo wameifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, nilienda ofisini kwake kwa suala la Mradi wa *Kibana Group*, mradi ambao una-*cover* kata nne lakini vijiji 13. Mwaka jana tuliweka *token* ya shilingi 200,000,000 pamoja na *VAT*, unahitaji shilingi 10,000,000,000. Tulishindwa kutangaza, lakini mwaka huu Ndugu yangu Mheshimiwa Waziri na *Engineer* Mwajuma tulikuwa pamoja juzi, tumetenga shilingi bilioni 1.8. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe, niombe, mmeniahidi kwamba tutatangaza, kwa hivyo nikuombe *Engineer* wangu wa maji wa mkoa yupo, naomba baada ya kupitisha bajeti kesho, naamini itapita, mwende mkakae, mradi hu utangazwe. Wananchi wa vijiji 13 na kata nne wapate mahitaji yao ya majisafi na salama. Hasa ukitilia maanani, Mkoa wa Morogoro, Jimbo la Morogoro Kusini ndilo linalotoa maji 76% kwa viwanda Dar es Salaam na Pwani. Kwa hivyo wana Morogoro wana haki ya kupata haki yao hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini natumia nafasi hii kumpongeza Ndugu yangu Mheshimiwa Aweso kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. Mwaka jana, kuna Mradi wa *Bwakila Juu Tower*, kuna fedha ilitengwa lakini haikupatikana, nadhani bajeti bado haijakamilika. Kuna Mradi wa Mvuha Dala, lakini kuna Mradi wa Lundi. Wakati ulipokuja kuna ahadi ulitoa ya kutoa fedha ili maji yafike kwenye Kijiji cha Milango Miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba wakati bajeti bado inaendelea Mheshimiwa Waziri, angali kwa namna moja au nyingine, unafanyaje kusudi miradi hii ikamilike na wanachi wetu wa Morogoro Vijijini ambao ndiyo wahifadhi wa maji kama nilivyosema wa Dar es Salaam, wao nao waone wanafaidika vipi na maji. Nakupongeza kwa visima vitano ambavyo tumevipata ambavyo tutakwenda kuchimba Lukulunge, Nige, Kibangile, Vihengele na Ikulo. Ni imani yangu kwamba vitaenda kusaidia kuondoa kero kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika hili, namwomba Mheshimiwa Waziri na watendaji wake hebu waangalie, sisi watu wa Morogoro kuendelea kupewa visima, siyo sawa. Sisi kama wahifadhi wa maji, tunahitaji tupate miradi ya maji ya mserereko, lakini nitumie nafasi hii kupongeza kwa ujenzi wa Bwawa la Kidunda umefikia 17.5%, lakini ziko changamoto ambazo ningependa nizi-*address* katika Bunge lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza, naomba Mheshimiwa Waziri anapokuja kuhitimisha hoja, atamke kwamba Mradi wa Kidunda utaenda kutoa maji kwa Halmashauri ya Morogoro Vijijini kwa sababu ndani ya mpangilio wake, haioneshi. Ninajua

ulinieleza kwamba tutapata maji lakini kwa kutamka ndani ya Bunge itakuwa ni kauli ya Serikali na sisi wananchi tutakuwa tunafaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado kuna changamoto kwa ndugu zangu wa *DAWASA* katika kulipa makaburi. Mwaka jana tuliambiwa kuna shilingi bilioni 1.8 lakini hadi tunavyozungumza sasa hivi hakuna kitu hicho. Kwa hiyo tunahitaji wananchi wale wafidiwe makaburi yao ili kusudi mradi uendelee. Vilevile, kuna changamoto kwenye hili suala la Mradi wa Kidunda, wakati unatangazwa, mimi nilikuwepo katika Bunge la Kumi na ndiye nilikuwa mtu wa kwanza katika kuhakikisha kwamba mradi huu unafanikishwa kwa kuwashawishi wanachi wangu wahame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokumbuka wakati wanafanya tathmini ya mazingira, niliomba wananchi wote wa vijiji ambavyo viko kwenye Kata ya Selembala waondoke kwa sababu nilijua athari ambayo itakayowakuta. Vilevile, wananchi ambao wako kwenye Kata ya Mkulazi kwa mdogo wangu Mheshimiwa Tale Kijiji cha Kidunda nao tulisema waondoke. Walioondolewa waliondoka, waliobakia wamebakia. Hivi tunavyozungumza, mafuriko yamekuwa ni athari kubwa kwa wananchi hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakokwenda, tunaweza tukampeleka Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwenda kutoa pole wakati siyo sahihi. Nakuomba Mheshimiwa Waziri, unapokuja kuhitimisha hoja, naomba unieleze, je, Wizara ina mpango gani wa kuwaondoa wananchi wa Kijiji cha Kiganila, Kijiji cha Bwila Juu na Kijiji cha Magogoni katika Jimbo la Morogoro Kusini lakini Kijiji cha Kidunda katika Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki ili tuondokane na adha hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kabisa, wakiendelea kuwepo watu hao, tunaweza tukaleta hatari kubwa sana. Vilevile nitumie nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Waziri, juzi wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anatoa taarifa za mafuriko, nilizungumzia jambo moja. Nini mpango wa Serikali katika kuvuna maji ambayo yanatokana na mafuriko, hata Mkoa wa Morogoro kila mwaka kuna mafuriko. Tuna mito mitano hiyo ambayo inakwenda katika

kutengeneza Bwawa la Kidunda, kama tutaweza kuitengenezea mabwawa kwa juu, tutaweza kuondoa matatizo makubwa ya mafuriko kwa wananchi wetu lakini hili siyo tu kwa Jimbo langu la Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natamani Wizara itueleze kwa Mkoa wa Morogoro wana mpango gani wa kuchimba mabwawa ambayo yatapunguza mafuriko lakini vilevile yatahifadhi maji kwa mifugo na hata kwa matumizi ya wanadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho nataka kumuomba Mheshimiwa Waziri kwenye suala la …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Innocent muda wako umeisha.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deus Clement Sangu.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi kuweza kuchangia mawazo yangu kwenye Wizara hii nyeti ya Maji. Kwanza kama wenzangu, nachukua fursa hii kumpongeza Rais ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayofanya na msukumo mkubwa anaoufanya kupeleka fedha nyingi kwende miradi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Waziri mwenye sekta, ndugu yangu Mheshimiwa Aweso pamoja na Naibu wako ndugu yangu Mheshimiwa Kundo, mnafanya kazi nzuri, pamoja na Naibu Waziri aliyemtangulia Mheshimiwa Kundo pia alifanya kazi nzuri akihudumu kwenye Wizara hii. Menejimenti yako nayo inafanya kazi nzuri mimi nawapongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa namna ya pekee, kwa kuwa mimi mkoani, nafanya timu na *RM* na timu ya wilaya, nampongeza Meneja wangu Boaz, anafanya kazi vizuri na *Engineer* Maganga, wanatupa ushirikiano mzuri na ndiyo maana mambo yanaenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitaongelea mambo mawili, la kwanza ni la jumla. Tumekuwa tukipiga kelele ndani ya Bunge hili, miradi ya maji haiendi. Kama nchi, shida siyo vyanzo vya maji, shida ni *financing* kwenye miradi ili maji yaweze kuwafikia wananchi. Tuna maji ya chini na *surface water* lakini ni namna gani tutayatoa yawafikie wananchi, ndiyo jambo linalotuumiza vichwa kama Taifa. Leo hii umetoa hotuba yako Mheshimiwa Waziri na *concentration* yako ulikuwa unaongelea habari ya *Green Bond* ya *Tanga UWASA*. Umeona kwamba *Tanga UWASA* ilivyo-*perform* na ukachukulia mfano ni wazi ndiyo taasisi ya kwanza Barani Afrika kutoa Hati Fungani ya Kijani kwa maana ya *Green Bond*. Sasa, huo ndiyo mwelekeo wa kutafuta *alternative financing* kwenye miradi ya maji. Tuking'ang'ania vyanzo vya *Water Funds, PforR*, sijui *Government Fund*, tutapiga *mark time* hapa, hatutaenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mchakato ulikuwa ni mrefu sana, haujaanza leo, umechukua muda mrefu. Kwa Bunge hili, nachukua nafasi hii, pamoja na kukupongeza wewe Mheshimiwa Waziri, nazipongeza taasisi mbalimbali zilizoshiriki kwenye mchakato huu. Kwa kuwa ndiyo uelekeo tunaoenda nao, lazima tuwape moyo ili tutakapokuja na jambo hili kwa taasisi nyingine, watuunge mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana *UNCDF (United Nations Capital Development Fund)*, wao ndiyo waliotusaidia katika michakato ya ku-*fund process* zote mpaka hii *Green Bond* ikaingia kwenye soko na sasa hadi tulipofikia ni hatua nzuri. Pia, tunawapongeza pia *Tanzania Capital Market and Security Authority (CMSA)* kwa ku-*support* mchakato huu na kutoa *approval* yote mpaka tumefikia hapo tulipo na ni *Green Bond* ambayo inatupa heshima katika Bara hili la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapongeza *Dar es Salaam Stock Exchange* (Soko la Hisa la Dar es Salaam), wamekuwa wakitoa ushauri mzuri sana pamoja na Benki ya *NBC* ambao ndiyo *financer* wanaosimamia hii *Green Bond* ya *Tanga UWASA*. Vilevile, kwa namna ya pekee Wizara ya Fedha, haikuwa rahisi kwa sababu hii *Green Bond* pia inahusika na *approval* kutoka Wizara ya Fedha na Ofisi ya Msajili Wa Hazina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitaongelea katika *aspect* ya uwekezaji. Tumeenda, tume-*subscribe*, tulikuwa tuna malengo ya kupata shilingi 53,120,000,000 lakini *within the time* tulivyoweka hii *bond* tumepata shilingi 54,722,600,000 yaani tume-*oversubscribe* sawa na 103% ambayo *it's over and above*. Kwa hiyo hili ni jambo kubwa na ndiyo *starting* ya *game changer* kwenye uwekezaji kwenye sekta ya maji. *Green bond* maana yake ni *bond* inayotolewa kwa ajili ya mazingira na dunia uelekeo wake ni kwenye utunzaji wa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, leo hii una mamlaka sita zenye *Category Class A*. Tuna hiyo Tanga imeshaodoka, *Tanga UWASA* imekuja na *Green Bond* ambayo inaenda ku-*finance* Mradi Mkubwa wa Maji Mkoa wa Tanga na ita-*extend* mikoa ya Jirani. Vilevile, kuna Mamlaka ya Maji Moshi, nayo iende kwenye uelekeo huo tukitoka hapo Mamlaka ya Maji ya Dar es Salaam, tayari najua wako kwenye *pilot study* wanataka waingie na *bond* ya shilingi 252,000,000,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba Mheshimiwa Waziri, kama tulivyofanya *Tanga UWASA*, nao hawa twende kwa *spirit* hiyo hiyo. Pia, Mamlaka ya Maji ya Kahama nao wako vizuri, nao ni *Category AA* wanaweza wakaingia kwenye mfumo huu. Pia, Mamlaka ya Maji ya Iringa, nao wako katika *category* hii, Mamlaka ya Maji ya Mwanza, zote hizi tutapunguza mzigo wa kugombaniana. Shilingi 60,000,000,000 leo zimetolewa na Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kwenda kulipa madeni lakini tunagombaniana, mara Mamlaka za Maji, mara *RUWASA* huku, kuna vurugu mechi kila mahali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tukiwa tuna vyanzo vya *financing*, tutaondokana na kugombania chanzo kimoja cha

fedha, tutakuwa na vyanzo vingi. Naendelea kuishukuru hii *Tanga UWASA*, mimi kupitia Kamati ya Uwekezaji, nimepitia tangu mwanzo *bond* hii inaanza, nimeifuatilia kwa sababu nilijua ndiyo itakuwa mkombozi. Kwa kweli Bodi ya Mamlaka ya Maji ya Tanga, naipongeza lakini na *Engineer* Godfrey Hilly ni shujaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona hata miradi mingine, walichukua mkopo wa shilingi bilioni 7.2 ambayo umeleta maji kule Tanga, wanavuna takribani lita 15,000,000, Shilingi bilioni 7.2 waliyochukua kwenye Benki ya Maendeleo ya Taifa. Sasa, ndiyo *spirit* tunayotakiwa twende kwenye Mamlaka za Maji, tusitegemee fedha kutoka kwenye Mfuko mkubwa wa Hazina. Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo mimi binafsi nimeona ni jema na wewe sasa unavyokuja kuliongelea, uliongelee kwa msisitizo kwa baadhi ya mamlaka kama *pilot* nilizokutajia hizi sita kubwa *giant* ili tuweze ku-*move* mbele kama Taifa. Kwa hiyo nilitaka kutoa hilo wazo kwenye *alternative financing* kwenye Miradi ya Maji, tusikariri chanzo kimoja tu ambacho tunagombaniana. *(Makofi)*

MMheshimiwa Mwenyekiti, la pili sasa kwa sababu ya muda, niongelee habari ya jimboni kwangu. Habari ya kwanza ni usafiri, nilikuomba mwaka jana. *DMO* wangu wa wilaya hana gari, gari tumeomba, wenzangu naona hapo wanakwambia tunakushukuru Mheshimiwa Waziri, mimi si kwamba sishukuru najua tu nipo kwenye *waiting list*. Naomba *brother* utuletee gari ili *DMO* wangu anayechapa kazi, afanye kazi kwa ustadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna madeni ya wakandarasi, kuna lile Bwawa la Kwela, ni bwawa ambalo ni mradi wa shilingi 6,000,000,000 lakini yule anadai shilingi 2,000,000,000 mwaka mzima wame-*stuck*. *Brother*, naomba katika shilingi 60,000,000,000 ulizopewa shilingi 2,000,000,000 hizi utuletee Kwela ili Mradi wa Kwela uweze ku-*take-off*. Pia, Mradi wa *Kaoze Group*, yule mtu mmempa kazi, ameenda kuchukua *Advance Payment Bond* benki kama *security* lakini hamjampa hela. *Advance payment* ya shilingi 300,000,000 *Kaoze Group* ime-*stuck* hamna kinachoendelea. Nakuomba brother, ukafanye haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine, Mamlaka ya Maji katika Mji Mdogo wa Laela. Mmeanza mchakato, mnataka muifanye Laela iwe na Mamlaka ya Maji ya Mji Mdogo wa Laela ambayo itaweza sasa kuwa na watumishi *permanent* na kuendesha mambo yake binafsi kama Mamlaka ya Maji. Naomba hili jambo uli-*push* na ukifanya hayo kuna mambo mengi nitakuandikia kwa maandishi yanayohusu kero ya maji Jimbo la Kwela na Mkoa wa Rukwa tukiwa na ajenda ya *Lake Tanganyika*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa uchangiaji wetu kwa siku ya leo. Natumia fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao tumepata fursa ya kuchangia. Baada ya kusema hayo, naahirisha Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.34 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,*
*Tarehe 10 Mei, 2024 Saa Tatu Asubuhi Asubuhi)*